**IASC** Kikosi kazi cha Kamati ya Kudumu

## Mwongozo

# UJUMUISHWAJI WA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA MAJANGA NA HUDUMA ZA KIBINADAMU

Julai 2019

Kikosi Kazi cha IASC katika Ujumuishi wa Watu Wenye Ulemavu katika Huduma za Kibinadamu

Imepitishwa na IASC Oktoba 2019

# Mwongozo

# UJUMUISHWAJI WA WA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA MAJANGA NA HUDUMA ZA KIBINADAMU

Julai 2019
Kikosi Kazi cha IASC Katika Ujumuishi wa Watu Wenye Ulemavu katika Huduma za Kibinadamu

---

Imepitishwa na IASC, Oktoba 2019

Hakimiliki © Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali (IASC) 2019.

Haki zote zimehifadhiwa. Mwongozo huu umetolewa kwa ajili ya usambazaji.

Kutoa nakala na kutafsiri imeruhusiwa, isipokuwa kwa matumizi ya kibiashara, hakikisha unatambua chanzo cha mwongozo huu kila unapoutumia.

"This translation/adaptation was not created by the Inter-Agency Standing Committee (IASC). The IASC is not responsible for the content or accuracy of this translation. The original English edition "Inter-Agency Standing Committee: [INCLUSION OF PERSONS WITH DISABILITIES IN HUMANITARIAN ACTION] shall be the binding and authentic edition".

"Tafsiri ya mwongozo huu haikuundwa na Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali. Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali haihusiki na kilichoandikwa au usahihi wa kilichotafsiriwa. Toleo la asili la Kiingereza: "Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali; [UJUMUISHWAJI WA WATU WENYE ULEMAVU KWENYE HUDUMA ZA KIBINADAMU KATIKA MAJANGA] ndio toleo la kisheria na halisi".

# YALIYOMO

Yaliyomo v
Vifupisho vii
Shukrani viii
Utangulizi x
Dibaji xiii
1. Utangulizi 1
2. Unachotakiwa kufahamu 5
3. Nini kifanyike 19
4. Usimamizi wa taarifa na takwimu 23
5. Ushirikiano na uwezeshaji wa taasisi za watu wenye ulemavu 33
6. Masuala Mtambuka 30
7. Uwajibikaji 43
8. Njia za kutoa huduma za kibinadamu 47
9. Wajibu na majukumu ya wadau 55
10. Masuala yanayopswa kufanywa na sekta 69
11. Uratibu na usimamizi wa kambi 73
12. Elimu 83
13. Usalama wa chakula na lishe 93
14. Riziki 103
15. Afya 111
16. Ulinzi 141
17. Malazi na Makazi 167
18. Maji na Usafi wa mazingira 177
19. Viambatanisho 189

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **5W** | Who does What, Where, When, for Whom (Nani anafanya nini, Wapi, Lini, Kwa ajili ya nani) |
| **AAP** | Accountability to affected populations (Uwajibikaji wa watu walioathiriwa) |
| **AOR** | Area of responsibility (Sehemu ya jukumu) |
| **CA** | Camp administration (Uendeshaji wa kambi) |
| **CAAP** | Commitments on Accountability to Affected (Dhamira ya uwajibikaji kwa watu walioathiriwa) |
| **CCCM** | Camp coordination and camp management (Uratibu wa kambi na usimamizi wa kambi) |
| **CHS** | Core humanitarian standards (Viwango muhimu vya masuala ya kibinadamu) |
| **CMT** | Camp Management Toolkit (Nyenzo ya usimamizi wa kambi) |
| **CRC** | Convention on the Rights of the Child (Mkataba kuhusu haki za mtoto) |
| **CRPD** | Convention on the Rights of Persons with Disabilities (Mkataba kuhusu haki za Watu Wenye Ulemavu) |
| **DHS** | Demographic and health survey (Utafiti wa idadi ya watu na afya) |
| **DFID** | Department for International Development (Idara ya kimataifa ya maendeleo) |
| **ERW** | Explosive remnants of war (Masalia ya vilipuzi vya kwenye vita) |
| **FAO** | Food and Agriculture Organization (Shirika la Chakula na Kilimo Duniani) |
| **GBV** | Gender-based violence (Unyanyasaji wa kijinsia) |
| **HC** | Humanitarian Coordinator (Mratibu wa huduma za kibinadamu) |
| **HCT** | Humanitarian Country Team (Timu ya watu wa huduma za kibinadamu) |
| **HLP** | House, land and property (Nyumba, ardhi na mali) |
| **HIS** | Humanitarian Inclusion Standards (Viwango vya ujuishwaji wa huduma za kibinadamu) |
| **HNO** | Humanitarian needs overview (mahitaji ya kibinadamu kwa ufupi) |
| **HPC** | Humanitarian programme cycle (Programu ya hatua za huduma za kibinadamu) |
| **HRP** | Humanitarian response plan (Mpango wa kutekeleza huduma za kibinadamu) |
| **IASC** | Inter-Agency Standing Committee (Kikosi kazi cha Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali) |
| **IFRC** | International Federation of the Red Cross and Red Crescent Societies (Shirikisho la kimataifa la msalaba mwekundu na jumuiya za msalaba mwekundu) |
| **IHL** | International humanitarian law (Sheria ya kimataifa ya huduma za kibinadamu) |
| **IHRL** | International human rights law (Sheria ya kimataifa ya haki za kibinadamu) |
| **IMAS** | International Mine Action Standards (Viwango vya kimataifa vya shughuli za uchimbaji madini) |
| **INEE** | Inter-Agency Network for Education in Emergencies (Mtandao wa ndani kwa ajili ya elimu nyakati za dharura) |
| **INGO** | International non-governmental organization (Shirika la kimataifa lisilo la kiserikali) |
| **IOM** | International Organization for Migration (Shirika la kimataifa la uhamiaji) |
| **mhGAP** | Mental Health Gap Action Programme (Programu ya kupunguza ulemavu wa akili) |
| **MHPSS** | Mental health and psychosocial support (Kusaidia wenye ulemavu wa akili na afya ya akili) |
| **MICS** | Multiple indicator cluster survey (Viashiria kadha wa kadha vya tafiti za pamoja) |
| **NCD** | Non-communicable diseases (Magonjwa yasiyoambukiza) |
| **NFI** | Non-food items (Vitu ambavyo si chakula) |
| **NGO** | Non-governmental organization (Shirika lisilokuwa la kiserikali) |
| **OCHA** | Office of the Coordinator for Humanitarian Affairs (Ofisi ya mratibu wa masuala ya huduma za kibinadamu) |
| **OECD - DAC** | Organization for Economic Cooperation and Development - Development Assistance Committee (Shirika la ushirikiano wa kiuchumi na maendeleo-Kamati ya kusaidia maendeleo) |
| **OFDA** | Office of US Foreign Disaster Assistance (Ofisi ya Marekani ya masuala ya kimataifa katika kutoa msaada kwa majanga) |
| **OHCHR** | Office of the High Commissioner for Human Rights (Ofisi ya Kamishina wa haki za binadamu) |
| **OPD** | Organization of persons with disabilities (Mahirika ya watu wenye ulemavu) |
| **PSEA** | Protection against sexual exploitation and abuse (Ulinzi dhidi unyanyasaji na unyonyaji wa kingono) |
| **RC** | Resident Coordinator (Mratibu Mkazi) |
| **SDGs** | Sustainable Development Goals (Malengo yanayoweza kutimia ya maendeleo) |
| **SGBV** | Sexual and gender-based violence (Unyanyasaji wa kingono na kijinsia) |
| **SRH/ SHRH** | Sexual health and reproductive health (Afya ya uzazi na kijinsia) |
| **UNHCR** | United Nations High Commissioner for Refugees (Shirika la kimataifa la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia wakimbizi) |
| **WASH** | Water, sanitation and hygiene (Maji na usafi wa mazingira) |
| **WHO** | World Health Organization (Shirika la Afya Duniani) |
| **WRC** | Women's Refugee Commission (Kamisiheni ya wanawake wakimbizi) |

# Shukrani

Kikosi kazi cha **Kamati ya Kudumu ya Mashirika Mbalimbali yaani *"Inter-Agency Standing Committee"* (IASC)** kinachoshughulikia ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika masuala ya hali ya ubinadamu, kimetengeneza mwongozo huu kwa kuzingatia njia za mashauriano, ushirikishwaji na ujumuishwaji. Mwongozo huu unaakisi maoni ya zaidi ya wadau 600 kutoka katika sekta za masuala ya ulemavu, mashirika yanayotoa huduma za kibinadamu pamoja na wadau wa maendeleo.

Mchakato wa kutengeneza mwongozo huu ulisimamiwa na kikosi kazi cha IASC pamoja na mwenyekiti mwenza ndugu Georgia Dominik (International Disability Alliance), ndugu Gopal Mitra wa (UNICEF), ndugu Ricardo Pla Cordero pamoja na Ulrike Last (Humanity & Inclusion). Mshauri elekezi katika kuandaa mwongozo huu alikuwa ni ndugu Valerie Scherrer. Ndugu Asma Maladwala (UNICEF) pia alitoa mchango mkubwa katika kuandaliwa kwa mwongozo huu.

Wenyeviti wenza wa IASC pia wanatoa shukrani zao kwa wajumbe wote wa kikosi kazi cha IASC kwa ushirikiano wao kutoka mwaka 2016. Kikosi kazi kilihusisha wawakilishi kutoka taasisi za umoja wa mataifa, mashirika yanayotoa huduma za kibinadamu, mashirika ya maendeleo, serikali na mashirika ya watu wenye ulemavu. Wenyeviti wenza pia wanawashukuru wajumbe wa IASC waliohusika na masuala ya jinsia na yale ya hali za kibinadamu, wale waliokuwa katika sekta ya afya ya akili, masuala ya ubia wa fedha na ujifunzaji wa pamoja, na kitengo cha masuala ya ulinzi cha ulimwengu kwa mchango na ushiriki wao.

Kikosi kazi kinatoa shukrani kwa wajumbe wa makundi mbalimbali kwa michango yao ambao ni Facundo Chavez-Penillas kutoka (OHCHR), Isabelle De Muyser-Boucher(OCHA), Georgia Dominik(International Disability Alliance), Kirstin Lange(UNHCR), Ulrike Last (Humanity & Inclusion), Boram Lee (Women's Refugee Commission), Asma Maladwala (UNICEF), Anita Marini(MHPSS Reference Group) Gopal Mitra(UNICEF), Mina Mojtahedi (International Federation of the Red Cross/International Committee of the Red Cross) na Ricardo Pla Cordero kutoka (International Rescue Committee).

Pia tunawashukuru wafuatao kwa michango yao: - Sien Andries, Astrid Arne, Orsolya Bartha, Elena Bertozzi, Mariangela Bizzari, Estelle Bloom, Sabrina Ebert, Greta Gamberini, Priscille Geiser, Vidar Glette, Jessica Justus, Janet Lord, Meghna Manaktala, Melissa Marshall, Juliette Myers, Tom Palmer, Stephen Perry, Emma Pearce, Marcie Roth, Roberto Saltori, Delphine Sokchearta, Haakon Spriewald na Janet Aderemi Toyin.

Mwongozo huu usingeweza kuandaliwa bila ya kushauriana kwa kina yaliyofanyika pamoja na taasisi za watu wenye ulemavu zilizohudhuria na kushirikiana kwa karibu na kikosi kazi cha IASC. Kipekee tunawashukuru *African Disability Forum; the Arab Organization of Persons with Disabilities; Inclusion International; the Latin American Network of Non-Governmental Organizations of Persons with Disabilities na familia zao (RIADIS), pamoja na The Pacific Disability Forum. Pia tunawashukuru the Centre for Disability in Development (Bangladesh), The European Disability Forum, Human Rights Watch na Women's Refugee Commission* kwa michango yao katika mashauriano ya kikanda. Shukrani nyingine zinaenda kwa ndugu Dragana Jocic na Stacy Cokson wa IDA ambao wamefanya kazi usiku na mchana kuhakikisha tunapata vipindi na warsha nyingi za kushauriana.

Kwa ujumla zaidi tunawashukuru watu wote walioshiriki katika kuandaa mwongozo huu kwa kupitia dodoso la mtandaoni na kufanya utafiti wa awali. Tunawashukuru wale waliosaidia kupitia rasimu za awali na wale walioandaa sura mahususi za kisekta katika Mwongozo huu. Tunawashukuru wote walioshiriki katika warsha za mapitio ya mwongozo huu, michakato ya kimakundi ya kupitia kwa pamoja na makundi mengi ya kisekta yaliyowezesha mwongozo huu kutengenezwa.

Tunamshukuru ndugu Christine Dinsmore, Robert Archer na Adam Woolf kwa msaada wao katika uhariri wa mwongozo, ndugu Slimane Sorour kwa kazi yake ya usanifu na ndugu Prashant Verma kwa kuwezesha mwongozo huu kuwa rafiki kwa watu wenye ulemavu.

Sekretarieti ya IASC imetoa mchango mkubwa na maelekezo: kipekee tunamshukuru Isabelle de MuyserBoucher Nuhad Al-Alfi, Tanja Schuemer-Cross na Mervat Shelbaya. Pia, kikosi kazi kinawashukuru wenyeviti wenza wa IASC ambao ni Bernadette Castel-Hollingsworth (UNHCR) na Meritxell Relaño (UNICEF).

Mwongozo wa IASC kuhusu ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika masuala ya ubinadamu usingeweza kufanikiwa bila ya msaada wa kifedha uliotolewa kwa hisani ya mashirika yafuatayo: - *Australian Department of Foreign Affairs and Trade, Australian Permanent Mission's International Development Fund, the European Civil Protection and Humanitarian Aid Operations (ECHO), the Finnish Ministry of Foreign Affairs, the German Federal Foreign Office* na *the Luxembourg Ministry of Foreign Affairs.*

Mwisho, tunatambua kazi ya IASC, kwa uamuzi wake wa kuunda kikosi kazi pamoja na wenye viti wenza watatu, na kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu na wawakilishi kutoka kwenye taasisi za watu wenye ulemavu wanapata fursa na kushiriki kikamilifu katika kuandaa mwongozo huu kuanzia hatua za awali.

# Utangulizi

Mnamo mwaka 2011, wakati wanajeshi wenye silaha wakichoma moto makazi ya watu huko Tawergha nchini Libya, mwanamke mmoja aitwaye Hawa alikuwa hawezi kukimbia kutokana na ulemavu wake. Kwa bahati, alikuwa na dada zake wawili ambao walimbeba mpaka mahali salama. Katika miaka nane ya kuishi kwenye kambi, Hawa anasema aliwahi kumuona daktari mara moja tu.

Nimekutana na watu mbalimbali kama Hawa ambao wana ulemavu, na wanaishi uhamishoni kutokana na sababu za migogoro au kutokana na majanga yatokanayo na hali ya hewa. Kuweza kumudu hali na maisha mapya ni changamoto kwa kila mmoja. Lakini tunapozungumza na watu wenye ulemavu walio katika kuhitaji wa misaada ya huduma za kibinadamu kutoka Bangladesh mpaka Haiti, tunaona ugumu wa ziada wanaoupata katika kukabiliana na changamoto zao ikiwa jitihada na huduma zetu hazizingatii masuala yao muhimu.

Wajibu wetu ni kuhakikisha kuwa watu wenye hali kama ya Hawa wanahesabiwa kama watu wengine katika huduma za misaada ya kibinadamu nyakati za majanga. Ni haki yake ya msingi- na ni haki ya maelfu ya watu wengine - kupata usalama na ulinzi sawa, kama inavyofanywa kwa watu wengine.

Pia, tunapaswa kuhakikisha mkazo maalum unawekwa kwa makundi yaliyoachwa pembeni kama vile watoto na wazee ambao mara nyingi hukumbwa na hatari ya kutoonekana katika kipindi cha majanga.

Ili kuweza kufanikisha hili, jitihada za kamati ya IASC kuhusu mwongozo wa ujumuishi kwa watu wenye ulemavu katika masuala ya huduma za kibinadamu, zinakaribishwa kama hatua ya kimkakati iliyokuja wakati muafaka ili kutoa muelekeo sahihi. Ninatoa shukrani kwa wajumbe wa kikosi kazi cha IASC pamoja na mwenyekiti mwenza kutoka UNICEF, *Humanity & Inclusion*. Pia, shirikia hili hujulikana kama *Handicap International*, pamoja na taasisi ya *International Disability Alliance* kwa kazi nzuri ya kuandaa Mwongozo huu kwa niaba ya IASC. Mwongozo huu unakuja wakati kuna ongezeko la hamasa kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu ulimwenguni.

Mwongozo huu wa kwanza na wa aina yake, utahakikisha ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika kila sekta na katika nyanja zote za huduma za kibinadamu. Mwongozo huu ni matokeo ya mchakato wa kushauriana uliohusisha zaidi ya wadau 600 kutoka katika taasisi zinazotoa huduma za kibinadamu, pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu ulimwenguni. Kwa muktadha huu, na ili kuokoa maisha na kupunguza mateso kwa binadamu wakati wa majanga, Umoja wa Mataifa na taasisi zake utatekeleza mwongozo huu kulingana na nafasi yake pamoja na maamuzi kutoka katika vyombo vyake vya kiutawala.


Wazo la kuandaa mwongozo huu limetokana na mkataba wa ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika huduma za kibinadamu yaani *"Charter on Inclusion of Persons with Disabilities in Humanitarian Action"* uliozinduliwa mwaka 2016 katika mkutano wa viongozi wa dunia kuhusu masuala ya kibinadamu huko mjini Istanbul. Mtakaba huu umesainiwa na wadau takribani 220, yakiwemo mataifa 30 wajumbe wa Umoja wa Mataifa na taasisi 14 za Umoja wa Mataifa.

Mwongozo huu ni muhimu katika kuchangia sekta ya huduma za kibinadamu katika mkakati wa Umoja wa Mataifa wa ujumuishi yaani *'United Nations Disability Inclusion Strategy (UNDIS)'* ambao ulizinduliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa mwezi Juni mwaka 2019.



Kila mmoja anafaidika tunapoondoa vikwazo na kutoa fursa kwa watu wenye ulemavu. Shirika la Kazi Duniani limegundua kuwa kuwatenga watu wenye ulemamvu katika ulimwengu wa kazi kunashusha pato la taifa kwa asilimia 7.

Sio tu kwamba tunafanya jambo sahihi, jitihada zetu pia katika kutoa huduma za kibinadamu zinapata ufanisi mkubwa pale ambapo sauti za wasio na sauti zinapewa kipaumbele na pale tunapokuwa na uhakika kuwa hatumuachi mtu yeyote nyuma.



**Mark Lowcock**
Katibu Mkuu-Masuala ya
Huduma za Kibinadamu na
Mratibu wa Afua za Dharura

# Dibaji

Mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu wa mwaka 2006, unatoa mwelekeo mpya kwa watu wenye ulemavu. Mkataba huu umebadili sera na utekelezaji wake kutoka katika mtazamo wa hisani na kimatibabu na kujikita katika misingi ya haki za kibinadamu.

Mfumo wa kimataifa umekuwa jumuishi kufuatia kupitishwa kwa Agenda ya 2030 ya maendeleo endelevu mwaka 2015, ambayo inasisitiza umuhimu wa kutomuacha mtu nyuma na kwamba wale walio nyuma zaidi wapewe kipaumbele. Mfumo wa Kupunguza Hatari ya Maafa wa Sendai yaani '*Sendai Framework for Disaster Risk Reduction* (2015)' na taarifa ya "*One Humanity Shared Responsibility*" kwa Katibu Mkuu wa World Humanitarian Summit iliyofanyika mwaka 2016, inatoa kanuni zile zile kama zilivyotolewa kutoka kwenye mkutano wa viongozi wa dunia kuhusu masuala ya kibinadamu ikiwemo mkataba wa *ujumuishwaji kwa watu wenye ulemavu katika masuala ya huduma za kibinadamu*.

Umoja wa Mataifa kwa sasa unapitia mifumo na sera zake ili ziweze kuwa jumuishi zaidi kwa watu wenye ulemavu. Mnamo mwezi Machi 2019, Umoja wa Mataifa ulipitisha Mkakati wa ujumuishi wa umoja wa mataifa (*UN Disability Inclusion Strategy*) chini ya taasisi zake, wawakilishi kutoka katika kila taifa, na timu za masuala ya huduma za kibinadamu zitapima na kufuatilia ufanisi kuhusu ujumuishi wa watu wenye ulemavu.

Mkutano wa kilele wa kimataifa wa masuala ya huduma za kibinadamu (The World Humanitarian Summit) wa mwaka 2016 ulifikia maazimio ya kutengeneza mwongozo unaoungwa mkono kimataifa na kujumuisha watu wenye ulemavu katika masuala ya huduma za kibinadamu (mkataba wa ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika masuala ya ubinandamu). Mwongozo huu umebuniwa ili kutoa taarifa sahihi kwa wadau wa masuala ya kibinadamu pamoja na wadau wengine. Mwongozo huu unamuweka mtu mwenye ulemavu kama kipaumbele katika masuala ya haki na huduma za kibinadamu.

**Angalizo**

Mwongozo huu unatoa kanuni za kujumuisha watu wenye ulemavu katika huduma za kibinadamu. Katika hatua nyingine za utekelezaji, IASC itaandaa vitendeakazi na nyenzo mahususi. Taasisi washirika wa IASC wanashauriwa kuwa vinara katika kusimamia na kukuza utekelezaji wa Mwongozo huu kwa kutumia zana na nyenzo kutoka katika taasisi wanazoziongoza.

Zana na nyenzo zilizoorodheshwa kama mifano katika mwongozo huu, zinaweza kuwa hazijahuishwa kutokea kupitishwa kwa Mkataba wa haki za watu wenye ulemavu mwaka 2008, na zingine zinaweza kuwa hazishabihiani sana na viwango vya mkataba huo. Viwango hivyo hujumuisha upatikanaji wa idhini ya hiari, kutokuwekwa katika taasisi na makazi maalumu, kutokuwa huru, na kutolazimishwa, kati ya mengineyo. Kushindwa kuheshimu viwango hivi hupelekea ukiukwaji wa haki za binadamu ambapo watu wenye ulemavu huathiriwa zaidi. Rasilimali na nyenzo zimekubaliwa na kuwekwa katika mwongozo huu kwakuwa ni za muhimu katika kukuza ujumuishaji na ushiriki wa watu wenye ulemavu katika masuala ya huduma za kibinadamu.

# 1 Utangulizi


## Mwongozo huu unahusu nini?

Mwongozo huu unaweka hatua muhimu za kuchukuliwa na wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu, ili kupata namna bora ya kutambua mahitaji na haki za watu wenye ulemavu, ambao kwa sehemu kubwa wapo katika hatari ya kusahaulika na kuachwa nyuma katika huduma za kibinadamu.

Mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa katika kila sura ya mwongozo huu yanawaweka watu wenye ulemavu katika kitovu cha masuala ya huduma za kibinadamu, kama wadau na kama wajumbe wa jamii zilizoathiriwa. Mwongozo huu ni mahususi kwa watu wenye ulemavu katika muktadha wa huduma za kibinadamu na umejengewa katika kuendeleza viwango vilivyowekwa na miongozo mbalimbali inayojulikana kwa kitaalamu kama *Core Humanitarian Standard, Sphere Handbook* na *viwango vya ujumuishi wa huduma za kibinadamu kwa ajili wazee na watu wenye ulemavu*.

Huu ni mwongozo wa kwanza kutengenezwa kwa kushirikiana na watu wenye ulemavu na kupata uwakilishi kutoka katika taasisi za wadau wa huduma za kibinadamu. Mwongozo huu umepatikana kwa kuzingatia matokeo ya mchakato wa mashauriano kati ya mashirika ya wadau wa huduma za kibinadamu. Pia, mwongozo huu umebuniwa kuhamasisha utekelezaji wa viwango vya jitihada na programu za kibinadamu katika nyanja zote katika kila eneo, pamoja na kuanzisha na kukuza ujumuishi wa watu wenye ulemavu pamoja na ushiriki wao katika kufanya maamuzi ya masuala yanayowahusu.

**Mchoro namba1 |** Malengo manne ya mwongozo huu




## Kwanini mwongozo huu ni muhimu?

Inakadiriwa kuwa asilimia 15 ya watu duniani wana aina tofauti za ulemavu.[1] Katika muktadha wa huduma za kibinadamu asilimia hii inaweza kuwa ni kubwa zaidi. Kundi hili ni miongoni mwa makundi yaliyosahaulika katika jamii ambazo zinakumbwa na majanga,[2] pia huathiriwa zaidi katika nyakati za migogoro na dharura. Nyakati za majanga, idadi yao ya vifo huwa ni kati ya mara mbili au nne zaidi ukilinganisha na watu wasio na ulemavu.[3]

Watu wenye ulemavu hawalingani, wanatofautiana katika uzoefu wao kulingana na jinsi vizuizi vya kimazingira na kimawasiliano vinavyochangia kukwamisha ushiriki wao katika masuala ya kibinandamu pamoja na masuala mengine mfano umri, jinsia, kabila, mahali anapotokea na rangi. Kutokana na muingiliano wa hizi sababu, watu wenye ulemavu wanakabiliana na ukandamizwaji pamoja na vitendo vya kibaguzi. Mfano, watoto wenye ulemavu wapo katika hatari kubwa wakati majanga ya dharura ya kibinadamu yanapojitokeza. Wanawake wenye ulemavu pia wapo katika hatari kubwa ya kunyanyaswa kijinsia.[4]

**Mchoro namba 2 |** Takwimu za watu wenye ulemavu ulimwenguni[5]




[1] Shirika la Afya na Benki ya Dunia, *Taarifa ya Dunia kuhusu Ulemavu* (2011).

[2] Taarifa ya Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika mkutano wa kimataifa wa masuala ya kibinadamu, *umoja wa utu, kushirikiana majukumu*.

[3] Katsunori Fujii, '*Tetemeko kuu la Japan ya Mashariki na watu wenye ulemavu*'. Katika Kituo cha taarija juu ya ulemavu, Japan.

[4] *Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto, Kujumuisha watoto wenye ulemavu katika masuala ya kibinadamu-Mwongozo wa jumla* (2017).

[5] Vyanzo: Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia, *Taarifa ya Dunia Juu ya Ulemavu* (2011) UNDESA, *Kuzeeka na Ulemavu*; Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto, *Watoto na Vijana wenye Ulemavu* (2013).







## Mwongozo unamhusu nani?

Mwongozo huu umebuniwa kutumika na wadau wa huduma za kibinadamu kitaifa, kikanda na kimataifa ambao wanahusika kutengeneza sera, uratibu, mipango, na ufadhili wa fedha kama vile:

- Serikali;
- Viongozi wa taasisi za huduma za kibinadamu;
- Viongozi wa kisekta;
- Wapangaji wa programu katika mashirika yanayotoa huduma za kibinadamu na yale yanayohusu maendeleo;
- Wafadhili;
- Mashirika ya watu wenye ulemavu, kitaifa, kikanda na kimataifa[6]

Mwongozo huu pia utakuwa na manufaa kwa wafanyakazi waliopo kwenye utendaji kwa kuwa unaelezea mchakato wa ujumuishi wa watu wenye ulemavu na kutoa mapendekezo mahususi.

## Mwongozo huu unaweza kutumika wapi?

Katika hali zote, wadau wa masuala ya kibinadamu kwa pamoja na taasisi za watu wenye ulemavu, wanapaswa kuzitambua na kuzifanyia kazi sababu zinazosababisha watu wenye ulemavu kupata ugumu katika kupata usaidizi na ulinzi (angalia katika kipengele cha vizuizi), pamoja na sababu za kuhamasisha ujumuishwaji pamoja na ulinzi. Hii ni muhimu katika kuhakikisha kuwa kila mdau ambaye ameathirika, anapata huduma anazostahili ili kuimarisha uwajibikaji katika utoaji wa afua.

Vigezo maalum vinavyotakiwa kuzingatiwa wakati wa kutekeleza mwongozo huu ni kama vile:-

- Kiwango ambacho ulemavu unatambuliwa na kueleweka katika nchi zilizoathirika;
- Kiwango cha utaalamu katika masuala ya ulemavu uliopo katika nchi iliyoathirika;
- Viwango vya ubora vya misingi ya kisiasa na kisheria kuhusu masuala ya ulemavu katika nchi iliyoathirika;
- Kiwango cha upatikanaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu na ufikikaji;
- Uwepo wa taasisi za watu wenye ulemavu na kama zina ujuzi unaohitajika na rasilimali za kutosha;
- Uwepo wa taarifa zenye viwango kuhusu watu wenye ulemavu na kiwango cha upatikanaji wa taarifa sahihi zinazooneshа utofauti katika idadi ya watu wenye ulemavu katika kila nchi.

Kwa kutilia mkazo, taasisi za watu wenye ulemavu katika maeneo yaliyoathirika yana rasilimali chache au hayana ujuzi na huenda hayawawakilishi watu wenye ulemavu. Endapo sababu itakuwa ndio hii, basi kutakuwa na haja ya kuwajengea uwezo katika masuala ya huduma za kibinadamu au kuunda na kuwezesha makundi rika ya watu wenye ulemavu. Lengo ni kuwezesha taasisi za watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika mashauriano, usaidizi na ulinzi katika nyakati zote za kuchukua jitihada dhidi ya majanga ya kibinadamu (ikiwa ni pamoja na mikakati ya kujiweka tayari, kutoa huduma na urejeshaji wa jamii katika hali ya kawaida).

Kwa kutilia mkazo, taasisi za watu wenye ulemavu katika maeneo yaliyoathirika yana rasilimali chache au hayana ujuzi na huenda hayawawakilishi watu wenye ulemavu. Endapo sababu itakuwa ndio hii, basi kutakuwa na haja ya kuwajengea uwezo katika masuala ya huduma za kibinadamu au kuunda na kuwezesha makundi rika ya watu wenye ulemavu. Lengo ni kuwezesha taasisi za watu wenye ulemavu kushiriki kikamilifu katika mashauriano, usaidizi na ulinzi katika nyakati zote za kuchukua jitihada dhidi ya majanga ya kibinadamu (ikiwa ni pamoja na mikakati ya kujiweka tayari, kutoa huduma na urejeshaji wa jamii katika hali ya kawaida).

Katika hali zote, wadau wa masuala ya kibinadamu kwa pamoja na taasisi za watu wenye ulemavu, wanapaswa kuzitambua na kuzifanyia kazi sababu zinazosababisha watu wenye ulemavu kupata ugumu katika kupata usaidizi na ulinzi (angalia katika kipengele cha vizuizi), pamoja na sababu za kuhamasisha ujumuishwaji pamoja na ulinzi. Hii ni muhimu katika kuhakikisha kuwa kila mdau ambaye ameathirika, anapata huduma anazostahili ili kuimarisha uwajibikaji katika utoaji wa afua.

[6] Mwongozo unalenga kufikia mahitaji ya wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu walio rasimishwa, ikiwemo mashirika ya watu wenye ulemavu na wadau wa maendeleo kuhusishwa katika masuala ya kibinadamu, kuliko mashirika yaliyobobea katika ulemavu. Angalia kumbukumbu za mkutano wa wadau wa *warsha ya IASC* iliyofanywa Oktoba 2017.

# 2 Unachotakiwa kufahamu

## Muundo wa sheria na sera

Kamati ya IASC[7], kimsingi ni chombo cha awali katika kuratibu masuala ya kibinadamu katika ngazi ya kimataifa. IASC inasisitiza umuhimu wa sheria za kimataifa katika majanga ya kibinadamu, hasa sheria ya kimataifa ya masuala ya huduma za kibinadamu, haki za binadamu na masuala ya wakimbizi[8]. Vyombo vya kisheria vinatoa muundo wa kisheria unaojikita katika masuala ya kibinadamu katika mfumo unaokubalika kimataifa, kikanuni na viwango na kukazia haki za watu wote wanaoathiriwa na majanga. Sheria ya kimataifa ya haki za binadamu ambayo hutumika, inatengeneza daraja kati ya vitendo vya kibidanamu na maendeleo. Inaweza kutumika katika kueleza sababu na athari, kubainisha na kufikia mahitaji ya kibinandamu na kuanzisha vigezo vinavyotakiwa kufuatwa kabla mhusika kufurahia haki zilizokubaliwa kimataifa.

Wadau katika nchi ndio wawajibikaji wakuu kwa mujibu wa sheria ya kimataifa ya haki za binadamu.[9] Hao ndio wana jukumu la kwanza la kulinda, kuheshimu na kutimiza haki za watu katika himaya zao au chini na maeneo yao. Watu walioathiriwa na majanga na dharura wana haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni, ambazo zinatakiwa kulindwa na kutekelezwa.

Mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu ni mkataba wa kimataifa unaozitaka nchi wanachama kuutekeleza na kuuridhia.[10] Mkataba huo unazitaka nchi wanachama kulinda na kukuza haki za watu wenye ulemavu katika sheria, sera na utendaji na kuendana na viwango vya mkataba huo wanapofika katika mashirikiano ya kimataifa.

Ibara ya 11 ya mkataba kipekee inazitaka nchi wanachama, kulingana na matakwa ya sheria za kimataifa, kuchukua hatua zote stahiki kuhakikisha ulinzi na usalama wa watu wenye ulemavu katika hali zote za hatari, ikiwemo na nyakati za vita, dharura za kibinadamu na majanga ya asili.[11]

Ibara zingine za mkataba huu ni muhimu katika masuala ya huduma za kibinadamu na maendeleo, na kusaidia ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu. Mkataba huo unazingatia afua zote za kibinadamu. Ili kufanya hivyo wadau wanapaswa kutafiti na kutathmini

---

[7] Kamati ya Kudumu ya mashirika tofauti (IASC) ilianzishwa mwaka 1992 katika kuitikia maazimio ya baraza kuu la Umoja wa Mataifa azimio namba 46/182. Wajumbe wake wanajumuisha mashirika ya Umoja wa Mataifa na yasiyo ya Umoja wa Mataifa yanayohusiana na masuala ya kibinadamu. Kwa taarifa zaidi angalia *tovuti ya IASC*.

[8] Angalia IASC, *Sera ya IASC katika ulinzi wa masuala ya kibinadamu* (2016); na *IASC, tamko la kanuni za IASC: Kiini cha Ulinzi katika masuala ya kibinadamu* (2013); kiambatishi namba 1 cha sera ya IASC kuhusu ulinzi kinatoa taarifa muhimu kuhusu sheria zinazofaa za kimataifa.

[9] Chini ya sheria ya kimataifa ya masuala ya kibinadamu, vikundi vinavyomiliki silaha (NSAGs) zinazoshiriki katika migogoro ya kivita wanapashwa kuheshimu sheria ya kimataifa ya masuala ya kibinadamu. Kwa kuongezea taasisi au NSAGs zinazofanya majukumu kama ya kiserikali au kudhibiti maeneo wanaendelea kutegemewa kuheshimu sheria za kimataifa za haki za binadamu pale ambapo vitendo vyao vinaathiri haki za binadamu au watu waliopo chini yao.

[10] Mataifa 179 na Umoja wa Ulaya ni washirika wa mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu tangu Juni 2019.

[11] Angalia, *Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu na Protokali ya hiari*.

michakato na matokeo ili kuhakikisha haki za watu wenye ulemavu zinalindwa na kukuzwa kama inavyotakiwa katika sheria za kimataifa.

## Sheria ya kimataifa ya haki za binadamu

Sheria ya kimataifa ya haki za binadamu inathibitisha kuwa watu wote wana haki za kiraia, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kitamaduni na imeainisha haki hizo. Katika kutekeleza haki za watu, mkataba wa haki za watu wenye ulemavu umebadilisha namna watu wenye ulemavu wanadhaniwa. Ulemavu unatambulika kama hali inayojitokeza ambapo watu wenye vikwazo wanapokutana na vizuizi katika jamii zao. Suala hili ni muhimu si katika kutambua ulemavu tu bali katika namna ya kuhusika na watu wenye ulemavu, ikiwemo katika muktadha wa masuala ya huduma za kibinadamu. Ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wananufaika na haki zao, ni muhimu kuondoa vikwazo vyote vya kijamii, kisheria, kisiasa, kimazingira ambavyo vinasababisha kutonufaika na haki zao, ikiwemo mitazamo na tabia ambazo zinawabagua na kuwakandamiza. Pia, ni muhimu kuwajumuisha watu wenye ulemavu katika kufanya maamuzi kuendana na usemi wa "Hakuna chochote kuhusu sisi, bila sisi".

## Sheria ya Kimataifa ya Ubinadamu

Wakati wa migogoro ya kivita, sheria ya kimataifa ya huduma za kibinadamu inatoa ulinzi wa kijumla kwa raia na watu wote ikiwemo watu wenye ulemavu bila ya ubaguzi.[12] Katazo la ubaguzi linaruhusu wadau wa huduma za kibinadamu kutoa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu, hata kama ikibidi kuchukua hatua mahususi. Afua zinazotolewa na huduma za kibinadamu zinapaswa kuhakikisha kwa mfano chakula, maji, afya, utengemao na malazi vinapatikana na kufikiwa na watu wenye ulemavu. Vifungu vya sheria ya kimataifa ya ubinadamu vinaweza kutumika kuzuia au kupunguza madhara kwa watu wenye ulemavu nyakati za hatari. Kwa kutambua kuwa watu wenye ulemavu husahaulika wakati wa majanga, sheria inahitaji watu hawa wapewe kipaumbele katika uokoaji. Sheria ya kimataifa ya haki za binadamu na ya huduma za kibinadamu zinahitaji watu wenye ulemavu walindwe katika mazingira ya kivita; jukumu hili pia linapatikana katika kifungu namba 11 cha mkataba wa haki za watu wenye ulemavu.

Mikataba ya kupunguza matumizi ya silaha inahitaji ulinzi kwa wahanga baada ya migogoro kuisha.

## Miundo mingine ya kisheria na kisera

### Malengo ya Maendeleo Endelevu

Agenda ya Maendeleo Endelevu ya mwaka 2030 inasisitiza kuwa mataifa yote yanao wajibu wa kuheshimu, kulinda na kukuza haki za binadamu bila ya ubaguzi wa aina yeyote ikiwemo haki za watu wenye ulemavu. Lengo namba 17 linatoa muundo uliokubalika kimataifa kuhusu mikakati ya kitaifa na kimataifa ya kuleta maendeleo mpaka kufikia mwaka 2030. Ajenda hii pia inahusisha azimio la kuhakikisha 'Hakuna mtu anayeachwa nyuma'.

Lengo namba 96 linahusu ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika masuala ya kibinadamu. Lengo hili linathibitisha mahitaji ya kukuza jamii zenye amani na ambazo ni jumuishi kwa maendeleo endelevu, kutoa haki kwa wote na kutengeneza taasisi zenye ufanisi, zinazowajibika na jumuishi katika ngazi zote. Lengo namba 9 linatoa wito kwa jamii kutengeneza miundombinu imara, hasa katika maeneo ambayo majanga hutokea. Lengo namba 11 na 13 linatukumbusha kuwa hakuna suala ikiwemo la kuzuia majanga na kuleta unafuu linaloweza kueleweka, kuelezewa au kufanyiwa kazi kwa ufahasa likiwa peke yake.

### Muundo wa Kupunguza Hatari ya Majanga wa Sendai 2015-2030[13]

Muundo wa Sendai unalenga kupunguza hatari ya majanga na upotevu wa maisha na mali. Muundo huu unakuza mtazamo wa 'Jamii yote' ambao unahusisha watu wenye ulemavu. Muundo huu unakuza ujumuishi,[14] ufikiwaji,[15] na utumiaji wa viwango vya kimataifa,[16] na kutambua kuwa watu wenye ulemavu pamoja na mashirika yao wana jukumu la kufanya katika kila hatua ya mipango ya kupunguza hatari ya majanga.[17]

[12] Angalia ICRC, *Unyanyapaa*.

[13] *Mfumo wa Kupunguza Majanga wa Sendai 2015-2030*, uliopitishwa katika kongamano la tatu ya Umoja wa Mataifa huko Sendai, Japan tarehe 18/03/2015.

[14] *Ibid*, aya ya 7.

[15] *Ibid*, aya ya 19(d).

[16] *Ibid*, aya ya 30(c).

[17] *Ibid*, aya ya 36(a)(iii).

[18] Angalia ajenda kuhusu utu, *angalia taarifa na maazimio*.

[19] *Ibara ya tatu ya mkataba wa kimataifa wa watu wenye ulemavu*.

[20] Kuhusu utu, kutoegemea upande wowote, na kutopendelea, angalia *Azimio la Baraza Kuu azimio namba 46/182* (1991). Kuhusu uhuru angalia azimio la Baraza Kuu, azimio namba 58/114 (2004).





### Mkutano wa kilele wa masuala ya huduma za kibinadamu wa mwaka 2016 na agenda ya maazimio ya ubinadamu.

Hali ya watu wenye ulemavu ilijadiliwa wakati wa mkutano wa kilele wa masuala ya kibinadamu huku mashirika kadhaa yakidhamiria kujumuisha watu wenye ulemavu katika masuala ya huduma za kibinadamu.[18] Nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, mashirika yasiyo ya kiserikali na wadau wengine walitambua kuwa sera za kibinadamu, taratibu na programu ambazo zinahusisha kuwajumuisha watu wenye ulemavu, zinapaswa kuimarishwa na kuwekewa mifumo.

*Mkataba wa Ujumuishi Kwa Watu Wenye Ulemavu Katika Masuala ya Kibinadamu*, uliozinduliwa wakati wa mkutano wa kilele, umejengwa katika misingi ya sheria za kimataifa za masuala ya kibinadamu pamoja na sheria za kimataifa za haki za binadamu. Mkataba huu uliweka maazimio matano ya kutendewa kazi: kutobaguliwa, ushirikishwaji: sera jumuishi, kutoa huduma jumuishi; ushirikiano na uratibu.

Kwa nyongeza, Mikataba ujulikanayo kitaalamu kama "*Global Compact on Refugees*" na "*The Global Compact for Safe, Orderly and Regular Migration*" umeingiza vipengele mahususi kuhusu watu wenye ulemavu ambavyo vinahamasisha ushiriki wao katika masuala ya ukimbizi na uhamiaji.

## Misingi ya Mwongozo wa IASC

Mwongozo wa IASC wa ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika masuala ya kibinadamu umejengwa katika msingi wa kutoa haki kwa watu wenye ulemavu ambao utaheshimiwa, utalindwa na kukuzwa katika muda wote wa kujiandaa, kujiweka tayari, kutoa huduma na kurejesha jamii katika hali yake ya kawaida baada ya majanga.

Mkataba wa Kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu unahusisha kanuni ambazo zinakubalika katika masuala ya huduma za kibinadamu. Kanuni hizi zinahusu heshima na utu, ushiriki na ujumuishi, kutobaguliwa na usawa wa fursa na usawa kati ya wanaume na wanawake. Mkazo zaidi unawekwa lakini kwa mlingano sawa katika kanuni ya ufikiwaji wa huduma, kuheshimu tofauti, kuwakubali watu wenye ulemavu kama sehemu ya utofauti wa binadamu, heshima katika ukuaji wa uwezo wa watoto wenye ulemavu, uhuru binafsi katika kufanya maamuzi binafsi; na uhuru wa watu.

Kanuni hizi zinaingiliana na kila haki inayotolewa na mkataba wa haki za watu wenye ulemavu. Kama zitatekelezwa sambamba na viwango vya misingi ya kibinadamu, ikiwemo mkataba wa masuala ya kibinadamu pamoja na kanuni za maadili, zinahakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanajumuishwa katika kila hatua za matayarisho na kutoa huduma katika masuala ya dharura za kibinadamu.

Masuala ya kibinadamu pia yanawezeshwa na taarifa kutoka katika kanuni zinazohusu utu, kutofungamana na upande wowote, kutopendelea na uhuru uliojengwa, na maamuzi ya baraza kuu la Umoja wa Mataifa.[20] Kanuni hizi ni nguzo muhimu katika kazi za mashirika ya kibinadamu, ambapo mengi kati yao yamejikita katika kulinda haki za binadamu, heshima na utu wa jamii zilizoathiriwa na kuimarisha uwajibikaji kwa kuidhinisha Kanuni za maadili au kuidhinisha utekelezaji wa misingi tisa ya viwango vya masuala ya kibinadamu. Kanuni za kibinadamu zinasisitiza umuhimu wa kuendeleza na kuboresha uwajibikaji, ubora na ufanisi katika masuala ya kibinadamu. Kanuni hizi ni muhimu katika juhudi za kuhakikisha ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika huduma za kibinadamu.

## Je, watu wenye ulemavu ni akina nani?

Kwa muktadha wa mwongozo huu, watu wenye ulemavu ni pamoja na wale wenye ulemavu wa afya ya akili, pamoja na upungufu mwingine ambao ukiingiliana na vizuizi, husababisha watu wenye ulemavu kushindwa kushiriki au kufikia programu za kibinadamu, huduma au ulinzi.[21]

Mtazamo unaozingatia haki za binadamu kwa watu wenye ulemavu, unawapa kipaumbele watu wenye ulemavu na hupunguza vikwazo na hatari wanazokumbana nazo. Inahitaji wadau wa masuala ya kibinadamu kutambua uwezo wa watu wenye ulemavu katika kuchangia kwenye jitihada za huduma katika majanga ya kibinadamu.

Watu wenye ulemavu wanatofautiana. Wana ulemavu wa aina mbalimbali pamoja na utambulisho tofauti (wanawake, watu asili, watoto, n.k). Kutokana na muingiliano wa hali hizi watu wenye

ulemavu hukumbana na aina mbalimbali za ubaguzi. Ili kuhakikisha watu wenye ulemavu hawaachwi nyuma, uelewa wa tofauti hizi unapaswa kusaidia kuelezea mitazamo na hatua zinazochukuliwa kutoka awali katika huduma za kibinadamu.

## Dhana muhimu na ufafanuzi

**Ufikivu** ni moja ya kanuni nane ambazo zinawezesha haki zilizowekwa katika mkataba wa watu wenye ulemavu kuweza kutafsiriwa. Dhana hii inatambua haki ya watu wenye ulemavu kufurahia "Ufikivu kama watu wengine, katika mazingira, vyombo vya usafiri, taarifa na mawasiliano, ikiwemo mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano, pamoja na miundombinu na huduma zilizo wazi au kutolewa kwa umma, mijini na vijijini".[22] Ufikivu ni kigezo kimojawapo cha ujumuishi, kinapokosekana, watu wenye ulemavu hawawezi kujumuishwa ipasavyo.

**Usanifishaji miondombinu kwa wote yaani "*Universal design*"**, ni dhana inayotoa utetezi kuwa "Usanifu wa bidhaa, mazingira, programu na huduma zinapaswa kusanifiwa na kubuniwa kwa namna ambayo zinaweza kutumika na watu wote, kwa kiwango kinachowezekana, bila kuwa na mahitaji ya urekebishaji, ubunifu au "Usanifu maalum".[23] Kanuni za usanifishaji kwa wote inawezesha ufikivu wa huduma na masuala mbalimbali kwa watu wenye ulemavu.[24]

**Teknolojia saidizi**-vifaa na visaidia jongevu ni vifaa vinavyoonekana (vifaa, zana, nyenzo, au programu) ambazo zimetengenezwa na zinapatikana kwa ajili ya kuboresha ufanyaji kazi na uhuru wa mtu binafsi, ushiriki na ustawi wa mtu kwa ujumla.[25] Zinaweza pia kuzuia kutokea kwa hali ya pili ya ulemavu au tatizo la kiafya. Mfano wa vifaa saidizi na teknolojia ni pamoja na viti mwendo, viungo bandia, vifaa vya usikivu, vifaa vya uoni na mfumo wa programu za kompyuta ambazo zinaboresha ujongevu, usikivu, uoni au uwezo wa kuwasiliana.

**Vikwazo** ni sababu zilizomo katika mazingira binafsi ambazo zinazuia ushiriki na kusababisha ulemavu. Kwa watu wenye ulemavu, vinazuia ufikivu na ujumuishi katika jamii. Vikwazo vinaweza kuwa ni vya kimtazamo au vya kitaasisi.

**Vikwazo vya kimtazamo** ni mtazamo hasi ambao mizizi yake inatokana na imani za kidini na kitamaduni; chuki, mgawanyo wa madaraka usiolingana, unyanyapaa, ubaguzi, ujinga na upendeleo, ikiwa ni miongoni wa sababu. Wanafamilia au watu walio karibu na watu wenye ulemavu wanaweza kukabiliwa na unyanyapaa unaosababishwa na ukaribu/uhusiano wao na watu wenye ulemavu, Vikwazo vya kimtazamo ndio kiini cha ubaguzi na kutengwa.

**Vikwazo vya kimazingira** ni pamoja na vizuizi katika mazingira asili au mazingira yaliyojengwa ambayo "Yanazuia ufikivu na kuathiri fursa za ushiriki",[26] pamoja na mifumo ya mawasiliano isiyofikika. Jambo hili linazuia watu wenye ulemavu kufikia taarifa na ujuzi na hivyo

[21] *Imeboreshwa kutoka ibara ya kwanza ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu*.

[22] *Ibara namba 9 ya mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu*.

[23] *Ibara namba 2 ya mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu*.

[24] Mamlaka ya kitaifa ya ulemavu, *usanifishaji kwa wote ni nini?*

[25] Shirika la afya la duniani, *mwongozo wa marekebisho stahiki wa masuala ya afya*, uk. 35.

[26] Shirika la afya duniani na Benki ya Dunia, *Ripoti ya dunia kuhusu ulemavu* (2011), uk. 4 na 263.





kuzuia fursa za ushiriki.[27] Kukosekana kwa huduma au vikwazo katika utoaji wa huduma pia ni vikwazo vya kimazingira.[28, 29]

**Vikwazo vya kitaasisi** ni pamoja na sheria, sera, mikakati pamoja na utendaji kazi wa kitaasisi ambao unawabagua watu wenye ulemavu au kuzuia ushiriki wao kwenye jamii.[30]

Vikwazo vinaweza kuainishwa kama tishio iwapo vitawekwa kwa makusudi. Vikwazo vinakuwa hatarishi iwapo hutokea kwa ghafla. Katika hali zote, vikwazo husababisha kutojumuishwa, kupelekea watu wenye ulemavu kukumbana na vitisho zaidi na kuwa katika hatari kuliko wengine walioathirika kwa majanga.

**Ujumuishi wa watu wenye ulemavu** unafanikiwa iwapo watu wenye ulemavu watashiriki kikamilifu kwa kuzingatia ulemavu mbalimbali walionao, haki zao zinapokuzwa, na masuala yote yanayohusu ulemavu yanasikilizwa kwa kuzingatia mkataba wa kimataifa kuhusu ulemavu.[31] Hii inahusiana na dhana ya "Jamii jumuishi" ambayo imefafanuliwa kama "Mchakato unaohitaji juhudi kufanywa kuhakikisha fursa sawa kwa watu wote bila kujali historia zao kuweza kufikia ndoto zao katika maisha. Juhudi hizi ni pamoja na sera na hatua za kukuza ufikivu sawa wa huduma za umma pamoja na kuwezesha raia kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi juu ya masuala yanayoathiri maisha yao."[32]

**Unyanyapaa katika misingi ya ulemavu** inahusu aina zozote za kukumbatia utofauti, kutenga au kuzuia kwa kigezo cha ulemavu na kwa malengo ya kutotambua ulemavu au kutoruhusu ushiriki kwa namna sawa na wengine katika kufurahia haki za binadamu na misingi ya uhuru wa kisiasa, kiuchumi, kijamii, kitamaduni, kiraia au eneo jingine lolote. Hii ni pamoja na aina zote za unyanyapaa, ikiwemo kushindwa kutoa mahitaji stahiki (kwa mfano kukataa kufanya marekebisho stahiki).[33]

*Marekebisho stahiki* yanahitaji watu pamoja na taasisi kurekebisha kanuni au huduma pale panapokuwa na ulazima ili kuondoa mzigo kwa watu wenye ulemavu au kuwawezesha kupata haki na uhuru wao katika hali ya usawa na wengine.[34]

*Aina mbalimbali za unyanyapaaji unaoingiliana hutokea* pale ambapo watu hukumbwa na kunyanyapaliwa katika maeneo mawili au zaidi. Katika hali hii athari za unyanyapaaji huongezeka maradufu. Mfano, mwanamke mwenye ulemavu anaweza kunyanyapaliwa kwa sababu ya jinsi yake na pia kwa kuwa ni mtu mwenye ulemavu. Unyanyapaaji mjumuiko hutokea pale ambapo aina mbalimbali za unyanyapaa hukutana na kumuweka mtu katika hali ya kuathirika na kubaguliwa zaidi.

Unyanyapaaji kwa misingi ya ulemavu unaweza kuwalenga watu ambao kwa sasa wana aina fulani ya ulemavu, wale ambao wamekuwa na ulemavu wakati uliopita, wale ambao wanaweza kupata ulemavu katika siku za mbeleni, wale waliodhaniwa kuwa na ulemavu na wale wanaohusiana na watu wenye ulemavu. Aina hii ya mwisho inaitwa unyanyapaaji kutokana na mahusiano au kuwa na ukaribu na watu wenye ulemavu.

**Viwezeshi** ni hatua za kuondoa vikwazo, au kupunguza athari na kuboresha uthabiti au ulinzi kwa watu wenye ulemavu.

[27] Wapling & Downie,*Mwongozo wa wafadhili kuhusu ujumuishi* (2012 PPUA Penca (Kituo cha ufikivu wa uchaguzi kwa wakazi wenye ulemavu), chaguzi fikivu kwa watu wenye ulemavu katika nchi tano za kusini mashariki mwa Asia. USAID & AGENDA (2013), uk. 5, 11; Shirika la afya duniani na Benki ya Dunia, *Ripoti ya dunia kuhusu ulemavu* (2011), uk. 4.

[28] Shirika la afya duniani na Benki ya Dunia, *Ripoti ya dunia kuhusu ulemavu* (2011), uk. 262.

[29] GSDRC, *Vizuizi vya Ujumuishi kwa watu wenye ulemavu*.

[30] Wapling & Downie, *mwongozo wa wafadhili kuhusu ujumuishi* (2012), uk. 21; DFID: *Ulemavu, Umaskini na Maendeleo* (2000), uk. 8; Shirika la afya duniani na Benki ya Dunia, *Ripoti ya dunia kuhusu ulemavu* (2011), uk. 6, 262; *Bruijn et al.* (2012), *Nihesabu, jumuisha watu wenye ulemavu katika miradi ya kimaendeleo* (2012), uk. 23

[31] *Tovuti ya mkakati wa Umoja wa Mataifa ya Ujumuishi kwa watu wenye ulemavu* na UNDIS, *kiambatisho namba I, dhana muhimu na ufafanuzi*

[32] Idara ya uchumi na masuala ya kijamii ya Umoja wa Mataifa, *ujumuishi wa jamii*.

[33] Angalia *Ibara namba 4 ya mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu*.

[34] Angalia *Ibara namba 2 ya mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu*.

**Bajeti jumuishi** hutokea pale ambapo shirika au taasisi, katika wakati za kutengeneza mipango yao, hutenga pesa kwa ajili ya kuondoa vikwazo na kukuza ushiriki wa watu wenye ulemavu na kupanga shughuli ambazo zinawalenga watu wenye ulemavu. Bajeti jumuishi inapaswa kuweka gharama za kuboresha ufikivu wa maeneo, kufanya marekebisho stahiki na kuweka bidhaa maalum zisizo za chakula, vifaa saidizi, vifaa jongezi na mawasiliano fikivu.[35]

**Ridhaa huru** hutokea pale ambapo mtu huridhia kufanya jambo au kuruhusu jambo (kwa mfano, afua za kitabibu, kuhamishwa, kutoa taarifa binafsi, kuhamisha taarifa, n.k) kwa namna ambayo anafahamu hatari, faida, njia mbadala na madhara ya kukataa. Watu wenye ulemavu hasa wale wenye ulemavu wa afya akili mara nyingi hukosa haki ya kutoa ridhaa huru. Jambo hili hukiuka haki zao chini ya mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu.[36]

Watoto wanayo haki ya kuulizwa na kutoa ridhaa kulingana na kiwango ambacho uwezo wao unawaruhusu.

**Muingiliano wa unyanyapaa** yaani "*Intersectionality*" ni dhana ya uchambuzi inayoonesha namna aina mbalimbali za ukandamizaji (kama vile ubaguzi wa rangi, jinsia, n.k) zinavyoingiliana, ili kutambulisha kundi maalum la kijamii. Dhana ya muingiliano wa unyanyapaa inatukumbusha kuwa madhara na ukiukwaji unaohusiana na ulemavu, rangi, kabila, jinsi na aina nyingine hauwezi kueleweka vya kutosha kwa kuyafanyia kazi kama masuala tofauti.

Ili kuona kwa usahihi namna zinavyoweza kuathiri ufikivu wa rasilimali na kusababisha hatari kwa watu wenye ulemavu, ni muhimu kuangalia namna ulemavu, umri, jinsia na sababu nyingine zinavyohusiana na kutathmini athari zote kwa pamoja.[37]

**Ukondoishaji** ni mchakato wa kuhusisha mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu katika kanuni za ulinzi, kukuza usalama na kuthamini utu wa watu wenye ulemavu na kuhakikisha wanapata huduma katika huduma za usaidizi wa huduma za kibinadamu na kwamba wanashiriki kikamilifu katika afua za kibinadamu. Dhana ya ujumuishi haiangalii nini kimefanyika isipokuwa inaangalia ni namna gani kimefanyika. Ulemavu unatakiwa kujumuishwa katika nyanja na hatua zote za programu za huduma za kibinadamu.

**Mashirika ya watu wenye ulemavu** yanapaswa kujikita katika kutekeleza mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu na wanapaswa kuheshimu kanuni na haki ambazo zimewekwa katika Mkataba. Mashirika hayo yanapaswa kuongozwa na kusimamiwa na watu wenye ulemavu. Idadi kubwa ya wajumbe au wanachama inapaswa kuwa ni watu wenye ulemavu.[38]

**Watu wenye ulemavu** inajumuisha watu wenye ulemavu wa viungo, ulemavu wa muda-mrefu wa akili,[39] ambao ukikutana na vikwazo mbalimbali huzuia ushiriki wao katika jamii kwa namna iliyo sawa watu wengine".[40]

**Ustahimilivu** unaelezea uwezo wa mfumo, mtu, jumuiya au jamii kupinga, kukabili, kubeba au kubadilika na kurejea kutoka katika athari za hatari kwa muda muafaka na kwa ufanisi. Ikiwemo kuzuia na kurejesha miundombinu na utendaji kazi kupitia mfumo wa usimamizi na udhibiti hatari.

[35] Ili kufikia mahitaji ya kimazingira ya ufikivu ya watu wenye ulemavu (kwa mfano, wakati wa kujenga majengo au miundombinu ya maji na usafi wa mazingira) inakadiriwa kwamba kati ya asilimia 0.5 na asilimia 1 inapaswa kuongezwa katika bajeti. Katika kutoa vifaa maalum visivyo vya bidhaa za chakula na vifaa vya ujongevu kwa watu wenye ulemavu, inashauriwa makadirio yawe kati ya asilimia 3 hadi 4 na mpaka asilimia 7 inapaswa kuongezwa. Angalia Help-Age, CBM, Handicap International, *viwango vya ujumuishi wa huduma za kibinadamu kwa watu wazima na watu wenye ulemavu*, na Light for the World, *kitabu cha rasilimali kuhusu ujumuishi kwa watu wenye ulemavu*, 2017), uk. 36.

[36] Kamati ya haki za watu wenye ulemavu, mapendekezo ya jumla na. 1 (2014) katika ibara namba 12: Utambuzi sawa mbele ya sheria *CRPD/C/GC/1*, 19 Mei 2014. Angalia pia kamati ya haki za watu wenye ulemavu, mapendekezo ya jumla namba 6 (2018) kuhusu usawa na kutokubaguliwa, *CRPD/C/GC/6*, 26 Aprili 2018, aya ya 66. Sera ya IASC kuhusu ulinzi katika masuala ya kibinadamu inasema kwamba taarifa na takwimu zinapaswa kutotolewa pasipokuwa na hiari na ridhaa huru. Angalia sehemu ya ufafanuzi.

[37] Angalia bunge la Ulaya, Kurugenzi ya sera za ndani, *unyanyasaji unaosababishwa na muingiliano wa jinsia na ulemavu* (2013). Angalia pia kamati ya haki za watu wenye ulemavu, mapendekezo ya jumla namba 6 kuhusu usawa na kutokubaguliwa, CRPD/C/GC/6, 26 Aprili 2018, aya ya 19.

[38] Kamati ya haki za watu wenye ulemavu, *mwongozo wa ushiriki wa mashirika ya watu wenye ulemavu (DPO) na asasi za kiraia katika kazi ya kamati. Kiambatisho namba 2 cha CRPD/C/11/2*, aya ya 3 angalia pia kamati ya CRPD, mapendekezo ya jumla namba 7 (2018) kuhusu ushiriki wa watu wenye ulemavu ikiwemo watoto wenye ulemavu kupitia mashirika yanayo wawakilisha katika utekelezaji na ufuatiliaji wa mkataba, CRPD/C/GC/7, 9 Novemba 2018.

[39] Mkataba wa haki za watu wenye ulemavu unaohusu ulemavu wa akili. Kamati ya CRPD ulipendkekeza kutumia ulemavu wa afya.

[40] *Ibara namba 1 ya mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu*.





## Uchambuzi wa hatari na vikwazo vya ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika huduma za kibinadamu


### Kupunguza hatari, kuboresha ustahimilivu na kuongeza ulinzi

Watu wenye ulemavu wanakabiliana na vikwazo ambavyo vinaongeza hatari katika muktadha wa huduma za kibinadamu. "Vikwazo vinaweza kuainishwa kama vitisho kama vitawekwa kwa makusudi na wadau au kama athari zinatokea kwa ghafla. Katika hali zote vikwazo hivi hupelekea kutengwa, ambapo inaongeza uwezekano wa watu wenye ulemavu kukabiliana na vitisho na kuathirika kwa kiwango kikubwa kuliko watu wengine katika maeneo yaliyoathiriwa na majanga."[41] Kwa kutumia viwezeshi (kama vile huduma za msaada katika makambi, kuwezesha ufikivu katika vituo vya kusambaza chakula, au kutumia vifaa saidizi) watu wenye ulemavu wanaweza kuboresha ustahimilivu wao. Kupunguza hatari na kuongeza ustahimilivu hukuza ulinzi.

### Nini tunapaswa kujua ili kushughulikia vikwazo

Eneo hili linaelezea vikwazo vya ujumla ambavyo watu wenye ulemavu wanakabiliana navyo nyakati za majanga ya kibinadamu. Sura ya 11 mpaka ya 18 zinabainisha vikwazo mahsusi. Ili kutambua hatua muhimu, kupanga na kutekeleza programu fikivu na jumuishi za huduma za kibinadamu, ni muhimu kutambua ulemavu, ufikivu na dhana ya vikwazo.

**Mchoro namba 3 |** Vikwazo na viwesheshi vya ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika masuala ya huduma za kibinadamu




[41] *Ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika operesheni za masuala ya kibinadamu yanayofadhiliwa na chi za Ulaya*.

Watu wenye ulemavu mara kwa mara wanakumbana na vikwazo vya kimtazamo, kimazingira na kitaasisi katika maisha yao ya kila siku. Majanga ya kibinadamu huzidisha na kutengeneza vikwazo vipya. Hupunguza ufikivu katika kupata usaidizi na ulinzi na kuzuia ushiriki katika masuala ya huduma za kibindamu. Pia, ni muhimu kutambua kuwa watu wenye ulemavu zaidi ya aina moja wanaweza kupitia vikwazo tofauti kutokana na sababu nyingi ikiwemo jinsi, umri, tamaduni na hadhi ya kiuchumi na kijamii. Aina hizi za muingiliano wa unyanyapaa wa ulemavu na aina mbalimbali ni ngumu na zinahitaji tathmini tofauti tofauti.

## Jukumu la familia na mitandao ya kijamii

Familia na mitandao ya kijamii inaweza kufanya kazi kama viwezeshi katika kuondoa au kupunguza vikwazo ambavyo vinazuia ushiriki wa watu wenye ulemavu. Familia zinazotoa ushirikiano kwa kiasi kikubwa zinasaidia kupunguza gharama za kukuza ujumuishi hasa kwa watu wenye ulemavu ambao wametengwa au kubaguliwa. Hata hivyo familia zinaweza kuwa ni kikwazo katika uwezeshaji wa watu wenye ulemavu. Wadau wa huduma za kibinadamu wanapaswa kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanawekwa mbele katika utoaji wa afua stahiki.

Katika safu ya upande wa kushoto ya jedwali kuna orodha ya vikwazo vinavyotokea katika muktadha wa huduma za kibinadamu. Safu ya upande wa kulia wa jedwali inaelezea huduma jumuishi zinazozingatia masuala ya ulemavu. Orodha hii haijakamilika; taarifa zaidi kuhusu vikwazo zinapatikana katika sura ya 11 mpaka ya 18.

A. **Vikwazo vya kimtazamo katika muktadha wa huduma za kibinadamu.** Dhana na mitazamo potofu katika jamii na ubaguzi dhidi ya watu wenye ulemavu zinaweza kusababisha makisio yasiyo sahihi.

| Mifano ya vikwazo na dhana potofu | Mifano ya viwezeshi na nadharia zake |
|---|---|
| Watu wote wenye ulemavu walifariki kwa sababu hawakuweza kukimbia. | Ingawa baadhi ya watu wenye ulemavu walifariki, wengi waliweza kusalimika. Watu wenye ulemavu ni wachache kati ya wanaosalimika. |
| Watu wenye ulemavu ni wahanga na wanapaswa kusaidiwa kikamilifu. | Watu wenye ulemavu wanahitaji msaada kama makundi mengine yaliyoathirika katika jamii, pia wanao uwezo, rasilimali na sauti na wengi wanaweza kuchangia katika huduma za kibinadamu. |
| Watu wenye ulemavu wana matatizo ya kiafya na wanahitaji uangalizi wa kitabibu. | Watu wenye ulemavu wana mahitaji sawa na watu wengine na baadhi yao wana mahitaji maalum na hutakiwa kupata uangalizi wa kitabibu. Hata hivyo, sio watu wote wenye ulemavu wanahitaji uangalizi wa kitabibu. |
| Watu wenye ulemavu wana matatizo ya kiafya na wanahitaji uangalizi wa kitabibu. | Wadau wa huduma za kibinadamu wanaweza kutoa vifaa saidizi kwa kupitia njia mbalimbali. Wanapaswa kutambua aina zipi za vifaa ambazo watu wenye ulemavu wanazihitaji katika kuongeza uwezo wa kufanya kazi katika muktadha husika na katika kuongeza uwezo na ustahimilivu. |





| Mifano ya vikwazo na dhana potofu | Mifano ya viwezeshi na nadharia zake |
|---|---|
| Watu wenye ulemavu hawana uwezo wa kufanya maamuzi, wengine wanapaswa kufanyiwa maamuzi kwa niaba yao ili kulinda maslahi yao. | Watu wenye ulemavu wanayo haki ya kufanya maamuzi katika masuala yanayowaathiri na wengi wanaweza kufanya hivyo. Wachache wakiwemo wale wenye matatizo ya afya ya akili wanahitaji msaada wa kueleweshwa na kufanya maamuzi. |
| Watu wenye ulemavu hawawezi kufanya kazi hivyo mashirika ya huduma za kibinadamu yasiwaajiri. | Watu wenye ulemavu wana uwezo wa kufanya kazi na kutoa mchango wenye faida kazini. Ni muhimu kujadiliana nao moja kwa moja ili kujua ujuzi walionao na maeneo ambayo wanapenda kufanya kazi. |
| Watu wenye ulemavu husababisha watu wanaowazunguka kutokuwa na raha. | Jambo hili linawezekana pale tu ambapo kuna kiwango kikubwa cha ubaguzi na kutoelewana. Ni muhimu kuandaa shughuli za kukuza uelewa juu ya ulemavu na kutoa changamoto ya mabadiliko ya imani potofu. |
| Kutoa mahitaji stahiki kwa watu wenye ulemavu ni kazi ngumu na inagharimu, hili ni jukumu la mtu mwingine. | Kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu ni suala rahisi pale tu utakapotambua mahitaji yao na namna ya kuyafikisha. Uliza mahitaji yao, katika hali ya kawaida unaweza kupata njia rahisi na ya gharama nafuu katika kuwasaidia. Wadau wote wa masuala ya huduma za kibinadamu wanapaswa kuchukua jukumu la kuhakikisha kuwa programu zao ni fikivu na kuhakikisha kuwa wanafanya marekebisho stahiki pale inapowezekana. |

**Desturi na tamaduni za maeneo husika ndio chanzo kikubwa cha ubaguzi na unyanyapaa dhidi ya watu wenye ulemavu. Ainisha vikwazo vya kitamaduni na kidesturi, na andaa namna ya kuvishughulikia katika njia zinazokubalika katika tamaduni husika.**

B. **Vikwazo vya kimazingira katika muktadha wa huduma za kibinadamu.** Vikwazo vya kimazingira vinaweza kuwepo tayari. Wadau wa huduma za kibinadamu na jamii katika maeneo husika wanaweza kuongeza vikwazo vipya bila ya kukusudia.

| Mifano ya vikwazo | Mifano ya viwezeshi |
|---|---|
| Maeneo ya usajili na usambazaji yamewekwa mbali, eneo la mwinuko, katika maeneo korofi, usafiri sio fikivu. | Maeneo ya usajili na usambazaji yawekwe katika eneo ambalo linafikika na kila mtu. Kama hili haliwezekani, toa usafiri au fikisha huduma kwa wale ambao hawataweza kuzifikia wao wenyewe. |
| Vifurushi vya chakula ni vizito, kiasi cha kushindwa kubebwa na watu wenye ulemavu. | Chagua watu ambao watasaidia kubeba chakula kwa ajili ya watu wenye ulemavu. |
| Maliwato ni finyu kiasi cha kutoruhusu mtu anaetumia kitimwendo kuweza kuingia na kiti chake. | Tengeneza mwongozo wa kuhakikisha maliwato yanavyojengwa ni rafiki kwa watu wanotumia viti mwendo. |
| Mahema na nyumba za muda mfupi zina ngazi na huwa na mlango mwembamba wa kuingilia | Tengeneza mwongozo kuhakikisha mahema na nyumba za muda mfupi zinakuwa fikivu kwa watu wanaotumia viti mwendo. |

| Mifano ya vikwazo | Mifano ya viwezeshi |
|---|---|
| Maliwato ni finyu kiasi cha kutoruhusu mtu anaetumia kitimwendo kuweza kuingia na kiti chake. | Tengeneza mwongozo wa kuhakikisha maliwato yanavyojengwa ni rafiki kwa watu wanotumia viti mwendo. |
| Mahema na nyumba za muda mfupi zina ngazi na huwa na mlango mwembamba wa kuingilia | Tengeneza mwongozo kuhakikisha mahema na nyumba za muda mfupi zinakuwa fikivu kwa watu wanaotumia viti mwendo. |
| Maliwato ni finyu kiasi cha kutoruhusu mtu anaetumia kitimwendo kuweza kuingia na kiti chake. | Tengeneza mwongozo wa kuhakikisha maliwato yanavyojengwa ni rafiki kwa watu wanotumia viti mwendo. |
| Mahema na nyumba za muda mfupi zina ngazi na huwa na mlango mwembamba wa kuingilia | Tengeneza mwongozo kuhakikisha mahema na nyumba za muda mfupi zinakuwa fikivu kwa watu wanaotumia viti mwendo. |
| Maliwato ni finyu kiasi cha kutoruhusu mtu anaetumia kitimwendo kuweza kuingia na kiti chake. | Tengeneza mwongozo wa kuhakikisha maliwato yanavyojengwa ni rafiki kwa watu wanotumia viti mwendo. |

C. **Vikwazo na viwezeshi vya kitaasisi katika muktadha wa huduma za kibinadamu.** Katika nchi nyingi kuna sera chache au kutokuwepo kabisa kwa sera za kukuza au kuhakikisha ujumuishi wa watu wenye ulemavu.

| Mifano ya vikwazo | Mifano ya viwezeshi |
|---|---|
| Sera za kiserikari na miundo ya kisheria ambayo inahusiana na masuala ya huduma za kibinadamu pamoja na sera za mashirika ya kibinadamu hazikuzi au kuhakikisha ujumuishi wa watu wenye ulemavu. | Sera za serikali zinawezesha mitazamo jumuishi inayoendana na mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu. Pale inapowezekana taasisi za Umoja wa Mataifa, ofisi za Umoja wa Mataifa katika nchi husika pamoja na timu za masuala ya kibinadamu zizingatie *mkakati wa Umoja wa Mataifa wa ujumuishi*. |
| Programu za kazi na malipo pamoja na programu za ajira hazitilii maanani uwezo wa watu wenye ulemavu na hivyo kutowaajiri. | Programu za kazi na malipo pamoja na programu zingine za ajira zinapaswa kutilia maanani uwezo wa watu wenye ulemavu na huduma za usaidizi, Kuheshimu uhuru wao (na kutoa usaidizi binafsi na utafsiri). |

[42] Eneo au jengo linafikika iwapo mtu mwenye ulemavu anaweza kulifikia, kuingia, kuzunguka kutoka chumba kimoja au eneo moja au lingine, na kutumia huduma zinazotolewa.





| Mifano ya vikwazo | Mifano ya viwezeshi |
|---|---|
| Watoa huduma waliopata mafunzo na wenye sifa pamoja na wafanyakazi wenye weledi (kama vile waalimu na madaktari) hawapatikani. | Nyaraka za kutoa ajira zinapaswa kuzingatia ujumuishi na kuhimiza uzoefu katika masuala ya ulemavu. Programu zipange kutoa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya misingi ya ujumuishi na njia zinazoweza kukuza ujumuishaji. |
| Ujumuishi sio kinachohitajika kwa wafadhili. | OECD-DAC pamoja na wafadhili wengi wanaoongezeka wameingiza vigezo vya kuzingatia masuala ya ulemavu na wanataka kujikita zaidi katika watu wenye ulemavu.[43] Taasisi za Umoja wa Mataifa zina wajibu wa kuripoti juu ya ufanisi wao katika masuala ya ulemavu chini ya Mkakati wa Umoja wa Mataifa wa ujumuishi. |
| Nyaraka nyingi za kutoa ajira katika masuala ya huduma za kibinadamu zinatoa sharti la waombaji kuwa na afya njema na pia wanaweza kuwatenga watu wenye ulemavu kwa kigezo cha masuala ya ulemavu au masuala ya kiafya. | Sera za ajira zinapaswa kuzingatia viwango vya mkataba wa haki za watu wenye ulemavu, na kutathmini waombaji kwa kigezo cha uwezo wao wa kufanya kazi katika majukumu yaliyoainishwa katika tangazo la ajira pamoja na usaidizi iwapo utahitajika.[44] |
| Sheria za kitaifa zinazuia watu wenye ulemavu kufungua akaunti katika taasisi za kifedha (hali hii inawaondolea uwezo wa kufikia usaidizi wa kifedha) kupata mikopo au kumiliki ardhi. | Kazi ya serikali ni kuendeleza sera jumuishi ambazo zinaendana na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu. Inawezesha taasisi za kifedha kuweka urahisi kwa watu wenye ulemavu kupata fedha taslimu kwa usalama na kisheria mpaka pale ambapo sheria mpya au mahakama zitaruhusu watu wenye ulemavu kuweza kufungua akaunti katika taasisi za kifedha. |
| Uwezo wa kisheria kwa watu wenye ulemavu ni mdogo au umezuiliwa, [45] hivyo kupelekea uwezo mdogo wa kufikia ulinzi wa kisheria pamoja na mamlaka ya kufanya maamuzi na kutoa ridhaa kwa hiari. | Serikali ziwezeshe sera jumuishi zinazoendana na mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu ili kuwasaidia watu wenye ulemavu na upatikanaji wa huduma za kuwasaidia watu wenye ulemavu kufanya maamuzi sahihi, kuwalinda na kuhakikisha hawafanyi maamuzi kutokana na shinikizo. Sera za mashirika ya kibinadamu zisiweke vikwazo kwa kigezo cha uwezo wa kisheria. |
| Mashirika ya kibinadamu hayana sera ambazo ni jumuishi na zinakosa mifumo ya uwajibikaji katika kupima ufanisi wao katika masuala ya ujumuishi wa watu wenye ulemavu. Jambo hili linazuia kuendelea kwa utamaduni wa shirika unaoweza kuwasaidia watu wenye ulemavu. | Sera zihakikishe ujumuishi wa watu wenye ulemavu, kuwepo kwa mifumo ya uwajibikaji katika kupima maboresho katika ufanisi. Mwongozo wa Ujumuishi wa Umoja wa Mataifa unapaswa kufuatwa na mashirika ya kibinadamu wakati wanatengeneza miundo ya ujumuishi.[46] |
| Mfumo wa masuala ya huduma za kibinadamu hauna maeneo ya majukumu kwa watu wenye ulemavu. | Ulemavu ni ajenda inayojitegema katika vikao vya kitaasisi na vikao vinavyohusu ulinzi. Mtu husika huteuliwa kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu. |
| Tathmini ya mahitaji haijanyambulishwa kwa kigezo cha ulemavu. Jambo hili linazuia kupata uelewa wa kiasi gani watu wenye ulemavu wanapitia aina fulani ya hatari. | Watu wenye ulemavu ndio walengwa katika tathmini ya mahitaji. Taarifa zimechambulishwa na hatari zote zimefanyiwa tathmini kwa kina. |

[43] Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo, *kitabu cha alama ya ujumuishi na uwezeshaji kwa watu wenye ulemavu* (2019).

[44] Shirika la Kazi Kimataifa, *kukuza anuwai na ujumuishi kupitia marekebisho eneo la kazi: muongozo wa vitendo*.

[45] "Uwezo wa kisheria" unahusu haki ya mtu kufanya vitendo vinavyokubalika kisheria, kuoa, kuingia katika mkataba wa kazi, kutumia pesa zake, kukubali au kukataa matibabu, n.k. Nchi nyingi zinakataa haki za watu wenye ulemavu wa akili na wa kisaikilojia, ingawa inavunya mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu (CRPD).

[46] *Shirika la Umoja wa Mataifa, mkakati wa ujumuishi wa watu wenye ulemavu*. Angalia pia *moduli ya Shirika la Kazi Duniani ya zana* za tathmini binafsi zilizotengenezwa kwa ajili ya kazi kama mfano.

Mpango jumuishi unahitaji hatua kadhaa za afua stahiki, kwa kuwa watu wenye ulemavu wana mahitaji maalum, mkataba wa kimataifa juu ya haki za watu wenye ulemavu unataka mipango iwe katika nyanja mbili (i) kuendeleza mazingira fikivu na jumuishi pamoja na afua stahiki, na (ii) kuweka mipango na suluhu zitakazowezesha mtu mwenye ulemavu kushiriki mara moja.

Pale ambapo hakuna suluhu kuhusu ujumuishwaji, wadau wanapaswa kutoa marekebisho stahiki ili kufikia malengo ya watu wenye ulemavu.

**Chukua hatua kuhakikisha kuwa marekebisho stahiki yanapatikana**

Marekebisho stahiki maana yake ni marekebisho muhimu yanayostahili katika kuondoa unyanyapaa na mzigo usiofaa, ili kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanashiriki katika misingi yenye usawa pamoja na wengine, katika kufurahia haki za binadamu pamoja na misingi ya uhuru (Kifungu namba 2 cha mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu).

Kuelezea namna wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu wanavyoweza kuleta suluhu za ujumuishi na kutoa masuluhisho ya kimuundo pamoja na marekebisho kwa mtu binafsi, zingatia masuala ya ufikivu. Wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu ambao wanataka kuboresha ufikivu mara zote hufuata hatua zifuatazo:- (i) kufanya tathmini; (ii) kutathmini hatua mbadala;
(iii) kuandaa mchakato wa manunuzi na nyaraka; (iv) kufanya manunuzi ya bidhaa, chakula, vifaa, teknolojia na ujuzi, n.k; na (v) kusambaza na kutoa bidhaa zilizochaguliwa pamoja na huduma kwa kulingana na ratiba iliyopangwa. Kutofanya marekebisho stahiki kuleta ubaguzi. Wadau wa masuala ya kibinadamu pia wanaweza kutoa majawabu sahihi pale inapohitajika.

**Kuziba mapengo kati ya ufikivu na marekebisho binafsi**

| Programu au huduma huwa fikivu iwapo... | Marekebisho stahiki yatafikiwa iwapo... |
|---|---|
| Yanaweza kutekelezwa kwa haraka. | Yanaweza kutolewa mara moja (kuepuka unyanyapaa na kutengwa). |
| Inatoa suluhisho la jumla. | Ni suluhisho mahsusi. |
| Inapatikana na ni fikivu bila kujali kama inahitajika. | Inatolewa kwa mtu wenye ulemavu iwapo anahitaji na pale ambapo hawezi kupata ufikivu. |
| Inaongozwa na kanuni za ujumla za usanifishaji kwa ajili ya watu wote. | Ni mahsusi kufikia mahitaji binafsi na imebuniwa kwa kushirikiana na mtu husika. |
| Inakidhi vigezo vya ufikivu. | Inakidhi kipimo cha uwiano. |





**Marekebisho stahiki** ni kipimo ambacho kinamnufaisha mtu binafsi lakini huleta manufaa makubwa. Kwa mfano njia ambayo imefanywa kuwa fikivu kwa mtu mmoja inaweza kutumiwa na watu wengine pia. Pia, huweza kutumika katika kubadili utaratibu wa kutoa na kupata fedha, kubadilisha mbinu za usambazaji chakula au kupangilia kazi ya kufikia mahitaji ya watu wenye ulemavu (angalia kiambatanisho namba 1: kinaonesha marekebisho stahiki).

Ufikivu unatoa mfano mmoja wa sababu za marekebisho stahiki. Michakato ya uwajibikaji inaweza kurekebishwa kwa baadhi ya watu ambao hawawezi kuzingatia kwa kipindi kirefu; programu za fedha taslimu zinaweza kuongeza wigo ili kutoa fursa kwa mahitaji ya mtu ambaye kusafiri ni kikwazo kikubwa.[47]

## Dhana zinazohusu masuala ya haki

Maneno yanayotumiwa kutambulisha watu wenye ulemavu yanaweza kuwadumaza au kuwapa uwezo. Yafuatayo ni baadhi ya maneno yanayotumiwa:

**Watu walio katika mazingira magumu**. Watu wenye ulemavu hawapo katika mazingira magumu kiasili. Isipokuwa mazingira magumu huwakumba ikiwemo vikwazo na kukosa msaada. Lugha sahihi iliyojikita katika haki hutumia neno kundi lenye urahisi wa kuathirika lakini kwa hadhari. Mfano wasichana wenye ulemavu wapo katika hatari ya kuathirika zaidi kutokana na ukatili wa kijinsia wanapokuwa wametengwa na familia zao au walezi wao. Au wavulana wenye ulemavu wapo katika hatari zaidi ya kuathiriwa wanapofanyiwa uonevu na wavulana wasio na ulemavu'.

**Mlezi/mtoa huduma.** Mlezi hutambuliwa kama mtu (mwanafamilia au mtu anaelipwa kusaidia) ambaye mara kwa mara anakuwa mwangalizi wa mtoto, mgonjwa, mzee au mtu mwenye ulemavu. Wadau wa haki wanapenda kutumia neno msaidizi kuliko neno mlezi, hususani ni pale tunapozungumzia watu wazima wenye ulemavu (kwa mfano msaidizi binafsi, msaidizi wa kundi rika na mtoa huduma).

**Mahitaji maalum.** Mahitaji ya binadamu (ya chakula, malazi, huduma za kiafya, n.k) huhitajika kwa watu wote. Watu wenye ulemavu wanashiriki katika mahitaji hayo kama binadamu wengine. Watu wenye ulemavu wanahitaji hatua ili kufikia mahitaji maalumu yanayowahusu (ufikivu, mawasiliano, usaidizi binafsi, n.k). Wadau wa masuala ya haki wanasisitiza kuwa katika kutambua haki za watu wenye ulemavu.

Dhana za ziada zinatakiwa kuzingatiwa:

- **Tanguliza** utu kabla ya hali (kwa mfano chagua kutumia 'Mtu mwenye ulemavu kuliko kutumia "Mlemavu" na msichana asiyeona au msichana mwenye ulemavu wa kuona kuliko kutumia msichana kipofu.
- Epuka kutumia maneno yatakayoleta maana hasi kama vile 'Wanateseka, wahanga au kilema. Tumia neno 'mtumiaji wa kitimwendo' kuliko kusema 'Mfungwa wa kitimwendo'.
- Tumia neno 'Watu wasio na ulemavu' kuliko kusema 'Mtu wa kawaida'.
- Usitumie vifupisho kutambulisha watoto au watu wenye ulemavu, mfano kifupisho WWU.[48]
- Tumia maneno sahihi kutambulisha aina za ulemavu ikiwemo ulemavu wa viungo, uoni, uziwi na ulemavu wa akili.

[47] \Analia Shirika la Kazi Duniani, *kukuza anuai na ujumuishi katika eneo la kazi, muongozo kwa vitenzo* (2016).

[48] Mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu unatumia neno 'Watoto wenye ulemavu' na 'Watu wenye ulemavu' kwa sababu watoto na watu wazima wenye ulemavu wanabaguliwa mara kwa mara na wanakumbana na unyanyapaa, wanapendelea kuitwa mtoto au mtu kuliko kuitwa kwa kifupisho.

# 3 Nini kifanyike: Mbinu muhimu katika kupanga programu

Watu wenye ulemavu wanatakiwa kupata usaidizi wa huduma za kibinadamu na afua stahiki kwa kuzingatia vigezo sawa na watu wengine wasio na ulemavu katika jamii. Hii inahitaji mfumo pacha ambao unahusisha ukondoishaji wa programu za pamoja, pamoja na kuwa na afua stahiki kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

Mosi, katika kukondoisha programu za kibinadamu na afua zilizokusudiwa kwa jamii nzima ili kujumuisha watu wenye ulemavu, mipango, muundo, utekelezaji na tathmini inapashwa kufikia malengo yafuatayo. Kwa mfano:

- Taarifa zinapashwa kusambazwa katika mfumo unaofikika (kwa sauti, kwa maandishi, kwa lugha ya alama, kwa lugha rahisi ya kusomeka, n.k).
- Maeneo ya usambazaji yanapaswa kuwekwa katika maeneo yanayofikika kirahisi kwa kila mmoja wakiwemo watu wenye ulemavu.
- Maliwato katika maeneo ya umma yanapaswa kuwa fikivu kwa watu wenye ulemavu. Ufukikwaji wa maeneo yalipo maliwato unatakiwa kuwa rahisi, na kuwepo na alama za kuelekeza yalipo.

Pili, programu za kibinadamu zinatakiwa kuangalia mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu kwa kutoa afua stahiki kwa walengwa wenye ulemavu, kwa mfano:

- Iwezeshe vifaa saidizi kupatikana.
- Inapaswa kutoa fedha ya usafiri kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kufikia huduma.
- Wanapaswa kutoa chakula na bidhaa zisizo za chakula kwa watu wenye ulemavu ambao hawana uwezo wa kufika katika maeneo ya usambazaji.

Njia hizi pacha ni muhimu kwa ajili ya kujumuisha watu wenye ulemavu katika masuala ya huduma za kibinadamu. Zinapaswa kuzingatiwa na wadau wote katika nyanja zote.

## Hatua za lazima

'Hatua za lazima' zinahitajika iwapo watu wenye ulemavu wanapaswa kujumuishwa kikamilifu katika kila awamu ya masuala ya kibinadamu, na zinahitaji kuchukuliwa na kila mdau katika kila sekta na muktadha wowote.

Hatua nne za lazima zimeelezwa hapo chini na zinapaswa kuzingatiwa wakati wa kusoma au kutekelezwa katika kila sekta, pamoja na vipengele vya wajibu na majukumu ya wadau.

### Kukuza ushiriki wenye tija

Mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu[49] unatilia mkazo haki ya kushiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi. Watu wenye ulemavu wanayo haki ya kushiriki katika kufanya maamuzi ambayo yanahusu masuala ya huduma za kibinadamu.

[49] *Mfumo wa kupunguza hatari ya majanga wa Sendai*, *makubaliano ya kidunia kwa wakimbizi*, *makubaliano ya kidunia kwa uhamiaji*, pamoja na zingine nyingi, pia inahitaji wadau wa masuala ya kibinadamu na wadau wengine kutafuta ushauri na kuwahusisha watu wenye ulemavu katika programu zao na maamuzi.

Katika msingi wa haki na kwa sababu wana maarifa na ujuzi wa kuchangia, watu wenye ulemavu wanaweza kuwa ni wadau muhimu na rasilimali watu katika jitihada za masuala ya huduma za kibinadamu.

### Hatua muhimu

- Wezesha watu wenye ulemavu kushiriki katika michakato yote ya kutathmini, kupanga, kubuni, kutekeleza, kufuatilia au kutahmini programu za huduma za kibinadamu katika awamu zote na katika ngazi zote.
- Ajiri watu wenye ulemavu kama wafanyakazi katika ngazi zote za mashirika ya kibinadamu, ikiwemo wafanyakazi wanaotakiwa kufanya kazi katika mstari wa mbele katika kutoa huduma, na wahamasishaji katika jamii.
- Tafuta ushauri ushauri na kushirikiana na mashirika ya watu wenye ulemavu wakati wa kuweka mikakati ya kuwahusisha watu wenye ulemavu katika maeneo yaliyoathiriwa.

## Ondoa vikwazo

Sio ujumuishi wala ushiriki unaoweza kufanikiwa wakati vikwazo havijaondolewa. Kuondoa vikwazo vya kitabia, kimazingira na kitaasisi ni muhimu katika kutatua hatari zinazoweza kuwakumba watu wenye ulemavu.[50]

### Hatua muhimu

- Ainisha vikwazo vyote vya kimtazamo, kimazingira na kitaasisi ambavyo vinawazuia watu wenye ulemavu kuzifikia huduma na programu za huduma za kibinadamu. Ainisha viwezeshi ambavyo vinawezesha ushiriki wa watu wenye ulemavu.
- Chukua hatua stahiki kuondoa vikwazo na kukuza viwezeshi na kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wana ufikivu na usaidizi na kushiriki kikamilifu.

## Wezesha watu wenye ulemavu; wasaidie katika kukuza uwezo wao

Wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu, yakiwemo mashirika ya watu wenye ulemavu, wanahitaji kukuza ufahamu wao binafsi juu ya haki na uwezo wa watu wenye ulemavu. Pia, watahitajika kufanya kazi na watu wenye ulemavu katika kukuza na kuendeleza uwezo wao. Hatua hizi kwa pamoja zinawezesha makundi ya wadau katika kushiriki kuhakikisha kuwa, watu wenye ulemavu wamejumuishwa kikamilifu katika nyanja zote za masuala ya usaidizi wa kibinadamu pamoja na ulinzi.

Kukuza uwezo kunaweza kuwa kwa namna mbalimbali. Zingatia, mfano kutoa mafunzo ya uhamasishaji na vipindi vya kujifunza na ushauri kwa wafanyakazi. Kupitia nyenzo za mafunzo ikiwemo masomo ya utangulizi katika mafunzo; kuanzisha wanajamii wa kuwafanyia majaribio; kukusanya uzoefu na kutambua utendaji bora; kutoa msaada wa kitaalamu ikiwemo wataalamu wa masuala ya ujumuishi; stadi za mawasiliano kupitia ushauri na madawati ya msaada, n.k.

### Hatua muhimu

- Ikiwa kama ni kipaumbele, kuza uwezo wa watu wenye ulemavu na mashirika yao katika nyanja za masuala ya huduma za kibinadamu. Wapatie maarifa, stadi na mbinu za uongozi wanazohitaji katika kushiriki na kunufaika kutokana na afua na usaidizi wa huduma za kibinadamu na ulinzi.[51]
- Jenga uwezo wa wafanyakazi katika masuala ya huduma za kibinadamu. Wasaidie kubuni na kutekeleza programu jumuishi za masuala ya kibinadamu ambazo ni fikivu kwa watu wenye ulemavu kwa kuimarisha uelewa wao juu ya haki za watu wenye ulemavu pamoja na misingi ya mitazamo ya utendaji ambao unakuza ujumuishi na kupunguza vikwazo vya ujumuishi.

[50] Angalia kipengele cha vizuizi.

[51] Husisha nadharia muhimu za kibinadamu na nyenzo katika kutoa mafunzo.





## Changanua takwimu kwa ajili ya kufuatilia ujumuishi

Ili kufuatilia ujumuishwaji, taarifa kuhusu vikwazo na mahitaji ya watu wenye ulemavu ni muhimu. Taarifa za kibinadamu zinapaswa kuchanganuliwa kwa kigezo cha ulemavu ili kuhakikisha kuwa hatua za kibinadamu katika kupanga, kutekeleza na kufuatilia ni fikivu na zinawahusisha watu wenye ulemavu. Taarifa kuhusu hatari na vikwazo wanavyo kutana navyo watu wenye ulemavu zinapaswa kukusanywa na kuchanganuliwa. Suala hili litaimarisha wadau wa masuala ya kibinadamu kuelewa vikwazo vya ujumuishi ambapo itawawezesha kuviondoa na kufuata hatua za kukuza ujumuishi.

### Hatua muhimu

- Paleambapo takwimu hazipo, wadau wa masuala ya kibinadamu kwa kushirikiana na mashirika ya watu wenye ulemavu wanapaswa kukusanya takwimu kwa kuzingatia jinsi, umri na ulemavu kwa kutumia zana mbalimbali ambazo zinazingatia muktadha wa masuala ya huduma kibinadamu. Hii ni pamoja na maswali yaliyoandaliwa na kikundi cha Washington pamoja na Moduli ya Kundi la Washington kuhusu mwenendo wa mtoto wa UNICEF, pamoja na taarifa zinazohusu hatari na vikwazo.
- Tumia takwimu kuhusu ulemavu katika kufuatilia ufikivu sawa, kubuni programu jumuishi na kupanga juu ya utekelezaji wake. Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanaweza kushiriki katika kila hatua.
- Changanua takwimu kwa kuzingatia jinsia, umri na ulemavu ili kuwezesha katika kutengeneza viashiria sahihi na kuvitumia katika kufuatilia ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika kila awamu ya masuala ya kibinadamu.

Angalia pia kipengele cha takwimu na namna ya utunzaji wa taarifa.

# 4 Usimamizi wa taarifa na takwimu

## Utangulizi: Kwanini tunakusanya takwimu za watu wenye ulemavu?

Programu za masuala ya kibinadamu zenye ubora, zinajengwa katika kutambua mahitaji na vipaumbele vya watu wenye ulemavu nyakati za majanga. Uelewa huu unatokana na yafuatayo: (1) Kutambua idadi ya watu wenye ulemavu; (2) Kuainisha hatari ambazo watu weye ulemavu wanaweza kuzipata na mambo yanayochangia kuwepo kwa hatari hizo; (3) Kutambua vikwazo ambavyo vinazuia watu wenye ulemavu kupata usaidizi wa huduma za kibinadamu na (4) Kutambua majukumu na uwezo wa watu wenye ulemavu katika jitihada wa masuala ya kibinadamu.

Ili kujenga msingi wa uelewa, inapaswa kupata takwimu za watu wenye ulemavu. Taarifa hizi zinahitajika kwa malengo yafuatayo:

1. Kutambua watu wenye ulemavu, mmoja mmoja na makazi ambayo yatawahusisha, ili kuweza kufuatilia hali zao, kupata usaidizi na kuweka vipaumbele katika jitihada za huduma za kibinadamu.

2. Kutambua idadi kamili ya watu wenye ulemavu katika maeneo ambayo yaliathiriwa. Hii inasaidia katika kuhesabu kwa usahihi mahitaji ya jumla na yale ambayo ni maalumu kwa watu wenye ulemavu katika maeneo yaliyoathiriwa pamoja na kukusanya rasilimali ili kufikia mahitaji hayo.

3. Kuelewa jinsi majanga yanavyowaathiri watu wenye ulemavu, ikiwemo athari za vifo, lishe na usalama wa chakula, riziki, afya, ulinzi na mahitaji mengine muhimu.

   Taarifa hizi zinawezesha kutambua namna ya kupunguza hatari ambazo watu wenye ulemavu wanakabiliana nazo katika kustahimili.

4. Kuelewa maoni na vipaumbele vya watu wenye ulemavu. Bila ya taarifa hizi mashirika ya kibinadamu hayataweza kuwajibika katika jamii zilizoathiriwa.

5. Kuainisha uwezo na rasilimali za mashirika yanayochangia katika kukabili hatari, ikiwemo mashirika ya watu wenye ulemavu. Taarifa hizi zinawezesha kukuza ushirikiano na juhudi za kutambua mapungufu ya kiuwezo kwa jitihada zinazochukuliwa.

6. Kufuatilia kiwango cha watu wenye ulemavu kupata usaidizi, huduma na vifaa, na kutambua vikwazo vya kitabia, kimazingira, kitaasisi na kimawasiliano vinavyozuia ufikikaji wa huduma. Bila ya taarifa mashirika ya kibinadamu hayawezi kuboresha programu na taratibu, kuondoa vikwazo, au kuongeza ushiriki wa watu wenye ulemavu. Taarifa na takwimu hizi zinasaidia katika kufanya maamuzi juu ya mafunzo, kukuza uelewa na kuziba mianya katika kujenga uwezo.

7. Kuimarisha uthibitisho ambao utakuwa kama ushahidi katika shughuli za uchechemuzi na kugema rasilimali.

Ukusanyaji wa takwimu za watu wenye ulemavu, pia ni jukumu la nchi wanachama ambao wameridhia Mkataba wa Kimataifa wa Watu wenye Ulemavu. Kifungu namba 31 cha mkataba, kinachozungumzia takwimu na

ukusanyaji wa taarifa sadifu, kinazitaka nchi wanachama kukusanya taarifa sahihi, ikiwemo takwimu na taarifa zitokanazo na utafiti, na pia inataka takwimu ziwe zimenyambulishwa kwa usahihi, na kutumiwa katika kutathmini jinsi nchi wanachama zinavyotekeleza wajibu wake kwa kuzingatia mkataba huo, kutambua na kuchughulikia vikwazo wanavyovipata watu wenye ulemavu katika kupata haki zao.

## Ni aina gani ya takwimu zinazohitajika?

Maamuzi au jitihada zilizoamuliwa kutumika katika masuala ya huduma za kibinadamu, ndizo zitakazoamua aina ya takwimu zinazotakiwa kukusanywa.

| | |
|---|---|
| **Takwimu kuhusu kiasi (Takwimu ambazo zinaweza kupimwa na kuhesabiwa) zinaweza kutumika.** | • Kuwatambua watu wenye ulemavu na kukokotoa idadi yao kwa kuwahesabu watu wenye ulemavu katika maeneo yaliyoathirika, (kwa kutumia taarifa za uandikishaji, utafiti, makadirio ya kaya, n.k).<br>• Kutambua maeneo ambayo yanafikika na yasiyofikika.<br>• Kunyambulisha taarifa za mahitaji na hatari, (Mfano idadi au uwiano wa kaya zenye uhaba wa chakula ambazo zinasimamiwa na watu wenye ulemavu).<br>• Kufuatilia ufikivu wa usaidizi (mfano kokotoa idadi au uwiano wa washiriki katika programu za kupata riziki ambao ni watu wenye ulemavu).<br>• Kufuatilia masuala ya ulinzi (mfano kutambua idadi ya visa vya ukiukwaji wa haki za binadamu, aina ya ukiukwaji wa haki za binadamu, uzoefu wa yaliowakumba watu wenye ulemavu). |
| **Taarifa za maelezo zinaweza kutumika.** | • Kuunganisha maoni na vipaumbele vya watu wenye ulemavu, mfano kupitia mrejesho na mchakato wa kukusanya malalamiko.<br>• Kutambua hatari na vikwazo ambavyo watu wenye uleamavu wanakabiliana navyo pamoja na viwezeshi mfano kupitia vikundi vya majadiliano na wasahiliwa mahsusi.<br>• Kuainisha aina ya hatari, vikwazo na viwezeshi katika kufikia usaidizi ambavyo watu wenye ulemavu wanakabiliana navyo, mfano kuchambua sera na nyaraka mbalimbali.<br>• Kufuatilia masuala yatokanayo na ulinzi mfano kudadisi, watu wenye ulemavu kuhusu ukiukwaji wa haki za watu wenye ulemavu.<br>• Kupata taarifa za kina kuhusiana na uelewa, tabia na mtazamo wa wadau wa masuala ya kibinadamupamoja na jamii kuhusiana nawatu wenye ulemavu mfano kupitia tafiti na mahojiano.<br>• Kuainisha mashirika ya watu wenye ulemavu na huduma zipatikanazo mfano kusanya taarifa kuhusu nani anafanya nini, lini, wapi na kwa ajili ya nani?). |





## Zana za kuchanganua takwimu kwa kigezo cha ulemavu

Ni muhimu kuchanganua taarifa zinazohusiana na ulemavu ili kufahamu njia mbalimbali ambazo watu wenye ulemavu wanayakabili majanga na kufuatilia usaidizi wanaoweza kupata. Kimsingi taarifa zilizochanganuliwa kwa kigezo cha umri zinapaswa pia kunyambulishwa kwa kigezo cha ulemavu.

Kwa sehemu kubwa zana zilizojaribiwa katika kupata ulinganifu wa taarifa kuhusiana na watu wenye ulemavu ni "Maswali ya Kundi la Washington na Shirika la Umoja wa Mataifa kuhusu jedwali la tathmini ya ulemavu. Kumekuwa na ukuaji wa dhana[52] kuwa kwa kutumia zana hii kunasaidia kutengeneza ulinganifu wa takwimu ambazo zinakubalika kimataifa na ambazo zinaweza kunyambulishwa na kukusanywa bila ya ubaguzi na kuongezwa kiurahisi kwenye sensa na tafiti bila gharama. Zana hizi zimekuwa zikitumiwa katika muktadha wa masuala ya huduma za kibinadamu (angalia kiambatisho namba 2 kwa muhtasari wa zana hizi kwa ufupi pamoja na maelezo ya ziada kuhusu jinsi ya kutumiwa katika muktadha wa masuala ya kibinadamu).

Ni muhimu kutambua ya kuwa zana hizi zinaweza kutumika katika kuchanganua taarifa lakini haziwezi kusaidia katika kutambua hali fulani ya kiafya au uchunguzi wa makundi fulani.[53] Zana hizi zisitumike katika kufanya tathmini kwa mtu mmoja mmoja au katika hali ambayo hakuna taarifa za ziada kuhusu mahitaji au hali za hatari ikiwa ni pamoja na vikwazo.

## Hatua muhimu katika kukusanya na kutumia takwimu za watu wenye ulemavu

Taarifa za watu wenye ulemavu zinahitaji kukusanywa katika kila hatua ya mzunguko wa programu za huduma za kibinadamu. Zifuatazo ni hatua ambazo zinatakiwa kuchukuliwa katika kila awamu:

**1. Bainisha mahitaji ya takwimu**

Ni swali gani linalotakiwa kujibiwa au maamuzi gani yanayotakiwa kufanywa? Zingatia kwa nini takwimu za watu wenye ulemavu zinakusanywa. Dhumuni linakuwa kuelewa athari za majanga: kubainisha vikwazo vinavyozuia watu wenye ulemavu kupata usaidizi; kuainisha rasilimali na uwezo.

Dhumuni la kukusanya takwimu ni kutambua aina zipi za takwimu zinakusanywa.

**2. Kutambua vyanzo vya takwimu kuhusu watu wenye ulemavu**

Taarifa zipi zinahitajika kujibu maswali muhimu? Mara zote anza na zile taarifa zilizopo.

- Tumia vyanzo rasmi vya taarifa kama vile kanzidata za serikali, mifumo ya kimataifa ya ufuatiliaji (ikiwemo taarifa za taasisi za Umoja wa Mataifa za haki za binadamu kama vile tume ya haki za binadamu na Mapitio ya mara kwa mara ya Ulimwengu yaani "*Universal Periodic Reviews*", jukwaa la siasa katika maendeleo endelevu na taarifa za Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa), na taarifa ambazo zimeandaliwa na wadau wa masuala ya kibinadamu, miradi ya maendeleo na mashirika ya watu wenye ulemavu (Angali kiambatisho namba 3 kina maelezo zaidi juu ya vyanzo vya taarifa na matumizi yake).
- Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa takwimu hizi zinaweza kwa kiasi kikubwa kutoa makadirio madogo ya idadi ya watu wenye ulemavu na kuelezea mahitaji yao, maoni na vipaumbele vyao kwa usahihi mdogo. Kwa hiyo ni muhimu kutathmini ubora, utoshelevu na usahihi wa taarifa kuhusu watu wenye ulemavu (angalia kiambatishi namba 4 kwa ushauri wa namna ya kutathmini taarifa za watu wenye ulemavu).
- Kunaweza kutokea mabadiliko tokea taarifa zimekusanywa. Kimahususi, inaweza kuwa hali imebadilika kutokana na majanga ya kibinadamu hasa pale ambapo idadi kubwa ya watu wanapokuwa wamehamishwa au kukosa makazi. Idadi ya watu wenye ulemavu pamoja na uwiano wao katika jamii, mara kwa mara hubadilika kutokana na matokeo ya majanga, kwa kuwa huduma huathiriwa, vikwazo vipya huibuka na kusababisha maumivu ya kisaikolojia pamoja na msongo wa mawazo.

[52] Daniel Mont na Nora Groce, *Kuhesabu Ulemavu: Makubaliano yanayoibuka kuhusu kundi la maswali la Washington*, *The Lancet*, Julai 2017.

[53] Daniel Mont, *Ni kwa namna gani WG-SS inatofautiana na vigezo vya kutambua ulemavu?* (2017), kundi la Washington kuhusu takwimu za ulemavu.

3. **Tafuta mapungufu kwenye takwimu muhimu**

- Jumuisha maswali sadifu kwa watu wenye ulemavu katika zana ya kutathmini mahitaji, na katika kufuatilia na kufanya mchakato wa tathmini.
- Andaa mkakati mahususi wa kukusanya taarifa zinazolenga watu wenye ulemavu pekee, pale inaposadifu na kuwezekana kufanya hivyo. Ukusanyaji wa taarifa mahususi unaweza kuwa na manufaa pale ambapo uchambuzi umethibitisha kuwa watu wenye ulemavu wanakabiliwa na hatari na mapungufu katika ufikiwaji.
- Taarifa za ziada zinasaidia katika kutambua matatizo kwa undani zaidi. Ni muhimu kushirikisha mashirika ya watu wenye ulemavu katika mchakato huu.
- Andaa mfumo mzuri wa ulinzi wakati wa kukusanya, kuchambua, kutunza, kutoa, kutumia, kuharibu na *kuweka kumbukumbu taarifa nyeti za mtu binafsi*.[54]

Rejea katika kipengele cha **Kusimamia taarifa** kwa kufuata viwango vya kitaalamu.

**Umuhimu wa kutoa idhini huru katika ukusanyaji na utumiaji wa taarifa**

Watu wote wana haki ya kufanya maamuzi kuhusu ukusanyaji na matumizi ya taarifa zao binafsi. Wale wanaokusanya taarifa binafsi wanahitaji kuwa na uwezo wa kuelezea ni kwa namna gani na kwa madhumuni gani taarifa zitatumika na kutoa hakikisho la kuzingatia usiri.

Ili kuwawezesha watu wenye ulemavu kutoa ridhaa, taarifa juu ya matumizi ya taarifa zao inahitaji kutolewa katika miundo tofauti, pia ni muhimu kutenga muda wa kutosha wa kutoa maelezo na kufikia maamuzi. Baadhi ya watu wenye ulemavu wanaweza kuhitaji kupata mtu watakayemuamini ili kuwasaidia katika kufikia maamuzi.
Taarifa na takwimu za watu wenye ulemavu zinatakiwa zilindwe. Kwa mfano, zuia kuwatambua watu ambao kwa namna moja au nyingine wanaweza wakazalilishwa, wana mashitaka ya kujibu au kuuliwa.

## Taarifa za watu wenye ulemavu katika nyanja zote za programu za masuala ya huduma za kibinadamu

### Maandalizi/Kuyaweka tayari

Ukusanyaji taarifa au takwimu sahihi kuhusu watu wenye ulemavu ni kipengele muhimu katika kufanya maandalizi kabla janga halijatokea. Angalia kiambatanishi namba tatu kinajadili vyanzo vya taarifa, ambavyo ni pamoja na:

- Kanzidata za serikali kama vile mfumo wa usimamizi wa takwimu za afya na elimu. Tahadhari inatakiwa kuchukuliwa wakati tunapotumia vyanzo hivi vya takwimu mara baada ya majanga kutokea kwa sababu hali itakuwa imebadilika na taarifa hizo zinaweza kuakisi idadi ya watu au mahitaji ya maeneo yaliyoathirika.
- Tafiti linganifu za kaya kama vile tafiti za viashiria kwa makundi na demografia na tafiti za kiafya.
- Afua mbalimbali katika ngazi za wilaya ambazo zinakusanya taarifa za watu wenye ulemavu pamoja na kaya zenye watu wenye ulemavu kama vile sensa za kitaifa au mifumo ya kitaifa ya hifadhi za jamii.
- Taarifa ambazo zinakusanywa na mashirika ya watu wenye ulemavu au mashirika yasiyo ya kiserikali, kama vile taarifa za miradi.

Hatua zingine za kukusanya taarifa wakati wa kujiandaa na majanga zinahusisha:

- Kuainisha taarifa kuhusu mashirika ya watu wenye ulemavu pamoja na huduma katika ngazi za chini mpaka kitaifa kwa ajili ya watu wenye ulemavu, kama vile wakalimani wa lugha ya alama, kampuni zinazotoa usafiri rafiki, na wanaotoa vifaa saidizi.
- Kuainisha majengo ya umma pamoja na miundombinu mingine inayoweza kutumika kama vituo vya kutolea huduma. Kuunganisha taarifa katika seti za taarifa za pamoja ambazo zinaweza kuendelezwa na ofisi ya kuratibu masuala ya huduma za kibinadamu katika ngazi ya nchi.
- Toa mafunzo kwa wafanyakazi au washirika katika matumizi ya zana za kukusanya taarifa za watu wenye ulemavu. Ainisha na toa mafunzo kwa wadau wakiwemo mashirika ya watu wenye ulemavu na wanaokusanya takwimu[55].
- Tafsiri katika lugha mbalimbali zana za kukusanyia taarifa za watu wenye ulemavu[56].

### Tathimini na uchambuzi wa mahitaji

Ingawa taarifa za kupima kiasi hupatikana zaidi, sio tu kwa sababu ya kusambaa kwa utumiaji wa maswali ya kundi la Washington, mapungufu ya taarifa hayakosekani, na taarifa kuhusu watu wenye ulemavu bado hukosa ubora na hupelekea kushindwa kulingana. Licha ya upatikanaji wa taarifa rejea, nazo pia zinaweza kuwa si za kuaminika kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo uelewa tofauti juu ya ulemavu, kutoa taarifa kwa kiasi kidogo kutokana na unyanyapaa, vigezo tofauti vinavyotumika kupanga au kupima ulemavu, kuainisha vikwazo, kutolingana kwa maswali yanayoulizwa au pia kwa kuwa vyanzo vya taarifa vimepitwa na wakati (angalia kiambatanisho namba 4 kwa ajili ya maelezo zaidi).

Wakati tathmini ya sekta mbalimbali inapofanyika kujua hali na mahitaji ya jamii, inapaswa pia kutathmini athari kwa watu wenye ulemavu pamoja na familia zao. Taarifa za kaya hutumika kama chanzo cha taarifa katika tathmini ya sekta mbalimbali. Taarifa za ulemavu zinapaswa kukusanywa ambapo zitawezesha kuainisha taarifa zote kwa kutumia pia kigezo cha ulemavu.

Pale ambapo taarifa zenye ubora hazipo, inashauriwa kutumia nadharia ya makadirio kuwa asilimia 15 ya jamii inayoathiriwa na majanga ni watu wenye ulemavu.[57] Kadirio la asilimia 15 linasaidia katika kupangilia pamoja na kufuatilia ufikikaji wa usaidizi (kwa mfano itakadiriwa kuwa asimilia 15 ya majengo yanatakiwa kufikika).

Ili tathmini ya mahitaji iwe jumuishi, watu wenye ulemavu wanapaswa kuwa ndio watoaji wa taarifa na wanapaswa kushiriki katika makundi ya majadiliano.

| Malengo ya kundi majadiliano la tathmini mahitaji jumuishi. | |
|---|---|
| | • Kutambua namna madukuduku mbalimbali yanayotokea katika jamii yanavyopokelewa na wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wenye ulemavu wa aina mbalimbali. Pia, na kutambua masuala mahsusi ambayo watu wenye ulemavu wanapitia.<br>• Kutambua majukumu ya watu wenye ulemavu katika jamii, pia jumuisha mchango wao katika jamii pamoja na namna jamii inavyowasaidia.<br>• Kutambua uzoefu wa watu wenye ulemavu katika nyakati za dharura, kubainisha vikwazo walivyokumbana navyo pamoja na namna walivyokabiliana. |

[54] Angalia ICRC, viwango vya kitaalamu vya kazi ya ulinzi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na wadau wa haki za binadamu katikamigogoro ya kivita na katika hali nyingine za vurugu (2018), Sura ya 6, usimamizi wa data na taarifa kuhusu matokeo ya ulinzi uk. 106-108 na CRPD, ibara ya 22(2).

[55] Rasilimali muhimu, ikiwemo jarida la mafunzo kwa watakwimu katika kutumia kundi la maswali mafupi la Washington kuhusu ulemavu, inaweza kupatikana katika shirika la Humanity and Inclusion. *Taarifa za ulemavu katika wadau wa masuala ya kibinadamu*.

[56] Angalia *Kundi la Washington katika tafsiri ya mbinu na vifaa vya kutoa mafunzo* mtandaoni.

[57] Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia, *Ripoti ya dunia kuhusu Ulemavu* (2011).

| | |
|---|---|
| **Chagua vikundi mahususi** | • Jitahidi kutafuta watu wenye ulemavu ambao wataweza kuwakilisha maoni na vipaumbele vya kundi lao.<br>• Kwa kutumia kundi wakilishi, chagua aina anuwai kubwa za watu wenye ulemavu. Zingatia tofauti ya hatari na vikwazo, angalia muingiliano na mpishano katika umri, jinsi na utofauti. Jumuisha watu wenye ulemavu wa aina tofauti.<br>• Toa fursa ya kujadiliana na wale ambao watashindwa kufika katika makundi ya majadiliano. |
| **Tengeneza/Andaa utaratibu** | • Shauriana na mashirika ya watu wenye ulemavu na watu wenye ulemavu ili kukubaliana namna ya kuwasiliana.<br>• Toa mafunzo kwa wawezeshaji katika mfumo rafiki wa mawasiliano.[58]<br>• Chagua kumbi ambazo ni salama na zinazofikika kwa ajili ya kuhojiana na watu wenye ulemavu. |

Zaidi ya kuchanganua taarifa kwa aina ya ulemavu, mahitaji yanapaswa kuwa na taarifa zenye ubora ambazo ni zenye manufaa kwa watu wenye ulemavu:

- Je, watu wenye ulemavu wanakumbana na namna yeyote maalum ya ubaguzi au ukatili wa makusudi?
- Ni vikwazo gani huwakabili watu wenye ulemavu wakati wanajaribu kufikia usaidizi?
- Ni mifumo gani ya mawasiliano inafikiwa kiurahisi na watu wenye ulemavu?
- Je, watu wenye ulemavu wanahitaji huduma mahsusi (kama vile teknolojia), na je, zinapatikana au hazipatikani?
- Je, ni imani gani au tamaduni gani katika jamii zilizoathiriwa zinazohusu watu wenye ulemavu ambazo ni hatari au zimeshamiri?

Je, maswali hayo juu yanaweza kuulizwa kwa wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu wakiwemo walio mstari wa mbelle kukabiliana na majanga.

Majibu yatasaidia katika kupanga jitihada za huduma za kibinadamu, na sio tu kuelewa ufahamu wa wenyeji, mtazamo na uzoefu, bali pia yatasaidia katika kubuni programu za ulinzi, utetezi na shughuli sahihi za kujenga uwezo.

## Mpango mkakati

Ili kupanga huduma jumuishi za kibinadamu na muitikio jumuishi, ni muhimu kuwa na taarifa juu ya watu wenye ulemavu, kwa mfano:

- Taarifa zilizochanganuliwa kwa aina ya ulemavu zinaweza kuonesha namna ulemavu unavyohusiana na hatari kwenye kupata riziki/kazi au usalama hafifu wa chakula, ukatili, unyonywaji na unyanyaswaji au hatari nyingine yoyote. Taarifa hii inaweza kusaidia katika kutoa kipaumbele kwa aina ya huduma za kibinadamu zinazohitajika au usaidizi unaokusudiwa.
- Taarifa zilizochanganuliwa zinaweza kuonesha maeneo ambayo watu wenye ulemavu wanashindwa kupata usaidizi, na kuwezesha kupangilia upya au kuimarisha huduma na kuondoa mapungufu ya ufikiwaji. Tathmini na ufuatiliaji inaweza kuhitajika kuchambua vikwazo na kuweka hatua za kuviondoa.
- Taarifa za ubora na maelezo kuhusu maoni na mitazamo ya watu wenye ulemavu, zitasaidia wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu kuitikia zaidi kwa kuzingatia ujumuishi.
- Taarifa za ubora na maelezo kuhusu mbinu za kukabiliana wanazotumia watu wenye ulemavu zitasaidia wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu kupanga afua stahiki ambazo zitaongeza ustahimilivu wa watu wenye ulemavu.

[58] Kwa ufafanuzi zaidi kuhusu mawasiliano jumuishi, angalia Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na watoto (UNICEF), Ulemavu, *Moduli ya mawasiliano jumuishi*.





- Taarifa za idadi ya watu wenye ulemavu katika maeneo yaliyoathirika (ikiwemo nadharia ya makadirio ya asilimia 15)[59] inaweza kusaidia nyanja mbalimbali kupanga na kutoa mwongozo katika kuweka mipango na kufuatilia na kuhakikisha kuwa mipango yote ina rasilimali za kutosha na inafikika.

## Ugemaji wa rasilimali

Taarifa za watu wenye ulemavu zinaweza kusaidia kukusanya rasilimali kwa kuonesha athari za majanga kwa watu wenye ulemavu. Pia huonesha hatari ambazo watu wenye ulemavu na familia/kaya zao wanakumbana nazo, hii ni pamoja na kuonesha gharama zinazohitajika katika kufikia mahitaji ya watu wote wenye ulemavu walioathiriwa na majanga.

Kwa kusema hivi, kupanga bajeti za ufikiwaji, zisitegemee ukusanyaji wa taarifa peke yake. Makadirio yanaonesha ili kufikia mahitaji ya ufikiwaji kwa ajili ya mahitaji ya watu wenye ulemavu (mfano kujenga majengo na miundombinu ya huduma ya maji safi na usafi wa mazingira), inashauriwa kati ya asilimia 0.5 na 1 inatakiwa kuongezwa katika bajeti. Asilimia 3 hadi 7 ya bajeti inahitajika ili kupata bidhaa zisizo za chakula na vifaa kwa ajili ya watu wenye ulemavu.[60]

Wafadhili wanaweza kuimarisha ujumuishi wa watu wenye ulemavu kwa kuwataka wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu kuainisha taarifa kwa kigezo cha ulemavu, kutoa matokeo ambayo yanalenga kuwa na viashiria maalumu kwa ajili ya watu wenye ulemavu, na kuweka na kutumia nyenzo za kutambua miradi jumuishi.

Matokeo ya fursa sawa za ufikiwaji na ujumuishi zinaweza kutambuliwa kwa ufasaha kwa njia ya kunyambulisha taarifa wakati wa kufanya ufuatiliaji. Ili kufafanua, njia mojawapo ni kwa kuweka viashiria mahususi kuhusu ulemavu, mfano idadi ya watoto wenye ulemavu wanaopata elimu. Hata hivyo, matokeo mazuri zaidi yanaweza kufikiwa kama maswali ya jumla (Idadi ya watoto wanaopata elimu) yatachanganuliwa kwa aina ya ulemavu. Kwa ujumla italeta maana kama tutaangazia zaidi masuala ya ulemavu kwa kuzingatia viashiria ili kupata matokeo. Viashiria hivi vinaweza kuzingatia hatua zinazochukuliwa katika kuboresha ufikikaji wa usaidizi, kupima ushiriki au kutoa msaada kwa watu wenye ulemavu.

Kiambatanisho namba 5 kinaonesha namna ambavyo viashiria vya matokeo vinavyoweza kutengenezwa ili kutambua kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanajumuishwa. Viashiria hivi pia vinatumika katika kufuatilia utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Watu wenye Ulemavu ikiwemo kIfungu namba 11 kinachohusu ulemavu na masuala ya kibinadamu. Angalia *kipengele kinachohusu kuziba pengo*.

## Utekelezaji na Ufuatiliaji

Kufuatilia utekelezaji kunapaswa kutambua namna ya usaidizi wa huduma za kibinadamu unaowafikia watu wenye ulemavu na namna gani mahitaji yao yanavyobadilika wakati majanga yanapotokea.

Taarifa zilizochanganuliwa zilizokusanywa kutokana na ufuatiliaji husaidia katika kutambua mapungufu katika ufikiwaji wa watu wenye ulemavu. Wakati ufuatiliaji umeibua mapungufu hayo, zoezi la kukusanya taarifa (ikiwemo kupitia makundi ya majadiliano ya pamoja na mahojiano na watu wenye ulemavu kutoka katika maeneo yaliyoathiriwa, mashirika ya watu wenye ulemavu katika eneo husika pamoja na wadau wa masuala ya kibinadamu) ni muhimu kufanyika ili kuelewa aina ya vikwazo ambavyo watu wenye ulemavu wanakabiliana navyo na kupangilia hatua za kuviondoa.

Ili kukuza mfumo wa ufuatiliaji wa ufikiwaji wa usaidizi, huduma za kibinadamu zinapaswa kuhakikisha kuwa mikataba na nyaraka za ufuatiliaji kwa ajili ya wadau wanaotekeleza zipo, ili waweze kutoa taarifa kuhusu idadi au uwiano wa watu wenye ulemavu waliofikiwa katika miradi yao. Taarifa kuhusu hali halisi, masuala ya kibinadamu na masuala mengine ya kutoa taarifa yanapaswa kuelezea kuhusu hatua katika kuwafikia watu wenye ulemavu, ikiwemo matumizi ya taarifa zilizochanganuliwa.

Ufuatiliaji wa masuala ya ulinzi ni nyenzo muhimu katika kutambua hatari ambazo watu wenye ulemavu wanakabiliana nazo. Taarifa hii inasaidia katika kutoa huduma na kupunguza hatari na kusaidia ustahimilivu wa watu wenye ulemavu. Pale inapowezekana,[61]

[59] Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia, *Ripoti ya dunia kuhusu ulemavu* (2011).

[60] Angalia *viwango vya ujumuishi wa masuala ya kibinadamu kwa wazee na watu wenye ulemavu na nuru ya dunia*, na Light for the World, *kitabu cha ujumuishi wa ulemavu*.

[61] Hili haliwezekani mara zote, halitawezekana kwa mfano, wakati tukio linapotolewa taarifa na mtu mwingine kama shahidi au wakati tukio linahusisha jamii au kikundi kuliko mtu binafsi.

taarifa za ufuatiliaji wa masuala ya ulinzi zinapaswa kuchanganuliwa kwa aina ya ulemavu. Mchakato huo unatakiwa kulenga katika kutambua hatari zinazowapata watu wenye ulemavu kama vile ukatili, vitendo vya kikatili, kutumia vizuizi na kuwaweka watu wenye ulemavu katika taasisi.

### Tathmini

Ili kukuza ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika tathmini ya masuala ya kibinadamu, hadidu za rejea za kuhusu tathmini zinahitaji taarifa kuchanganuliwa kwa aina ya ulemavu, iwapo taarifa zinakusanywa kwa watu binafsi (iwe ni wanufaika au wanachangia katika huduma). Pia, tathmini inatakiwa kuwajumuisha watu wenye ulemavu kama wahusika wakuu katika kutoa taarifa na kuuliza maswali yanayoweza kuibua taarifa mahsusi kuhusu watu wenye ulemavu.

Kwa kuzingatia maudhui, tathmini inatakiwa kuzingatia namna watu wenye ulemavu wanafikia huduma za usaidizi, wanavyoshiriki katika kila miradi ya masuala ya huduma za kibinadamu, na namna miradi hiyo imepunguza hatari ambazo watu wenye ulemavu wanakabiliana nazo katika kukuza ustahimilivu wao. Katika kulifikia hilo, mifano mizuri ya ujumuishi lazima iwekwe wazi. Wafanya tathmini wanatakiwa watengeneze viashiria mahususi katika kupima maendeleo na katika kuwafikia na kuwahusisha watu wenye ulemavu; mfano, kupima uwiano wa watu wenye ulemavu katika kufikiwa na miradi na kupata huduma stahiki.

Kiambatanisho namba 6 kinaweka vigezo vya kufanya tathmini katika masuala ya kibinadamu kwa kutumia tafsiri ya vigezo vya "*OECD-DAC*". Vigezo hivi vinatumika kwa kuzingatia mtazamo wa watu wenye ulemavu kwa mfano kupendekeza masuala ambayo yatajadiliwa katika mtizamo wa masuala ya huduma za kibinadamu.

## Muhtasari wa mambo muhimu; ukusanyaji wa taarifa na usimamizi wa taarifa

### Maandalizi

- Tengeneza mwongozo wa namna wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu wanaweza kuimarisha ukusanyaji wa taarifa ili kuwezesha ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu kwa kuzingatia utunzaji na faragha ya taarifa.
- Tambua vyanzo vya taarifa kuhusu watu wenye ulemavu ikiwemo taarifa za sensa, kanzidata za kiutawala na taarifa zilizokusanywa na mashirika ya watu wenye ulemavu au mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Ainisha taarifa kuhusu mashirika ya watu wenye ulemavu, huduma zinazofikika pamoja na majengo ya umma.
- Jengea uwezo wa kukusanya taarifa za watu wenye ulemavu kwa kutoa mafunzo kwa wadau katika eneo husika na kubainisha na kutafsiri nyenzo muhimu za kukusanyia taarifa.
- Tafiti zinapofanyika kama zile za DHS, MICS na sensa za kitaifa katika nchi ambazo hatari za masuala ya kibinadamu zipo juu, msisitizo unatakiwa uwe katika kujua thamani ya kutumia nyenzo ambazo zimepimwa katika muktadha wa huduma za kibinadamu, kama vile maswali ya "Kundi la Washington kuhusu ulemavu na moduli inayohusu ufanyaji kazi wa mtoto iliyotengenezwa na UNICEF." Ainisha maeneo mengine ya kukusanya taarifa katika muktadha wa huduma za kibinadamu ambapo njia hizi zinaweza kutumia, kwa mfano Nyenzo ya Kutambua Watu Waliohamishwa ambayo imetengenezwa na shirika la "IOM".

### Tathmini ya mahitaji na uchambuzi

- Mashirika yenye uwezo yanapaswa kufanya kazi na wafanya tathimini ili kuhusisha masuala ya ulemavu katika tathimini ya mahitaji na uchambuzi mwingine.
- Kusanya taarifa kuhusu huduma ambazo zinawahusisha na kuwalenga watu wenye ulemavu katika muktadha wa masuala ya huduma za kibinadamu. Ili kufanya hivyo, rekebisha zana za usimamizi kwa kufuata viwango vinavyokubalika, kwa mfano hatua za "5W".
- Katika majanga ya muda mrefu, wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu wana fursa ya kuboresha mbinu za ukusanyaji wa taarifa iwapo hali inaruhusu kuchukua takwimu za watu, lakini mara nyingi mizunguko ya jamii iliyoathirika hulazimisha kuwa mbinu za kibunifu za kukusanya takwimu zinapaswa kutumia sampuli nasibu.

Pale ambapo taarifa za kuaminika kuhusu watu wenye ulemavu hazipatikani au zimepitwa na wakati, tumia nadharia ya makadirio ya asilimia 15[62] kama msingi wa kufanya mipango.

### Mpango mkakati

- Tumia taarifa za watu wenye ulemavu katika kuweka mipango na katika kuweka vipaumbele na usaidizi stahiki.

### Ugemaji rasilimali

- Mahitaji ya taarifa kuhusu watu wenye ulemavu katika masuala ya huduma za kibinadamu utaimarishwa na sera za wafadhili na mahitaji ya taarifa wanazozihitaji, jedwali la matokeo linalohusisha viashiria vinavyowahusu watu wenye ulemavu na nyenzo za kufuatilia rasilimali ili kubaini ujumuishi wa watu wenye ulemavu.
- Malengo yanayohusisha watu wenye ulemavu yanatakiwa kurejerewa wakati wa kuomba fedha za miradi na rufaa.

### Utekelezaji na Ufuatiliaji

- Taarifa zilizochanganuliwa kupitia nyenzo za ufuatiliaji ni muhimu katika kutambua ufikiwaji na mapungufu mengine kwa watu wenye ulemavu.
- Rekebisha nyenzo za ukusanyaji taarifa pamoja na kanzidata zinazotumiwa katika masuala ya kibinadamu ili kuweza kupata taarifa ya namna ufanisi wa programu na afua stahiki zinavyoweza kuwafikia watu wenye ulemavu.
- Mikataba na kielekezo cha taarifa kwa ajili ya wadau wanaotekeleza masuala ya kibinadamu inahitaji kufafanua na kutoa taarifa kuhusu idadi au uwiano wa watu wenye ulemavu ambao wanafikiwa na afua stahiki.
- Zaidi ya hapo, tathmini zinapaswa kuhusisha watu wenye ulemavu miongoni mwa watoa taarifa, na maswali yanapaswa kuulizwa yakiwa na mlengo mahususi wa kupata taarifa kuhusu watu wenye ulemavu.
- Wafanya tathmini wanaweza kuibua viashiria mahususi ili kupima maendeleo katika kuwafikia watu wenye ulemavu, viashiria hivi vinaweza kupima, kwa mfano asilimia ya watu wenye ulemavu waliofikiwa na miradi na afua stahiki.

## Dhana muhimu[63]

**Taarifa za upimaji kiasi** zinatoa mwanga katika kuonesha ukubwa na kipimo cha athari za majanga ya kibinadamu kwa kutoa maelezo ya kitakwimu juu ya athari katika jamii husika. Taarifa za upimaji zitasaidia katika kujibu maswali kwa namba, kwa mfano kiasi gani, ngapi, na kwa mara ngapi'.

**Taarifa za upimaji ubora** zinaonesha ukubwa wa majanga ya kibinadamu kwa kutoa maelezo ya uzoefu wa athari katika jamii zilizoathiriwa. Taarifa za ubora zitajibu maswali yanayohusisha maoni, maadili, imani pamoja na dhana. Kwa nini mikakati imekabiliana au imeshindwa kukabiliana na majanga? Mtu mwenye ulemavu aliyehamishwa anajisikiaje? Ni kitu gani anaamini kingeweza kuboresha hali yake?

**Taarifa za msingi** hukusanywa moja kwa moja kutoka katika jamii iliyoathiriwa kupitia timu ya kufanya tathmini. Taarifa za msingi zinaweza kuwa ni zile zinazopima kiasi au ubora.

**Taarifa za rejea** hukusanywa kutoka katika tafiti za kitakwimu na za kiuchambuzi (sensa, taarifa kutoka tafiti za nyuma). Taarifa za rejea zinaweza kuwa ni zile zinazopima kiasi au ubora.

# 5 Ushirikiano na uwezeshaji wa taasisi za watu wenye ulemavu

## Utangulizi: Mashirika ya watu wenye ulemavu ni yapi?

**Mashirika ya watu wenye ulemavu** ni mashirika yenye uwakilishi wa watu wenye ulemavu. Mengi kati yao hutawaliwa na kuongozwa na watu wenye ulemavu wenyewe. Endapo katika eneo husika mashirika hayo hayajawakilishwa, kikanda, kitaifa na kimataifa mashirika ya watu wenye ulemavu yanaweza kutafutwa kupitia mitandao ya kimataifa.

Mashirika ya watu wenye ulemavu hufanya kazi ya utetezi, kutoa mwongozo, mafunzo, usaidizi wa kitaalamu na kukuza haki kupitia *moduli wa haki za kijamii ambao ni ujumuishaji na uwezeshaji*. Mashirika ya watu wenye ulemavu yamefanikiwa sana katika kuleta mabadiliko ya sheria za kitaifa na kukuza uelewa, na mengi wametoa mafunzo kwa wadau wa huduma za kibinadamu, katika jamii, serikali na ofisi za kitaifa za majanga kuhusu haki za watu wenye ulemavu.

Mashirika ya watu wenye ulemavu ni tofauti na mashirika ambayo yanatoa huduma moja kwa moja kwa watu wenye ulemavu.

**Mashirika ya watu wenye ulemavu yanaweza kufanya yafuatayo:-**

- Kufanya kazi katika eneo husika, kitaifa, kikanda na kimataifa.
- Kujihusisha na aina moja ama aina mbalimbali za ulemavu.
- Kuwakilisha kundi maalum (kwa mfano wanawake, watu asili ya eneo husika au wenye ulemavu).
- Kuwakilisha kundi kubwa au dogo, shirika la watu wenye ulemavu linaweza lisiwakilishe watu wote wenye ulemavu.
- Kuwa katika mtandao katika eneo husika au kitaifa ambao unaweza kuwa moja ya mitandao ya kikanda au kimataifa.

## Ushirikiano na mashirika ya watu wenye ulemavu

Ushirikiano unaweza kuboresha ufanisi na uwajibikaji katika huduma za kibinadamu. Ushirikiano unasaidia kufikia ujumuishi na kuhakikisha kuwa masuala ya kibinadamu yanawanufaisha na kuchangia katika maendeleo. Katika kuheshimu jamii ya watu wenye ulemavu na kuzingatia dhima ya (pasiwepo chochote kutuhusu sisi bila sisi), wadau wa masuala ya kibinadamu wanapaswa kufanya kazi na watu wenye ulemavu na kupata uwakilishi wa mashirika yao kuliko kupanga au kufanya maamuzi kwa niaba yao.

Kama ilivyo ada kwa ushirikiano wowote masuala ya maslahi ya pamoja, kuongeza thamani, matarajio na kukuza uwezo vinapaswa kuwa kwenye makubaliano tokea awali.

Ushirikiano kati ya mashirika ya watu wenye ulemavu na wadau wa huduma za kibinadamu kabla ya majanga, wakati wa majanga na baada ya majanga:

- Kutoa utaalamu juu ya masuala ya watu wenye ulemavu, uzoefu, maarifa na mazingira wanamoishi kwa wadau wa masuala ya kibinadamu.

- Tengeneza stadi na maarifa yatakayosababisha huduma za kibinadamu na usaidizi kuwa jumuishi, zinazowezeshwa na taarifa kutoka kwa watu ambao wanafanyakazi kwa ukaribu na wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu.
- Kuza maelewano na maarifa.
- Jenga uwezo na kuza utamaduni wa kujifunza baina ya mashirika ya watu wenye ulemavu na wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu.
- Hakikisha muendelezo wa jitihada na afua, kwa sababu mashirika ya watu wenye ulemavu huendelea kubaki hata baada ya majanga kupita.
- Imarisha na unganisha jamii kuzunguka maeneo yenye kuhitaji na yenye matatizo.
- Imarisha utetezi na ulinzi wa watu watu wenye ulemavu waliohamishwa.

Si mashirika yote ya watu wenye ulemavu yana dhima ya kufanya kazi katika huduma za kibinadamu. Katika hali nyingi mashirika ya watu wenye ulemavu yanaweza kuwa hayajawahi kufanya kazi katika nyanja ya masuala ya kibinadamu, na mzunguko wa programu za huduma za kibinadamu, uratibu, ufadhili, muitikio na urejeshaji wa hali na michakato ya ufadhili. Mara nyingi, mashirika ya watu wenye ulemavu hupata fursa finyu ya kushirikiana na mashirika ya huduma za kibinadamu. Ni muhimu kuweka sawa matarajio ya kila mmoja.

Wakati wadau wa masuala ya kibinadamu wanahitaji kuendeleza ushirikiano na mashirika ya watu wenye ulemavu, uwezo wao wa kufanya hivyo unakwamishwa na uhaba wa maarifa juu ya harakati za watu wenye ulemavu, ubaguzi kwa watu wenye ulemavu na mitazamo kwamba masuala ya watu wenye ulemavu yanapaswa kushughulikiwa na mashirika yanayohusu ulemavu pekee.

**Wajibu wa mashirika ya watu wenye ulemavu** katika kushirikiana na wadau wa huduma za kibinadamu utategemea na uwezo wao wa awali katika kukabiliana na majanga, mamlaka yao, na uwezo wao kwa kuwawakilisha watu wenye uleamavu au kundi maalum la watu wenye ulemavu. Wakati mashirika ya watu wenye ulemavu hayapo, au yale yaliyopo hayana uwezo unaohitajika, wadau wa huduma za kibinadamu wanapaswa kutengeneza mahusiano na mitandao ya kikanda au kimataifa ya mashirika ya watu wenye ulemavu.

Mashirika ya watu wenye ulemavu yanaweza kufanya majukumu mengi. Orodha ifuatayo hapo chini sio kamilifu, lakini inaweza kuwa yenye manufaa kwa kuanzia pale ambapo wadau wa huduma za kibinadamu wanakusudia kufanya kazi na kujadili kuhusu ushirikiano.

Mashirika ya watu wenye ulemavu yanaweza kufanya:

- Kuwa kama wawakilishi katika jamii zao kwa kutumia utaalamu wao katika masuala ya watu wenye ulemavu.
- Kutoa taarifa muhimu kuhusu watu wenye ulemavu katika maeneo waliyopo kuhusu hali zao, vikwazo vinavyowazuia katika kufikia usaidizi wa huduma za kibinadamu, vitisho na ukiukwaji wa haki za binadamu, n.k.
- Kutoa usaidizi wa kitaalamu juu ya masuala ya ulemavu katika mashirika ya kibinadamu kwa mfano kwa nia ya kukuza uelewa, kuainisha na kuondoa vikwazo, kuwezesha ufikivu wa rasilimali, kujenga uwezo wa masuala ya kibinadamu ambayo ni jumuishi, kulinda na kukuza haki au kupunguza athari za majanga kwa watu wenye ulemavu.
- Kuhamasisha watumishi wa serikali na wadau wa masuala ya kibinadamu kujifunza kuhusu masuala ya ulemavu, kubadili na kupitia upya sera, mabadiliko ya sheria, au kurekebisha na kutumia nyenzo na michakato inayoimarisha ulinzi na usaidizi unaopatikana kwa watu wenye ulemavu wakati wa majanga.
- Kutoa huduma zinazowalenga watu wenye ulemavu, mara nyingi kwa kutumia mtindo wa usaidizi kupitia makundi rika.

## Ushirikiano wakati hakuna uwakilishi wa kutosha kutoka kwa mashirika ya watu wenye ulemavu katika maeneo yaliyoathirika

Katika muktadha wa masuala ya huduma za kibinadamu, katika eneo husika, mashirika ya watu wenye ulemavu yanaweza kukosekana, na hata kama yanapatikana yanaweza kuwa yamedhoofishwa na majanga au uwezo mdogo au yanaweza yasiwe na uwakilishi wa kutosha wa watu wenye ulemavu. Jamii inapokuwa imehamishwa kwa mfano, wajumbe wa mashirika ya watu wenye ulemavu wanaweza kutawanyika katika maeneo mbalimbali na inaweza kuwa vigumu kwa wao kuwasiliana au kujipanga katika kufanya jitihada wakati wa majanga au kusaidia katika jitihada za huduma za kibinadamu.

Iwe mashirika ya watu wenye ulemavu yamepatikana au la! Jitihada za huduma za kibinadamu zinapaswa kujumuisha watu wenye ulemavu na zinapaswa kufanyia kazi vipaumbele na mahitaji yao. Pale ambapo mashirika ya watu wenye ulemavu hayapo au hayawezi kutoa uwakilishi kikamilifu katika jamii iliyohamishwa, mikakati ifuatayo inaweza kutumika:





- Husisha watu wenye ulemavu na familia zao katika mchakato wa mashauriano na katika vyombo vya maamuzi ikiwemo uongozi wa makambi. Waalike na tumia maarifa kuhusu ulemavu katika kutengeneza mikakati ya kuondoa hatari kwa watu wenye ulemavu.
- Tambua watu wenye sifa ambao wana aina mbalimbali za ulemavu, umri na jinsi tofauti kisha waajiri kama wafanya kazi au watu wanaojitolea.
- Tengeneza na hamasisha muundo rasmi au usio rasmi wa vikundi (kwa ajili ya usaidizi wa makundi rika) na wajengee uwezo wa kuwakilisha wenzao katika utawala na uratibu wa jitihada za huduma za kibinadamu. Wanaweza kuchangia katika kutambua vikwazo, kufikia mahitaji na kupunguza hatari za kiulinzi, na kwa ujumla waweze kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanatumia sauti zao kusikika.
- Pale ambapo wahusika ni wakimbizi, ratibu kwa kushirikiana na nchi inayowahifadhi au mashirika ya watu wenye ulemavu. Kama inawezekana, waalike kuhamasisha watu wenye ulemavu waliopo katika makambi na jamii zinazowahifadhi. Hamasisha na saidia mashirika ya watu wenye ulemavu kujumuisha wakimbizi na watu wengine waliohamishwa katika mitandao yao.

## Rejea

- *Mikutano Fikivu na Orodha ya Kukagulia Tukio*
- Mtandao wa kitaifa, *mwongozo wa mpango wa kutengeneza matuko ya muda mfupi kuwa fikivu kwa watu wenye ulemavu*.
- *Mtandao wa kitaifa, matukio fikivu, mpango na maandalizi ni muhimu*.

# 6 Masuala Mtambuka

## Umri, Jinsia na Uanuwai[64]

Tofauti halisi au ya kudhaniwa katika sifa za mtu, kwa kiasi kikubwa hushawishi aina ya uzoefu, fursa, uwezo, mahitaji na mazingira magumu anayopitia. Migogoro na uhamishwaji wa mara kwa mara huzidisha utofauti na kukuza ukandamizaji, unyonyaji au kutengwa, kwa sababu huongeza ukosefu wa usalama, kuharibu mifumo ya usaidizi katika jamii, kupunguza fursa za kupata kipato na kubadili mazingira ya kijamii na ya kimwili.

Umri, jinsia na ulemavu pamoja na uanuwai ni masuala ambayo yapo katika jamii zote ulimwenguni. Ni muhimu kuyazingatia na kujua namna yanavyoingiliana, katika awamu zote za programu za huduma za kibinadamu ili kuhakikisha kuwa watu wote walioathirika wakiwemo wenye ulemavu wanaweza kupata haki zao na kushiriki kikamilifu katika jitihada husika. Katika misingi ya usawa, na ili kuweza kuwajibikaji katika jamii zilizoathirika, wadau wa huduma za kibinadamu wanapaswa kutambua kuwa muingiliano wa umri, jinsia na ulemavu pamoja na aina zingine za anuwai zinaathiri kwa namna tofauti ustahimilivu, ulinzi na usawa wa watu katika jamii zilizoathiriwa. Kwa mfano, mwanamke mzee mwenye ulemavu anaweza kuwa katika hatari ya kukumbana na ukatili wa kijinsia kutokana na ubaguzi wa umri, dhana potofu za masuala ya jinsia na vikwazo vinavyoletwa na ulemavu; mabinti balehe wanaweza kutengwa katika kutoa maamuzi kutokana na unyanyapaa kuhusu watu wenye ulemavu na dhana potofu za kijinsia; vijana wa kiume balehe wenye ulemavu wapo katika hatari ya kupelekwa katika vikundi vya kijeshi kutokana na umri na ulemavu wao.

Ili kuondoa athari za majanga ya kibinadamu, ni muhimu kuelewa namna ambavyo majanga yanapunguza uwezo wa watu wenye ulemavu katika kufikia na kushiriki katika usaidizi wa kibinadamu na ulinzi. Ili kuondoa unyanyapaa na udhalimu, ni muhimu kufikia maeneo yote ya jamii yaliyoathiriwa, sio tu wale ambao wanaonekana kirahisi.

Mwongozo huu unazingatia watu wenye ulemavu kwa kigezo cha umri, jinsia, hali ya kisaikolojia na historia yake.

### Umri

Umri unahusisha tafsiri ya kijamii na ya kimuktadha ya hatua ambazo mtu anapitia katika mzunguko wa maisha yake. Uwezo na mahitaji ya mtu hubadilika kwa kadiri umri unayoongezeka. Umri unaweza kuwezesha au kudidimiza uwezo wa mtu katika kupata haki yake. Ili kupata afua stahiki katika makundi mbalimbali ya umri (watoto, vijana, watu wa wazima, watu wa makamu na wazee wenye ulemavu), wadau wa masuala ya kibinadamu wanapaswa kuzingatia mahitaji mbalimbali, vikwazo na vitisho ambavyo watu wenye ulemavu wanakabiliana navyo katika hatua mbalimbali za umri na maisha yao.

### Jinsia

Jinsia inahusisha tofauti zilizopo kijamii kati ya wanawake, wanaume na wengine, na mahusiano kati yao na baina yao, katika mzunguko wa maisha yao. Tofauti hizi ni za kimuktadha na za muda maalum na hubadilika kwa kipindi fulani na katika tamaduni mbalimbali. Jinsia pamoja na umri hubainisha mwelekeo wa wajibu, majukumu, mamlaka na ufikivu wa rasilimali.

[64] Imechukukiwa kutoka katika kitabu kuhusu dharura cha shirika la wakimbizi duniani (UNHCR).

Matokeo pia huathiriwa na sababu nyingine za anuwai kama vile ulemavu, hadhi katika jamii, rangi, tabaka, historia ya kikabila au kidini, hali ya uchumi, hali ya ndoa, hali ya uhamiaji, kuhamishwa, eneo ya mjini au vijijini.[65] Ili kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu walioathirika wana ufikivu sawa na wa salama katika usaidizi wa kibinadamu na ulinzi, wadau wa masuala ya kibinadamu wanapaswa kubuni programu ambazo zinazingatia uwanda mpana wa namna watu wenye ulemavu wanatambuliwa katika masuala ya kijinsia na yale yanayohusu kujamiiana katika jamii walizopo.

## Uanuwai

Uanuwai inahusisha tofauti katika maadili, tabia, mtazamo wa kitamaduni, imani, historia ya kikabila, utaifa, utambulisho wa kijinsia, afya na hadhi katika jamii, ulemavu pamoja na sifa maalum za mtu. Wakati kipimo cha umri na jinsia vinapatikana kwa watu wote tabia zingine zinatofautiana kwa watu tofauti. Kama watahitaji kusaidia watu walioathirika, wakiwemo watu wenye ulemavu na kuhamasisha ushiriki wao, wadau wanaoshughulikia masuala ya huduma za kibinadamu wanapaswa kutambua na kuelewa tofauti hizi.

# Kuandaa programu mtambuka

## Kukondoisha ulinzi[66]

Kutokana na sura mbalimbali za vitisho vya ulinzi na muktadha mgumu vinapoibukia, mashirika na mamlaka zinazotoa huduma za kibinadamu zinapaswa kuratibu na kufanya kazi katika mfumo shirikishi na wa kutegemeana. Suala la ulinzi linatakiwa kuwa kitovu katika masuala ya kibinadamu na huhitaji mfumo mpana wa makubaliano[67]. Wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu wanahitaji kujumuisha masuala ya ulinzi katika programu zao, kwa kuzingatia umri, jinsi, ulemavu na anuwai, pia kwa kufuata mambo makuu manne ili kukondoisha masuala ya ulinzi:

1. **Zingatia usalama na utu wa mtu na zuia maumivu.** Zuia na punguza kwa kadiri iwezekanavyo aina yoyote ya madhara yasiyokusudiwa katika afua zinazochukuliwa ambazo zinaweza kuongeza hatari za kimwili na kisaikolojia kwa watu.

2. **Ufikivu unaofaa.** Andaa mazingira kwa ajili ya watu kupata ufikivu, usaidizi na huduma kwa uwiano ili kutokuwa na vikwazo vyovyote au ubaguzi. Weka umakini zaidi kwa watu au makundi ya watu wanaokumbana na hatari kubwa ya usalama au vikwazo katika kupata usaidizi na huduma.

3. **Uwajibikaji.** Unda mifumo sahihi ambayo jamii zilizoathirika zinaweka kupima utoshelevu wa afua stahiki na kuhakikisha masuala na malalamiko yao yanafanyiwa kazi.

4. **Ushiriki na uwezeshaji.** Saidia kutengeneza uwezo binafsi wa kujilinda na sadia watu kudai haki zao, ikiwemo haki ya makazi, chakula, maji na usafi wa mazingira, afya na elimu.

## Zingatia usalama, utu wa watu na zuia maumivu

Kanuni hii ya kwanza hapo juu (zingatia usalama, utu wa watu na zuia muumivu[68]) inapaswa kuwa jumuishi kwa watu wenye ulemavu. Haipaswi kutumiwa katika kuzuia misaada, kueneza vitendo vya kibaguzi au kuunda vikwazo katika kusaidia watu wenye ulemavu. Mashirika yanayofanya kazi bila ya kushauriana na watu wenye ulemavu yanaweza kuweka vipaumbele au kupanga mipango vibaya, na hivyo kuwaweka watu wenye ulemavu katika hatari kubwa. Kupuuza au kuacha kuchukua hatua stahiki ili kuzuia madhara mabaya, kunaweza kusababisha maumivu makubwa.

[65] Imechukuliwa kutoka IASC, *kitabu cha jinsia kwa masuala ya kibinadamu* (2017), uk. 385.
[66] Angalia sekta ya ulinzi kidunia, *kurasimisha ulinzi*.
[67] Sera ya *IASC kuhusu ulinzi wa masuala ya kibinadamu* (2016).
[68] Angalia sekta ya ulinzi kidunia, *mafunzo ya urasimishaji wa ulinzi* (2014).





### Hatua muhimu

- Shauriana na watu wenye ulemavu katika kuhakikisha kuwa maamuzi yaliyochukuliwa yanazingatia matakwa yao na hayana athari zozote katika maisha yao (angalia suala zima la ridhaa).
- Epuka mikakati na vitendo ambavyo vinaendeleza ubaguzi kwa watu wenye ulemavu. Kwa mfano, huduma za marekebishaji/utengamao ni muhimu kuwepo katika jitihada zinazotakiwa kuchukuliwa, lakini hakutatui changamoto zote za mtu na inabidi kwenda sambamba na hatua zingine ambazo watu wenye ulemavu wanazipendekeza.

**Zingatia usalama, utu wa mtu na zuia maumivu**

| Kutochukua hatua husababisha madhara | Kufanya makosa husababisha madhara |
|---|---|
| Kuweka programu au miradi (kama vile usambazaji wa chakula au vituo vya maji) bila ya kuzingatia iwapo watu wenye ulemavu wanaweza kufikia maeneo yaliyochaguliwa. | Kutenda bila kupata ridhaa ya hiari kwa watu husika inaweza kuwa na athari kubwa katika afya zao. |
| Kushindwa kutoa taarifa kuhusu programu au miradi katika miundo fikivu na katika lugha ambayo kila mmoja anaweza kuelewa. | Kutenda bila ya kushauriana na wanufaika wakiwemo watu wenye ulemavu, kunaweza kupelekea wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu kuweka vipaumbele visivyo sahihi na kuweka mipango mibovu hivyo kuwaweka wanufaika katika hatari kubwa. |

## Afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia

Afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia uhusisha msaada unaolenga kulinda na kukuza ustawi wa kisaikolojia na kuzuia au kudhibiti mdororo wa hali ya afya ya akili.[69] Wakati wa majanga ya kibinadamu, sababu nyingi kama vile (ukatili, matukio ya ghafla, kupotelewa na mwanafamilia, kupoteza makazi) vinaweza kuathiri afya ya akili kwa watu, familia na jamii); Watu wenye ulemavu wanaweza kuathiriwa kwa kiasi kikubwa. Kwa kuhusisha MHPSS katika programu, wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu wanaweza kuboresha afya ya akili kwa watu wote walioathirika wakiwemo wenye ulemavu wa viungo, matatizo ya afya ya akili. Kuhusisha na msaada wa afya ya akili na kisakolojia katika maeneo ya dharura kunahusisha hatua mbalimbali na msaada unaoratibiwa katika nyanja mbalimbali (katika piramidi za afua na afya ya akili katika dharura):[70]

1. Hatua zitakazorejesha utu na usalama wakati wa dharura kwenye maeneo yaliyoathirika wakati tukihamasisha ufikivu sawa katika huduma za msingi, ni muhimu kwa ajili ya afya ya akili na ustawi wa kisaikolojia (Hatua ya Kwanza).

2. Afua nyingine muhimu ni kuimarisha mshikamano wa kijamii na kusaidia jamii na familia (Hatua ya pili).

3. Afua zinazolenga watu binafsi, familia na makundi, ambazo zinatoa usaidizi wa kihisia na utendaji zinasaidia katika afya ya akili (hatua ya tatu).

[69] IASC, *mwongozo wa afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia katika nyakati za dharura* (2007).
[70] *Ibid.*

Afua hizi zinaweza kutolewa na watu wasio na taaluma au wasaidizi wa afya katika kundi rika katika huduma za afya, elimu na jamii (Hatua ya 3).

4. Inapobidi, wataalamu wanaweza kutoa afua huduma za afya ya akili ambazo zinaweza kuwa ni za kisaikolojia au kifamasia (Hatua ya 4).

Afua za Huduma za Afya ya Akili zimejikita katika muundo wa haki za binadamu na zinakuza na kulinda haki za watu wenye ulemavu. Huduma za afya ya akili zinawanufaisha watu wote walioathiriwa wakiwemo watu wenye ulemavu ambao wanakabiliana na mfadhaiko wa kisaikolojia.

# 7 Uwajibikaji kwa watu walioathirika na kuwalinda dhidi ya unyonyaji wa kingono na dhuluma

Uwajibikaji kwa jamii zilizoathirika[71] ni jukumu la pamoja kwa mashirika yanayotoa msaada na wadau wengine (wafadhili, serikali), kuazimia kutumia mamlaka na rasilimali zao kwa maadili na kiuwajibikaji, kwa namna ambayo inawapa watu kipaumbele katika masuala ya kibinadamu. Wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu wana wajibu wa kuhakikisha kuwa afua zao zinaleta matokeo mazuri kwa makundi yote ambayo yameathiriwa na majanga ikiwemo makundi ambayo hayatambuliki kirahisi kama vile watu wenye ulemavu. Wanapaswa kufanikisha hili kwa kutumia utaalamu na viwango vya ubora; kuratibu jitihada zao ili kuongeza eneo la kuhudumia na kupunguza hatari, mapungufu na kujirudiarudia kwa afua, kusikiliza na kuwahusisha watu walioathirika na kuyafanyia kazi maoni yao.

Uwajibikaji kwa jamii zilizoathirika inalenga masuala ya haki, utu na kulinda jamii zilizoathiriwa katika ujumla wake. Inahitaji wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu kuainisha na kueleza mahitaji ya watu walio katika hatari katika maeneo yaliyoathirika. Pia, inawahitaji kutambua na kuunganisha uwezo, maarifa na matakwa ya jamii hizo.

Ili kuhakikisha kuwa uwajibikaji unatokea kwa watu wote walioathirika, wakiwemo watu wenye ulemavu, michakato ya uwajibikaji lazima iwe fikivu kwa watu wenye ulemavu na izingatie mahitaji yao. Jukumu hili linahusisha kuangazia ujumuishi kupitia programu za kibinadamu, kuhakikisha watu wenye ulemavu wanashiriki katika mchakato wa kufanya maamuzi, na kuwasilisha taarifa kwao katika njia fikivu.

Kiambatisho namba 7 kinajadili namna wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu wanavyoweza kufikia maazimio na vigezo vya ubora vilivyowekwa katika viwango vya misingi ya kibinadamu kwa kufanya kazi kwa ufanisi na kuwajumuisha watu wenye ulemavu.

## Maazimio ya kamati ya IASC kuhusu uwajibikaji kwa watu walioathirika


Mnamo mwaka 2017, kamati ya IASC ilipitisha toleo la uwajibikaji kwa jamii zilizoathirika lililoboreshwa liitwalo "Maazimio kuhusu uwajibikaji kwa watu walioathirika na kuweka ulinzi dhidi ya unyonywaji wa kijinsia na dhuluma" yaani "*Commitments on Accountability to Affected People and Protection from Sexual Exploitation and Abuse* (CAAP and PSEA)." Mapitio ya toleo hili yalizingatia Mwongozo mpya wa sera za huduma za kibinadamu, ikiwemo viwango vya msingi vya kibinadamu na matokeo ya Mkutano wa kimataifa wa Masuala ya kibinadamu wa Grand Bargain.[72]

Mapitio ya Maazimio katika uwajibikaji kwa jamii zilizoathirika yaani yanaweka msisitizo mkubwa katika uwajibikaji wa pamoja. Wadau wa masuala ya kibinadamu wanategemewa kufanya kazi mmoja mmoja na kwa pamoja ili kuwezesha na kujumuisha uwajibikaji kwa jamii zilizoathirika katika jitihada na afua zao. Majukumu yao ni muhimu. Kiambatisho namba 7 kinaelezea namna ya kuhakikisha ujumuishi wa watu wenye ulemavu kwa kuzingatia maazimio manne.

[71]Kuhusu tamko la hivi karibuni kuhusu sera hii, angalia IASC, *maazimio kuhusu uwajibikaji kwa watu walioathirika na ulinzi kutoka katika unyanyasaji wa kijinsia* (CAAP na PSEA) (2017). Kuhusu tamko la awali, angalia IASC, *kikosi kazi cha IASC kuhusu uwajibikaji kwa jamii iliyoathiriwa na ulinzi kutoka katika unyanyasaji wa kijinsia*.

[72]Angalia tovuti ya IASC kuhusu *Brand Bargain*.

**Mchoro namba 4 |** Uwajibikaji kwa jamii zilizoathirika[73]




## Muhtasari wa vipengele vya uwajibikaji kwa watu walioathirika na kuwalinda na unyonyaji wa kingono na dhuluma

### Tathmini ya mahitaji na uchambuzi

Tathmini ya mahitaji na uchambuzi inaunga mkono uwezo wa jitihada za huduma za kibinadamu kukuza viwango wakati ikihifadhi ubora na kuhakikisha kuwa uwajibikaji kwa jamii zilizoathirika unazingatiwa. Hatua muhimu zinazoshauriwa kuchukuliwa ni:

- Kuhakikisha watu wenye ulemavu wanahusishwa katika kufanya tathmini ya mahitaji.
- Jumuisha angalau maswali matano yanayohusu kupata taarifa kuhusu ubora katika nyenzo zote za kufanyia tathmini.
- Changanua taarifa kwa jinsi, umri na ulemavu wakati wa kuchambua hatari za kuhusu masuala ya ulinzi au vikwazo vya ufikivu.
- Kuonesha maoni, vipaumbele na matakwa ya watu walioathirika na kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wamehusishwa katika kufanya zoezi la uchambuzi wa mahitaji.

Wakati huo huo, tumia tathmini ya mahitaji kutambua:

- Maandalizi ya utoaji wa usaidizi ambayo watu wenye ulemavu wanapendekeza (eneo, muda, n.k).
- Njia za mawasiliano ambazo watu wenye ulemavu wanapendekeza (ana kwa ana, kwa kutumia redio, ujumbe na nyinginezo).
- Sababu zingine zinaweza kushawishi mikakati ya afua stahiki (kuhusisha jinsia, ufikivu, ulinzi, sababu za kitamaduni na kiuchumi, n.k).

[73] Imechukuliwa kutoka IASC, *uwajibikaji kwa jamii zilizoathiriwa; Muhtasari*.



### Utekelezaji na ufuatiliaji

- Wasiliana, ajiri na toa mafunzo kwa watu wenye ulemavu ambao wanaweza kushiriki katika utekelezaji.
- Tengeneza utaalamu husika, viashiria vyenye ubora na vya kiuwajibikaji kwa ajili ya ufuatiliaji.
- Tengeneza mfumo wa kutoa maoni na kupokea malalamiko ambao utawahusisha watu wenye ulemavu na ambao unafikika.
- Mara kwa mara fuatilia kiwango ambacho watu wenye ulemavu kama kundi dogo la jamii la watu walioathirika, kama wanaridhika na ubora na ufanisi wa huduma za misaada ya kibinadamu.

### Ufuatiliaji na kutoa taarifa

- Ainisha utaalamu unaofaa na utendaji wa mfano, na uziweke katika muktadha wa huduma kipindi cha majanga, chagua mitazamo ambayo itahakikisha ujumuishi wa watu wote na kundi la watu wenye ulemavu.
- Fuatilia na kuza matumizi endelevu ya viwango vinavyokubalika kitaalamu na vyenye ubora.
- Kusanya na fanya uchambuzi na fanyia kazi taarifa zitokanazo na kazi za ufuatiliaji, ikiwemo maoni kutoka kwa watu wenye ulemavu.
- Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanashiriki katika kutoa huduma na ufuatiliaji.
- Kwa kuzingatia mrejesho, fanya marekebisho na maboresho katika afua, mikakati na mipango.

## Ulinzi dhidi ya unyonyaji wa kingono na dhuluma

Kushirikisha jamii ni suala la msingi katika kuhakikisha uwajibikaji kwa jamii zilizoathirika; hapa ndipo kazi kubwa ya ulinzi dhidi ya unyonywaji wa kingono na dhuluma hufanyika. Kazi ya kupunguza unyonywaji wa kingono[74]na dhuluma[75] katika muktadha wa huduma za kibinadamu hulenga vitendo vinavyofanywa na wafanyakazi katika masuala ya huduma za kibinadamu ambayo vinawadhuru watu walioathirika.

Unyonywaji wa kingono na dhuluma ni miongoni mwa mambo makubwa ambayo yanavunja misingi ya uwajibikaji. Mnamo mwaka 2015, kamati ya IASC ilitoa tamko rasmi juu ya azimio la kuzuia na kushughulikia suala la unyonywaji wa kingono unaofanywa na wafanyakazi katika huduma za kibinadamu. Watu wenye ulemavu hasa wanawake na wanaume wapo katika hatari kubwa na wanahitaji kulindwa kutokana na hali ya kutokuwa na ulinganifu wa kimadaraka baina ya wafanyakazi.

Ni muhimu kukuza uelewa wa watu wenye ulemavu katika jamii zao. Wanapaswa kutambua haki zao, vitu wanavyostahili, na wanapaswa kuwa na ufikivu katika mifumo yenye ufanisi ambayo wanaweza kufikisha malalamiko na kutoa taarifa ili kupata usaidizi na ulinzi. Wakati jitihada na miradi inatekeleza Sera za Ulinzi dhidi ya Unyanyasaji wa Kingono, zinapaswa kutumia mitazamo ya kina ambayo inazuia, inatoa suluhu, inaratibu na kusimamia ipasavyo.

## Rejea


- *Maazimio kuhusu uwajibikaji kwa watu walioathiriwa na kutoa ulinzi dhidi ya unyanyasaji na unyonjwaji wa kingono* (2015).
- *Kikosi kaazi cha ulinzi dhidi ya unyonywaji na unyanyaswaji wa kijinsia unaofanywa na wafanyakazi wetu*
- USAID, *Afua za Mabadiliko ya Kijamii na Kitabia*


[74] Unyonywaji wa kijinsia unahusisha 'matumizi mabaya ya nafasi kwa walio katika hatari, kutumia nguvu au kuaminiwa kwa ajili ya ngono. Angalia *jarida la Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kuhusu hatua maalum za kuwalinda kutoka unyanyasaji wa kijinsia na unyonywaji* (PSEA) (ST/SGB/2003/13).
[75] Unyanyasaji wa kijinsia unahusisha 'Kuingiliwa mwili au kutishiwa katika hali ya kingono'. *Ibid.*

# 8 Njia za kutoa huduma za kibinadamu[76]

Usaidizi na utoaji wa huduma za kibinadamu unahusisha uchambuzi na uridhiaji wa jitihada kadhaa, kama vile:

- Utoaji wa bidhaa kwa hisani.
- Usaidizi wa kifedha na vocha.
- Utoaji wa huduma moja kwa moja.
- Usaidizi wa kitaalamu.
- Kujenga uwezo.
- Vifaa na usimamizi wa ugavi.

Muunganiko wa jitihada mbalimbali zinazochaguliwa hubadilika kulingana na wakati. Ili kutambua jinsi huduma za kibinadamu zinavyoweza kutolewa kwa watu wenye ulemavu, ni muhimu kushauriana na watu wenye ulemavu pamoja na wale wanaowawakilisha.

Sura hii inajikita katika usaidizi wa fedha taslimu na vocha, kwa kutambua kuwa njia hii hutumika zaidi. Wasomaji wanatakiwa kufahamu kuwa sura hii haijajitosheleza peke yake. Mwongozo wake unafanya kazi katika nyanja zote na unapaswa kusomwa sambamba na sura nyingine.

## Afua za kifedha/usaidizi wa kifedha na vocha

Utafiti unaonesha kuwa, katika maeneo ya masoko, afua za kifedha zina uwezo wa kuwafikia watu wenye kuhitaji kwa haraka na kwa gharama nafuu kuliko aina zingine za usaidizi katika dharura. Hii inawawezesha watu kufanya uamuzi wa aina ya usaidizi na huduma kulingana na kanuni zilizothibitishwa na Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu, na wakati huo huo kudumisha uchumi wa ndani. Wadau wa masuala ya kibinadamu wanawekeza katika afua za kifedha kwa kiwango kikubwa na kwa uthabiti, wakiakisi maazimio yaliyowekwa katika majadiliano ya pamoja yaani "*Grand Bargain*" ambayo yalihusisha zaidi ya wafadhili wakubwa 30 na watoaji wa huduma za misaada.

Afua za kifedha ni moja ya mifumo ya usaidizi ambayo imekuwa ikitumika kwa miaka mingi katika nyanja ya hifadhi ya jamii jumuishi kwa watu wenye ulemavu, na mpango wa kunusuru kaya masikini katika mpango wa maendeleo. Wadau wa masuala ya utoaji wa huduma kibinadamu wanaweza kupata uzoefu wakati wanafanya jitihada za majaribio na kukuza usaidizi wa fedha wakati wa dharura.[77]

Hata hivyo, utoaji wa fedha tasilimu ni aina moja ya afua. Inaweza kusaidia au kusaidiwa na afua nyingine kama vile za utoaji wa usaidizi kwa hisani katika maeneo ya usambazaji au katika ngazi ya kaya.[78] Bado kuna pengo kubwa la ushahidi, pamoja na uelewa mdogo juu ya ahueni ambazo afua za kifedha zinaweza kuleta katika kulinda na kuwezesha

[76] Sura hii imechukuliwa kutoka katika *kitabu cha Sphere* (2018).

[77] UNICEF na Wizara Mambo ya Shirikisho na Maendeleo huko Nepal inatoa mfano. walianza mfumo kabambe wa usaidizi katika mwitikio wa janga la tetemeko mwaka 2015. Angalia ushirikiano wa mafunzo ya fedha, *Ripoti ya hai ya fedha ya dunia- programu ya uhamishaji wa fedha katika misaada ya kibinadamu* (2018), uk 114.

[78] Angalia vipengele vya kisekta kwa ajili ya taarifa kuhusu umuhimu wa usambazaji wa hiari.

watu wenye ulemavu katika muktadha wa huduma za kibinadamu au hatari ambazo watu wenye ulemavu wanaweza kukumbana nazo wakati wanajaribu kufikia afua hii.[79]

### Sheria na miundo mingine

- Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu. Kifungu namba 11, 12, 27 na 28 kipekee vinataja hatua za kibinadamu na zinaibua umuhimu wa ufikivu wa usaidizi wa kifedha.
- Majadiliano ya pamoja yaani "*Grand Bargain*"
- Ushirikiano wa mafunzo ya fedha, *muundo wa kuchochea vitendo wa kimatai, muhtasari wa maazimio kuhusu mipango ya uhamishaji wa fedha*.

## Dhana muhimu[80]

Maneno kama uhawilishaji fedha taslimu, afua za kifedha, programu za uhawilishaji fedha, usaidizi wa kifedha, misaada ya kifedha na usaidizi wa vocha zenye fedha yanatumika kwa kubadilishana katika kutambulisha programu zote (za malazi, chakula, afya, n.k) ambazo zinatoa fedha au vocha kwa wanufaika na kuwawezesha kununua bidhaa au kupata huduma moja kwa moja. Katika muktadha wa kibinadamu, fedha tasilimu au vocha zenye fedha zinaweza kutolewa kwa watu binafsi, kaya au jamii. Programu kama hizi hazihusishi shughuli za kifedha au usaidizi kwa serikali au mashirika wakati wa kutoa afua za kibinadamu.

## Viwango na miongozo rejea

- *Ushirikiano wa mafunzo ya fedha*
- *Zana bora za usaidizi wa kifedha*
- *Viwango vya chini vya tathmini ya masoko*
- Shirika la Help Age, CBM, Hndicap International, *viwango vya ujumuishi wa masuala ya kibinadamu kwa wazee na watu wenye ulemavu* (2018).

## Mambo muhimu ya kufanya

Hatua za lazima zinapaswa kufanyika katika awamu zote wakati wa kutekeleza programu jumuishi za utoaji fedha kwa watu wenye ulemavu.

### Ushiriki

- Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanawakilishwa katika mifumo na michakato rasmi na isiyo rasmi. Zingatia aina mbalimbali za ulemavu pamoja na umri, jinsi na anuwai. Tafuta kwa upekee kukuza ushiriki wa makundi ya watu wenye ulemavu ambayo yana uwakilishi mdogo ikiwemo watu wenye ulemavu wa akili, watu wenye asili ya eneo hilo, wanawake na wasichana.
- Shauriana na watu wenye ulemavu wa umri na jinsi mbalimbali kuhusu namna wanaweza kupata fedha, na njia wanayopendelea kuzifikia fedha, namna wanavyofikia masoko na huduma na mahitaji wanayohitaji. Hakikisha kuwa gharama zinazohusianisha na kuwawezesha kushiriki zinajumuishwa katika bajeti.
- Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu, familia zao na mashirika ya watu wenye ulemavu yamehusishwa kikamilifu katika kuainisha vikwazo na katika kupanga, kubuni na kutekeleza, kufuatilia na kutathmini afua za kifedha. Zingatia atari za ulinzi, mifumo ya kuziondoa na faida zinazopatikana katika kila hatua.
- Ainisha matakwa ya wanufaika wenye ulemavu kwa kuzingatia thamani, mzunguko na muda wa uhawilishaji wa fedha.
- Tengeneza ushirikiano na mashirika ya watu wenye ulemavu pamoja na mashirika mengine yanayotoa afua za kifedha. Mashirikiano yanaweza kusaidia watu wenye ulemavu katika kutumia programu za uhawilishaji wa fedha, pamoja na kutetea na kukuza huduma jumuishi na usaidizi.

### Kubainisha vikwazo

- Ainisha tabia za wafanyakazi ambao wanawabagua watu wenye ulemavu (ambao wanapendekeza, kwa mfano watu wenye ulemavu hawana uwezo wa kuzifikia na kusimamia fedha, au kushiriki katika kazi ya kuratibu fedha, shughuli za kiuchumi au program za kukuza ujuzi).
- Zingatia mahitaji mbalimbali ya ufikivu kwa watu wenye ulemavu. Zingatia wale wanaoishi maeneo ya vijijini na wale wanaoishi mijini, wenye aina mbalimbali za changamoto za ufikivu wa kifedha na kiteknolojia, vikwazo vya kimazingira na kitaarifa (kwa mfano umbali kutoka eneo moja mpaka lingine, upatikanaji na gharama za usafiri unaofikika).
- Tathmini aina mbalimbali za utoaji wa fedha unaofikika (fedha taslimu, fedha kwa njia ya kuponi au kwa njia ya simu, n.k).
- Zingatia kuwa baadhi ya aina za uhawilishaji wa fedha (kama vile fedha zilizozuiliwa) zinaweza kupunguza ufikivu katika vifaa saidizi ambavyo vinatambuliwa kama gharama zihusianazo na masuala ya kiafya).

### Kusaidia na Kujenga uwezo

- Kabla ya afua yoyote, tathmini sera na michakato ya afua za kifedha; uwezo wa mashirika yanayotoa afua za kifedha na uwezo wa wafanyakazi katika kubuni na kutekeleza afua za kifedha ambazo zinawajumuisha watu wenye ulemavu.
- Toa msaada na mafunzo kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kufikia usaidizi wa kifedha na kutumia mfumo wa usambazaji wa fedha kama vile benki. Toa elimu ya msingi na elimu ya usimamizi wa fedha pale ambapo teknolojia itakayo tumia haifahamiki kwa walengwa.

### Ukusanyaji wa taarifa na ufuatiliaji

- Fuatilia kama watu wenye ulemavu wana ufikivu sawa wa fedha na vocha katika kaya zao na kama wana uwezo wa kuzitumia.
- Fuatilia kama watu wenye ulemavu wanapatwa na unyonyaji na dhuluma katika muktadha wa jitihada za programu za uhawilishaji fedha au kama wanakabiliana na vikwazo wakati wanatafuta kuvifikia au kutumia fedha.
- Kusanya ushahidi na shirikisha wengine kwenye mafunzo yaliyopatikana kuhusu mbinu zinazofanya kazi. Je, ni jitihada gani zilizoongeza ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika afua za kifedha?

[79] Ushirikiano wa mafunzo ya fedha, *kama harakati za uhamishaji wa programu za fedha, namna gani tunaweza watu wenye ulemavu hawabaki nyuma katika programu za uhamishaji wa fedha wakati wa dharura* (2015). Shirika la Wakimbizi duniani (UNHCR) na shirika la mpango wa chakula (WFP), *Kuondoa hatari za matumizi mabaya ya madaraka katika usaidizi wa kifedha katika Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo* (2018).

[80] Kwa taarifa zaidi angalia Ushirikiano wa mafunzo ya fedha, *istilahi za jumla kwa ajili ya usaidizi wa Fedha na vocha* (2017).

**Mchoro namba 5 |** Vikwazo vya ufikivu na ujumuishi katika afua za kifedha

### NAMNA ATHARI ZA MAJANGA ZINAVYOONGEZEKA KWA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA AFUA ZA KIFEDHA

**ATHARI ZA MAJANGA**

Kudorora kwa uchumi, ukosefu wa usalama, kuharibika kwa mitandao ya kijamii, miundombinu, kuhamishwa na kufungwa kwa huduma.

**KUONGEZEKA KWA VIKWAZO**

**Vikwazo vya kimazingira:**

- Ukosefu wa taarifa fikivu juu ya taratibu za usajili na mifumo ya upokeaji wa fedha
- Ukosefu wa teknolojia fikivu ya uhawilishaji wa fedha kupitia simu au kadi za mashine za kutolea fedha
- Kutofikika kwa vituo vya kusambaza vocha
- Kutofikika kwa maduka au masoko yanayopokea vocha
- Ukosefu wa usafiri unaofikika

**Vikwazo vya kimtizamo:**

- Mitazamo na maarifa ya wafanyakazi juu ya watu wenye ulemavu

**Vikwazo vya kitaasisi:**

- Ukosefu wa uwezo wa kitaalamu katika kuweka mifumo jumuishi ya kupima masuala ya ulemavu yanayolenga usaidizi
- Ukosefu wa viwango, miongozo, na sera zinazozingatia watu wenye ulemavu
- Utawala wenye urasimu na usiofikika pamoja na ugumu wa taratibu za usajili

**Hatari zinazowakumba watu wenye ulemavu**

Ukatili, umaskini, hatari za kimazingira, kudorora kwa afya, kutengwa, kujitenga, kutelekezwa



Mwongozo hapo chini utasaidia wadau wa huduma za kibinadamu na kushughulikia vikwazo ambavyo watu wenye ulemavu (pamoja na wale wanaowasaidia) wanaweza kukumbana navyo wakiwa watafuta programu za kibinadamu za uhawilishaji wa fedha.

**UKONDOISHWAJI/UJUMUISHWAJI**

Andaa programu za afua za kifedha ambazo ni jumuishi kwa wote ikiwepo watu wenye ulemavu na weka miundombinu fikivu na mpangilio wa mawasilliano.

**WALENGWA**

Toa elimu ya fedha kwa watu wenye ulemavu ambao wamekuwa wakitengwa kutoka katika mfumo wa elimu.

## Hatua zinazoshauriwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na mipango** | | | |
| Wafundishe wafanyakazi kubaini vikwazo na hatari za ulinzi zinazohusiana na afua za kifedha ambazo watu wenye ulemavu wanakumbana nazo. | X | | |
| Ainisha programu za uhifadhi wa jamii zilizopo na tathmini ufikivu wa taratibu na michakato ya kiutawala. Tathmini kama wataweza kuhimili kama programu za huduma za kibinadamu zitakuzwa. Rekebisha malengo ya programu na weka mpango wa kushughulikia vikwazo kiutawala. | X | | |
| Ainisha vikwazo katika ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika afua za kifedha (kwa mfano, kutofikika kwa maeneo ya masoko). | X | X | X |
| Ainisha wadau ambao wanafanya kazi na watu wenye ulemavu; tengeneza ushirikiano mpya na fanya kazi na mashirika ya watu wenye ulemavu, pamoja na viongozi wa watu wenye ulemavu katika kutambua na kuondoa vikwazo na hatari ambazo watu wenye ulemavu wanakabiliana navyo. | X | | |
| Tathmini kiwango ambacho masoko yanafikika kwa watu wenye ulemavu na unafuu ambao watu wenye ulemavu wanaweza kupata katika kupata taarifa za masoko. | X | X | X |
| Fanya uchambuzi wa mifumo ya masoko na huduma ambazo zinaweza kusaidia katika kuwalinda watu wenye ulemavu. Zingatia huduma mbadala za afya, vifaa saidizi, huduma za kisheria, usafiri fikivu na elimu. Tathmini namna watu wenye uelamvu kwa sasa wanafikia huduma hizi pamoja na vikwazo wanavyokabiliana navyo. | X | | X |
| Zingatia gharama na hatari ambazo watu wenye ulemavu wanaweza kukumbana nazo iwapo wanaweza kutegemea wawakilishi/mtu wa kati katika kuchukua na kugawa bidhaa. | X | | X |
| Tathmini namna fedha zinavyoweza kutumika katika kuondoa vikwazo pamoja na kuimarisha ustahimilivu wa kaya zenye watu wenye ulemavu. | X | X | X |

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Weka mpango ambao wadau wa masoko wanaweza kusaidiwa katika kufanya masoko na huduma kuwa na ufikivu zaidi kwa watu wenye ulemavu (kwa mfano kuboresha ufikivu wa maeneo au mawasiliano).[81] | X | | |
| Tathimini kiwango ambacho afua za kifedha na za kiteknolojia zinafikika kwa watu wenye ulemavu. | X | | X |
| Zingatia gharama nyingine zinazohusu ulemavu, ikiwemo gharama za ziada za kaya zikiwemo zenye watu wenye ulemavu ambazo hugharimia wanapofuata fedha (gharama za usafiri, vifaa na vifaa saidizi, n.k). | X | | X |
| Toa taarifa sahihi katika mifumo fikivu na katika lugha rahisi na ya kueleweka wakati wa kutoa afua za kifedha, muda wa afua hizo na programu mbadala zilizopo. | X | X | X |
| Hakikisha kuwa taasisi za kifedha zimeandaliwa kuhakikisha kuwa afua za kifedha zinafikika kwa watu wenye ulemavu. Hakikisha wanakubali kufanya tathmini kuhusu hali halisi na mazingira magumu. | X | | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Tathmini iwapo programu za uhifadhi wa jamii kwa watu wenye ulemavu zinaweza kutumika kama mifumo ya utoaji afua. | X | X | |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Hakikisha kuwa watu wote walioathirika wana fursa sawa za kufikia programu za malipo ya fedha taslimu, kwa kufanya kazi na kuwa wanalipwa kiasi sawa na thamani ya kazi waliyofanya. Usielekeze watu wenye ulemavu kufanya kazi ya malipo kidogo kwa kigezo cha ulemavu wao. | | | X |
| Hakikisha kuwa mazingira na hali ya kazi kuhusu program ya malipo ya kazi kwa pesa na programu ya malipo ya kazi kwa chakula zinawafikia watu wenye ulemavu. | X | | X |
| Chagua maeneo ya usambazaji ambayo ni salama na yanayofikika kwa watu wenye ulemavu. | X | X | |
| Zingatia kuweka magulio au masoko yanayotembea katika maeneo ya vijijini au sehemu ambazo ni ngumu kufikika, ili watu wenye ulemavu waweze kushiriki. | | | X |
| Tathmini iwapo kumtaja mtu mwenye ulemavu kama mnufaika aliyesajiliwa kunaweza kumuweka katika hatari. | | | X |
| Elezea kwa usahihi dhumuni la usaidizi. Kwa kufanya hivyo kuondoa ubaguzi, mila potofu na husuda zinazoweza kuwakumba wanufaika wenye ulemavu. | X | X | X |
| Zingatia mifumo mbadala kama vile programu za kufikia watu au huduma za nyumba kwa nyumba ambazo zinaruhusu watu wenye ulemavu katika kupata usaidizi wao wenyewe, moja kwa moja. | X | X | X |

[81] Angalia ushirikiano wa mafunzo ya fedha na Huduma za Katoliki za kufariji, usaidizi wa afua za masoko katika muktadha wa kibinadamu- angalia chapisho la dondoo (2018).





| | Preparedness | Response | Recovery |
|---|---|---|---|
| **4. Uratibu** | | | |
| Husisha watu wenye ulemavu katika kulinda na katika juhudi za kuratibu masuala ya kifedha, kwa mfano, watu wenye ulemavu wawe katika makundi ya ulinzi na makundi yanayoshughulikia masuala ya fedha. | X | X | X |
| Ungana na programu za kitaifa na mifumo ambayo inatoa huduma za uhamishaji wa fedha kwa watu wenye ulemavu. | X | | |
| Fanya uratibu na sekta zingine katika kuhakikisha kuwa afua za kifedha zinawawezesha watu wenye ulemavu kuzifikia huduma zingine za kibinadamu (kama vile maeneo rafiki kwa watoto au elimu ). | X | X | X |
| **5. Tathmini na ufuatiliaji** | | | |
| Mara kwa mara kusanya maoni kutoka kwa watu wenye ulemavu wa umri tofauti na jinsi, kuhusu vikwazo na hatari wanazokabiliana nazo wakati wa kizifikia huduma za uhawilishaji wa fedha. | | X | X |
| Wakati wa kufanya ufuatiliaji baada ya usambazaji, shauriana na watu wenye ulemavu katika kuainisha vikwazo wanavyokumbana navyo wakati wanafikia mfumo wa usajili wa wanuafaika. | | | X |
| Fanya ukaguzi wa ufikivu wa mifumo ya utoaji wa huduma na mifumo ya maoni na malalamiko. | | | X |
| Fanya ukaguzi wa ufikivu wa masoko na toa mapendekezo ya maboresho kufanya maeneo hayo kuwa fikivu. | | | X |
| Fanya uchambuzi wa taarifa kwa kigezo cha jinsia, umri na ulemavu, tumia nyenzo zilizokubalika katika muktadha wa kibinadamu kama vile maswali ya kundi la Washington. | | | X |
| Tumia mifumo fikivu na taratibu za kuwawezesha watu wenye ulemavu kuridhia ili kutumia taarifa zinazowahusu. Hakikisha kuwa wanafahamu namna taarifa hizi zitatumiwa na nani (kwa mfano mashirika ya kibinadamu, serikali, n.k). | | | X |

## Rejea


- Ushirikiano wa Mafunzo ya Fedha
- Shirika la CBM, *zana za kazi kuhusu huduma za kibinadamu za CBM*[82]
- Ushirikiano wa mafunzo ya fedha, zana bora za usaidizi wa fedha
- Mkataba wa kuondoa aina zote za unyanyapaa dhidi ya wanawake, kifungu namba 11 na namba 14
- Ushirikiano wa mafunzo ya fedha, utafiti wa fedha salama na zana muhimu
- Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi na mwongozo wa kulinda afua za kifedha
- Tume ya wakimbizi wanawake na vikose vya huruma, urasimishaji wa uzingatiaji wa ukatili wa kijinsia katika afua za kifedha na kutumia fedha katika kutoa huduma dhidi ya ukatili wa kijinsia. Zana kwa ajili ya kuongeza afua za kifedha kwa ajili ya ulinzi kutokana na ukatili wa kijinsia
- Tume ya wakimbizi wanawake, kikundi kuhusu riziki na tathmini ya hatari


[82] Programu ya Kumbukumbu na mafunzo kwa wafanyakazi wa misaada ya kibinadamu.

# 9 Wajibu na majukumu ya wadau

Jedwali lifuatalo linaainisha wajibu na majukumu ya makundi mbalimbali ya wadau katika kipindi chote cha mzunguko wa programu za kibinadamu, katika kusaidia watu wenye ulemavu pamoja na wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu, na kuhakikisha wanajumuishwa na kushiriki katika jitihada za masuala ya kibinadamu.

## Serikali

| | |
|---|---|
| **Kujiweka tayari** | • Hakikisha kuwa mpango wa dharura unazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu na kwamba mipango ni jumuishi na fikivu. Kwa mfano toa mafunzo kukuza uelewa wa sheria zinazohusika; anzisha mawasiliano fikivu, mfumo wa kupokea maoni na malalamiko, na kuhamasisha ukusanyaji na matumizi ya taarifa kwa kutumia nyenzo zilizojaribiwa katika muktadha wa huduma za kibinadamu kama vile *maswali ya kundi la Washington*.<br>• Zingatia ushiriki wa mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo yanawakilisha anuwai za watu wenye ulemavu. Wahusishe katika kutengeneza na kupitia sera za kupunguza hatari ya majanga, sera nyinginezo za masuala ya kibinadamu, sheria, mipango ya kitaifa na programu pamoja na michakato. Hakikisha kuwa miundo ya kisheria inasaidia katika ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika jitihada za huduma za kibinadamu.<br>• Hakikisha kuwa mifumo ya kitaifa ambayo inatoa huduma (utengamao, elimu, afya usaidizi wa makundi rika, n.k), ina uwezo wa kuchukua hatua iwapo mzunguko wa watu wengi utatokea. Ainisha rasilimali zilizopo kuhusu masuala ya ulemavu katika ngazi za chini (wakalimani, wataalamu wa masuala ya ujumuishi, watoa huduma) pamoja na kuanzisha kitabu cha kumbukumbu.<br>• Kwa kushauriana na mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo yanawakilisha anuwai za watu wenye ulemavu, teua wawakilishi wa watu wenye ulemavu ili kushauriana na timu za kitaifa za masuala ya huduma za kibinadamu na timu za uratibu kwa niaba ya taasisi za serikali. |
| **Tathmini ya mahitaji na uchambuzi** | • Wawezeshe wadau wa masuala ya kibinadamu kuzifikia taarifa au takwimu za watu wenye ulemavu kwa ajili ya aina zote za tathmini (tathmini za haraka za mahitaji, *tathmini za mwanzo* na *tathmini baada ya majanga*). Tathmini ubora wa taarifa zinazohusu jamii ya watu wenye ulemavu.<br>• Hu sisha mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo yanawakilisha anuwai za watu wenye ulemavu na watoa huduma kwa watu wenye ulemavu, katika kupanga na katika utekelezaji wa shughuli za ukusanyaji taarifa; kusanya na toa taarifa juu ya vikwazo na viwezeshi; hamasisha matumizi ya nyenzo za ukusanyaji taarifa zilizojaribiwa katika muktadha wa huduma za kibinadamu kama vile *maswali ya kundi la Washington* (angalia kipengele cha usimamizi wa taarifa). |

| | |
|---|---|
| **Kupanga mkakati wa jitihada za kuchukua hatua/kutoa huduma** | • Husisha mashirika ya watu wenye ulemavu katika kupanga mipango.<br>• Chukua hatua na hakikisha kuwa jitihada zinazochukuliwa zinajumuisha watu wenye ulemavu na kutumia mtazamo unaozingatia haki za binadamu zinazoendana na sheria za kitaifa, mikataba ya kikanda na kimataifa. |
| **Ugemaji rasilimali** | • Gema rasilimali kutoka katika bajeti za kitaifa na kimataifa (mashirika ya watu wenye ulemavu, watoa huduma, mifuko ya fedha). Hakikisha kuwa ujumuishi wa watu wenye ulemavu unahusisha wakimbizi na wengine kama vile watu wenye ulemavu waliohamishwa; hakikisha wanapata msaada na kulindwa katika hatua zote za programu za masuala ya kibinadamu. |
| **Ufuatiliaji na utekelezaji** | • Pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo yanawakilisha anuwai za watu wenye ulemavu, fuatilia kiwango ambacho watu wote wenye ulemavu wanaweza kufikia huduma za misaada na kulindwa.<br>• Hakikisha kuwa usaidizi na huduma zinatolewa na serikali pamoja na wadau wengine wa masuala ya kibinadamu zinafikika kwa watu wenye ulemavu.<br>• Wezesha huduma za hifadhi ya jamii kuchukua jukumu la kuwa na mifumo ya kuwezesha huduma za kibinadamu. Anzisha na wezesha ufikivu[83] katika kutumia huduma za hifadhi ya jamii pale inapoanza kutumika kama mifumo ya kuwezesha huduma za kibinadamu. |
| **Tathmini** | • Fanya tathmini ya papo kwa hapo ili kufahamu kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanaweza kufikia huduma za kibinadamu na kulindwa, kwa lengo la kuboresha ujumuishi wao.<br>• Hakikisha kuwa thathmini zote zinahusisha kigezo ambacho kinachunguza suala la fursa sawa, ushiriki na kulindwa kwa watu wenye ulemavu.<br>• Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanashiriki katika tathmini za kisekta na zile za muingiliano wa sekta tofauti. |
| **Uratibu** | • Alika mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo yanawakilisha anuwai za watu wenye ulemavu, na watoa huduma binafsi na wa serikali ili waweze kufanya kazi pamoja na wadau wa masuala ya kibinadamu na kushirikiana na kupeana taarifa.<br>• Kwa mpangilio maalum, hakikisha ajenda za vikao na taratibu za kutoa taarifa zinahusisha masuala ya watu wenye ulemavu. |
| **Usimamizi wa habari** | • Toa taarifa rasmi kuhusu watu wenye ulemavu ikiwemo taarifa kuhusu vikwazo, hatari, huduma zilizopo na mafunzo.<br>• Tengeneza, tekeleza, tumia sheria katika kuimarisha usimamizi fikivu wa taarifa wakati wa dharura. Muundo wa kisheria wa kulinda taarifa unapaswa kuweka wazi masuala yanayohusu ukusanyaji wa taarifa, usambazaji sahihi wa taarifa na ufikivu wa taarifa.[84] |

[83] Kwa mfano rahisisha taratibu za kupata utambulisho wa ulemavu, katika kufikia mifumo ya, malipo, n.k.

[84] Angalia ICRC, *viwango vya kitaalamu vya kazi ya ulinzi iliyofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na wadau wa haki za kibinadamu katika migogoro ya kivita na hali zingine za vurugu* (2018), Sura ya 6, usimamizi wa data na taarifa za matokeo ya ulinzi, uk. 106–148; na CRPD, Ibara ya 22(2).





## Uongozi katika huduma huduma za kibinadamu (Mratibu mkazi, timu za kitaifa za masuala ya kibinadamu)[85]

**Katika kipengele hiki angalia**–*Mwongozo wa kuimarisha ujumuishi katika mipango ya jitihada za huduma za kibinadamu*.

| | |
|---|---|
| **Kujiandaa na kujiweka tayari** | • Weka masuala ya ujumuishi katika *hadidu za rejea za timu za kitaifa kuhusu masuala ya kibinadamu*.<br>• Himiza serikali kuteua wawakilishi husika wa kuangazia masuala ya wenye ulemavu kwa ajili ya timu za kitaifa kuhusu masuala ya kibinadamu.<br>• Hakikisha kuwa mipango yote ya kujiweka tayari na jinsi ya kuyafanyia kazi masuala ya dharura ni jumuishi kwa watu wenye ulemavu. Himiza miongozo ya IASC katika ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika masuala ya huduma za kibinadamu, hakikisha kuwa mashirika ya watu wenye ulemavu wanashiriki katika hatua zote muhimu; jenga uwezo kuhusu masuala ya ulemavu katika timu za kitaifa kuhusu masuala ya kibinadamu. |
| **Tathmini ya mahitaji na uchambuzi** | • Hakikisha kuwa taratibu za tathmini ya mahitaji zinakadiria ukubwa wa mahitaji kwa namna inayozingatia athari za hali za watu wenye ulemavu na familia zao.<br>• Hakikisha kuwa tathmini ya mahitaji ya sekta mbalimbali yanazingatia mahitaji, hatari, ujuzi, uwezo na maoni na mitazamo ya watu wenye ulemavu.<br>• Zingatia kuwa taarifa zote zinazokusanywa wakati wa tathmini ya mahitaji ya sekta mbalimbali zinachambuliwa kwa kuzingatia masuala ya jinsi, umri na ulemavu (kwa kutumia nyenzo za kukusanya taarifa zilizojaribiwa katika muktadha wa huduma za kibinadamu, kama vile *maswali ya kundi la Washington*. |
| **Kupanga mkakati wa jitihada za kuchukua/kutoa huduma** | • Ingiza masuala ya ulemavu katika mikakati na muundo wa matokeo tarajiwa ya jitihada zinazochukuliwa; hakikisha namna ya kutoa taarifa inaakisi aina anuwai za watu wenye ulemavu.<br>• Hakikisha kuwa mipango yote ya kimkakati ya jitihada za kibinadamu zitakazochukuliwa (mpango wa huduma za kibinadamu, mpango wa huduma za haraka, n.k), unahusisha watu wenye ulemavu walio katika uhitaji.<br>• Eleza katika mpango, namna ambavyo huduma zitakazotolewa zitakavyopunguza kuongeza kwa hatari kwa watu wenye ulemavu. |
| **Ugemaji rasilimali** | • Himiza wafadhili kutenga rasilimali kwa ajili ya watu wenye ulemavu pamoja na kufanya huduma na jitihada zao kuwa jumuishi.<br>• Kuweka vigezo vya ujumuishi kwa watu wenye ulemavu kwa ajili ya rufaa, fedha za dharura, fedha zilizotengwa katika nchi na fedha zingine za dharura.<br>• Hakikisha kuwa wapangaji wa bajeti wanapata mafunzo kuhusu masuala ya ujumuishi. Hakikisha kuwa rasilimali za kutosha zinatengwa katika kuboresha ufikivu na kufanya marekebisho stahiki. |

[85] Angalia pia Umoja wa Mataifa, *mkakati wa ujumuishi wa ulemavu* (2019) ambayo inaweka matarajio mahususi kwa viongozi wa mashirika ya Umoja wa Mataifa.

| | |
|---|---|
| **Utekelezaji na ufuatiliaji** | • Hakikisha ujumuishi na ulinzi kwa watu wenye ulemavu katika agenda za vikao vya kamati za ndani ya nchi.<br>• Hakikisha kuwa nyenzo za ufuatiliaji zinatatua changamoto za watu wenye ulemavu; kama vile masuala ya ufikivu, hatari na usimamizi wa majanga, mahitaji mahsusi, maoni na mitazamo. Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanashiriki katika ufuatiliaji, kufanya tathmini ya mahitaji, jitihada na huduma zote katika upana wake. |
| **Tathmini** | • Himiza sekta na sehemu zote kujumuisha masuala ya ujumuishaji wa watu wenye ulemavu (kulindwa, usalama na fursa sawa) katika tathmini zao.<br>• Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanashiriki katika tathmini za kisekta na zile za ndani ya sekta.<br>• Hakikisha matokeo ya tathimini katika mifumo fikivu. Hakikisha kuwa sekta zote zinatumia matokeo ya tathmini walizofanya wakati wanaweka mipango ya programu zao au wanapofanya marekebisho katika programu zao. |
| **Uratibu** | • Hakikisha kuwa wawakilishi wa watu wenye ulemavu au pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu wanahusika katika vikao husika.<br>• Kuza ukondoishwaji wa watu wenye ulemavu katika kila hatua ya huduma za kibinadamu (nyenzo, viwango) kwa kutumia mwongozo huu. |
| **Usimamizi wa taarifa**[86] | • Fanya makubaliano, ikiwemo na serikali, kuhusu mifumo ya ukusanyaji na usambazaji wa taarifa kuhusu watu wenye ulemavu, sambamba na maadili ya taarifa na misingi ya ulinzi.[87]<br>• Toataarifa kuhusu watu wenye ulemavu, pale ambapo taarifa hazipatikana, toa taarifa kuwa 'hakuna taarifa'.<br>• Hakikisha kuwa taarifa zote zinazokusanywa, zinaainishwa na kuchambuliwa kwa kigezo cha jinsia, umri na hali ya ulemavu. |

[86] Usimamizi wa taarifa unahusisha ukusanyaji, tathmini na usimamizi wa takwimu na taarifa katika mzunguko wa programu za kibinadamu.

[87] Angalia ICRC, *viwango vya kitaalamu kwa kazi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na haki za binadamu katika hali za vurugu* (2018), sura ya 6, usimamizi wa data na taarifa za matokeo ya ulinzi uk. 106–148; na CRPD, *Ibara 22(2)*.





## *Viongozi wa vitengo* na sekta[88]

Katika kipengele hiki rejea sera ya Kamati ya IASC kuhusu uwajibikaji kwa jamii iliyoathiriwa.[89]

| | |
|---|---|
| **Kujiandaa na kujiweka tayari** | • Husisha mashirika ya watu wenye ulemavu ya kitaifa na kimataifa katika vitengo na sekta na tafuta ushauri kuhusu mbinu nzuri na changamoto husika.<br>• Teua mwakilishi wa watu wenye ulemavu katika kila kitengo.<br>• Ainisha hatari za kiusalama na kiulinzi na huduma jumuishi zinazopatikana katika kila sekta. Tathmini uwezo wa watu wenye ulemavu na hakikisha kuwa wanahusishwa katika mipango mahsusi ya kisekta ya dharura. Hakikisha mipango ya dharura inajumuisha uwepo wa vifaa saidizi (kama vile viti mwendo, magongo, fimbo nyeupe, vifaa ya kusaidia kusikia, mifumo ya usaidizi wa makundi rika) katika kubadili zile ambazo zitakuwa zimeharibika.<br>• Hakikisha mipango ya dharura inaweka mifumo ya mawasiliano ambayo ipo wazi ikiwemo, mifumo ya kutoa tahadhari za awali, na mfumo wa kutoa maoni, mrejesho na huduma jumuishi. Mpangilio wa mawasiliano unapaswa kuzingatia mahitaji ya mawasiliano kwa watu wenye ulemavu na unapaswa kuwa fikivu. |
| **Tathmini ya mahitaji na uchambuzi** | • Hakikisha kuwa mchakato wa tathmini ya mahitaji inakadiria ukubwa wa mahitaji na kuzingatia athari za hali ya watu wenye ulemavu na familia zao.<br>• Hakikisha kuwa tathmini za mahitaji ya kisekta zinazingatia mahitaji, hatari, ujuzi, uwezo, maoni na mitazamo ya watu wenye ulemavu.<br>• Hakikisha kuwa tathmini ya mahitaji inatambua watu wenye ulemavu na mahitaji yao. Wakati taarifa za msingi zinapokusanywa zizingatie kutumia nyenzo zilizojaribiwa katika muktadha wa kibinadamu kama vile *maswali ya Washington*.<br>• Shauriana na jamii zilizoathiriwa wakiwemo watu wenye ulemavu. Tenga asilimia 15 hadi 20 ya muda wa kutoa ushauri pamoja na rasilimali kwa ajili ya watu wenye ulemavu. |
| **Kupanga mkakati wa jitihada za kuchukua/kutoa huduma** | • Husisha mashirika ya watu wenye ulemavu yanayowakilisha anuwai za watu wenye ulemavu katika mchakato wa kupanga jitihada za huduma za kibinadamu. Jumuisha uchambuzi wa taarifa zinazohusiana na watu wenye ulemavu.<br>• Anzisha na tumia viashiria sahihi vya kupima ujumuishi wa watu wenye ulemavu, tumia mapendekezo ya mwongozo huu.<br>• Bunimtazamo pacha na mkakati wa huduma stahiki, ikiwemo viwango vya utaratibu wa uendeshaji kwa kuzingatia Mwongozo wa kisekta na viwango vya ujumuishi wa watu wenye ulemavu. Mpango na mkakati unatakiwa kuzingatia muingiliano wa masuala ya jinsia, umri, ulemavu pamoja na sababu zingine anuwai. |

[88] Angalia Umoja wa Mataifa, *mkakati wa ujumuishi wa ulemavu* (2019) unaoweka matarajio maalum kwa viongozi wa mashirika ya Umoja wa Mataifa.

[89] Kikosi kazi cha IASC katika AAP. Sekta ya ulinzi wa kidunia na OCHA. *Mapendekezo ya hatua za uratibu wa makundi wa sekta katika kuimarisha uwajibikaji kwa jamii zilizoathiriwa na ulinzi katika masuala ya programu za kibinadamu* (2016).

| | |
|---|---|
| **Ugemaji rasilimali** | • Hakikisha kuwa bajeti zote za kisekta na mahitaji ya kifedha yanatenga kiwango cha kutosha ili kupata programu jumuishi. Zingatia msingi wa usanifishaji kwa wote katika majengo ya zamani au majengo mapya, fanya marekebisho katika majengo yaliyopo na marekebisho stahiki, weka mifumo ya kufikia walengwa wa mbali, wakalimani, n.k). Wakati wa kupanga bajeti, pata ushauri kutoka katika mashirika ya watu wenye ulemavu na watu wanaoshughulikia watu wenye ulemavu.<br>• Husisha mashirika ya watu wenye ulemavu yanayowakilisha anuwai za watu wenye ulemavu katika kamati za kupitia miradi iliyochaguliwa (kwa mfano, fedha za masuala ya dharura na fedha za jumla) ili kuhakikisha kuwa mapendekezo yanahusisha na kuelezea mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa utoshelevu na kwa usahihi. |
| **Utekelezaji na ufuatiliaji** | • Fuatilia na toa taarifa juu ya kiwango ambacho watu wenye ulemavu watafikiwa na usaidizi husika na kulindwa. Hakikisha taarifa zinachambuliwa kwa kuzingatia jinsia, umri na ulemavu.<br>• Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanajumuishwa katika kutoa taarifa za vitengo.<br>• Kwa kushirikiana na mashirika ya watu wenye ulemavu, kuza na sambaza jumbe za utetezi wa haki na ulinzi kwa watu wenye ulemavu walioathirika na majanga. |
| **Tathmini** | • Andaa tathmini za sekta na shiriki katika tathmini za sekta mbalimbali zinazopima ujumuishi wa watu wenye ulemavu.<br>• Jumuisha wawakilishi wa watu wenye ulemavu, vikosi kazi kwa ajili ya masuala ya ulemavu, na mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo yanawakilisha anuwai ya watu wenye ulemavu katika mchakato wa kufanya tathmini. |
| **Uratibu** | • Hakikisha kuwa sekta na vitengo vinasawazisha kazi wanazozifanya ili kuhakikisha programu zinajumuisha masuala ya ulemavu.<br>• Himiza mashirika ya watu wenye ulemavu, mashirika yanayojihusisha na watu wenye ulemavu na watoa huduma kushiriki katika mikutano ya vitengo. Hakikisha kuwa mikutano inafanyika katika maeneo fikivu, fanya marekebisho stahiki pale yanapohitajika.<br>• Ratibu ukuaji wa mifumo jumuishi katika vitengo, kwa ajili ya rufaa na kufuatilia ufikivu kwa watu wenye ulemavu. |
| **Usimamizi wa taarifa**[90] | • Hakikisha kuwa mfumo wa usimamizi wa taarifa unahusisha taarifa juu ya kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanapata huduma stahiki na ulinzi na kushiriki katika shughuli ambazo ni muhimu kwao.<br>• Hakikisha kuwa taarifa zinazokusanywa kuhusu watu wenye ulemavu ni za kuaminika na si za muda mrefu, na tambua mifano ya utendaji na mifano mizuri inayohusu usaidizi na ushiriki wa watu wenye ulemavu. Sambaza katika vitengo kwa kupitia mifumo fikivu. Zingatia maadili na mifumo ya kulinda taarifa.[91] |

[90] Usimamizi wa taarifa unahusisha ukusanyaji, uchambuzi na usimamizi wa takwimu na taarifa katika mzunguko wa programu za kibinadmu.

[91] Angalia ICRC, *viwango vya kitaalamu kwa kazi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na haki za binadamu katika hali za vurugu* (2018), sura ya 6, usimamizi wa data na taarifa za matokeo ya ulinzi uk. 106–148; na CRPD, *Ibara 22(2)*.





## Watengeneza programu (katikika huduma za kibinadamu na mashiirka ya maendeleo)[92,93]

| | |
|---|---|
| **Kujiandaa na kujiweka tayari** | • Tafuta ushauri, na husisha watu wanaoshughulika na wa masuala ya watu wenye ulemavu, watu wenye ulemavu, na mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo wanawakilisha anuwai za watu wenye ulemavu katika hatua zote za kushughulikia kupunguza hatari ya majanga na katika programu za dharura.<br>• Andaa vipindi vya kukuza uelewa na kujengea uwezo wafanyakazi, na wadau kwa kushirikiana na mashirika ya watu wenye ulemavu, kuhusu ujumuishi wa watu wenye ulemavu.<br>• Saidia mashirika ya watu wenye ulemavu kupata uwezo wa kufanya kazi katika mazingira ya huduma za kibinadamu, katika ngazi zote za kiutawala, rasilimali watu, uwajibikaji, usimamizi wa fedha na uandishi wa maandiko ya miradi. |
| **Tathmini ya mahitaji na uchambuzi** | • Fanya uchambuzi wa sababu zinazochangia kusababisha hatari kwa watu wenye ulemavu katika jamii. Kwa kuzingatia tathmini ya mahitaji, ainisha vikwazo ambavyo vinawazuia watu wenye ulemavu kupata huduma stahiki na kulindwa, na ainisha viwezeshi vinavyochangia ufikivu na usaidizi na kulindwa.<br>• Hakikisha kuwa mchakato wa tathmini ya mahitaji ni fikivu kwa watu wenye ulemavu. Fanya marekebisho stahiki pale inapohitajika, ili kurahisisha na kuwezesha ukusanyaji wa taarifa kutoka na kwa watu wenye ulemavu.<br>• Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanashiriki kama watu mahususi katika kutoa taarifa katika vikundi vya majadiliano na timu za kufanya tathmini ya mahitaji. |
| **Kupanga mkakati wa jitihada za kuchukua a/kutoa huduma** | • Hakikisha kuwa, kufikia mahitaji ya watu wenye ulemavu ni miongoni mwa malengo ya mpango wa utekelezaji wa masuala ya kibinadamu. Buni na weka viashiria ambavyo vitapima ujumuishi wa watu wenye ulemavu.<br>• Tumia mpango pacha wa utekelezaji wa miradi na mikakati ambayo inahakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanafurahia huduma sawa na kupata usaidizi na kulindwa. Kwa madhumuni haya, zingatia kufikia watu mahali walipo, huduma za nyumbani, miundombinu fikivu, kufanya marekebisho stahiki, n.k.<br>• Shauriana na wadau wa maendeleo wenye mtazamo unaowazingatia watu wenye ulemavu, watoa huduma, na mashirika ya watu wenye ulemavu yanayowakilisha anuwai za watu wenye ulemavu. |
| **Kugema rasilimali** | • Tengeneza bajeti jumuishi ambayo inazingatia umuhimu wa ufikivu na marekebisho stahiki. Husisha mashirika ya watu wenye ulemavu na wawakilishi wa watu wenye ulemavu katika kuweka vipaumbele na kuangalia rasilimali ambazo zitahitajika katika kuondoa vikwazo ambavyo watu wenye ulemavu wanakabiliana navyo wakati wanajaribu kupata huduma, usaidizi na kulindwa.<br>• Ajiri watu wenye ulemavu na wale wenye taaluma katika masuala ya watu wenye ulemavu kama wafanyakazi au kama washauri. |

[92] Baadhi ya hatua katika kipengele hiki ni muhimu pia katika uchambuzi na usimamizi wa taarifa za maofisa.

[93] Angalia pia Umoja wa Mataifa, *Mkakati wa ujumuishi wa Ulemavu* (2019) ambayo inaweka matarajio maalumu kwa viongozi wa mashirika ya Umoja wa Mataifa.

| | |
|---|---|
| Utekelezaji na ufuatiliaji | • Hakikisha kuwa shughuli za ufuatiliaji zinatumia viashiria ambavyo ni jumuishi vilivyochambuliwa kwa jinsia, umri na hali ya ulemavu.<br>• Fanya mapitio na chambua kiwango ambacho watu wenye uhitaji wanaweza kuzifikia programu na chukua hatua stahiki inapohitajika.<br>• Toa taarifa kuhusu vikwazo na hatari ambazo watu wenye ulemavu wanakabiliana nazo wakati wanapojaribu kufikia usaidizi wa huduma za kibinadamu na ulinzi. Sambaza mifano ya utendaji wenye tija, sambamba na kutumia viwango[94] na nyenzo stahiki. |
| Tathmini | • Tafuta ushauri kutoka kwa mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo yanawakilisha anuwai za watu wenye ulemavu wakati wa kubuni na kupanga na kutekeleza tathmini ambayo inahusisha masuala ya ulemavu (ulinzi, usalama na ufikivu sawa).<br>• Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanafikia michakato ya tathmini na wanashiriki kikamilifu katika michakato hiyo.<br>• Sambaza taarifa za tathmini katika mifumo fikivu. Tumia mapendekezo yaliyomo katika taarifa ya tathmini kurekebisha programu kama inavyohitajika. |
| Uratibu | • Husisha mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo yanawakilisha anuwai za watu wenye ulemavu katika michakato ya uratibu.<br>• Kuza ushirikiano wa vitengo katika masuala yanayohusu ujumuishi wa watu wenye ulemavu. Anzisha mifumo ya rufaa, hamasisha shughuli za kujifunza, toa mafunzo kwa kutumia wataalamu wa kisekta na mashirika ya watu wenye ulemavu. |
| Usimamizi wa taaarifa[95] | • Hakikisha kuwa taarifa zinazohusu ulemavu zinapima na kutoa matokeo, na viashiria vilivyo ekelezwa na mpango wa huduma za kibinadamu.<br>• Toa mafunzo kwa wafanyakazi kwenye eneo la kukusanya na kuchambua taarifa zinazohusiana na ulemavu ikiwemo vikwazo vya ujumuishi na sababu zinazowezesha ujumuishi.<br>• Tengeneza na tumia nyenzo za kupata taarifa ambazo zitatoa taarifa kuhusu kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanaweza kufikia huduma na kupata ulinzi na kushiriki katika shughuli ambazo zinawahusu.<br>• Hakikisha na tumia nyenzo za kupata taarifa ambazo zitatoa taarifa kuhusu kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanaweza kufikia huduma na kupata ulinzi na kushiriki katika shughuli ambazo zinawahusu.[96] |

[94] Kama vile viwango vya Sphere, viwango vya ujumuishi wa masuala ya kibinadamu, na programu ya nyenzo za kibinadamu.

[95] Usimamizi wa taarifa unahusisha ukusanyaji, uchambuzi na usimamizi wa data na taarifa katika mzunguko wa programu za kibinadamu.

[96] Angalia ICRC, viwango vya kitaalamu kwa kazi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na haki za binadamu katika hali za vurugu (2018) sura ya 6, usimamizi wa taarifa na taarifa za matokeo ya ulinzi uk. 106–148; na CRPD, Ibara 22(2).





## Wafadhili

| | |
|---|---|
| Kujiandaa na kujiweka tayari | • Jumuisha vigezo na sera zinazohusiana na ujumuishi katika kuandaa matangazo ya miradi na mikataba ya makubaliano.<br>• Hakikisha kuwa wafanyakazi wamepewa mafunzo juu ya ujumuishi wa watu wenye ulemavu, na kuwa mwakilishi anayeshughulikia masuala ya watu wenye ulemavu ameteuliwa. Andaa Mwongozo wa masuala ya ulemavu kwa ajili ya wadau watekelezaji kwa kutumia mwongozo huu.<br>• Wekeza katika kujenga utayari na kutoa fedha kusaidia kukuza uwezo ili kuhakikisha wadau wa huduma za kibinadamu, yakiwemo mashirika ya watu wenye ulemavu, yanajiandaa kujumuisha watu wenye ulemavu katika masuala ya kibinadamu.<br>• Eleza umuhimu wa kuhusisha ukusanyaji wa taarifa kuhusu watu wenye ulemavu ikiwemo kuhusu ufikivu, kuondoa vikwazo na ubora wa huduma katika kuandaa taarifa za miradi. Sisitiza kuwa taarifa lazima zichambuliwe kwa kigezo cha jinsi, umri na ulemavu. |
| Tathmini ya mahitaji na uchambuzi | • Saidia wadau wa uwekezaji katika kuwezesha tathmini ya mahitaji na uchambuzi ambao utahusisha watu wenye ulemavu. Hii inatakiwa kuelezea hatari zilizopo, ufikivu wa ulinzi na usaidizi, ubora wa huduma na vikwazo kwa watu wenye ulemavu. |
| Kupanga mkakati wa jitihada za kuchukua/muitikio | • Watake wadau wanaotekeleza miradi kubuni na kujumuisha mikakati ya ujumuishi wa masuala ya ulemavu kama sehemu ya kigezo cha kupata fedha.<br>• Kuza na saidia wadau kuendeleza mitazamo ambayo inatambua, inachambua na kuelezea hatari ambazo watu wenye ulemavu wanakabiliana nazo. |
| Kugema rasilimali | • Weka ujumuishi wa watu wenye ulemavu kama kipaumbele cha kufadhiliwa na tenga fedha kulenga na kukuza ufikivu na ushiriki.<br>• Tumia viashiria vya masuala ya ulemavu pamoja na viashiria vingine kama vile jinsia, umri katika kusaidia kuchagua na kufuatilia andiko la mradi.<br>• Tengeneza motisha kwa ajili ya programu ambazo zinajumuisha masuala ya ulemavu kwa kuzingatia maazimio ya kimataifa kuhusu ushiriki.<br>• Hakikisha kuwa rufaa za maandiko ya kifedha zinatumia mfumo ambao unafikika kwa mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo yanawakilisha anuwai za watu wenye ulemavu. Badilisha vigezo vya ufadhili pale inapohitajika ili kufanya mashirika ya watu wenye ulemavu yakidhi vigezo. |
| Utekelezaji na ufuatiliaji | • Shauriana na watu wenye ulemavu wakati wa kufanya tathmini ya programu za wadau. Chambua ufikivu wao katika masuala ya usaidizi na ulinzi.<br>• Tathmini taarifa au kufuatilia utekelezaji wa wadau, ufanisi wao kwa kutumia vigezo vitokanavyo na Mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu. Toa mrejesho na ushauri kwa wadau.<br>• Fuatilia juhudi za wadau katika kujumuisha watu wenye ulemavu. |

| | |
|---|---|
| **Tathmini** | • Himizawadau kufanya ujumuishi na ushiriki wa watu wenye ulemavu katika mifumo ya tathmini.<br>• Toa matokeo ya tathmini katika mifumo fikivu ya mawasiliano.<br>• Fuatilia mapendekezo ya tathmini kuhusu ujumuishi na ushiriki wa watu wenye ulemavu. |
| **Uratibu** | • Saidia katika kuteua wafanyakazi wenye weledi katika masuala ya ujumuishi (kama watu muhimu katika masuala ya ulemavu, wajumbe wa masuala ya kibinadamu katika timu za kitaifa, mifumo ya uratibu ya kisekta).<br>• Himiza na saidia mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo yanawakilisha anuwai ya watu wenye ulemavu kuweza kuhusika na afua za kibinadamu na mifumo ya uratibu. |
| **Usimamizi wa taarifa**[97] | • Himiza wadau kunyambulisha taarifa, ikiwemo taarifa kuhusu vikwazo na kuviondoa, kwa jinsia, umri na ulemavu.<br>• Toa ripoti kuhusu maendeleo yanayofanyika katika hujumuisha watu wenye ulemavu. Toa mrejesho kuhusu mambo uliyojifunza na mifano bora.<br>• Pale ambapo taarifa hazipatikani kuhusu janga au uwepo wa hatari kwa watu wenye ulemavu walioathirika, saidia wadau kukusanya data kuhusu ulemavu.<br>• Hakikisha kuwa ukusanyaji, utunzaji na uchakataji wa taarifa binafsi za siri unafanywa kwa kuzingatia miiko ya ukusanyaji data na misingi ya ulinzi.[98] |

[97] Usimamizi wa taarifa unahusisha ukusanyaji, uchambuzi na usimamizi wa data na taarifa katika mzunguko wa programu za kibinadamu.

[98] Angalia ICRC, *viwango vya kitaalamu kwa kazi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na haki za binadamu katika hali za vurugu* (2018), sura ya 6, usimamizi wa data na taarifa za matokeo ya ulinzi uk. 106–148; na CRPD, *ibara 22(2)*.





## Mashirika ya Watu Wenye Ulemavu

Wadau wa masuala ya kibinadamu wanapaswa kuhusisha mashirika ya watu wenye ulemavu yanayowakilisha anuwai za watu wenye ulemavu katika nyanja zote katika mzunguko wa programu wa masuala ya kibinadamu. Watu wenye ulemavu wanaweza kutoa maarifa na utaalamu kuhusu ulemavu, na kuongoza kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wamehusishwa kikamilifu na kushiriki katika masuala ya kibinadamu. Pale ambapo mashirika ya watu wenye ulemavu hayapo, wadau wa masuala ya kibinadamu wanapaswa kuhusisha makundi rika na watu wenye ulemavu kibinafsi.

| | |
|---|---|
| **Kujiandaa na kujiweka tayari** | • Kuza matumizi ya nyenzo zilizojaribiwa katika muktadha wa kibinadamu kama vile maswali ya kundi la Washington ambayo husaidia katika kuchambua taarifa kwa jinsia, umri na ulemavu.<br>• Fanya utetezi wa haki za watu wenye ulemavu katika mazingira ya hatari na dharura na katika programu zote za kupunguza hatari ya majanga na dharura. Programu za utayari zinapaswa kuwa zinafikika kwa watu wenye ulemavu.<br>• Kuza uelewa na toa mafunzo kwa wanajamii, watu wenye ulemavu na wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu na walio katika mstari wa mbele katika kutoa huduma za kibinadamu kuhusu haki na uwezo wa watu wenye ulemavu. Elezea mahitaji yao ya kimawasiliano.<br>• Fanya utetezi kwa ajili wa wakimbizi wenye ulemavu ili wapate huduma na mifumo ya kitaifa. |
| **Tathmini ya mahitaji na uchambuzi** | • Shiriki katika tathmini ya mahitaji na ukusanyaji wa taarifa za kuonyesha kiasi na zile za ubora. Shiriki katika kuainisha vikwazo vinavyozuia ujumuishi wa watu wenye ulemavu na viwezeshi vinavyosaidia ujumuishi.<br>• Saidia katika kukuza nyenzo na kubuni tathmini fikivu kuhusu mahitaji. Hii inapaswa kuruhusu marekebisho stahiki na inapaswa kujumuisha watu wenye ulemavu katika timu za tathmini na majadiliano ya vikundi. |
| **Mpango wa kutoa huduma** | • Tumia mtazamo wa haki katika ulemavu ili kufanya wadau wa masuala ya kibinadamu pamoja na serikali kuwajibika wakati wanabuni mipango kuhusu huduma za kibinadamu, pamoja na nyenzo nyingine na mipango katika masuala ya kibinadamu.<br>• Wakilisha maeneo ya masuala ya ulemavu katika mikutano na katika utetezi wa haki za watu wenye ulemavu.<br>• Fikia watu wenye ulemavu kutoka katika jamii zilizoathirika ikiwemo wakimbizi na maeneo mengine ya watu waliohamishwa na wahusishe katika mitandao ya mashirika ya watu wenye ulemavu. |
| **Kugema rasilimali** | • Saidia kuandaa bajeti ambazo zitafadhili shughuli za ujumuishi wa watu wenye ulemavu. Bajeti zinapaswa kuweka fedha kwa ajili ya marekebisho stahiki, makazi sahihi na ushiriki wa mashirika ya watu wenye ulemavu.<br>• Saidia utetezi wa ujumla kuhusu kuongeza utoaji wa fedha katika huduma za majanga.<br>• Changia na wezesha ukusanyaji wa rasilimali katika hatua zote. |

| | |
|---|---|
| **Utekelezaji na ufuatiliaji** | • Shiriki katika ukusanyaji wa taarifa za ufuatiliaji na taarifu kuhusu ufikivu wa huduma na usaidizi, kulindwa na hatari, ukiukwaji wa haki za binadamu na matumizi ya fedha, n.k.<br>• Saidia afua ambazo zinawanufaisha makundi yaliyo katika hatari ikiwemo watu wenye ulemavu.<br>• Toa ushauri katika kuendeleza miundombinu fikivu, majengo na vifaa vya mawasiliano. |
| **Tathimini** | • Saidia timu ya tathmini katika kutathmini ufikivu na kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanaweza kushiriki kikamilifu katika kufurahia haki za binadamu kwa kuzingatia jinsi, umri na anuwai za ulemavu.<br>• Ainisha maswali sahihi kwa ajili ya kutathmini ujumuishi. Kwa kuzingatia watu wenye ulemavu, tathmini inapaswa kugusa masuala ya ufikivu, upatikanaji, unafuu, uwajibikaji na ubora wa huduma pamoja na ufanisi, athari na umuhimu wa huduma.<br>• Kwa kushirikiana na serikali pamoja na wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu, kusanya na sambaza mifano ya utendaji wenye tija pamoja na mambo ya kujifunza kuhusu ujumuishi na ufikivu wa huduma, usaidizi na ulinzi wa watu wenye ulemavu.<br>• Fanya utetezi kuwa matokeo ya tathmini ni lazima yaingizwe katika mipango ya programu na utekelezaji. |
| **Uratibu** | • Ainisha wawakilishi katika mashirika ya watu wenye ulemavu ambao wanaweza kushiriki katika vikao vya vitengo na baina ya vitengo katika ngazi zote, ikiwemo kama wajumbe wa timu za kutoa huduma za kibinadamu.<br>• Ratibu mashirika ya watu wenye ulemavu (kitaifa na kimataifa na katika eneo husika) na changia maoni yao kwa kutumia nyenzo ya "5W" katika mchakato wa uratibu wa masuala ya kibinadamu.[99]<br>• Shiriki katika kukusanya taarifa juu ya hatari na vikwazo ambavyo watu wenye ulemavu wanakabiliana navyo ikiwa ni pamoja na tatizo la kufikia huduma. Toa mrejesho kwa wadau wa masuala ya kibinadamu na wawakilishi wa watu wenye ulemavu. |
| **Usimamizi wa taarifa**[100] | • Himiza wasimamizi wa habari kukusanya na kuchambua taarifa juu ya kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanafikia huduma na ulinzi.<br>• Saidia katika kutafsiri na kuchambua taarifa juu ya mwenendo wa masuala ya ulemavu na programu za ulemavu.<br>• Hakikisha kuwa taarifa zinasambazwa kwa kupitia mifumo fikivu kwa mashirika ya watu wenye ulemavu na hadhira nyingine.<br>• Wasilisha taarifa na tathmini kuhusu watu wenye ulemavu kwa wawakilishi wa watu wenye ulemavu na mifumo ya uratibu.<br>• Hitaji ukusanyaji, utunzaji au uchakataji wa taarifa muhimu uendane sambamba na maadili na kanuni za ulinzi.[101] |

[99] Nani anafanya nini, wapi, wakati gani, na kwa nani (5W) zana hii inatumika kukusanya takwimu kutoka katika eneo katika kutengeneza taarifa za bidhaa kama vile ramani, na majeduari ya mafanikio. Zana ya 5W inatumika kuondoa uchapishaji usiotarajiwa na mashirika mbalimbali, na kusaidia wadau, ikiwemo jamii zilizoathirika na serikali katika kuanisha mapungufu.

[100] Usimamizi wa taarifa unahusisha ukusanyaji, uchambuzi na usimamizi wa takwimu na taarifa katika mzunguko wa programu za kibinadmu.

[101] ICRC, *viwango vya kitaalamu kwa kazi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na haki za binadamu katika hali za vurugu* (2018), sura ya 6, usimamizi wa data na taarifa za matokeo ya ulinzi uk. 106–148; na CRPD, *Ibara 22(2)*.

# 10 Masuala yanayopswa kufanywa na sekta

## Uratibu wa kisekta na baina ya sekta

Uratibu wa masuala ya kibinadamu unalenga kuboresha ufanisi wa huduma za kibinadamu kwa kuimarisha makisio, uwajibikaji na ushirikiano.

Uratibu wa kisekta na baina ya sekta unatoa mwongozo wa utekelezaji wa masuala ya huduma za kibinadamu kwa kukubali maazimio na hatua za kuboresha ujumuishi na ushiriki. Mifumo ya uratibu inaweza kuwa ya aina tofauti na inaweza kutekelezwa sambamba katika nchi moja.

Uratibu wa vitengo na sekta unaanzishwa (pale unapohitajika) na mratibu wa masuala ya dharura au mratibu wa masuala ya kibinadamu au mratibu mkazi au timu za kitaifa za masuala ya kibinadamu na serikali husika. Uanzishwaji huu huchochea *mzunguko wa programu za huduma za kibinadamu*.

Wakati mifumo ya uratibu inajitahidi kujumuisha masuala ya ulemavu kupitia vikosi kazi, uratibu hubakia kuwa wa kushtukiza na usio na mpangilio. Ulemavu bado haujumuishwi kimpangilio na kwa utaratibu katika taasisi.

Wakati mfumo wa uratibu katika vitengo na sekta bado haujaanzishwa au umeanzishwa kwa sehemu ndogo, serikali husika inaweza kujenga mfumo wake wa uratibu. Aina yoyote ya uratibu itakayotumiwa, ni muhimu kujumuisha mashirika ya watu wenye ulemavu katika uratibu unaoratibiwa na serikali pamoja na mikakati mingine ya huduma za kibinadamu.

## Kufanyia kazi masuala ya ulemavu katika mifumo ya uratibu

Ujumuishi wa masuala ya ulemavu ni fursa katika kuimarisha uratibu baina ya sekta. Uratibu baina ya sekta unatakiwa kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata usaidizi na ulinzi kwa usawa kama watu wengine walioathiriwa na majanga, na unapaswa kuzingatia mashirika ya watu wenye ulemavu kuwa wadau katika masuala ya kibinadamu. Kufikia haya malengo katika ngazi zote za kitaasisi, kisekta na baina ya sekta kutahamasisha umuhimu wa ulinzi, kuongeza mtazamo wa haki, na kuongeza uwajibikaji katika jamii zilizoathiriwa.

Hatua ambazo zinapaswa kuchukuliwa na mifumo ya uratibu ya kibinadamu katika kuhamasisha ujumuishi wa watu wenye ulemavu, umeainishwa katika jedwali la majukumu na wajibu kwa wadau.

## Masuala muhimu ya kufanya

Masuala muhimu ya kufanya yanatakiwa kuzingatiwa muda wote wa uratibu wa kisekta na baina ya sekta katika awamu zote za masuala ya huduma kibinadamu kwa ajili ya ufanisi wa ujumuishi wa watu wenye ulemavu.

### Ushiriki

- Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu na familia zao pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu wanahusishwa kikamilifu katika mifumo ya uratibu, tathmini ya mahitaji ya kisekta na baina ya sekta na katika

*kutengeneza mahitaji ya kibinadamu* na *mpango wa utoaji wa huduma za kibinadamu*.

- Hakikisha makundi anuwai ya watu wenye ulemavu yamewakilishwa. Zingatia aina mbalimbali za ulemavu pamoja na jinsi na umri. Chukua jitihada za makusudi katika kuhamasisha makundi yaliyo na uwakilishi mdogo ikiwemo watu wenye ulemavu wa akili, watu wazawa katika eneo husika, wanawake na wasichana.

## Kushughulikia vikwazo

- Wakati wa kufanya tathmini ya mahitaji, ainisha vikwazo na hatari ambazo watu wenye ulemavu wanakabiliana nazo.

- Wakati wa kuandaa mpango wa huduma za kibinadamu, tumia taarifa za kupima idadi na zile za kupima ubora kuhusu watu wenye ulemavu ili kupata taarifa zao, kutambua hatari na vikwazo wanavyokabiliana navyo na mbinu za kuondoa vikwazo hivyo.

## Uwezeshaji na kukuza uwezo

- Hakikisha kuwa uratibu unajumuisha mashirika ya watu wenye ulemavu katika juhudi za kujenga uwezo.

- Wajengee uwezo watu wanaofanya uratibu kuhusu masuala ya ujumuishi, husisha vipengele vya ujumuishi katika kuratibu mafunzo.

- Anzisha njia za rufaa za kisekta ambazo zitaongeza ujumuishi wa watu wenye ulemavu.

## Ukusanyaji wa taarifa/takwimu na ufuatiliaji

- Tumia taarifa zilizopo katika mahitaji ya watu wenye ulemavu ya kisekta na husisha uchambuzi wa pamoja wa kisekta ili kupata uelewa mpana wa hali ya mahitaji.

- Pale ambapo taarifa za uhakika hazipatikani au haziwezi kukusanywa, tumia kanuni ya asilimia 15 katika kukadiria uwepo wa watu wenye ulemavu.[102]

- Hakikisha kuwa mipango ya utoaji huduma za kibinadamu katika sekta zote zinatambua ulemavu na kwa uwazi zinapendekeza kuwa na malengo na viashiria vinavyochambua taarifa kwa ulemavu.

- Hakikisha kuwa taarifa za ufuatiliaji za timu za kitaifa mara kwa mara zinajumuisha hali ya watu wenye ulemavu (ikiwemo mbinu wanazotumia kufikia huduma za kibinadamu, changamoto wanazokumbana nazo, mafanikio na mambo waliyojifunza).

- Toa taarifa kuhusu watu wenye ulemavu (zilizochambuliwa kwa umri, jinsi na ulemavu) katika taarifa za kisekta kwa kutumia mifumo fikivu.


[102] Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia, *Ripoti ya dunia kuhusu ulemavu* (2011).

# 11 Uratibu na usimamizi wa kambi

## Utangulizi

Uratibu na usimamizi wa kambi (UKUK) ni sekta ya kiufundi. Dhana hii inahusu uratibu rasmi ambao unaweza kutumika katika shughuli za wakimbizi (kupitia *Mwongozo wa uratibu wa wakimbizi*), na pia katika shughuli za kulinda watu waliohamishwa ndani ya nchi (kupitia kitengo cha UKUK).[103] Lengo la msingi la sekta ya UKUK ni kulinda haki za kundi la watu wanaoathiriwa na kuhamishwa kwa lazima (lakini pia familia na jamii wenyeji).

Katika utendaji, sekta hii inafanya kazi kuhakikisha wale wanaoishi katika umoja au mazingira mipangilio ya kijamii ya walio uhamishoni wanapata huduma ya ulinzi na usimamizi kwa usawa. Hili linapatikana kwa kuratibu na kufuatilia utolewaji wa huduma na kuanzisha uwakilishi na utawala unaowajibika na miundo shirikishi katika ngazi za eneo husika (usimamizi wa kambi); kutoa uratibu wa kimkakati na kiutendaji.




Tazama Sura ya 10, Makao, Makazi, Maji na usafi wa mazingira.

Utaratibu wa maeneo (makambi); na usimamizi wa huduma za kibinadamu (utawala wa kambi). Muundo wa ushiriki na utawala unaweza kuwa katika mfumo wa kamati, makundi yenye ushawishi, au watu wenye nia njema, au kupitia mifumo ya kupokea maoni na kero, n.k, kwa pamoja miundo hii inahakikisha kuwa kila mmoja anaweza kupaza sauti na kusikika na kushiriki katika maamuzi yanayowahusu.

Kwa ujumla katika maeneo ambayo yanatunza kundi la watu waliohamishwa, sekta ya UKUK ina wajibu wa msingi katika kuratibu na ufuatiliaji wa huduma za misaada ya kibinadamu na ulinzi. Inahakikisha kwamba mahitaji yanatambulika na kupatikana na kwamba sekta husika au watendaji wanachukua jitihada za kuziba mapungufu na kuhakikisha huduma katika sehemu moja hazijirudii. Vikao vya uratibu wa ngazi ya eneo mara nyingi huudhuriwa na sekta zote, ikijumuisha watu wa maji na usafi wa mazingira, maji, makazi na ulinzi, elimu na usambazaji, sambamba na wawakilishi kutoka katika jamii ya waliohamishwa, ulinzi wa kambi na jamii wenyeji.

### Sheria na mifumo mingine

- *Mkataba wa haki za watu wenye ulemavu*
- *Njia za kukabiliana na wakimbizi ulimwenguni*
- *Njia za kukabiliana na uhamiaji salama, unaoratibiwa ulimwenguni mara kwa mara*

[103] Shirika la Wakimbizi Duniani, kitabu *kuhusu dharura: uratibu wa kambi, usimamizi wa kambi*.

## Dhana muhimu

**Kambi/eneo.** Neno "Kambi" au "Eneo" inahusiana na makazi tofauti tofauti ya muda mfupi yanayohusisha kambi zilizopangwa, kambi za makazi binafsi, vituo vya mkusanyiko, vituo vya mapokezi, vituo vya usafiri na vituo vya uokoaji[104]. Kwa sababu neno "Kambi" ni nyeti katika muktadha tofauti, watendaji wa UKUK wanatumia dhana mbalimbali kumaanisha makazi ya uhamiaji. Inatambulika kuwa makambi sio suluhu kwa watu walio uhamishoni, lakini ni moja kati ya njia pekee za kulinda na kusaidia watu waliohamishwa. Wajibu wa sekta hii si kuhamasisha uhamishaji wa makambi.

**Utawala wa makambi.** Utawala wa kambi unatimiza majukumu ya serikali au mamlaka za taifa katika makambi na shughuli za kambi.[105]

**Usimamizi wa makambi.** Usimamizi wa makambi unaratibu na kufuatilia utoaji wa huduma, ulinzi na misaada katika kambi moja au eneo kulingana na miundo ya kisheria ya kitaifa na kimataifa, pamoja na viwango vya chini vya huduma za kibinadamu.[106] Inahimiza ushiriki hai na wenye maana kwa kundi la watu walio uhamishoni. Usimazi wa makambi ni suala la kiutaalamu na la kijamii kwani linahitaji kutoa hali sahihi ya maisha (kupitia mifumo ya ushiriki, mrejesho na miundo ya utawala). Uongozi na usimamizi wa kambi unaweza kufanywa na watendaji na watoa huduma za kibinadamu (kama vile UNHCR, IOM, asasi za kiraia za kitaifa na za kimataifa, mashirika ya sekta binafsi au mamlaka za serikali au taifa.[107]

**Uratibu wa makambi.** Uratibu wa makambi unahusisha uratibu wa huduma katika maeneo mbalimbali ili kutoa huduma za kibinadamu na ulinzi katika maeneo ya wenyeji na kundi la watu walio uhamishoni. Inaratibu wajibu na majukumu ya utoaji wa huduma za kibinadamu juu ya uhamishwaji makazi na inaongozwa na UNHCR na/au IOM, sanjari na mamlaka za kitaifa. Kitengo cha UKUK (katika hali za watu waliohamishwa) au shirika kiongozi (katika hali za ukimbizi) kina lengo la kutoa huduma za kibinadamu kwa uratibu mzuri, ufanisi na ubora katika hali ambazo kundi la watu walio uhamishoni na kulazimika kutafuta hifadhi katika makazi ya muda. Inaboresha hali ya maisha katika kipindi cha kuwauhamishoni, inatoa misaada na ulinzi, inatafuta suluhisho la kudumu ili kumaliza janga la kuwa uhamishoni kwa muda, na kisha inasimamia ufungaji wa maeneo yaliowapatia makazi ya muda kundi la watu walio uhamishoni. Shirika kiongozi au kitengo husika kinatafuta kumaliza suala la uhamishwaji wa watu kwa kutafuta suluhu ya kudumu. IOM na UNHCR kwa pamoja wanaongoza kwa ushirikiano na vitengo vingine ulimwenguni kuangazia majanga ya asili na ya kibinadamu, hali za waliohamishwa ndani ya nchi yaliyoletwa na ugomvi uliosabaisha kuwepo kwa wakimbizi wa ndani, pia na vitengo vingine vilivyopo, mara nyingi sanjari na mamlaka za taifa.[108]

**Vituo vya uokoaji.** Ni majengo yanayotumika kutoa makazi ya muda mfupi kwa watu wanaokimbia tishio maalumu na la haraka, kama vile mapigano, au majanga asilia, mfano vimbunga au matetemeko. Shule, viwanja vya mipira na nyumba za ibada na majengo ya kiraia mara nyingi hutumika kwa lengo hilo. Inapowezekana, vituo vya uokoaji wa dharura vinatakiwa vitambulike na kuandaliwa kabla majanga hayajatokea.[109]

**Kamati ya utayari ya eneo husika.** Ni miundo ya kijamii au kiserikali inayosimamia hatua za kujiandaa na majanga.[110]

## Vikwazo

Uhamishwaji mara nyingi huwa ni kitendo cha ghafla, na huwa na muda mfupi wa kujiandaa. Ni tukio lenye taharuki ambalo linaweza kuzidisha au kutengeneza vikwazo kwa watu wenye ulemavu. Katika makazi ya muda mfupi yanayohifadhi watu walio uhamishoni, watu wenye ulemavu mara nyingi hushindwa kumudu mahitaji yao ya kimsingi au kupata msaada stahiki na ulinzi.

Watu wenye ulemavu wanaohifidhiwa katika makazi ya muda mfupi wana haki ya kupokea msaada wa huduma za kibinadamu. Hii inamaanisha kuwa watoa huduma wanaotoa huduma za kibinadamu wanatakiwa kutambua na kuondoa vikwazo vya kimazingira, kimtazamo na kitaasisi vinavyozuia upatikanaji wa misaada na ulinzi kwa watu wenye ulemavu. Watu wenye ulemavu katika makambi pia wana haki ya kutumia haki yao ya kushiriki katika maisha ya makambi na kutoa maamuzi yanayowahusu.

[104] IOM, Tume ya wakimbizi ya Norway, Shirika la Umoja wa Mataifa la Wakimbizi, *nyenzo za usimamizi wa kambi* (2015), uk. 9.
[105] Kwa vitendo, pale ambapo serikali au mamlaka za kitaifa zinasimamia makambi au kutaribu makambi, na utawala wana shiriki katika majukumu kwa namna mbalimbali.
[106] Angalia kwa mfano, *viwango vya Sphere*, *viwango vya masuala ya kibinadamu*, shirika la Help Age, CBM, *viwango vya ujumuishi vya Handicap International kwa wazee na watu wenye ulemavu*, pamoja na nyinginezo.
[107] Angalia IOM, tume ya wakimbizi ya Norway, shirika la umoja wa mataifa la wakimbizi, *nyezo za usimamizi wa makambi* (2015) na *nyezo ya mafunzo ya CCCM*.
[108] Angalia IOM, Tume ya wakimbizi ya Norway, Shirika la Umoja wa Mataifa la Wakimbizi, *nyenzo za usimamizi wa makambi* (2015), uk. 14.
[109] *Ibid*, uk. 18.
[110] Uratibu wa kambi wa kidunia na usimamizi wa kambi wa CCCM, *Mwongozo wa MEND-Mwongozo madhubuti wa mpango wa uokoaji katika majanga ya asili* (2014), uk. 23.





Hii inamaanisha kwamba watoa huduma za kibinadamu wanatakiwa kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanashiriki katika utawala wa maeneo na miundo ya uwakilishi. Wanatakiwa kupewa fursa madhubuti ya kupata taarifa na mrejesho na utaratibu wa kutoa malalamiko, na kuhakikisha kwamba wanaweza kushiriki katika matukio ya kijamii na shughuli za kiuchumi. Majukumu ya kuondoa vikwazo na kukuza ujumuishi wenye tija na ushiriki unatakiwa katika hatua zote za maisha ya eneo/kambi, kuanzia kipindi cha kupanga na kuanzisha kambi, kutoa matunzo na matengenezo, mpaka kufungwa kwa kambi na kupatikana kwa suluhu ya kudumu.

## Viwango na miongozo rejea

- Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi, *kufanya kazi na watu wenye ulemavu walio katika uhamisho wa kulazimisha* (2019).
- Sphere, *kitabu cha viwango cha Sphere* (2018).
- Shirika la Help Age, CBM, *Handicap International*, *viwango vya ujumuishi wa masuala ya kibinadamu kwa wazee na watu wenye ulemavu* (2018).
- IOM, kamati ya wakimbizi ya Norway, shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi, *kifaa cha uangalizi wa kambi* (2015).
- Konga ya CCCM, *kituo cha pamoja cha miongozo CCCM* (2010).
- *Kanuni za kuongoza uhamisho wa ndani* (2004).
- CCCM, *uhamisho mijini na mapitio ya nje ya kambi* (2013).
- Konga ya CCCM, *MHPSS katika Muktadha wa Dharura; Mambo ambayo Mratibu wa kambi na viongozi katika kambi wanapaswa kufanya* (2014).

## Masuala ya muhimu na ya 'lazima kufanya'

'Masuala ya lazima kufanya', lazima yafanyike katika hatua zote za huduma za kibinadamu, pale ambapo utekelezaji wa programu jumuishi za UKUK kwa watu wenye ulemavu unafanyika.

### Ushiriki

- Husisha watu wenye ulemavu kikamilifu, familia zao na mashirika ya watu wenye ulemavu katika kutambua vikwazo. Hakikisha wanashiriki katika kupanga, kubuni, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini miundombinu ya eneo, na kulinda huduma za msaada katika maeneo ya wahamiaji.
- Hakikisha watu wenye ulemavu wanawakilishwa kwa usawa katika utaratibu wa utawala wa maeneo, mfano kamati za usimamizi, kamati za ufundi kwa ajili ya makazi, maji na usafi wa mazingira, mgawanyo wa chakula, usalama na ulinzi, na miundo mingine ya ushiriki ambayo ni rasmi ama isiyo rasmi, mfano makundi ya jamii, makundi ya wanawake, makundi ya vijana, n.k. Uwakilishi unapopangwa, zingatia aina mbalimbali za ulemavu sambamba na umri, jinsia na anuwai. Chukua jitihada za lazima kuinua makundi ya watu wenye ulemavu yasiyo na uwakilishi wa kutosha, mfano watu wenye ulemavu wa afya ya akili, watu wa asili ya eneo husika, wanawake na wasichana.
- Husisha watu wenye ulemavu katika shughuli za jamii na mrejesho na mfumo wa utoaji malalamiko. Kuza upatikanaji wenye ufanisi na usio na vikwazo ambao utaheshimu kila aina ya ulemavu.

**Mchoro namba 6 |** Vikwazo vya upatikanaji na ujumuishi katika UKUK

**JINSI MADHARA YA MIGOGORO YANAVYOONGEZEKA KWA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA UKUK**

**MATOKEO YA MIGOGORO**

Kukosa usalama, kuharibika kwa mitandao ya kijamii, uharibifu wa miundombinu, uhamishwaji, kufungwa kwa huduma

**VIKWAZO VINAVYOKUZWA**

**Vizuizi vya mazingira:**

- Kambi isiyofikika kirahisi, mfumo na miundombinu isiyo salama. Kambi na miundombinu isiyofika na ambayo si salama,
- Huduma za usimamizi wa kambi na vifaa hazipatikani. Kutofikika au kutopatikana kwa huduma za kiutawala na vifaa vya kambi,
- Ukosefu wa mawasiliano yanayopatikana kiurahisi, yanayohusiana na maisha ya kambi,
- Upungufu wa maeneo ya majengo ya umma,
- Kutopatikana kwa vifaa vya uhamiaji, vifaa na teknolojia saidizi, pamoja na msaada wa huduma maalumu utolewao katika kambi.

**Vizuizi vya mtazamo:**

- Unyanyapaa dhidi ya watu wenye ulemavu katika kipindi cha uhamishoni,
- Wafanyakazi wa UKUK hufikiri kila mtu mwenye ulemavu hana uwezo wa kuchangia kwenye uongozi au kufanya maamuzi katika ngazi ya jamii.

**Vizuizi vya taasisi:**

- Ukosefu wa uwezo wa kitaalamu kuhusu kukuza ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu katika UKUK,
- Ukosefu wa kutokuwazingatia watu wenye ulemavu katika viwango vya kisekta, miongozo na sera,
- Hakuna utolewaji wa bajeti kwa ajili ya ufikiwaji na utunzaji wa watu wenye ulemavu katika kambi.

**Hatari zinazowakabili watu wenye ulemavu**

Ukatili, umaskini, majanga ya mazingira, kuzorota kwa afya, kunyanyapaliwa, kutengwa, kuachwa.



## Kushughulikia vikwazo

- Tambua na fuatilia vizuizi vinavyozuia watu wenye ulemavu kupata huduma katika makazi ya muda mfupi. Tafuta suluhisho ambalo litaondoa vizuizi na chukua hatua ili kutoa malazi ya kuridhisha.
- Himiza wakandarasi wote watumie au wafuate kanuni ya usanifu wa miundombinu kwa ajili ya watu wote yaani "*Universal design*" wanapopanga na kujenga maeneo.
- Hakikisha kila taarifa na mawasiliano (yanayohusu huduma za msaada na ulinzi, suluhu za kudumu, taratibu za ufungwaji wa maeneo, n.k) zinapatikana katika miundo mbalimbali inayoweza kupatikana kirahisi. Zingatia mahitaji ya viziwi, wasioona, wenye ulemavu wa afya ya akili.
- Tekeleza mikakati ili kupunguza ubaguzi na unyanyapaaji wa watu walemavu. Ongeza uelewa wa jamii juu ya haki za watu wenye ulemavu. Anzisha vikundi vya misaada. Himiza watu wenye ulemavu wa afya ya akili kuwa watetezi wao wenyewe.
- Hakiki sera za kisekta, miongozo na zana ili kuhakikisha kwamba zinataja wazi haki za watu wenye ulemavu kwenye upatikanaji na ujumuishaji.

## Kuwezesha na kukuza uwezo

- Jenga uwezo wa watendaji wa UKUK na wadau wanaofanya kazi katika makazi ya muda mfupi (walio msitari wa mbele, wafanya kazi, watoa huduma, makandarasi). Toa mafunzo ya ufahamu juu ya haki za watu wenye ulemavu, kwa kuzingatia dhana ya muingiliano wa ulemavu na masuala ya umri, jinsia, hali ya uhamiaji, dini na hali ya ujinsia.
- Fundisha mashirika ya watu wenye ulemavu katika UKUK ili kuunga mkono huduma jumuishi na kuwezesha ushiriki wenye tija kwa watu wenye ulemavu.
- Ajiri watu wenye ulemavu na mashirika ya watu wenye ulemavu ili waweze kuchangia kwenye shughuli za kujenga uwezo ambazo makambi yanatoa.

## Ukusanyaji wa takwimu na ufuatiliaji

- Katika mzunguko mzima wa huduma za kibinadamu na kwa utaratibu unaofaa, kusanya na chambua takwimu juu ya watu wenye ulemavu kwa kuzingatia mchanganuo wa jinsia, umri na ulemavu. Tumia takwimu kupima kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanapata nyaraka na huduma zilizopo kwa ufanisi (mfano utaratibu wa kujisajili, vyeti vya hali ya ulemavu, usajili wa kuzaliwa). Kama hakuna taarifa za kuaminika au haziwezi kukusanywa, tumia kadirio la ulimwengu la asilimia 15% ya ulemavu.[111]
- Tengeneza ramani na ainisha katika ramani njia za huduma na upatikanaji wake; Tengeneza ramani ya upatikanaji wa vifaa na rasilimali na anzisha mifumo ya rufaa.
- Sambaza taarifa juu ya vikwazo vya upatikanaji ambazo zinahusiana na sekta maalum na wadau (maji na usafi wa mazingira, ulinzi na elimu) na hakikisha uratibu wa sekta mbalimbali pale utakapohitajika.
- Hakikisha kuwa maadili ya ukusanyaji takwimu na kanuni za ulinzi (mfano wa masuala ya usiri, utoaji wa taarifa, ridhaa ya hiari, ulinzi) zinaheshimiwa pale ambapo taarifa za watu wenye ulemavu zinapokusanywa na kutumika.[112]

[111] Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia, *Ripoti ya kidunia ya ulemavu* (2011)

[112] Angalia ICRC, *viwango vya kitaalamu kwa kazi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na haki za binadamu katika hali za vurugu* (2018) sura ya 6, usimamizi wa takwimu na taarifa za matokeo ya ulinzi, uk. 106–148; na CRPD, *Ibara 22(2)*.

| PROGRAMU ZILIZOKONDOISHWA | WALENGWA |
|---|---|
| Programu za UKUK na miundo ya uratibu imeundwa na kubadilishwa kuhakikisha kwamba huduma za msaada na ulinzi zitolewazo katika makazi ya muda mfupi, pamoja na miundo ya kiutawala na shughuli nyingine, zinajumuisha na zinapatikana kwa kila mmoja, ikiwemo watu wenye ulemavu. | Mashirika ya UKUK yanachukua hatua maalumu kutosheleza mahitaji ya watu wenye ulemavu na kuhakikisha kwamba wanakuwa na fursa ya kupata miundombinu ya maeneo, huduma, taarifa, na mfumo wa mahusiano wa njia mbili. Pia wanatafuta mbinu za kuwawezesha watu wenye ulemavu kupitia ushiriki na utaratibu wa utawala. |

Mwongozo ufuatao utasaidia watendaji wa UKUK kutambua na kuondoa vikwazo wanavyokumbana navyo watu wenye ulemavu, na familia, wasaidizi na walezi wao, wanapojaribu kutumia na kupata miundombinu, takwimu na huduma katika makambi.

## Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurudisha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi, na kupanga** | | | |
| Hakiki sera, miongozo, zana na taratibu za kawaida za uendeshaji kwa kutumia miongozo ya kamati ya IASC katika ujumuishaji wa watu wenye ulemavu. | X | | |
| Tengeneza uhusiano na mashirika ya watu wenye ulemavu. Waalike kuchunguza maeneo ya ushirikiano na kufundisha wafanyakazi wa UKUK na wadau kuhusu masuala ya watu wenye ulemavu. | X | | |
| Jenga ujuzi na maarifa ya watendaji wa UKUK na wadau juu ya ujumuishi wa watu wenye ulemavu. | X | | |
| Fanya ukaguzi wa utambuzi na ufikikaji wa pamoja/vituo vya uokoaji ikiwa ni pamoja na uanzishaji wa maeneo. | X | X | |
| Tambua na changanua hatari na vikwazo. Wakati wa kupanga, buni hatua za kukabiliana na vikwazo. | X | | |
| Orodha ya wadau inajumuisha mashirika yenye maslahi ya kitaifa na mawakala wa serikali wenye kitengo cha watu wenye ulemavu (mfano wizara ya afya, elimu, huduma za kijamii, nyumba, kazi za umma). Kuimarisha mitandao iliyopo. | X | | |
| Husisha, shauriana na tafuta mrejesho kutoka kwa watu wenye ulemavu na mashirika yao juu ya upatikanaji wa huduma na msaada na ulinzi. Tambua vikwazo na hatua za kuviondoa, pamoja na hatua zitakazo wezesha upatikanaji wa huduma. | | X | X |
| Tumia wafanyakazi waliofundishwa, andaa na tekeleza mfumo wa usajili unaowatambua watu wenye ulemavu kupitia taarifa za jinsia, umri, na ulemavu. Chukua hatua kujumuisha safu kamili ya aina za ulemavu.[113] | | X | X |
| Jumuisha watu wenye ulemavu katika tathmini, mipango ya utendaji, miundo ya kimkakati, utekelezaji wa programu na shughuli za ufuatiliaji. | | X | X |
| Hakikisha mipango inajumuisha mikakati ya kumaliza miradi na suluhu za kudumu, ambayo inafikika na kupatikana kwa watu wenye ulemavu na inaweza kubeba mahitaji yao. | | X | X |
| Hakikisha ukusanyaji, uhifadhi na uchakataji wa taarifa nyeti na taarifa binafsi unafanywa kwa kuzingatia misingi ya ulinzi sahihi wa taarifa. | | X | X |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Fikiria mahitaji ya watu wenye ulemavu tangu mwanzo, na kondoisha mahitaji yao katika kila hatua muhimu, juhudi za kutatua suala la kuhamishwa, uokoaji wa dharura, upatikanaji wa maeneo, upatikanaji wa huduma, utambuaji wa suluhu za kudumu, n.k. | X | X | X |
| Tambua maarifa na uzoefu unaohitajika katika timu. Fikiria kuajiri ili kupata utaalamu wa kutosha wa kiufundi. Ajiri wafanyakazi wenye ulemavu au wafanyakazi wenye ujuzi wa kujumuisha watu wenye ulemavu. Husisha mashirika ya watu wenye ulemavu ikiwezekana. | | X | |
| Hakikisha ufadhili unabadilika kutokana na mazingira. Fanya maboresho ya eneo ili kuondoa vizuizi. Chukua hatua za msingi na kutosheleza ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata huduma za moja kwa moja na wanaweza kushiriki katika nafasi za utawala na shughuli nyingine. (Angalia uwezekano wa utoaji usafiri, wakalimani wa lugha ya alama, n.k). | | X | |

[113] Angalia shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi, *kufanya kazi wa watu wenye ulemavu waliohamishwa kwa lazima* (2011), pia angalia zana za usajili na mahitaji maalum katika IOM, tume ya wakimbizi ya Norway, shirika la umoja wa mataifa la wakimbizi, *nyenzo za usimamizi wa kambi* (2015), uk. 141.

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurudisha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Husisha watu wenye ulemavu na mashirika ya watu wenye ulemavu katika kupanga maeneo na mikutano ya uboreshaji. Tafuta ushauri wao juu ya kuondoa vikwazo na kupunguza hatari za ulinzi. | | X | X |
| Saidia au anzisha utaratibu wa kiutawala ambao utahakikisha watu wenye ulemavu wana uwezo wa kushiriki katika michakato rasmi na isiyo rasmi ya mashauriano na kufanya maamuzi. | | X | X |
| Hakikisha kampeni za habari na njia za malalamiko na mrejesho zinapatikana kwa wote, bila kujali ulemavu, na zinasambazwa katika njia mbali mbali zinazoweza kupatikana (kwa mdomo, vipeperushi, lugha ya alama, lugha rahisi kusoma/iliyo wazi, n.k) na ni lugha inayoongelewa na jamii iliyoathiriwa. | | X | X |
| Fuatilia kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanafanikiwa kupata huduma kwa ujumla, ikilenga watu wenye ulemavu. | | X | X |
| Tengeneza kamati, kikundi cha maslahi, au kikundi cha msaada rika kwa makundi ya watu wenye ulemavu katika makambi. Chukua hatua kuhakikisha kwamba makundi na mashirika ya watu wenye ulemavu ndani na nje ya kambi yanawakilisha vya kutosha utofauti wa watu wenye ulemavu. | X | X | X |
| Hakikisha miundombinu ya kambi (vyoo, maji na makazi) vinatunzwa. Fanya mabadiliko na tambua rasilimali kukuza upatikanaji. | | X | X |
| Husisha watu wenye ulemavu katika kila shughuli na mchakato wa kufanya maamuzi unaohusiana na kutafuta suluhu za kudumu. Andaa ziara za 'Nenda na ukaone' na 'njoo useme'. | | | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Ratibu na tangaza utekelezaji wa viwango vya kimataifa katika kambi (ikiwemo mwongozo huu). Weka viwango na weka mbinu za kutathmini matumizi yake.[114] | X | X | X |
| Hakikisha kwamba sehemu za vikao zinafikika. Chukua hatua kutoa makao bora kwa watu wenye ulemavu (toa wakalimani, nyenzo rahisi kusoma, ongeza mwanga, n.k). | X | X | X |

[114] Angalia *mradi wa Sphere* (2018) na Help Age, CBM, Handicap International, *viwango vya ujumuishi wa masuala ya kibinadamu kwa wazee na watu wenye ulemavu* (2018).





| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurudisha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Saidia juhudi za mamlaka za kitaifa kushughulikia vizuizi vya upatikanaji na ujumuishaji ambao watu wenye ulemavu wanakumbana nao. Jadili suluhu na toa msaada unaofaa (kwa mfano, mafunzo na kujenga uwezo). | X | | |
| Pigia chapuo haki za watu wenye ulemavu; kwa ajili ya kuondolewa vikwazo ambavyo vinazuia ujumuishwaji na upatikanaji wa huduma na ulinzi; na kwa ajili ya ujumuishaji wa huduma zinazolengwa kwa watu wenye ulemavu katika majibu na mipango ya kisekta. | X | X | X |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Fanya utaratibu wa malalamiko na mrejesho kuwa rahisi kwa watu wote wenye kila aina ya ulemavu, bila kusahau wale wanaokaa katika makazi maalumu au nyumbani. | | X | X |
| Husisha wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana wenye anuwai ya uwakilishi katika shughuli za ufuatiliaji na timu za masuala husika. | | X | X |
| Kufuatilia upatikanaji wa maeneo na huduma, pamoja na hatari ya ulinzi (kujumuisha ukatili wa jinsia) ambayo yanaweza kuwaathiri watu wenye ulemavu. Fanya hivyo katika kaguzi za mara kwa mara. Shauriana na watu wenye ulemavu na timu za ulinzi, mashirika ya watu wenye ulemavu, n.k. | | X | X |
| Fanya tathmini na tumia matokeo yake kurekebisha programu na kuhakikisha ujumuishaji bora. Sambaza mafunzo na jumuisha mbinu bora katika mipango. | X | X | X |

## Rejea


- *Tovuti ya kitengo cha CCCM*
- Kitengo cha CCCM, *kituo cha pamoja cha miongozo* (2010)
- Kitengo cha CCCM, *Uhamisho wa Mijini na Mapitio Nje ya Kambi* (2013)
- *Kanuni za mwongozo wa uhamisho wa ndani* (2004)
- IASC, *afya ya akili katika muktadha wa dharura; mambo gani wadau wa afya wanapaswa kufahamu?* (2011)
- IOM, NRC, Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi, *mwongozo wa usimamizi wa kambi* (2015)
- Shirika la Umoja wa Mataifa la Wakimbizi, *hitimisho la wakimbizi wenye ulemavu na watu wenye ulemavu wanaolindwa na kusaidiwa na shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi* (2010)
- Taasisi za Umoja wa Mataifa za wakimbizi, *kufanya kazi na watu wenye ulemavu waliiohamishwa* (2019)

# 12 Elimu

## Utangulizi

Elimu nyakati za dharura huokoa na kudumisha hali ya kisaikolojia, kimwili na uwezo wa kiutambuzi. Inaweza kudumisha maendeleo ya watoto ambao walikuwa shule na kutengeneza fursa kwa wale walioikosa, kupitia programu za elimu ya mwendo wa haraka, mafunzo ya ufundi na programu zingine rasmi na zisizo rasmi za ujifunzaji. Kupitia elimu, watu wanaoishi katika majanga hujifunza ujuzi wa kuishi na mikakati ya kupunguza hatari, ikiwemo namna ya kujiokoa wenyewe kutoka katika unyanyasaji wa kijinsia, maambukizi na vifaa vya milipuko na kupata taarifa muhimu kuhusu haki zao na kuhusu elimu na lishe. Elimu inaweza kubadilisha, kujenga amani ambayo inaimarisha ustahimilivu kwa majanga ya baadaye na kutoa nafasi ya hali kurudi kawaida na utaratibu wa siku kwa siku kwa mtoto, vijana na watu wazima ambao wameathiriwa kwa kiasi kikubwa na majanga ya dharura.

Ujumuishi na elimu yenye usawa wakati wa dharura inaweza kuhamasisha fursa za ujifunzaji kwa wote, kuboresha matokeo na kuleta ubunifu, kusaidia serikali kurejesha hali ya ubora na kujenga mifumo jumuishi inayoibuka kutokana na majanga.

Wakati wa dharura, mashirika ya huduma za kibinadamu huwa na wajibu wa msingi katika kurejesha mifumo ya elimu kwa kusaidia juhudi za serikali. Hii inaweza kuwa ni fursa ya kimabadiliko, iwapo serikali itaridhia na kuweka kipaumbele cha ujumuishi kwa wanafunzi wenye ulemavu, na kuhakikisha kuwa miundo elimu ya kitaifa inaendana na viwango vinavyotambulika kimataifa na miongozo ya ujumuishi kwa watu wenye ulemavu.

Angalia pia kwenye kipengele cha maji na usafi wa mazingira yaani UKUK, Afya Lishe na Ulinzi.

### Rejea

- Lengo la 4 la maendeleo endelevu
- Mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu
- Mpango wa kuchukua hatua wa Dakar
- Tamko la Salamanca na mpango wa kuchukua hatua
- Mkataba wa kimataifa wa haki za watoto
- Mkataba wa kimataifa wa kuondoa aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake
- Mkataba wa Kimataifa wa haki za Kiuchumi, Kijamii na Kiutamaduni 1966
- Haki za binadamu zinazofanana ulimwenguni kote

## Dhana muhimu

**Elimu wakati wa dharura** inamaanisha programu ambazo zinatoa fursa za ujifunzaji katika hali za majanga kwa watu wa umri wote. Programu zinazotolewa zinahusisha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, elimu ya msingi, elimu ya sekondari, elimu isiyo rasmi, elimu ya ufundi, elimu ya juu, na elimu ya watu wazima. Elimu wakati wa dharura inatoa ulinzi wa kisaikolojia na kiutambuzi ambao inaweza kudumisha na kuokoa maisha. Elimu hii ni muhimu katika hali za migogoro, vurugu, kuhamishwa kwa nguvu, majanga na dharura za kiafya. Kimsingi elimu nyakati za dharura ni pana lakini ni kiungo muhimu cha "Huduma za elimu wakati wa dharura.[115]

**Mifumo ya elimu jumuishi** inahusisha wanafunzi wote na kuwakaribisha na kuwasaidia bila ya kujali historia, uwezo au mahitaji yao. Ili kufikia lengo hili, ufundishaji, mitaala, majengo ya shule, madarasa, maeneo ya michezo, usafiri, na maliwato vinatakiwa kuwa ni rafiki kwa watoto katika ngazi zote. Elimu jumuishi inamaanisha kuwa watoto wote wanajifunza pamoja katika shule moja.[116]

**Elimu maalum** inatoa elimu kwa watoto wenye ulemavu katika maeneo yaliyotengwa kama vile shule maalum au vituo, ambavyo mara nyingi vimetengwa mbali na jamii, pamoja na watoto wengine na shule za kawaida.[117] Shule maalum huandaliwa kulingana na aina ya ulemavu (kwa mfano shule ya wasioona na au viziwi [118]).

**Wanafunzi** inamaanisha ni wale ambao wamejiunga katika shughuli za kielimu na pia ambao wanatakiwa kuwa shule lakini wametengwa na mfumo wa elimu. Wanafunzi wenye ulemavu ni pamoja na wanawake, wanaume, wasichana na wavulana. Wanaweza kuwa na aina yoyote ya elimu rasmi au isiyo rasmi kutoka katika malezi ya awali ya mtoto na programu za maendeleo katika shule za msingi, sekondari au elimu ya juu au katika elimu za ufundi au mafunzo yanayosomwa maisha yote na endelevu.

**Walimu** ni pamoja na waelimishaji wanaojihusisha na kufundisha watoto moja kwa moja. Wanaweza kuwa waalimu wa madarasa, waalimu wa elimu maalum au aina nyingine ya waalimu. Wanaweza kufanya kazi na wanafunzi ndani ya darasa zima katika darasa, katika vikundi vidogo vidogo, au uso kwa uso na mwanafunzi mmoja mmoja au katika darasa la kawaida.[119]

**Ufikivu** unahusisha majengo, taarifa, mawasiliano, mitaala, vifaa vya elimu (ikiwemo vitabu vya kiada) mbinu za mafunzo, tathmini, lugha, huduma za usaidizi, usafiri wa shuleni, maji na usafi, bwalo za shule na maeneo ya burudani.

## Vikwazo

Wanafunzi wenye ulemavu huathirika na kutengwa katika mifumo ya elimu ikiwemo katika hali za dharura.

Vikwazo vinavyowafanya wanafunzi wenye ulemavu kuwa nje ya mfumo wa malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto, shule, vyuo na vyuo vikuu huongezeka wakati wa migogoro na hali za dharura. Vikwazo vinaweza kuwa ni vya kimazingira, kimtazamo au kitaasisi.

Neno '**Makutano ya hali tofauti**' linatambua vipengele vingi vya utambulisho wa mtu kama vile jinsia, kabila, umri, hadhi ya kiuchumi na ulemavu. Hali hizi huingiliana katika namna ambazo zinasababisha faida au hasara. Makutano ya hali tofauti yanaweza kuleta ushawishi katika kiwango ambacho mwanafunzi anaweza kuathiriwa au la, ikiwemo kujumuishwa katika juhudi za kujiweka tayari, kukabiliana na dharura, kupata huduma na urejeshaji hali ya kawaida. Pia ni muhimu kutambua kuwa hali hizi zinapatikana katika ulemavu. Mvulana mwenye ulemavu wa akili au ulemavu wa viungo wanakabiliwa na vikwazo tofauti na wanaweza kuwa na uwezo tofauti na mvulana ambaye ni kizivi au asiyeona. Watu wenye ulemavu wa akili, hasa wanawake na wasichana wanaweza kuathiriwa zaidi wakati wa kutoa huduma za kibinadamu.[120]

Hizi pamoja na sababu zingine ikiwemo eneo na umbali vinapaswa kuainishwa kwa utaratibu na kuondolewa kwa kutumia mikakati ya kuhakikisha kuwa elimu na mafunzo endelevu nyakati za dharura ni jumuishi.

[115] *Mtandao wa mashirika mbalimbali wa elimu wakati wa dharura*.

[116] UNICEF, *elimu jumuishi-ikiwemo watoto wenye uleamvu katika elimu bora, nini kinapaswa kufanywa* (2017).

[117] Shirika la kimataifa la Handicap, *Andiko la sera kuhusu elimu jumuishi* (2012), uk. 10–12.

[118] Shirika la Save the Children, *shule kwa wote, ikiwemo watoto wenye ulemavu katika elimu* (2002), uk. 10.

[119] INEE, *viwango vya awali vya elimu: utayari, mwitikio, urejesho* (2010), uk. 94.

[120] EENET, *Matokeo ua kuhakikisha kuwa ufikivu sawa na ujumuishi wa watu wenye ulemavu wa akili na afya ya akili katika kupunguza hatari ya majanga na masuala ya kibinadamu, mapitio ya nadharia* (2017).





**Mchoro namba 7 |** Vikwazo vya ufikivu na ujumuishi katika elimu

### NAMNA ATHARI ZA MAJANGA ZINAVYOONGEZEKA KWA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA ELIMU

**ATHARI ZA MAJANGA**

Kufungwa shule, kuharibika kwa miundombinu ikiwemo barabara za kuingia na kutoka shule, kuhamishwa kunakopelekea kupunguza uwezo wa waalimu, kukosekana kwa ulinzi, kuharibika kwa mitandao ya kijamii

**VICHOCHEO VYA VIKWAZO**

**Vikwazo vya kimazingira:**

- Usafiri usiofikika na usio salama, barabara, majengo, viwanja vya michezo, vifaa vya maji na usafi, n.k.
- Ukosefu wa vifaa vya usaidizi na mifumo mbadala ya mawasiliano.
- Majengo ya muda yasiyotosheleza na maeneo machache ambayo ni rafiki kwa watoto.

**Vikwazo vya kimtazamo:**

- Ubaguzi kwa wanafunzi wenye ulemavu
- Wafanyakazi wa elimu kudhania kuwa wanafunzi wenye ulemavu hawana uwezo wa kujifunza au kunufaika na elimu.

**Vikwazo vys kitaasisi**

- Ukosekana kwa uwezo wa kitaalamu wa kukuza ujumuishi kwa wanafunzi wenye ulemavu katika sera na mipango ya elimu,
- Kukosekana kwa sera ya elimu jumuishi na mipango,
- Kutokuwepo kwa bajeti kwa sababu ya elimu jumuishi.

**Hatari zinazowakabili watu wenye ulemavu**

Ukatili, umaskini, hatari za kimazingira, kuporomoka kwa afya, kutengwa, kujitenga, kuonewa, hatari za ukatili na unyayanyasaji wa kingono.

## Viwango na miongozo mingine

- Mtandao wa kitaasisi katika elimu wakati wa dharura, viwango vya elimu; kujiweka tayari na kurejesha jamii katika hali ya kawaida (2010)
- Shirika la Help Age, CBM, Handicap International, viwango vya ujumuishi kwa wazee na watu wenye ulemavu- kipengele cha elimu (2018)
- Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi, viwango vya elimu vya dharura (toleo 1.5)
- INEE, mwongozo wa usaidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu (2010)
- INEE, Elimu katika dharura: kujumuisha kila mtu (2009, INEE, mwongozo wa elimu jumuishi)
- Shirika la Umoja wa Mataifa, elimu katika dharura

## Mambo muhimu ya kufanya

Mambo muhimu ya kufanya yanapaswa kufanyika katika hatua zote za masuala ya kibinadamu wakati wa utekelezaji wa programu za elimu jumuishi kwa watu wenye ulemavu.

### Ushiriki

- Hakikisha kwa watu wenye ulemavu, watoto, familia zao na mashirika ya watu wenye ulemavu yanahusishwa na kushiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi, kuainisha vikwazo, kupanga, kubuni, kutekeleza, kufuatilia, na kutathmini sera na mipango yote inayosaidia ufikivu wa elimu kwa wanafunzi wenye ulemavu.
- Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanawakilishwa kwa kuzingatia aina mbalimbali za ulemavu wao pamoja na umri, jinsia na anuwai mbalimbali. Fanya juhudi za makusudi katika kuhimiza makundi yenye uwakilishi mdogo kama vile watu wenye ulemavu wa afya ya akili, watu wenye asili ya eneo hilo, wanawake, na wasichana katika mifumo rasmi na isiyo rasmi.
- Kuza ushirikiano na mashirika ya watu wenye ulemavu pamoja na mashirika yanayofanya kazi katika elimu, wahusishe katika kuwasaidia walimu na wanafunzi wenye ulemavu, kutoa usaidizi kwa mtu mmoja mmoja na hamasisha suala la elimu jumuishi.

### Kushughulikia vikwazo

- Ainisha na fuatilia vikwazo na suluhu kwa ajili ya elimu na ujifunzaji ili kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu kufikia mahitaji yao na mahitaji ya kisaikolojia.
- Ili kuhakikisha kuwa elimu ni fikivu kwa wanafunzi wenye ulemavu, wezesha wanafunzi wote kujiunga katika mafunzo ya pamoja na kufanya marekebisho stahiki katika kufikia mahitaji kwa kuondoa vikwazo katika kushiriki katika mazingira ya kawaida na ya kidijitali[121]. Weka maeneo ya ujifunzaji na maeneo ambayo watoto watacheza, watakula na kukusanyika[122].
- Himiza watoa huduma kutumia kanuni ya usanifishaji kwa ajili ya watu wote wakati wa kupanga na kujenga majengo ya elimu na ujifunzaji.
- Hakikisha kuwa tathmini ya elimu na nyenzo za kutoa taarifa pamoja na taarifa za mawasiliano vinatolewa katika mifumo fikivu, ili kufikia mahitaji ya watu wenye uziwi, wasioona na wenye ulemavu wa afya ya akili.
- Panga kufanya kampeni za kukuza uelewa ili kuelezea ubaguzi na unyanyapaa na himiza haki za watu wenye ulemavu.
- Pitia sera za kisekta, miongozo, na nyezo za kuhakikisha kuwa zinafuata misingi ya haki za watu wenye ulemavu katika ufikivu na ujumuishi.

[121] Kwa taarifa zaidi kuhusu ufukivu wa kidigitali, angalia CBM, Nyenzo za ufikivu wa kidigitali (2018).

[122] Angalia kiambatisho namba 7 kwa ajili ya orodha ya ufikivu wa maeneo ya kusomea, angalia ibara namba 9 ya CRPD kuhusu ufukivum kuainisha hatua zinazochukuliwa na nchi wanachama katika kuwezesha watu wenye ulemavu kuishi kwa kujitegemea na kushiriki katika nyanja zote za maisha.





### Uwezeshaji na kujengewa uwezo

- Kondoisha masuala ya ulinzi na ukingi katika shughuli zote za kielimu na ujifunzaji. Wajulishe wanafunzi wenye ulemavu kuhusu hatua za kupata ulinzi na hifadhi na namna ya kuzifikia. Tambua masuala ya kijinsia katika baadhi ya hatari zinazohusiana na ulinzi na uhifadhi.
- Jengea uwezo walimu na wafanyakazi wa shule (ikiwemo wafanyakazi wanaohusika katika usafirishaji, bwalo, na shughuli zingine zinazohusiana na huduma za kielimu). Toa mafunzo ya uelewa kuhusu misingi jumuishi ya ufundishaji na haki za watu wenye ulemavu.
- Jengea uwezo mashirika ya watu wenye ulemavu katika kuwezesha kuchangia katika kubuni, kutoa na ufuatiliaji wa program za elimu.
- Shirikisha watu wenye ulemavu na mashirika ya watu wenye ulemavu katika kuhamasisha jamii na shughuli za nje.
- Hakikisha kuwa mifumo ya elimu jumuishi (ikiwemo ushirikiano wa kimataifa) yanaweza kujumuisha na kufikia mahitaji ya watu wenye ulemavu.

### Ukusanyaji wa takwimu na ufuatiliaji

- Kusanya na chambua taarifa juu ya watu wenye ulemavu, chambua kwa mrengo wa jinsia, umri na ulemavu. Fanya kwa utaratibu maalum katika mzunguko wa programu zote za masuala ya kibinadamu, katika usimamizi wa mifumo ya taarifa za kielimu, kanzidata za utoaji taarifa kitaifa na mifumo mingine. Pale ambapo taarifa za uhakika hazipatikani au haziwezi kukusanywa tumia makadirio ya asilimia 15 kuhusu uwepo wa watu wenye ulemavu.[123]
- Ainisha huduma zinazopatikana, miundombinu ya elimu ambayo ni fikivu, mashirika ya watu wenye ulemavu na wadau muhimu na maeneo ambayo wanafunzi wenye ulemavu wanaishi.
- Kwa pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu pamoja na jamii, ainisha makundi au watu binafsi wenye ulemavu ambao wapo nje ya mfumo wa shule pamoja na wale wanaohitaji msaada wa haraka. Waunganishe katika huduma za uhifadhi, afya pamoja na huduma nyingine muhimu.
- Sambaza taarifa juu ya mahitaji ya watu wenye ulemavu katika sekta mbalimbali na katika uratibu wa kitaasisi (kama vile masuala ya usafi na maji, uhifadhi, afya, n.k) na hakikisha uratibu wa kisekta.
- Hakikisha kuwa maadili ya kupata taarifa na kanuni za uhifadhi taarifa (ikiwemo usiri, kutoa taarifa, kutoa ridhaa huru, na ulinzi) vinaheshimiwa popote ambapo taarifa kuhusu watu wenye ulemavu zitakusanywa na kutumiwa.[124]
- Pitia viwango vya elimu na nyezo na hakikisha kuwa zinapendekeza ukusanyaji wa takwimu juu ya wanafunzi wenye ulemavu na zinachambuliwa kwa jinsia, umri na ulemavu.

Miongozo hii inafuata viwango vya *"Mtandao wa Mashirika MbaliMbali Kuhusu Elimu Katika Majanga"*. Viwango hivi vinatumika katika dharura ikiwemo majanga ya asili na yale yanayosababishwa na binadamu, katika hali za migogoro, na majanga yanayotokea taratibu au kwa haraka, katika mazingira ya mijini na vijijini. Viwango hivi vinafuata haki, mahitaji na utu wa watu walioathiriwa na majanga.

Mamlaka za kielimu na mashirika ya kibinadamu yanapaswa kutumia mtazamo pacha wa kukuza elimu jumishi katika dharura. Afua mahsusi za ulemavu zinazolenga kufikia mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu zinapaswa kuwa nyongeza katika afua za kawaida ambazo zinawanufaisha wanafunzi wote.

[123] Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia, Ripoti ya dunia kuhusu ulemavu (2011)

[124] Angalia ICRC, viwango vya kitaalamu kwa kazi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na haki za binadamu katika hali za vurugu (2018), sura ya 6, usimamizi wa takwimu na taarifa za matokeo ya ulinzi uk. 106–148; na CRPD, Ibara 22(2).

**PROGRAMU ILIYOIKONDOISHWA**

Vifaa vya elimu, programu zinabuniwa na kutumika kuhakikisha kuwa zinajumuisha na ni fikivu kwa kila mtu, ikiwemo wanafunzi wenye ulemavu. (Kwa mfano waalimu wanapewa mafunzo kuhusu mbinu za ualimu jumuishi, mitaala inatoa kipaumbele kwa wanafunzi, n.k).

**WALENGWA**

Programu za kielimu zinabuniwa kwa kuzingatia mahitaji ya kipekee ya wanafunzi wenye ulemavu (kwa mfano vifaa vya ujifunzaji ni fikivu, vifaa vya usaidizi vinatolewa, n.k).

Miongozo ifuatayo itawasaidia wadau wa elimu katika kuanisha na kushughulikia vikwazo wanavyokabiliana navyo watu wenye ulemavu pamoja na familia, wasaidizi na walezi wao wakati wanafanya juhudi za kupata na kufikia programu za elimu katika muktadha wa huduma za kibinadamu.

## Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathimini, uchambuzi na mipango** | | | |
| Kwa kushirikiana na mashirika ya watu wenye ulemavu, fanya tathmini za kuainisha na kuchambua vikwazo vinavyosababisha watoto, vijana na watu wazima, wanafunzi wenye ulemavu kukosa fursa za kielimu. Fanya hivi kwa kushirikiana na sekta zingine (kama vile zinazohusu ulinzi wa mtoto, huduma za afya ya akili, maji na usafi) ili kuwa na programu zilizoratibiwa na kupunguza uchovu mkubwa katika kufanya tathmini. | | X | |
| Tumia Zana ijulikanayo kitalamu kama "the Global Education Cluster's Joint Education Needs Assessment Toolkit" katika (1) kuzuia kutengwa kwa wanafunzi wenye ulemavu katika mfumo wa kawaida; (2) kuhakikisha kuwa marekebisho stahiki yanafanyika wakati yanapohitajika; (3) kuelezea athari za majanga kwa wanafunzi wenye ulemavu pamoja na mifumo ya elimu. Ainisha mapungufu ya kiuwezo na mapungufu katika kutoa elimu jumuishi kwa wanafunzi wenye ulemavu. | X | | |
| Panga hatua za kuimarisha mifumo ya elimu jumuishi (kwa kupata mawazo na rasilimali rejea kutoka katika mfumo ujulikanao kitaalamu kama "*INEE, Pocket Guide to Learners with Disabilities*". | X | X | |
| Pata ushauri kutoka katika vyanzo vya mbalimbali vya taarifa katika kuchambua uwezo na mapungufu katika elimu jumuishi. | X | | |
| Anzisha mifumo ya rufaa katika kuwapa wanafunzi wenye ulemavu na familia zao aina mahsusi za usaidizi, weka usaidizi wa kifedha, viungo bandia na huduma za uhifadhi na ulinzi n.k). | X | X | X |





| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Ainisha na kusanya rasilimali (Usafiri unaofikika, programu za kijamii, aina zinginezo za usaidizi) katika kuongeza ufikivu wa elimu jumuishi. | X | X | |
| Tenga fedha na andaa bajeti jumuishi ambazo zitatenga rasilimali kwa ajili ya ufikivu na ujumuishi. | | X | X |
| Hakikisha kuwa elimu jumuishi inawekwa katika maandiko ya kuomba fedha, hakikisha kuwa maandiko ya kuomba fedha yanatenga rasilimali kwa ajili ya miundombinu fikivu, na vifaa vya usaidizi na kuweka marekebisho stahiki. | | X | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Kwa kushirikiana na mashirika ya watu wenye ulemavu, tengeneza mkakati wa kutoa huduma za kibinadamu ambao utaondoa vikwazo mahsusi katika elimu jumuishi vinavyowakabili wanafunzi wenye ulemavu. | | X | |
| Jengea uwezo na uelewa wafanyakazi wa sekta ya elimu (wakiwemo waalimu, madereva na wafanyakazi wa bwaloni) juu ya elimu jumuishi na tumia (na fuatilia) matumizi ya vifaa saidizi. Weka ratiba ya matengenezo /ukarabati stahiki. | X | X | |
| Zifanye jamii kuelewa juu ya umuhimu wa elimu jumuishi na umuhimu wa kupinga ubaguzi na unyanyapaa. | X | X | X |
| Tengeneza vifaa vya ujifunzaji ambavyo ni thabiti, vinavyozingatia tamaduni na kujumuisha wanafunzi wote. | X | X | X |
| Hakikisha kuwa wahandisi na wasanifu majengo wanatumia kanuni ya usanifishaji kwa ajili ya matumizi ya watu wote wakati wa kujenga shule pamoja na majengo mengine. | X | X | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Husisha mashirika ya watu wenye ulemavu katika vitengo na katika uratibu wa kitaasisi. | X | X | X |
| Tengeneza mifumo ya rufaa ambayo itawaunganisha watu wenye ulemavu katika huduma mahsusi (kama vile uchunguzi, utambuzi na tiba ya mazoezi ya kuongea) ili kukuza elimu jumuishi na kutambua wanafunzi wanaohitaji msaada mahsusi. | X | | |
| Fanya kazi na programu za uhawilishaji fedha katika kuondoa vikwazo vya kifedha (kama vile gharama za usafiri na vifaa vya usaidizi) ambazo zinazuia kaya ambazo zina watoto wenye ulemavu kuzifikia fursa za kielimu. Fanya kazi na programu za uwezeshaji kimaisha na hakikisha kuwa kaya zenye watoto wenye ulemavu zinaweza kukabili gharama hizo kwa muda mrefu. | | X | X |
| Fanya uratibu wa wadau wa lishe katika kutoa taarifa muhimu za lishe. Fanya kazi kwa pamoja katika kusaidia utendaji wenye tija wa lishe kwa watoto wenye ulemavu. Saidia katika kuanzisha michakato ya kutoa huduma kwa watoto wenye ulemavu ambao wapo nje ya shule au waweze kupata huduma za kielimu wakiwa nyumbani. | | X | X |

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **5. Tathmini na ufuatiliaji** | | | |
| Kusanya taarifa za msingi juu ya usajili wa wanafunzi wenye ulemavu katika kuwezesha ufuatiliaji katika ngazi ya programu na ngazi za kitaifa. Fanya utetezi kuhusu utendaji wenye tija pamoja na kutumia moduli ya Kundi la Washington Group kuhusu Ukuaji wa Watoto iliyotengenezwa na shirika la UNICEF katika mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa taarifa za kielimu. | X | X | |
| Fuatilia ufanisi wa uhifadhi na hatua za kulinda wanafunzi wenye ulemavu . | | X | X |
| Wahusishe wanafunzi wenye ulemavu, na wazazi wao na mashirika ya watu wenye ulemavu katika kufuatilia na kutathmini shughuli za kielimu. Hakikisha kuwa matokeo yanajadiliwa na kusambazwa . | | X | X |
| Tengeneza mfumo wa usimamizi wa maarifa katika kushirikisha mafunzo na utendaji wenye tija kuhusu elimu jumuishi. Anzisha mifumo ya usaidizi wa shule kwa shule ili kuimarisha uwezo. | X | X | X |

## Rejea


- Kamati kuhusu mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu, maelezo ya jumla namba 4 katika ibara ya 24, haki ya elimu (2016)
- INEE, *Mwongozo wa Kusaidia Wanafunzi wenye Ulemavu* (2010)
- INEE, *Mwongozo wa elimu jumuishi* (2009)
- INEE, *Mwongozo wa usaidizi wa kisaikolojia na ujifunzaji wa kihisia na kijamii* (2018).
- INEE, *Elimu jumuishi*
- INEE, *Walimu katika muktadha wa migogoro, mafunzo kwa walimu wa shule za msingi*
- *Kikosi kazi cha mashirika kuhusu elimu ya kuharakishwa*
- Kett, M., *hatari, ustahimilivu na ujumuishi katika masuala ya kibinadamu*, UNICEF, hali ya watoto ulimwenguni (2013)
- *Saebones, A. M., et al., Kuelekea katika Elimu jumuishi: andiko la awali kwa ajili ya mkutano wa Oslo (2015)*
- UNICEF, *Kuwajumuisha watoto wenye ulemavu katika masuala ya kibinadamu: Mwongozo wa elimu* (2018)
- Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi, *mwongozo wa elimu katika dharura*
- UNICEF, *Maendeleo ya awali ya mtoto katika muktadha wa dharura: Mwongozo wa programu zilizojumuishwa* (2014)
- UNICEF, *Maendeleo ya awali ya mtoto katika masuala ya kibinadamu*
- UNICEF na kundi la Washington kuhusu takwimu za ulemavu, *moduli za elimu jumuishi* (inayokuja)

# 13 Usalama wa chakula na lishe

## Utangulizi

Kila binadamu ana haki ya kupata chakula kinachotosheleza na kuwa huru dhidi ya janga/baa la njaa. Haki hii inatambuliwa katika vyombo vya kimataifa na sheria za kimataifa ikiwemo Sheria ya kimataifa ya ubinadamu ambayo inatoa mwongozo kuhusu hali za kivita.

Ulemavu unahusishwa na usalama wa chakula na lishe kwa namna nyingi. Ulemavu huathiri vibaya usalama wa chakula na lishe katika kaya. Utafiti unaonesha kuwa kaya ambazo zina watu wenye ulemavu hupatwa na changamoto ya uhaba wa chakula, kwa sababu wanakuwa na rasilimali chache za kiuchumi pamoja na fursa chache za kazi, huhitaji zaidi huduma za kiafya na kutumia muda mwingi wa ziada katika kazi ya ulezi na uangalizi. Wakati mtu mwenye ulemavu anaongoza kaya na akiwa ndio mkuu wa kutafuta kipato, uwezekano wa kuingia katika ukosefu wa chakula huongezeka. Viwango vya utapiamlo vinaweza kuongezeka baina ya watu wenye ulemavu wakati wanakabiliana na ugumu wa kula au kumeza wanapokuwa wagonjwa mara kwa mara au wanapopuuzwa.[125] Ni muhimu kukumbuka kuwa dharura zinazotokea taratibu au zile za haraka zinaweza kuwa na athari tofauti, hasa katika uhaba wa chakula kwa watu wenye ulemavu.

Angalia pia masuala ya Usafi wa maji, Afya na Elimu.

### Sheria muhimu na miundo mingine

- Mkataba wa haki za watu wenye ulemavu
- Lengo namba 2 la maendeleo endelevu
- Mkataba wa haki za watoto
- Mkataba wa haki za wanawake

## Dhana muhimu

**Uhawilishaji wa fedha** na **afua za fedha** ni maneno yanayoweza kutumiwa kwa kubadilishana katika kuelezea programu zinazotoa fedha taslimu au vocha kwa wanufaika katika kuwawezesha kununua bidhaa au huduma moja kwa moja. Katika muktadha wa kibinadamu, inamaanisha fedha taslimu au vocha zinazotengwa kwa ajili ya watu, kaya au jamii wanaopokea fedha; hii haihusishi fedha zilizotengwa kwa ajili ya serikali na wadau wengine wa serikali.[126]

**Ufikivu wa chakula** unamaanisha kuwa watu wa rika tofauti na jinsia kutoka katika anuwai mbalimbali wanaweza kupata viwango vya kutosha ya chakula kinachohitajika katika kutoa lishe bora, kwa kununua, kutengeneza nyumbani, kwa kubadilishana, kupitia zawadi au kuazimwa au msaada wa chakula

[125] Watoto wenye ulemavu wanaweza kuhitaji muda zaidi wa kuwasaidia kula iwapo watapata ujungu wakati wa kunyonya, kushika kijiko, kukaa wima, n.k. Nora Groce, Eleanor Challenger, Marko Kerac, *imara pamoja: mashirikiano ya lishe na ulemavu na mashirikiano, Muhtasari mfupi, UNICEF* (2017), *Kuhusisha watoto wenye ulemavu katika masuala ya kibinadamu. Lishe* (2011) uk. 13.

[126] Umechukuliwa kutoka katika ushirikiano wa mafunzo ya fedha, *kumbukumbu ya uhamishaji wa fedha*.

(lengo namba 2.1 la Maendeleo Endelevu). Watu wenye ulemavu wanaweza kukosa upatikanaji wa uhakika wa chakula Pamoja na chakula bora.

**Upatikanaji wa chakula** inamaanisha uwepo, uthabiti wa viwango toshelevu wa chakula katika kufikia mahitaji ya eneo husika. Inaweza kufikiwa kupitia uzalishaji wa ndani au kwa njia ya misaada kutoka nje.

**Ustahimilivu wa chakula** unamaanisha wingi, ugumu au ugiligili wa chakula ambacho kinatolewa kwa watoto na watu wazima, ikiwemo wazee ambao hupata shida ya kula. Ustahimilivu wa chakula unasaidia kujua urahisi au ugumu wa chakula kutafunwa na kumezwa. Kigezo kikubwa cha ustahimilivu wa chakula ni chakula ambacho hakijabadilishwa, chakula laini (kama vile ndizi) chakula cha kusagwa au kilichochanganywa.[127]

**Usalama wa chakula** unafikiwa wakati jamii ina ufikivu wa kimazingira, kijamii na kiuchumi wa chakula toshelevu, salama na bora katika juhudi za kupata chakula pendwa na mahitaji ya chakula bora kwa ajili ya maisha yenye afya bora (Malengo endelevu 2.3, 2.4).[128]

**Utoshelevu wa chakula** inamaanisha upatikanaji wa vipimo vyote vya ufikivu wa usalama wa chakula. Inagusia uhitaji wa jamii katika upatikanaji wa chakula kwa kipindi fulani.

**Matumizi ya chakula** inamaanisha athari za lishe wakati wa uchakataji, upikaji na kutumia chakula. Inahusisha upikaji, utunzaji, na hali za usafi, afya binafsi, maji na mazingira, kula na mazoea ya ushirikiano katika kaya.[129]

**Msaada wa chakula kwa ajili ya mafunzo/mali** inaelezea juhudi ambazo zinalenga kufikia mahitaji ya moja kwa moja ya chakula kwa jamii iliyoathirika kupitia fedha tasilimu, vocha au uhaulishaji wa chakula, wakati wa ujenzi au ukarabati wa mali ambao utaboresha usalama wa chakula wa muda mrefu pamoja na umadhubuti.[130]

**Usaidizi wa hisani** unamaanisha ni utoaji wa bidhaa moja kwa moja (chakula) au huduma kwa wanufaika. Usaidizi wa hisani utabakia kuwa suluhisho muhimu katika nyakati za majanga.

**Riziki** inamaanisha namna zote ambazo watu wanapata mahitaji yao kwa ajili ya maisha, inahusisha wigo mpana wa aina mbalimbali za kazi, ambazo zinalipwa kwa aina mbalimbali (kwa mfano kazi kwa chakula, kwa pesa tasilim au kwa mshahara.

**Utapiamlo** ni hali ya kisaikolojia inayosababishwa na hali ya kuwa na uhaba wa virutubisho au kuwa na virutubisho visivyo na uwiano au kutumia virutubisho vingi kupindukia.[131]

**Hali ya lishe**[132] ni hali ya kisaikolojia ya mtu ambayo inatokea katika mahusiano ya ulaji wa virutubisho na mahitaji na uwezo wa mwili katika kumeng'enya, kuchukua na kutumia virutubisho.

## Rejea


- Handicap International, CBM, Helo Age Interational, *viwango vya ujumuishi katika masuala ya kibinadamu kwa wazee na watu wenye ulemavu* (2018). Angalia sehemu ya chakula, lishe na riziki
- *Kitabu cha Sphere* (2018). Angalia kipengele cha usalama wa chakula na lishe
- *Mwongozo na viwango vya dharura kwa mifugo*
- *Matakwa ya Chini ya Kurejesha Uchumi katika Hali yake ya Kawaida* (2017)
- Cash Learning Partnership, *matakwa ya chini ya uchambuzi wa masoko*,(2018)


[127] UNICEF, *Kuhusisha watoto wenye ulemavu katika masuala ya kibinadamu, Lishe* (2017), uk. 108.

[128] Imechukuliwa kutoka IFAD, WFP, FAO, *hali ya usalama wa chakula ulimwenguni: hatua mtambuka katika usalama wa chakula* (2018), uk. 50.

[129] Kwa ufafanuzi wa Shirika la mpango wa chakula (WFP) kuhusu ufikivu wa chakula, upatikanaji na matumizi, angalia *kitabu cha tathmini ya usalama wa chakula katika dharura* (EFSA)-Toleo la pili (2009).

[130] WFP, usaidizi wa chakula kwa ajili ya mali.

[131] IFAD, WFP, FAO, *hali ya usalama wa chakula ulimwenguni: hatua mtambuka katika usalama wa chakula* (2018), uk. 50.

[132] Hakuna mwongozo uliopo kwa sasa wa kupima hali ya lishe kwa watu wenye ulemavu. Njia za kawaida kama MUAC (Mid-Upper Arm Circumference), inaweza kutumika, lakini hizi njia zinaweza kupotosha kwa mfano iwapo watu wenye ulemavu wanatumia mikono katika kusaidia ujongevu. Chanzo: *Viwango vya ujumuishi katika masuala ya kibinadamu kwa wazee na watu wenye ulemavu*.





**Mchoro namba 8 |** Vikwazo vya ufikivu na ujumuishi katika usalama wa chakula na lishe

**NAMNA ATHARI ZA MAJANGA ZINAVYOONGEZEKA KWA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA MUKTADHA WA USALAMA WA CHAKULA NA LISHE**

**ATHARI ZA MAJANGA**

kuharibika kwa miundombinu ikiwemo barabara kuelekea katika usaidizi, kuhamishwa, kukosa usalama, kuharibika kwa mitandao ya kijamii, kufungwa kwa huduma.

**VICHOCHEO VYA VIKWAZO**

**Vikwazo vya kimazingira:**
- Maeneo ya usambazaji wa chakula yasiyo salama na yasiyofikika
- Kukosekana kwa taarifa na mawasiliano yasiyofikika yanayohusiana na haki ya kupata chakula, usambazaji pamoja na programu za lishe
- Usafiri usiofikika, majengo na utaratibu wa ufungashaji wa shakula

**Vikwazo vya kimtazamo:**
- Waokozi kukosa uelewa na maarifa kuhusu watu wenye ulemavu
- Kukosa uelewa na maarifa kuhusu mahitaji mahsusi ya lishe kwa watu wenye ulemavu

**Vikwazo vya kitaasisi:**
- Kukosekana kwa uwezo wa kitaalamu katika kukuza ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika sera na programu za usalama wa chakula na lishe
- Sera na programu za serikali za usalama wa chakula na lishe kutokuwa jumuishi kwa watu wenye ulemavu, na kukosekana kwa taarifa sahihi za watu wenye ulemavu na maeneo yao mahususi
- Ukosefu wa takwimu sahihi za watu wenye ulemavu na wanapoptatikana

**Hatari zinazowakumba watu wenye ulemavu**

Ukatili, umaskini, hatari za kimazingira, kudorora kwa afya, kutengwa, kujitenga, vikwazo katika kufikia usaidizi wa chakula, utapiamlo.

## Mambo muhimu ya kufanya

Mambo muhimu ya kufanya yanapaswa kufanyika katika hatua zote za masuala ya kibinadamu wakati wa kutekeleza programu jumuishi za chakula na lishe kwa watu wenye ulemavu.

### Ushiriki

- Hakikisha watu wenye ulemavu na familia zao pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu wanashiriki kikamilifu katika kuainisha vikwazo katika kupanga, kubuni, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini sera na programu za chakula na lishe. Zingatia wigo mpana wa masuala mbalimbali ikiwemo maeneo sahihi, muda, idadi, ugawaji na mipango ya usaidizi.
- Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanawakilishwa kwa kuzingatia wigo mpana wa aina za ulemavu pamoja na umri, jinsia na anuwai. Fanya juhudi za makusudi katika kuhimiza ushiriki wa makundi yenye uwakilishi mdogo wakiwemo watu wenye ulemavu wa akili, watu wenye asili ya eneo hilo, wanawake, na wasichana, katika mifumo na michakato rasmi na isiyo rasmi katika kushughulikia masuala ya usalama wa chakula na lishe.
- Tambua kuwa kukiwa na lishe bora, watu wenye ulemavu wanaweza kushiriki katika shughuli za kijamii kwa usawa pamoja na wengine.

### Kushughulikia vikwazo

- Ainisha na fuatilia vikwazo na masuluhisho ambayo yanazuia uwezo wa watu wenye ulemavu katika ufikivu wa usalama wa chakula na programu za lishe na huduma. Toa marekebisho stahiki katika kuhamasisha ujumuishi.
- Hakikisha kuwa tathmini na nyenzo za kutoa taarifa zinapatikana, pamoja na taarifa zinazohusiana na usalama wa chakula na lishe kupitia mifumo fikivu. Zingatia mahitaji ya watu wenye uziwi, uoni na ulemavu wa afya ya akili.
- Tekeleza mikakati ya kupunguza ulemavu na ubaguzi. Kuza uelewa katika jamii kuhusu haki za watu wenye ulemavu. Anzisha msaada wa makundi rika ambayo inahusisha watu wenye ulemavu wa afya ya akili.
- Pitia sera, miongozo ya kisekta pamoja na nyezo husika, hakikisha kuwa zinafuata misingi ya haki za watu wenye ulemavu katika ufikivu na ujumuishi.

### Uwezeshaji na kukuza uwezo

- Kondoisha masuala ya ulinzi, uhifadhi katika programu zote za usalama wa chakula na lishe. Wataarifu watu wenye ulemavu kuhusu huduma hizi na jinsi ya kuzifikia. Tambua masuala mahusus ya kijinsia katika baadhi ya hatari za uhifadhi na ulinzi.
- Jengea uwezo mashirika ya watu wenye ulemavu katika kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika hatua zote za programu za usalama wa chakula na lishe, ikiwemo kubuni, utekelezaji na ufuatiliaji. Wawezeshe katika kuwakilisha matakwa ya watu wenye ulemavu katika mifumo ya uratibu.
- Imarisha uwezo wa wadau wanaohusika na usalama wa chakula katika kuelewa hatari na vikwazo vinavyowakabili watu wenye ulemavu pamoja na namna ya kuviondoa kwa kufuata kanuni za misingi ya kibinadamu.
- Hakikisha wadau wa usalama wa chakula wanaelewa haki za watu wenye ulemavu na muingiliano uliopo kati ya ulemavu, umri, jinsia na hadhi ya uhamiaji, dini na jinsia.





### Ukusanyaji wa taarifa na ufuatiliaji

- Kusanya na chambua taarifa za usalama wa chakula na lishe kuhusu watu wenye ulemavu, chambua taarifa kwa jinsia, umri na ulemavu. Fanya kwa utaratibu katika awamu zote za programu za kibinadamu. Pale ambapo takwimu hazipatikani au haziwezi kukusanywa tumia makadirio ya asilimia 15 ya uwepo wa watu wenye ulemavu.[133]
- Tumia taarifa kuhusu mahitaji ya kisekta ya watu wenye ulemavu katika uratibu wa taasisi na mashirika (mfano maji, usafi, uhifadhi na afya) na hakikisha uratibu katika ya sekta zilizopo.
- Hakikisha kuwa maadili ya ukusanyaji taarifa na kanuni za uhifadhi (ikiwemo usiri, kutoa taarifa, idhini huru, ulinzi) zinaheshimiwa popote ambapo taarifa za watu wenye ulemavu zinakusanywa na kutumiwa.[134]

| PROGRAMU ILIYOKONDOISHWA | WALENGWA |
| --- | --- |
| Usambazaji wa chakula na lishe pamoja na programu zimebuniwa na kutumiwa katika hali inayohakikisha ujumuishi na ufikivu kwa kila mtu ikiwemo watu wenye ulemavu. | Programu za chakula na lishe zinatoa fursa kwa mahitaji binafsi ya watu wenye ulemavu, kwa kuzingatia miundombinu, mawasiliano, mgao wa chakula, ufungashaji na vifaa saidizi vinavyohusu chakula na lishe. |

Mwongozo ufuatao utasaidia wadau wa chakula na lishe katika kuainisha na kuondoa vikwazo vinavyowakabili watu wenye ulemavu pamoja na familia, walezi, na wasaidizi wao wakati wanapojaribu kufikia programu za chakula na lishe katika muktadha wa huduma za kibinadamu.

## Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
| --- | --- | --- | --- |
| **1. Tathmini, uchambuzi na mipango** | | | |
| Ainisha taarifa muhimu juu ya hali za watu wenye ulemavu ikiwemo kama programu na sera za serikali za usalama wa chakula na lishe ni jumuishi. Fanya uchambuzi wa hatari na vikwazo ambavyo vinawazuia watu wenye ulemavu kufikia usalama wa chakula na lishe. | X | | |

[133] Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia, *Ripoti ya Dunia kuhusu Ulemavu* (2011).

[134] Angalia ICRC, *viwango vya kitaalamu kwa kazi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na haki za binadamu katika hali za vurugu* (2018), sura ya 6, usimamizi wa data na taarifa za matokeo ya ulinzi uk. 106–148; na CRPD, *Ibara 22(2)*.

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Ainisha taarifa na rasilimali kuhusu chakula na lishe ambazo ni muhimu kwa watu wenye ulemavu (utaalamu, masoko, ufikivu wa huduma) katika ngazi ya jamii, wilaya na taifa. Tumia taarifa hizo katika kufanya mipango. | X | | |
| Wakati wa kufanya tathmini ya usalama wa chakula na lishe husisha watu wenye ulemavu katika jamii zilizoathirika. | | X | |
| Fanya tathmini za usalama wa chakula na lishe katika kulenga mahitaji ya watu wenye ulemavu. Weka mkazo kwa watoto, wajawazito, na kina mama wanaonyonyesha, na wazee wenye ulemavu. Zingatia usaidizi wa chakula na mahitaji ya mlo bora, pamoja na chakula chenye ubora ikiwemo vyakula vilivyotengenezwa (protini na virutubisho vingine), ainisha aina za vyakula vinavyohitajika (kama vile vyakula vya majimaji) na tumia vipimo na muundo wa ufungashaji wa chakula kama inavyotakiwa. | X | X | |
| Uliza maswali juu ya uwezo na mahitaji ya watu wenye ulemavu katika michakato ya tathmini pamoja na nyenzo. Zingatia hadhi ya lishe, vikwazo na viwezeshi vya usalama wa chakula, lishe, za shughuli za riziki, majengo na taarifa zinazohusiana na masuala hayo.[135] | X | X | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Himiza wadau wa masuala ya kibinadamu kukusanya rasilimali za kutosha za usalama wa chakula na lishe. Rasilimali zinapaswa kupatikana wakati wa dharura na katika kipindi chote cha utoaji wa huduma za kibinadamu na zinatakiwa ziwe fikivu kwa watu wenye ulemavu. | X | | |
| Tenga na kusanya rasilimali kwa ajili ya afua jumuishi za usalama wa chakula na lishe ambazo ni fikivu na zinazowalenga watu wenye ulemavu. Weka mpangilio wa uratibu. Tenga rasilimali za kutosha katika bajeti ili kulipia pia gharama zinazohusu ufikivu pamoja na ujumuishi. | | X | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Wafanye wadau katika jamii kuelewa umuhimu wa kutumia mtazamo jumuishi wa ulemavu katika usalama wa chakula na lishe nyakati za kujiandaa na kujiweka tayari kwa dharura, kuandaa mpango wa huduma za dharura, utoa huduma na urejeshaji wa hali ya kawaida. | X | X | |

[135] Kuwa na ulemavu haimaanishi kutokea kwa ukosefu wa chakula au utapiamlo, au mahitaji ya zana. Namna watu wenye ulemavu wanakabili dharura wanaweza kutofautiana; tathmini na malengo yanapaswa kuzingatia hili.





| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Andaa mpango wa dharura ambao utaweka mkakati wa huduma za awali pamoja na mpango wa operesheni ili kufikia mahitaji ya dharura ya chakula na lishe katika kupindi cha wiki tatu hadi nne za dharura. Hakikisha inahusisha watu wenye ulemavu na lipia usafiri wao na huduma ya mgao wa chakula. | X | | |
| Husisha mashirika ya watu wenye ulemavu pamoja na wadau wengine wanaofanya kazi na watu wenye ulemavu katika kubuni na kutoa tathmini jumuishi za usalama wa chakula na lishe. Ainisha vikwazo katika kutoa tathmini na katika kutekeleza afua. | | X | |
| Tathmini uwezo wa wafanyakazi kwa kutumia vigezo vya ujumuishi. Toa mafunzo kwa wafanyakazi na wadau, ikiwemo msimamizi wanaosimamia dharura na waokoaji. Mafunzo yanapaswa kuelezea haki na mahitaji ya watu wenye ulemavu na kuelezea kuwa mahitaji ya ulemavu yanatakiwa kuingizwa katika mipango ya kujiandaa na kujiweka tayari inayohusiana na usalama wa chakula na lishe.[136] | X | | |
| Tafuta njia za kufikia jamii zilizoathiriwa na zilizo tengwa ikiwemo watu wenye ulemavu wa afya ya akili ambao hawawezi kuhama au wakaokabiliana na vikwazo. Zingatia taratibu za usambazaji za kijamii katika kuandaa na kutoa chakula. | | X | X |
| Shirikiana na wadau katika kubuni programu jumuishi za usalama wa chakula na lishe na pia fanya uhamasishaji wa kuwa na mitazamo jumuishi katika shughuli za kisekta na baina ya sekta. | X | X | |
| Tengeneza ufuatiliaji wa kijamii, ainisha wafanyakazi ambao watawasaidia watu wenye ulemavu katika kufikia mgao wa chakula (katika kituo au nje ya kituo). Fanya marekebisho stahiki; husisha usaidizi wa usafiri, na malezi ya watoto kwa wazazi wenye watoto wenye ulemavu na kwa wazazi wenye ulemavu. | X | X | |
| Hakikisha kuwa wazabuni na maeneo ya usambazaji na masoko, huduma za lishe na majengo mengine yanatumia kanuni ya "Sambaza na tumia vigezo vya ufikivu". | | X | |
| Toa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya utendaji wenye tija wa lishe bora kwa ajili ya watu wenye ulemavu. | | | X |
| Fanya kazi na mifumo ya kitaifa ambayo ina wajibu wa kuangazia usalama wa chakula na lishe ikiwemo mifumo ya hifadhi ya jamii katika kuweka mipangilio ya kusaidia watu wenye ulemavu mara baada ya dharura kuisha. Anzisha mifumo ya rufaa kwa ajili ya watu wenye ulemavu wanaohitaji usaidizi unaohusiana na usalama wa chakula na lishe. | | | X |

[136] Kwa mfano wataalamu wanaweza kutoa utaalamu wao wa ukusanyaji wa takwimu, taarifa na huduma za usaidizi, n.k. *Muungano wa masuala ya ulemavu na maendeleo kimataifa*, orodha ya mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika katika nchi zinazoweza kutoa msaada.

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Toa ushauri kwa serikali pamoja na wadau wa kitaifa juu ya kuweka utendaji ambao ni jumuishi katika programu na mafunzo ya usalama wa chakula na lishe. | | | X |
| Toa ushauri juu ya kufuata vigezo vya ufikivu wakati wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu inayohusiana na lishe. Weka maeneo ya kutolea lishe na huduma zinazohusiana na usalama wa chakula. | | | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Kuza maarifa na ujuzi juu ya ulemavu, ingiza ulemavu katika hadidu za rejea zinazohusiana na orodha za dharura za usalama wa chakula na lishe pamoja za michakato ya kuongeza uwezo. Fanya hili katika kila eneo. | X | | |
| Fanya kazi na wadau wa mawasiliano, wataalamu wa ulemavu pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu katika kukuza jamii jumuishi na taarifa fikivu juu ya usalama wa chakula na lishe. | | X | |
| Kwa kushauriana na mashirika ya watu wenye ulemavu na wadau wa afya na lishe, tumia mifuko ya chakula katika kufikia mahitaji ya kilishe ya watu wenye ulemavu ambao wanakabiliana na ugumu wa kula, kutafuna au kumeza au wenye mahitaji maalum ya lishe. | | X | |
| Katika nyanja zote, fanya kazi na sekta husika katika kutengeneza mifumo ya rufaa ili kufikia mahitaji ya watu wenye ulemavu katika usalama wa chakula na lishe. | | X | |
| Fanya kazi na wadau wa kitaifa, ikiwemo wizara na watoa huduma ili kuwafanya watu wenye ulemavu kuwa na ustahimilivu kwa kuzingatia usalama wa chakula na lishe. Imarisha usalama wa chakula pamoja na sera na sheria za lishe, hakikisha kuwa unawajumuisha watu wenye ulemavu. | | | X |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Hakikisha kuwa mifumo ya kutoa maoni, mrejesho na malalamiko inafikika na kuwajumuisha watu wenye ulemavu. | | X | |
| Jumuisha watu wenye ulemavu katika timu za ufuatiliaji na | | X | |
| Ainisha na tengeneza viashiria mahsusi vya ulemavu katika kufuatilia hali ya usalama wa chakula na lishe kwa watu wenye ulemavu | | X | |
| Tathmini kiwango ambacho afua za usalama wa chakula na lishe na majengo yanafikika kwa watu wenye ulemavu ikiwemo majengo ya muda. Chukua hatua kufanya afua zote na majengo kufikika. | | X | |





| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Toa taarifa na kuhifadhi taarifa za maendeleo katika kufikia mahitaji ya usalama wa chakula na lishe kwa watu wenye ulemavu. Elezea maendeleo hayo katika taarifa za ufuatiliaji wa kisekta. | | X | |
| Orodhesha ujumuishi wa watu wenye ulemavu miongoni mwa vigezo vya tathmini ya programu na shughuli za usalama wa chakula na lishe. | | X | |
| Kwa utaratibu maalum hakikisha kuwa afua za usalama wa chakula na lishe zinawajibika kwa watu wenye ulemavu kwa kufanya taarifa kuwa fikivu, kutengeneza mifumo ya kutoa maoni na malalamiko na kuhusisha watu wenye ulemavu katika kufanya maamuzi na kuweka mipango. | | X | |
| Hifadhi masuala muhimu mliyojifunza kuhusu kuzingatia ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika afua za usalama wa chakula na lishe. | | | X |

## Rejea


- Ushirikiano wa mafunzo ya fedha na Shirika la kimataifa la Handicap, kutokana na harakati za programu za uhamishaji wa fedha zinakua, je ni namna gani tunaweza kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu hawaachwi nyuma katika programu za uhamishaji wa fedha katika dharura? (2016),
- Ushirikiano wa mafunzo ya fedha, viwango vya awali kwa ajili ya uchambuzi wa masoko (2017)
- Shirika la kimataifa la Handicap, ulemavu katika muktadha wa masuala ya kibinadamu, mtazamo wa watu walioathirika pamoja na mashirika yaliyopo katika maeneo husika (2015)
- Help Age, CBM, hirika la kimataifa la Handicap International, viwango vya ujumuishi Katika Masuala ya Kibinadamu kwa Wazee na Watu Wenye Ulemavu (2018). (Sehemu ya Programu ya ADCAP)
- Mradi wa Sphere, 'Viwango vya usalama wa chakula na lishe' katika kitabu cha Sphere (2018)
- UNICEF, Kujumuisha watoto wenye ulemavu katika masuala ya kibinadamu: Lishe (2017)
- Umoja wa Mataifa, mkataba wa ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika masuala ya kibinadamu (2016)
- Umoja wa Mataifa, mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu na mkataba wa hiari (2008)
- Shirika la Mpango wa Chakula, *mwongozo wa ujumuishi kwa watu wenye ulemavu katika usaidizi wa chakula*
- Shirika la afya duniani, mwongozo kuhusu ulemavu na usimamizi wa hatari za dharura katika afya (2013)

# 14 Riziki

## Utangulizi

Katika janga au migogoro, kupoteza riziki ni moja ya athari kubwa ambazo kaya inaweza kupata. Suala hili linaathiri uwezo wa watu kuishi. Kwa kuongezea, mali, na rasilimali zinaweza kuharibiwa au kukosekana, na mitandao ya msaada kwa kaya nyingi huvunjika. Programu ya riziki inasaidia watu kupata mahitaji yao ya msingi na kuweza kujitegemea wao binafsi kwa kuwasaidia kujipatia na kupata (au kupata kwa mara nyingine) fursa ya rasilimali na mali ambayo itawafanya kupata riziki kwa usalama na uendelevu.

Sheria ya kimataifa ya haki za binadamu inathibitisha kwamba kila mtu ana haki ya kufanya kazi, kuchagua kwa uhuru kazi na kulindwa na janga la kukosa ajira. Lakini, watu wenye ulemavu walio katika umri wa kufanya kazi wana viwango vya juu vya ukosefu wa ajira sawasawa katika nchi zinazoendelea na zilizoendelea. Katika uchumi unaokua, ukosefu wa ajira ni mkubwa mpaka asilimia 80-90.[137] Mambo kadhaa yanaelezea hili, ikiwa ni pamoja na upendeleo wa mwajiri, kutokuwepo kwa mahali pa kazi kupatikana, na upatikanaji mbovu wa taarifa na fedha. Ukweli ni kwamba, uwezo wa watu wenye ulemavu haujatambuliwa sana, mara nyingi hata na familia zao pia, hii ni sababu nyingine inayochangia janga la kukosa riziki na kazi kwa watu wenye ulemavu.

## Istilahi muhimu

**Riziki** shughuli zote na mali ambazo mtu hutumia kupata kipato cha kujikimu kila siku na kufikia mahitaji yao ya kila siku.

### Vitu muhimu kwenye sharia pamoja na miongozo mingine

- Mkataba kuhusu Haki za Watu wenye Ulemavu
- Lengo la 1 la mendeleo endelevu
- Mpango endelevu kuhusu riziki
- Mkataba wa masuala ya wakimbizi

Neno **riziki endelevu** linamaanisha uwezo wa mtu kujipatia na kumudu kipato na kuongeza ustawi wao na ule wa kizazi kijacho. Riziki ni **endelevu** inapokuwa na msingi wa soko, inaweza kukabiliana na kupona kutokana na majanga na mafadhaiko ya kiuchumi, na inaweza kudumisha uwezo na mali zake bila kudhoofisha mazingira ya asili.

Maneno **uhamisho wa pesa taslimu** na **muingilino wa pesa taslimu** yanaweza kutumika kwa kubadilishana, yakimaanisha kwamba juhudi za kutoa pesa taslimu au vocha kwa wanufaika ili kuwawezesha kununua bidhaa au huduma moja kwa moja. Katika muktadha wa kibinadamu, huusisha pesa taslimu au vocha zinazotolewa kwa watu binafsi, kaya au wapokeaji kwenye jamii; haijumuishi mgao kwa serikali au watendaji wengine wa serikali.[138]

[137] Umoja wa Mataifa, ukweli kuhusu ulemavu na ajira.

[138] Imechukuliwa kutoka ushirikiano wa mafunzo ya fedha, orodha ya uhamishaji wa fedha.

**Msaada wa ufadhili** ni utoaji wa moja kwa moja wa bidhaa (chakula) au huduma kwa wanufaika wa msaada. Msaada wa ufadhili ni moja kati ya suluhu katika hali za shida.

**Mikakati ya kukabiliana** ni vitu ambayo watu hufanya kipindi cha nyakati ngumu. Huruhusu watu kuendelea kupata mahitaji yao muhimu katika kipindi cha majanga. Mikakati inayoweza kumrudisha mtu katika hali yake (mfano, kupunguza chakula kinachotumika kwa muda mfupi, matumizi ya akiba), au inaweza kuwa ni mikakati hasi na migumu kumrudisha mtu katika hali yake (mfano, uuzaji wa mali za uzalishaji, kukimbilia shughuli za kudhalilisha au za jinai).

## Viwango na miongozo rejea

- Help Age, CBM, shirika la kimataifa la Handicap, *viwango vya ujumuishi wa masuala ya kibinadamu kwa wazee na watu wenye ulemavu* (2018). Angalia kipengele kuhusu usalama wa chakula na lishe.
- *Kitabu ya Sphere* (2018). Angalia kipengele kuhusu usalama wa chakula na lishe.
- *Kiwango na muongozo wa mifugo wakati wa dharura*.
- *Viwango vya uchumi vya urejesho* (2017).
- Ushirikiano wa mafunzo ya fedha, *viwango vya uchambuzi wa masoko* (2018).

## Masuala muhimu kufanya

'Masuala muhimu' lazima yafanyike katika nyanja zote za huduma za kibinadamu ambapo programu za riziki zinapotekelezwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

### Ushiriki

- Hakikisha kwamba watu wenye ulemavu, familia zao na mashirika ya watu wenye ulemavu, wanahusishwa kikamilifu katika kutambua vizuizi, na kupanga, kubuni, kutekeleza na kutathmini riziki na sera na programu za ujumuishaji kiuchumi. Jumuisha pia masuala ya upatikanaji wa masoko na huduma, urefu wa mafunzo na mpangilio wake, wingi na mpangilio wa misaada na kufanya maamuzi.
- Hakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanawakilishwa kwa usawa kwa kuzingatia utofauti wa ulemavu, pamoja na jinsia na umri. Fanya jitihada za lazima kukuza uhusishwaji wa makundi yasiyowakilishwa sana mfano watu wenye ulemavu wa afya ya akili, watu asilia ya eneo hilo, wanawake na wasichana katika muundo rasmi na isiyo rasmi.

Tengeneza ushirika na mashirika ya watu wenye ulemavu na mashirika mengine yanayofanya kazi katika maeneo ya riziki. Wahusishe katika kusaidia watu wenye ulemavu na kushawishi uwepo wa muundo jumuishi ya msaada na huduma.

### Kushughulikia vizuizi

- Tambua na fuatilia vizuizi na chukua hatua kuviondoa, hakikisha kwamba programu za riziki na ujumuishaji kiuchumi zinapatikana kwa watu wenye ulemavu. Toa makazi ya kuridhisha na wafikie watu wenye ulemavu kuhakikisha ujumuishaji kamili.
- Fanya kazi na watoa huduma wa mafunzo, watoa huduma wa kuendeleza biashara na huduma za kifedha, waajiri watarajiwa na watoa mafunzo ili kujumuisha watu wenye ulemavu na kuhakikisha kwamba majengo yote yanafikika.
- Hakikisha kwamba taarifa kuhusu zana za kupimia na kutolea taarifa, na programu (kujumuisha vigezo vya malengo, muda, na mpangilio wa msaada, n.k) zinapatikana katika njia tofati nyingi zitazozingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu wa kusikia, kuona na afya ya akili.
- Tekeleza mikakati ya kuondoa ubaguzi kuhusu ulemavu, chukua hatua kufanya jamii itambue haki za watu wenye ulemavu.





**Mchoro namba 9 |** Vizuizi vya upatikanaji wa mjumuisho katika kupata riziki

**JINSI ATHARI ZA MIGOGORO ZINAVYOLETA ATHARI KWA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA KUPATA RIZIKI**

**ATHARI ZA MIGOGORO**

Kukosa usalama, kutenguka kwa mitandao ya kijamii, uharibifu wa miundombinu, uhamishwaji, kufungwa kwa huduma.

**VICHOCHEO VYA VIZUIZI**

**Vizuizi vya mazingira:**

- M asoko yasiyo salama ama yasiyofikika kiurahisi, maeneo ya kazi na maeneo mengine yanayolingana na hayo (mfano maliwato)
- Kukosekana kwa taarifa kuhusu masoko, ulinzi wa kijamii, jinsi ya kutumia vifaa, nafasi za kujifunza maarifa, nafasi za kazi, mikopo midogomidogo na huduma zingine za kifedha,
- Usafiri usiopatikana kiurahisi na miundombinu ya barabara

**Vizuizi vya mtazamo:**

- Mitazamo hasi na ubaguzi wa watu wenye ulemavu katika maeneo ya kazi
- Kukosa ufahamu na maarifa kuhusu uwezo wa watu wenye ulemavu na mchango wao katika maeneo ya kazi
- Kukosa kujiamini kwa watu wenye ulemavu katika uwezo wao wa kutumia huduma za kifedha

**Vizuizi vya kitaasisi:**

- Ukosefu wa uwezo wa kiufundi wa kukuza ujumuishaji wa watu wenye ulemavu katika maeneo ya kazi na huduma za kifedha,
- Vizuizi kwa ajili ya kupata fursa ya kuingia katika mafunzo ya ufundi au miradi ya fedha ndogo kama sifa ya elimu, dhamana, n.k,
- Sera za kazi na programu hazijumuishi watu wenye ulemavu,
- Ukosefu wa taarifa sahihi juu ya watu wenye ulemavu.

**Hatari zinazowakabili watu wenye ulemavu**

Ukatili, umaskini, majanga ya mazingira, kuzorota kwa afya, kunyanyapaliwa, kutengwa, kuachwa.

Anzisha makundi ya msaada rika na kuhimiza watu wenye ulemavu wa afya ya akili kujitetea wenyewe.

- Hakiki sera za kisekta, miongozo na zana kuhakikisha kwamba zinatambua haki za watu wenye ulemavu kwenye upatikanaji na ujumuishaji.

## Kuwezesha na kukuza uwezo

- Kondoisha huduma za ulinzi na ukingi katika programu za riziki na uchumi jumuishi. Wajulishe watu wenye ulemavu kuhusu hatua hizi na jinsi ya kuzipata. Tambua masuala ya kijinsia katika baadhi ya hatari za ulinzi na ukingi.
- Jenga uwezo wa wadau wanaofanya kazi katika eneo la upatikanaji wa riziki. Toa mafunzo ya ufahamu juu ya haki za watu wenye ulemavu, mwingiliano wa ulemavu na umri, jinsia, hali ya uhamiaji, dini na jinsia.
- Imarisha uwezo wa wadau wanaofanya kazi katika eneo la upatikanaji wa riziki, kuelewa hatari na vikwazo vinavyowapata watu wenye ulemavu na jinsi ya kuviondoa kwa kufuata kanuni za huduma za kibinadamu.
- Jenga uwezo wa mashirika ya watu wenye ulemavu na kuwawezesha kuchangia katika kubuni, kutoa na kufuatilia programu za upatikanaji wa riziki, na kuwakilisha masuala ya wenye ulemavu katika uratibu wa miundo na utaratibu.

## Ukusanyaji wa takwimu na ufuatiliaji

- Hakikisha kwamba watu wote wenye ulemavu katika jamii wanatambuliwa.
- Kusanya na changanua taarifa za upatikanaji wa riziki kwa watu wenye ulemavu, kwa kuzingatia vigezo vya jinsi, umri, na ulemavu. Fanya hivyo kwa utaratibu katika ya programu za kibinadamu. Ikiwa taarifa kuhusu watu wenye ulemavu hazipatikani au haziwezi kukusanywa, tumia makadirio ya asilimia 15 ya kuenea kwa ulemavu duniani.[139]
- Sambaza taarifa juu ya mahitaji ya watu wenye ulemavu katika kila sekta katika mashirika na huduma zinazojiratibu (maji, usafi ulinzi, afya) na kuhakikisha uratibu wa sekta nzima.
- Hakikisha kwamba maadili ya taarifa na kanuni za ulinzi (kujumuisha masuala ya usiri, utoaji wa taarifa, idhini huru, ulinzi) yanaheshimiwa kila wakati taarifa ya mtu mwenye ulemavu inapokusanywa na kutumika.[140]

**PROGRAMU ILIYOKONDOISHWA**

Programu zinazohusiana na upatikanaji wa riziki zimeundwa kuhakikishazinajumuisha na zinapatikana kwa kila mmoja, wakiwemo watu wenye ulemavu.

**WALENGWA**

Programu za upatikanaji wa riziki kutosheleza mahitaji binafsi ya watu wenye ulemavu kwa kuzingatia miundo mbinu ya mawasiliano, vifaa, mali na mafunzo. (mfano kutoa teknolojia ya usaidizi, nafasi ya kazi iliyobadilishwa kulingana na mahitaji binafsi).

[139] Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia, *Ripoti ya dunia kuhusu ulemavu* (2011).

[140] Angalia ICRC, *viwango vya kitaalamu vya kazi ya ulinzi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na wadau wa haki za binadamu katika migogoro ya kivita na katika hali zingine za vurugu* (2018), sura ya 6, Usimamizi wa data na taarifa kuhusu matokeo ya ulinzi uk. 106-108 na CRPD, *Ibara ya 22(2)*





Mwongozo ufuatao utasaidia watendaji wanaofanya kazi kwenye nyanja ya riziki kutambua na kuondoa vikwazo vinavyowakumba watu wenye ulemavu, familia, wasaidizi na walezi wao, wanapojaribu kupata huduma katika program za upatikanaji wa riziki katika muktadha wa kibinadamu.

## Masuala yanayopendekezwa

| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesh a katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi, na kupanga** | | | |
| Tathmini uwepo wa mafunzo ya ujuzi na watoa huduma za kifedha na taarifa zinazohusu masoko, kwa ajili ya watu wenye ulemavu. | | X | X |
| Tambua mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo wanaweza kuwatambua, kuwapata na kusaidia watu wenye ulemavu. | X | X | X |
| Tambua na changanua hatari zinazohusiana na upatikanaji wa riziki kwa watu wenye aina mbalimbali za ulemavu na chukua hatua za kupunguza hatari. | X | X | X |
| Tathmini mahitaji ya afya ya akili na elimu na idadi ya watu wenye ulemavu, ili kuwasaidia wale ambao hawajapata njia za kujipatia riziki na fursa ya elimu. | | X | X |
| Tambua huduma za rufaa zinazopatikana katika maeneo husika. Jumuisha msaada wa afya ya akili, ukarabati wa mwili, vitu vya bandia, mifupa, n.k. | | X | X |
| Hakikisha vigezo vya kupata riziki vinazingatia tabia na ukubwa wa ulemavu. | | X | X |
| Toa mafunzo kuhusu riziki jumuishi kwa wafanyakazi wa mashirika ya kimataifa yasiyo ya kiserikali na wadau wengine. Pamoja na wakufunzi wa ufundi, vyama vya wakulima, vikundi vya wanawake, watu wa biashara, halmashauri, makampuni binafsi, wasimamizi kutoka nje, n.k. | X | | X |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Ajiri watu wenye ulemavu kujiunga na timu ya mradi. Hakikisha watu wenye ulemavu wanakuwa ni mfano wa kuwatia watu wengine wenye ulemavu kujiunga katika programu. | X | X | X |
| Hamasisha rasilimali; zitumie kuandaa zana zinazofaa, fanya miundombinu kuwa fikivu kiurahisi, panga mafunzo ya ziada (kwa mfano kuhusu kujifunza kusoma na kuandika), na toa usafiri na msaada mwingine wa kiufundi (ukarabati wa mwili, vifaa vya saidizi). | X | X | X |

| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Shughulikia mitazamo mibaya, fanya jamii iwe na ufahamu zaidi juu ya uwezo wa watu wenye ulemavu na mchango wanaochangia kwa jamii yao. | | X | X |
| Taarifu familia za watu wenye ulemavu juu ya haki na uwezo wa watu wenye ulemavu, pia haki na uwezo wao kufanya kazi. | X | X | X |
| Shawishi na himiza wafanyakazi, viongozi wa mitaa na vyombo vya serikali kuheshimu haki za watu wenye ulemavu, pia haki yao na fursa kamili ya kupata riziki. | X | X | X |
| Hakikisha watendaji wa huduma za kibinadamu wanaelewa kwamba watu wenye ulemavu ni watu ambao wana uzoefu mbalimbali, ujuzi na uwezo. Hakikisha hawabaguliwi au kuwekwa kwenye majukumu ya kibaguzi. Kwa mfano mwanamke mwenye uziwi anaweza kufanya kazi zinazohitaji nguvu. | X | X | X |
| Fanya kazi na watoa huduma za kifedha; wasaidie kubadili huduma zao kukidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu. | | X | X |
| Saidia vituo vya kutolea mafunzo ya stadi kazi au ujuzi wa biashara fanya mitaala na kozi wanazotoa kupatikana kiurahisi kwa watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali. | | X | X |
| Katika maeneo ya kazi, toa vifaa ambavyo vimetengenezwa kwa ajili ya matumizi ya watu wenye ulemavu. | X | | X |
| Fikiria kurekebisha miundombinu ya jamii (mfano masoko, na taasisi za mafunzo) ili zipatikane kiurahisi kwa watu wenye ulemavu. | | X | X |
| Fundisha wafanyakazi wa mradi jinsi ya kuchangamana na kuwasaidia watu wenye ulemavu wa aina mbalimbali. | | X | X |
| Endeleza ufikiaji wa makundi yaliyo mbali na michakato ya jamii ambayo inaweza kutambua na kuunganisha watu wenye ulemavu ambao 'Hawaonekani'. | X | | |
| Shirikiana na vyama vya watu wenye ulemavu na watendaji wengine ambao wanasaidia watu wenye ulemavu kubuni na kutoa riziki jumuishi na tathmini ya usalama wa kiuchumi. Vyama hivi vinatakiwa vitambue vikwazo vya utolewaji wa tathmini pamoja na vikwazo vya utekelezaji wa programu. | X | X | |





| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **4. Uratibu** | | | |
| Weka mtaalamu wa ujumuishaji kwenye kitengo cha usalama wa chakula na upatikanaji wa riziki. Yeye atatakiwa kusaidia washirika wa sekta kukondoisha ujumuishaji na kusaidia rufaa katika sekta husika. | X | X | |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Husisha mashirika ya watu wenye ulemavu katika kufuatilia huduma za kibinadamu na ulinzi. Viashiria vinatakiwa kuchanganuliwa kwa jinsia, umri na ulemavu.<br><br>Hakikisha mfumo wa kutoa mrejesho kwa wanufaika unapatikana kiurahisi na unajumuisha watu wenye ulemavu mbalimbali.. | | X | |
| Hakikisha mfumo wa kutoa mrejesho kwa wanufaika unapatikana kiurahisi na unajumuisha watu wenye ulemavu mbalimbali. | | X | |
| Kwa utaratibu, hakikisha kwamba programu za upatikanaji wa riziki zinawajibika kwa watu wenye ulemavu. Njia za usambazwaji wa taarifa na malalamiko na utoaji wa mrejesho unatakiwa upatikane kiurahisi. Watu wenye ulemavu wanatakiwa wawe na uwezo wa kushiriki katika kufanya maamuzi na kupanga mipango. | | X | X |
| Tambua huduma za mfano ambazo zimefanya ujumuishaji mzuri wa watu wenye ulemavu. Hifadhi katika maandishi na sambaza. | | | X |

## Rejea


- Ushirikiano wa mafunzo ya fedha, *viwango vya uchambuzi wa masoko*
- EMMA, *Nyenzo ya uainishaji na uchambuzi wa masoko wakati wa dharura*
- *Kituo cha riziki*
- *Viwango vya urejesho wa uchumi*
- *Kitabu cha Sphere* (2018)
- *Mwongozo wa kutathmini hatari kuhusu masuala ya riziki*
- Ofisi ya Kanda ya Asia na Pacific ya shirika la chakula duniani, *kitabu cha kuwafundisha walemavu kukuza kibiashara maeneo ya vijijini* (2003)
- Shirika la Kazi Duniani na Shirika la Chakula Duniani, *mwongozo kuhusu namna ya kuelezea kazi za vijijini kwa staha katika shughuli za nchi za shirika la afya: Toleo la pili* (2010)

# 15 Afya

Tazama pia usafi, Usalama wa chakula na lishe, Elimu na Ulinzi.

## Utangulizi

Kwa asili, majanga ya kibinadamu na mizozo hudhuru mifumo ya afya pamoja na afya ya watu ambao huwaathiri. Mbali na athari za moja kwa moja za majeraha na kiwewe, majanga hufanya matatizo ya kiafya ya umma kuwa magumu zaidi (ikiwa ni pamoja na matukio ya malaria, kipindupindu, utapiamlo, magonjwa yasiyoambukiza, na shida za afya ya kijinsia na uzazi) kwa sababu zinavuruga mifumo ya ulinzi wa jamii na vile vile huduma muhimu za afya. Kwa watu wenye ulemavu, ambao wengi wao hupata elimu na makazi na huduma zingine kwa mfumo wa rufaa kutoka katika huduma za afya, mizozo na majanga huharibu jinsi wanavyopata huduma, na kuharibu hali ya wale ambao tayari wametengwa.

Watu wenye ulemavu wana haki ya kupata huduma zote za afya na kupata taarifa kuhusu hali zao za kiafya na matibabu. Pia wana haki ya kufanya maamuzi juu ya matibabu (kutoa idhini). Wafanyakazi wengi wa kawaida wana mitizamo juu ya uwezo na mahitaji ya watu wenye ulemavu. Mara nyingi hudhani wanahitaji huduma zinazohusiana na ulemavu peke yao; au wanaruhusu wanafamilia, wafanyakazi wa matibabu au wawakilishi wengine kutoa idhini kwa niaba yao.

Kukosekana kwa huduma za afya au usumbufu wa kuzipata kunaweza kuwa na athari mbaya kwa watu wenye ulemavu. Kwa mfano, huwa inadhaniwa kuwa wanawake wenye ulemavu hawana mahitaji ya kingono, hivyo wanaweza kutengwa katika kupata huduma za afya ya uzazi, jambo ambalo linawaweka katika hatari kubwa zaidi za kupata ujauzito usiotarajiwa au maambukizo ya magonjwa ya zinaa.

### Mifumo ya kisheria na mifumo mingine

- Mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu
- Mkataba wa haki za watoto, shirika la afya, mfumo wa kutoa huduma wakati wa dharura
- Shirika la Afya Duniani, mpango kazi wa nyakati za dharura
- Kikosi kazi cha afya ya uzazi cha ISDR/WHO. Jukwaa mahsusi kwa ajili ya usimamizi wa hatari za majanga ya kiafya, muhtasari wa sera: kukondoisha afya ya uzazi katika dharura za kiafya na usimamizi wa hatari za majanga
- Mfumo wa kupunguza majanga wa Sendai 2015-2030.

Ikiwa watoto wenye ulemavu hawawezi kutambuliwa ipasavyo, watashindwa kupokea huduma za ukuaji wa watoto na wanaweza kushindwa kufikia uwezo na vipawa vyao.

## Dhana muhimu

**Mfumo wa afya** na mashirika yote, watu na jitihada zinazochukuliwa zenye nia ya kukuza, kurejesha au kudumisha afya.[141] Inazingatia njia za kushawishi mambo na shughuli zinazokuza na kuboresha afya moja kwa moja. Hivyo inatoa huduma za kuzuia, kukuza, kuponya na kufanya marekebisho kupitia watendaji na huduma za serikali na zisizo za serikali.[142]

[141] Shirika la afya duniani-kanda ya Magharibi ya Pacific, *mfumo wa afya wa shirika la afya duniani* (2018).

[142] Shirika la Afya Duniani, *kufuatilia ujenzi wa mifumo ya afya, kitabu cha viashiria na mikakati ya vipimo* (2010).

## Mchoro namba 10 | Vizuizi vya ufikiaji na ujumuishaji katika afya[143]

### JINSI MAJANGA YANAVYOONGEZA HATARI KWA WATU WENYE ULEMAVU

**ATHARI ZA MAJANGA**

Kutokuwepo kwa usalama, uvunjifu, kwa mitandao ya kijamii, uharibifu wa miundombinu, kuhamishwa, kufungwa kwa huduma.

**VIZUIZI VINAVYOONGEZEKA**

**Vizuizi vya kimazingira:**

- Vituo vya afya visivyofikika,
- Ukosefu wa mawasiliano fikivu wakati wa mashauriano (kufanya utambuzi wa ugonjwa na taarifa za matibabu) katika shughuli za kuendeleza afya na kuzuiwa kwa shughuli,
- Miundombinu ya usafiri na barabara isiyofikika,
- Taratibu za kutoa idhini hazifikiki,
- Kutopatikana kwa vifaa mwendo au vifaa vingine saidizi na teknolojia.

**Vizuizi vya kimtazamo:**

- Mtazamo hasi na unyanyapaaji kwa watu wenye ulemavu na wafanyakazi wa afya,
- Watendaji wa afya wanakosa uelewa na ufahamu kuhusu watu wenye ulemavu na mahitaji yao.

**Vizuizi vya kitaasisi:**

- Ukosefu wa uwezo wa kiufundi wa kukuza ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu,
- Usimamizi na mfumo wa hatari za dharura za afya wa kitaifa sio jumuishi kwa watu wenye ulemavu,
- Mfumo na miundombinu iliyopo ya afya haishughulikii mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu
- Kukosekana kwa uwajibikaji katika mifumo ya afya kuhusu rufaa na huduma mahususi za ulemavu
- Kukosekana kwa taarifa za ulemavu katika mfumo wa usimamizi wa taarifa za afya

**Hatari zinazowakabili watu wenye ulemavu**

Vurugu, umaskini, hatari za kimazingira, kuzorota kwa afya, kutengwa

[143] Orodha ya vizuizi maalum kwa huduma ya afya, angalia Shirika la Afya Duniani, ukweli kuhusu ulemavu na afya.



## Viwango na miongozo rejea

- Kamati ya kudumu ya mashirika mbalimbali ya IASC, mwongozo kuhusu afya ya akili katika muktadha wa dharura (2007)
- Shirika la afya duniani, timu za dharura za tiba: Viwango Vya kitaalamu na mapendekezo ya marekebisho (2016)
- Shirika la afya duniani, mwongozo kuhusu ulemavu na usimamizi wa hatari wakati wa dharura katika afya (2018)
- Kitabu cha Sphere (2018)[144]
- Shirika la Afya Duniani, mwongozo wa marekebisho ya kijamii
- Shirika la Help Age International, CBM, na Handicap International, viwango vya ujumuishi ya masuala ya kibinadamu kwa wazee na watu wenye ulemavu (2018)

## Masuala mengine muhimu ya kufanya

Masuala ya muhimu lazima yafanyike katika hatua zote za huduma za kibinadamu wakati wa kutekeleza programu za kiafya kwa watu wenye ulemavu.

### Ushiriki

- Hakikisha kwamba watu wenye ulemavu, wanafamilia, na mashirika ya watu wenye ulemavu wanashiriki kikamilifu katika kufanya maamuzi na katika kubuni, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini mipango ya afya.
- Kwa kushirikiana na watu wenye ulemavu na mashirika yao, waelekeze wafanyakazi wa afya kuhusu haki za watu wenye ulemavu, pamoja na muingilino wa ulemavu na jinsia, umri, hali ya uhamiaji, dini na ujinsia.

### Kushughulikia vizuizi/vikwazo

- Tekeleza mikakati ya kupunguza unyanyapaa kuhusu ulemavu. Fahamisha jamii kuhusu ulemavu. Anzisha vikundi vya kusaidia rika ambavyo vinajumuisha watu wenye ulemavu wa afya ya akili.
- Ongeza uelewa, kukomesha uelewa na dhana potofu, na kuza ushirika, hamasisha watu wenye ulemavu na wafanyakazi wa afya kufanya mazungumzo, kubadilishana mawazo na kubadilishana maarifa.
- Hakikisha vituo vya afya vinapatikana kwa watu wenye ulemavu. Kuza mipango ya kuwapa huduma ya usafiri watu wenye ulemavu wanaohitaji msaada wa afya, panua mageti ya kuingilia, boresha alama, na wezesha mzunguko wa watu katika eneo.
- Wasilisha habari juu huduma za afya katika miundo mingi inayoweza kupatikana, kwa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu wa kusikia, kuona, na akili.
- Shughulikia vizuizi vya uchumi na uchumi kwa afya, kama ukosefu wa elimu na kipato kidogo.

### Uwezeshaji na ukuzaji uwezo

- Imarisha uwezo wa programu za afya za mashirika ya watu wenye ulemavu. Wezesha ushiriki katika kubuni, kutekeleza na kufuatilia huduma za afya.
- Shirikisha wafanyakazi wa mashirika ya watu wenye ulemavu, watetezi wa kibinafsi wenye ulemavu wa afya ya akili, watumiaji wa huduma ya afya ya akili, wanafamilia, na walezi katika mafunzo ya taaluma ya afya inayohusu ulemavu.
- Pitia taratibu za kupata ridhaa huru katika kutoa matibabu na upasuaji na usambazaji wa taarifa (pamoja na rufaa) kuwezesha watu wenye ulemavu kufanya maamuzi yao wenyewe.

[144] Mradi wa Sphere, mkataba wa masuala ya kibinadamu na viwango vya mwitikio katika masuala ya kibinadamu (2011).

### Ukusanyaji wa takwimu na ufuatiliaji

- Tambua ni taarifa zipi zinazopatikana kuhusu idadi ya watu wenye ulemavu. Tathmini usahihi wa taarifa na tambua mapungufu. Ambapo taarifa hazipatikani, tumia makadirio ya asilimia 15 kuhusu uwepo wa ulemavu ulimwenguni.[145]

- Fanya tathmini ya afya, chunguza zana za ufuatiliaji, kusanya taarifa juu ya afya ya watu wenye ulemavu. Fanya hivyo kila wakati na kila hatua.

Changanua taarifa kwa jinsia, umri na ulemavu.

- Tengeneza mifumo ya wazi ya rufaa katika huduma tofauti. Andika na uangalie utendaji wao.

- Fanya uchambuzi wa muingiliano wa hali ili kuelewa hali ya kutokuwa na usawa kulingana na jinsia, umri na ulemavu na jinsi muingiliano huu unavyoathiri ufikiaji wa rasilimali fedha, uhamaji na uamuzi.

## Utoaji wa huduma bora za afya

Ili kuwa bora, huduma za afya lazima ziwe zinafikika kwa usawa. Bidhaa muhimu za matibabu na teknolojia bora; lazima ziwe salama, zenye ufanisi na gharama nafuu; na lazima ziwe zimethibitishwa kisayansi.

Katika mazingira ya kibinadamu, watu wote wanapaswa kupata huduma bora za afya, bila kujali ulemavu.

**PROGRAMU ILIYOKONDOISHWA**

Vituo vya afya na programu zinazingatia dhana ya usanifishaji kwa ajili ya watu wote, ni jumuishi na inapatikana kwa kila mtu, inajumuisha watu wenye ulemavu, kwa mfano wahudumu wa afya wamefunzwa kuhusu ulemavu na huduma zinawapa watu kipaumbele.

**WALENGWA**

Mipango ya afya huambatana na mahitaji ya mtu binafsi mwenye ulemavu. Kwa mfano vifaa saidizi hutolewa na bidhaa za matibabu zinakidhi mahitaji ya kibinafsi.

Mwongozo ufuatao utasaidia watendaji wa afya kutambua na kuondoa vizuizi vinavyowakabili watu wenye ulemavu, pamoja na familia, wasaidizi na walezi wao, pale wanapozifikia programu za afya katika mazingira ya kibinadamu.

[145] Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia, *Ripoti ya dunia kuhusu ulemavu* (2011).





## Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na upangaji** | | | |
| Ainisha mahitaji ya kuzuia majanga na mahitaji ya afya mapema. Zingatia afya ya uzazi, afya ya akili, msaada wa huduma za afya ya akili, magonjwa ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza na huduma kwa walioumia. Zingatia kutoa huduma fikivu na bora, nafuu, huduma za afya kwa wote, dawa muhimu, na vifaa vya kusaidia watu wenye ulemavu, bila kujali umri na jinsia. | X | | |
| Ainisha huduma zilizokondoishwa na zile mahusus i kwa afya ya watu wenye ulemavu. Fikiria vituo vya msingi vya huduma za afya, hospitali za magonjwa sugu na utengemao, huduma za awali na mapema, mipango ya kurekebisha jamii na afya ya akili katika ngazi ya jamii na hospitali, na wasaidizi na watengenezaji wa vifaa vya kusaidia. | X | X | |
| Ainisha mashirika ya watu wenye ulemavu yaliyopo, makundi rika yanayohusiana na afya, watumiaji wa huduma za afya ya akili, watetezi wa kibinafsi wenye ulemavu, walezi na wazazi, na mashirika yanayofanya kazi juu ya ulemavu. Washirikishe katika shughuli zote za kujiandaa na kujiweka tayari. | X | | |
| Endeleza uwezo wa wadau wa afya wa masuala ya huduma za kibinadamu kuhusisha watu wenye ulemavu katika programu. | X | X | |
| Fanya ukaguzi wa upatikanaji wa mashirika, vituo vya afya na huduma na bidhaa za afya. Andaa mpango kazi utakaosaidia katika ufuatiliaji na tathmini. | X | X | X |
| Na mashirika ya watu wenye ulemavu, kagua sera za kitaifa za afya ya dharura na uhakikishe zinatenga pesa kukidhi mahitaji ya afya na ustawi wa watu wenye ulemavu. | X | | X |
| Ainisha kituo cha afya kinachojumuisha watu walemavu au mtaalam kwa sekta ya afya ili kutoa mwongozo wa kiufundi juu ya kupanga huduma za afya zinazojumuisha watu wenye ulemavu na kusaidia rufaa za kisekta. | X | X | X |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Tenga pesa na kukusanya fedha ili kuhakikisha mwendelezo wa huduma za afya zinazotumiwa na watu wenye ulemavu, pamoja na huduma maalum ambazo ni muhimu. | X | X | X |

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Kuhamasisha wataalamu ambao wanaelewa na wanaweza kushughulikia mahitaji ya kiafya ya watu wenye ulemavu. Kuajiri wataalam katika kuzingatia ulemavu katika huduma za afya. | | X | |
| Anzisha kanzidata ya wahusika wa afya maalum na wa kawaida na watoa huduma ambao wako katika nafasi ya kuwezesha mfumo mzuri wa rufaa. | X | X | |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Kuongeza uelewa kati ya wafanyakazi wa afya na jamii kupunguza unyanyapaa dhidi ya ulemavu. Tekeleza mikakati ya kufikia lengo hili, kwa mfano kupitia mawasiliano na programu za kufikia watu. | X | X | X |
| Hakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanaweza kufikia vituo vyote vya afya, pamoja na vile vya muda. Wakati vituo vya afya vinajengwa upya au kutengenezwa, hakikisha wahandisi na wasanifu wanazingatia kanuni ya usanifishaji kwa ajili ya watu wote. | | X | X |
| Fanya vituo vya afya vifikike kwa watu wenye ulemavu. Fikiria maeneo ya kuingilia, vyumba vya kupumzika, urahisi wa kutembea ndani ya majengo, alama. | X | X | X |
| Hakikisha kuwa taarifa zote juu ya huduma za afya, zinatolewa kwa mfumo wa kuridhisha watumiaji na uwezekano wa kutoa mrejesho unapatikana katika miundo anuwai inayoweza kupatikana kirahisi. | | X | X |
| Hakikisha, baada ya dharura kuanza, taarifa ya mgonjwa inabaki inapatikana na kuweza kupatikana kwa madhumuni ya rufaa, michakato ya uhamishaji na ufuatiliaji. | | | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Jumuisha habari juu ya ulemavu katika mifumo ya taarifa za usimamizi wa afya. Fikiria rejista za vituo vya afya, hali ya uwajibikaji wa kituo, ufuatiliaji unaohusiana na afya. | X | X | |
| Anzisha vikundi vya uratibu. Shirikisha wadau wa afya na wawakilishi wa mashirika yasiyo ya watu wenye ulemavu, wakiwemo watu wenye ulemavu wa afya ya akili. | X | X | X |
| Hakikisha kuwa mifumo ya rufaa inaunganisha watoa huduma za afya na watendaji wa afya wenye utaalam katika ulemavu. | | X | |





| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Hakikisha kuwa mifumo ya mrejesho na malalamiko inapatikana kiurahisi na inajumuisha watu wenye ulemavu. | | X | |
| Kusanya taarifa juu ya afya; hakikisha taarifa zinachakatwa kwa kufuata hali ya jinsia, umri na ulemavu. | | X | X |
| Fuatilia na tathmini upatikanaji na ujumuishaji wa vituo vya afya, mipango na huduma, ili kuhakikisha kuwa wanashughulikia mahitaji ya wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wenye ulemavu, kwa miaka yote. | | X | X |
| Unapopima ubora wa utoaji wa huduma za afya, pia pima vigezo ambavyo vinapima ujumuishaji na upatikanaji na hakikisha unafuata viwango vya afya. (Angalia nyenzo hapa chini). | | X | X |

## Rejea


- mhGAP, _mwongozo wa mafunzo_ (2017)
- Shirika la afya duniani OECD, Benki ya Dunia, _utoaji wa huduma bora za Afya: Mpango wa dunia wa lazima wa afya kwa wote_ (2018)

## Wafanyakazi wa afya

Kikosi kazi kinachofanya vizuri kina fanya kazi, kina heshima, na kinajali haki na ufanisi. Kinafanya kazi kupata matokeo bora ya kiafya kadri iwezekanavyo, kutokana na rasilimali na hali ilizopo. Hii inamaanisha wafanyakazi ambao wamesambazwa kwa usawa, wenye uwezo na tija, na wa kutosha kutekeleza kazi inayohitajika.

## Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na upangaji** | | | |
| Fanya tathmini ya mahitaji ya kikosi kazi afya ili kutambua uelewa wao kuhusu ulemavu na umuhimu wa kujumuisha watu wenye ulemavu katika programu ya afya na utoaji wa huduma kwa pamoja. | X | X | X |
| Tambua mapungufu katika uwezo na uelewa wa wafanyakazi wa afya, na katika sera na mwongozo, kwa kuzingatia masuala ya ujumuishaji na ulemavu. | X | X | |
| Ainisha na uboreshe mara kwa mara idadi na eneo la wafanyikazi wanaofanya kazi na watu wenye ulemavu (wataalamu wa afya na ukarabati, wafanyakazi wa jamii, n.k). | X | X | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Ainisha Rasilimali. Jumuisha katika kikosi kazi cha afya watu wenye ulemavu ambao wana ujuzi na mafunzo ya afya. | X | X | X |
| Ajiri wafanyakazi wa kitaalamu ambao wana utaalamu katika kujibu mahitaji ya kiafya ya watu wenye ulemavu. | | X | |
| Hamasisha upatikanaji wa fedha ili kuimarisha utaalam wa ulemavu kwa wafanyakazi wa afya. Jumuisha ujuzi wa mawasiliano na mitihani ya afya. | X | X | X |
| Jumuisha wafanyakazi wa kufanya huduma za uboreshaji na urejeshaji hali katika timu za matibabu za dharura. | | X | |
| Hamasisha anuwai ya watoa huduma za afya (pamoja na wataalam wa kujifunza kuongea) kuwawezesha watu wenye ulemavu kupata huduma wanazohitaji. | | X | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Hakikisha programu zote za afya na mafunzo ya msingi kwa wataalamu wa afya yanajumuisha uelewa juu ya ulemavu na haki za watu wenye ulemavu. | X | | X |
| Wafunze wafanyakazi wa afya juu ya athari za majanga ya kibinadamu kwa afya ya watu wenye ulemavu. (Kwa mfano: watu wenye ulemavu wa akili wana dalili mbaya zaidi; ukosefu wa dawa hufanya kushindikana kwa kudhibiti kifafa, ugonjwa wa kisukari, nk. Watu walio na majeraha ya mgongo hawawezi kudhibiti vidonda vyao ikiwa wametenganishwa na watu wanaowapa msaada, n.k). | X | X | |
| Kuandaa mikakati ya ufikivu na utunzaji wa jamii, na huduma ya nyumbani, kuwezesha wafanyakazi wa afya kuwafikia watu wenye ulemavu ambao hawawezi kusafiri au wanaoishi mbali. | | X | X |
| Hakikisha kwamba njia zote za mrejesho na malalamiko zinapatikana kwa watu wenye ulemavu. | X | X | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Endeleza na pima njia za rufaa kati ya jamii na hospitali na kati ya huduma za afya na sekta zingine na huduma. | X | X | |
| Tengeneza kanzidata ya wafanyakazi wa afya katika ngazi zote ambao wamepata mafunzo ya ulemavu. | X | | |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Fuatilia mara kwa mara maarifa na ustadi wa wafanyakazi wa afya kwa kuzingatia watu wenye ulemavu na ujumuishaji wao. Pendekeza mafunzo ya ufuatiliaji. | X | X | X |
| Tathmini mafunzo juu ya ulemavu ambayo yanapatikana kwa kikosi kazi afya. | X | | X |

## Rejea


- Nguvukazi ya Kidunia ya wadau wa afya, kuongeza nguvukazi ya masuala ya afya kijamii kwa ajili ya dharura – tamko la pamoja (2011)
- Konga ya afya, benki ya marifa
- Shirika la afya duniani, kujenga nguvukazi ya kidunia kwa ajili ya mwitikio bora (2016)

## Usimamizi wa habari za kiafya

Mfumo mzuri wa usimamizi wa habari za afya unapaswa kuhakikisha kwamba habari juu ya hali ya afya, utendaji wa mfumo wa afya na hali ya afya inatolewa, kuchanganuliwa, kusambazwa na kutumiwa kwa uaminifu na mara moja.

## Hatua zilizopendekezwa

| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na upangaji** | | | |
| Kuchanganua tafiti za kitaifa na ufuatiliaji wa masuala ya afya kwa kuzingatia jinsia, umri na ulemavu. | X | | |
| Jumuisha taarifa zinazohusiana na ulemavu, ziliyotenganishwa kwa jinsia na umri, katika tafiti za idadi ya watu na afya. | X | | |
| Ainisha upatikanaji wa huduma muhimu za afya, pamoja na urekebishaji na uboreshaji wa hali ya mwili, tiba ya akili, na mafunzo ya mifupa. | X | | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Kuendeleza, kuwasiliana na kutoa mafunzo juu ya njia za ukusanyaji wa rasilimali zinazohusiana na ulemavu ambazo zimejaribiwa katika muktadha wa kibinadamu, kama vile seti fupi ya maswali ya ulemavu ya kundi la Washington na moduli itendayo kazi ya Kundi la watoto UNICEF-Washington. | X | | X |
| Wafunze wafanyakazi wanaokusanya taarifa juu ya miundombinu ya afya kukusanya taarifa kuhusu ufikivu kwa watu wenye ulemavu. | X | | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Buni mfumo wa usimamizi wa habari za kiafya ambao unachanganua taarifa kwa kuangalia jinsi, umri na ulemavu. | X | X | |
| Buni rejista za afya za kutumiwa katika vituo vya afya, na katika huduma za ufikiaji na za majumbani, ambazo hukusanya taarifa zilizochakatwa kwa jinsi, umri na ulemavu. | X | X | |
| Wafunze wahudumu wa afya kukusanya taarifa zilizochakatwa kwa jinsi, umri na ulemavu na kukagua upatikanaji wa vituo vya afya. | X | X | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Hitaji taarifa kujumuisha viashiria maalum vya ulemavu. | | | |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Hitaji zana za ufuatiliaji na tathmini kujumuisha viashiria maalum vya ulemavu. | | X | X |





## Rejea

- Kitengo cha afya, benki ya maarifa (Angalia taarifa na mpango)
- Uungwana na ujumuishwaji, kutumia maswali ya kundi la Washington katika msuala ya kibinadamu (nyenzo ya mafunzo katika ukusanyaji takwimu za ulemavu) (2019)
- Uungwana na ujumuishwaji, takwimu kuhusu ulemavu katika masuala ya kibinadamu

## Huduma muhimu za afya

Huduma muhimu za afya ni pamoja na huduma za afya zinazookoa maisha. Watu wengine wenye ulemavu wanahitaji utengamao na uboreshaji wa mwili au msaada wa kupumua au huduma nyingine maalum za afya ili kuhakikisha wanaishi na ustawi wao unakua.

## Hatua zailizopendekezwa

| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na upangaji** | | | |
| Tathmini ujuzi na maarifa ya wafanyakazi wa afya kwa kuzingatia utengamavu na uboreshaji hali ya: (1) watu wenye ulemavu; (2) watu wenye ulemavu ambao wamepata majeraha mapya;[146] na (3) watu wenye majeraha.[147] endeleza mpango mkakati (vifaa vya mafunzo, rasilimali) kutatua changamoto zilizoanishwa. | X | X | |
| Tambua na tathmini mahitaji ya kiafya ya watu walioathiriwa na ulemavu. Fikiria utunzaji wa afya ya akili na utengamavu na uboreshaji | X | X | |
| Ainisha mahitaji muhimu ya afya ya watu wenye ulemavu. Weka pia msaada wa kupumua, matumizi ya umeme, dawa na matibabu. | X | X | |
| Tambua vizuizi na hatari ambazo watu wenye ulemavu wanakutana navyo wakati wanapopata huduma muhimu za afya. | X | X | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Wahimize wafadhili kufadhili urejeshwaji au usambazaji wa huduma muhimu za afya kwa watu wenye ulemavu. | X | X | |

[146] Shirika la afya duniani, viwango na mapendekezo kwa ajili ya marekebisho (2016).
[147] *Ibid*.

| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Wahimize wafadhili kufadhili urejesho au usambazaji wa huduma muhimu za afya kwa watu wenye ulemavu. | | X | X |
| Rejesha huduma muhimu za afya na vifaa ambavyo watu walio na ulemavu wanahitaji ili kudumisha afya zao na kuishi. | | X | |
| Weka mfumo mzuri wa rufaa na peleka watu wenye ulemavu kwenye huduma za afya ambazo zilitambuliwa wakati wa hatua za kujiandaa na kujiweka tayari. Huduma hizi zinapaswa kuwa sahihi na zinazoheshimu tamaduni. | | X | X |
| Kurejesha bidhaa na dawa katika vituo vya utengemao na maboresho ya mwili, vituo vya afya na hospitali. Jumuisha vifaa vya kusaidia na dawa muhimu, na vituo vya afya akili sambamba na vya kimwili. | X | X | |
| Kuunganisha mahitaji muhimu ya afya yaliyokubaliwa ya watu wenye ulemavu katika huduma za afya. | | X | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Ratibu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, mashirika ya watu wenye ulemavu na wadau wengine husika. Pamoja nao, kubalianeni kuhusu huduma muhimu kwa watu wenye ulemavu. | X | X | |
| Shirikiana na mashirika ya watu wenye ulemavu, wahudumu na watoa huduma za afya wa eneo hilo ili kutambua mahitaji ya afya kabla ya majanga hayajatokea katika eneo lililoathirika. Jumuisha masuala ya utengemavu na uboreshaji wa mwili. | X | | |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Fuatilia kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanaweza kufikia huduma zote muhimu. Husisha ufikivu wa madawa, vifaa saidizi, pamoja na watoa huduma. | | X | X |

## Zana rejea

- Kitengo cha afya, *benki ya maarifa*





## Magonjwa yanayoweza kuambukizwa

Bila kujali umri na jinsi zao, watu wenye ulemavu wana uwezekano wa kuambukizwa zaidi na magonjwa yanayojitokeza katika mizozo ya kibinadamu, kwa sababu wana uwezekano wa kukosa maji salama, mipango ya kutosha ya usafi wa mazingira na kinga ya afya, na wanaweza kuishi katika hali isiyofikika na makazi ambayo yanahatarisha afya na maisha yao.

### Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na upangaji** | | | |
| Pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu na wadau wengine, tambua watu wenye ulemavu katika idadi ya watu walioathirika. | X | X | |
| Tambua vikwazo na hatari ambazo watu wenye ulemavu wanapata wakati wanapopata huduma za afya na mipango ya magonjwa ya kuambukizwa. Jumuisha chanjo na ufikiaji wa programu salama za maji. | X | X | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Hamasisha fedha na rasilimali watu ili kupanga huduma za ufikiaji watu, huduma za jamii na huduma za nyumbani, na kukuza afya na kampeni za kuzuia magonjwa. | X | X | |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Kusanya ufuatiliaji wa magonjwa na taarifa za uchunguzi wa kaya zilizochakatwa kwa kuzingatia vipengele vya jinsia, umri na ulemavu. | | X | |
| Shirikisha watu wenye ulemavu na mashirika ya watu wenye ulemavu katika kukuza vifaa vya habari, elimu na mawasiliano. | X | X | |
| Wasiliana na kuza afya na hatua za kuzuia magonjwa kwa njia anuwai na zinazofikia. Fanya vivyo hivyo katika masuala ya habari na rasilimali za elimu. | X | X | |
| Wakati wa kubuni hatua za kuzuia magonjwa ya kuambukiza ya kisekta kwa idadi ya watu walio katika hatari, shughulikia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu. | X | X | |
| **4. Uratibu** | | | |
| Kuratibu sekta zingine kuhakikisha watu wenye ulemavu wanapata maji, usafi wa mazingira, na makazi safi na salama, na wanaweza kukidhi mahitaji mengine ya dharura. | | X | |

| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Fuatilia kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanafikiwa na kampeni za kukuza na kuzuia magonjwa. | | X | |

## Rejea

- Kitengo cha afya, *benki ya maarifa*

## Afya ya mtoto

Kushindwa kuratibu huduma za watoto katika afya, elimu, ulinzi na lishe ni tishio kubwa kwa afya ya mtoto. Inazuia utimilifu wa haki za watoto, inapunguza uwezo wao wa maendeleo, na inaleta ugumu katika kupunguza hali ya kutokuwa na usawa wa kijamii na kiuchumi unaoathiri afya.

Watoto wenye ulemavu wana haki ya kupata huduma zote za afya zinazohusiana na watoto na vijana.

### Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na upangaji** | | | |
| Tafuta taarifa inayopatikana juu ya idadi ya watoto wenye ulemavu. | X | | |
| Ainisha zana za tathmini zinazotumiwa sana na watoto, pamoja na wakati wa mwanzo wa ukuaji wa watoto. Zibadilishe ili kukidhi mahitaji ya watoto wenye ulemavu na wafundishe wafanyakazi kuzitumia. | X | X | |
| Orodhesha watoa huduma za afya na upatikanaji wao. Jumuisha wataalamu wenye utaalam wa watoto, lishe, kuchukua hatua za mapema, ukuzaji wa watoto wa mapema na utengemao na uboreshaji mwili. | X | X | |
| Bainisha mahitaji ya afya ya akili na lishe ya watoto wenye ulemavu. (Kwa mfano, mtoto aliye na ulemavu aliyepoteza wazazi au walezi anaweza pia kuwa na utapiamlo au msongo wa mawazo). | X | X | |
| Tathmini ni mafunzo gani wafanyakazi wa afya wanahitaji ili kuzingatia watoto wenye ulemavu na ujumuishaji wao. | X | X | |





| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Unapochunguza watoto wenye ulemavu katika tathmini ya mahitaji na tafiti za kiafya, fikiria kutumia *Moduli ya Watoto ya UNICEF-Washington*, au zana nyingine za tathmini ambazo zimejaribiwa na watendaji na wadau wa kibinadamu. | X | X | |
| Tambua vizuizi na hatari ambazo watoto wenye ulemavu wanakumbana nazo wakati wanapopata huduma za afya ya mtoto. | X | X | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Panga, andaa bajeti na utekeleze mafunzo kwa wafanyakazi wa afya juu ya haki za watoto wenye ulemavu. Jumuisha maendeleo ya watoto, na jitihada za kugundua ulemavu mapema. | X | X | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Fanya huduma na mipango ya afya ipatikane kwa watoto na kundi balehe wenye ulemavu, na walezi wao, kwa kuondoa vikwazo ili kuhamasisha ujumuishaji wao. | | X | X |
| Shirikisha wasichana na wavulana wenye ulemavu, na walezi wao, katika kubuni, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini mipango ya afya. | | X | X |
| Unganisha taarifa za afya na usimamizi wa ulemavu katika programu na huduma za afya ya mama na mtoto. Jumuisha chanjo, utoaji wa huduma kabla na baada ya kujifungua, lishe, na afya ya kijinsia na uzazi. | X | X | X |
| Jumuisha utambuzi wa mapema na kugundua ulemavu katika ngazi ya wafanyakazi, ngazi ya jamii na watendaji wa afya ya jamii. Wasaidie kutambua watoto wenye ulemavu, pamoja na ulemavu wa afya ya akili uwapeleke kwa ajili ya huduma za awali. | | X | X |
| Jumuisha utambuzi wa mapema na kugundua ulemavu katika ngazi ya wafanyakazi, ngazi ya jamii na watendaji wa afya ya jamii. Wasaidie kutambua watoto wenye ulemavu, pamoja na ulemavu wa afya ya akili uwapeleke kwa ajili ya huduma za awali. | X | X | X |
| Ambapo mipango ya afya ya watoto hutolewa kupitia shule, endesha mipango ya kuwafikia watoto walio nje ya shule wenye ulemavu. | | X | X |
| Wahimize wazazi na walezi wa watoto wenye ulemavu kujiunga na vikundi vya msaada wa wazazi. Sambaza habari za afya ya mtoto na elimu kupitia vituo vya afya vya jamii. | X | X | X |

| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **4. Uratibu** | | | |
| Kuratibu na sekta zingine kuhakikisha kuwa watoto wenye ulemavu wanapata msaada na ulinzi. | | X | X |
| Kuandaa na kutekeleza mifumo ya rufaa kwa watoto wenye ulemavu. Jumuisha huduma zinazolengwa, kama tiba ya kujifunza kuongea. | X | X | X |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Jumuisha viashiria kuhusu wasichana na wavulana wenye ulemavu katika zana za utunzaji. Toa taarifa juu ya matokeo ya kiafya kwa wasichana na wavulana wenye ulemavu. | | X | X |

## Rejea

- Kitengo cha afya, benki ya maarifa
- Shirika la afya duniani, huduma za malezi kwa maendeleo ya awali ya mtoto: mfumo wa kusaidia watoto kuishi na kukua katika kubadili afya na uwezo wa mtu





## Haki ya afya ya uzazi na jinsi

Watu wenye ulemavu wana haki ya afya ya jinsia, mapenzi na uzazi, ambayo ni sehemu ya haki ya afya. Wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wenye ulemavu lazima wapate huduma zinazopatikana za ujinsia, mapenzi na uzazi, na taarifa zinazokidhi mahitaji yao maalum.

Kwa ujumla, afya ya ujinsia na uzazi kwa watu wenye ulemavu ni kipaumbele cha chini kwa wadau wa afya, kwa sababu ya dhana potofu kwamba watu wenye ulemavu hawawezi kufanya chaguzi juu ya maisha yao ya kimapenzi.

### Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na upangaji** | | | |
| Ainisha huduma za afya ya jinsia na uzazi, na vifaa, kwa watu wenye ulemavu, na upatikanaji wao. Jumuisha utunzaji wa mama na watoto wachanga, uzazi wa mpango na uzazi wa mpango wa dharura, afya ya jinsia na uzazi na rika balehe, kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa kijinsia, maambukizo ya magonjwa ya zinaa, na huduma za VVU/UKIMWI. | X | X | |
| Tambua kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanapata huduma za afya, huduma na vifaa. Panga jinsi ya kushughulikia mapungufu. (Kwa mfano, tumia maandishi makubwa au nukta nundu kufanya habari zipatikane zaidi). Punguza muda wa kusubiri. | X | X | |
| Shughulikia mahitaji ya afya ya ujinsia na uzazi kwa watu wenye ulemavu, pamoja na watu wenye ulemavu wa akili, kuandaa huduma za ufikiaji na utoaji wa vifaa kwa watu wenye ulemavu ambao wametengwa katika nyumba zao. Hakikisha kuwa programu za ufikiaji zinajumuisha taarifa sahihi za afya ya uzazi. | | X | |
| Tathmini masuala ya ulinzi wa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wenye ulemavu. Fikiria jinsi wanavyoweza kupata taarifa na huduma za afya ya uzazi kwa ukaribu. Shughulikia hatari za usalama ambazo watu wenye ulemavu hugundua au kupata. | X | X | X |
| Tambua vikwazo na hatari ambazo watu wenye ulemavu wanapata wakati wanapopata huduma na programu za afya ya uzazi na masuala ya uzazi kwa ujumla. | X | X | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Tenga fedha za kuwafundisha wafanyakazi wa afya juu ya athari za jumla za masuala ya ujinsia kwa kutenganisha umri, jinsi na ulemavu. | X | X | |
| Kuajiri watu wenye ulemavu ambao wana utaalam na uzoefu juu ya afya ya jinsia na uzazi. | | X | X |

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Jumuisha mada zinazohusu masuala ya ulemavu katika mafunzo yote ya afya ya ujinsia na uzazi kwa wafanyakazi. Fanya mafunzo yatolewe kwa watoa huduma, wafanyakazi wa msaada, wafanyakazi wanaoifikia jamii, wahamasishaji, na wafanyakazi wanaofanya kwenye masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na VVU. | X | X | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Jumuisha mahitaji ya watu wenye ulemavu katika huduma zote za kuzuia na kutoa huduma ya ujinsia na uzazi (habari, huduma na vifaa). Fanya hivyo katika afya ya ujinsia na uzazi; afya ya mama na mtoto mchanga; huduma za uzazi wa mpango; huduma za kuzuia na kutoa huduma kuhusu ukatili wa kijinsia; na huduma za kuzuia na kushughulikia maambukizo ya zinaa, pamoja na VVU/UKIMWI. | | X | X |
| Kwa kushirikiana na vyama vya watu wenye ulemavu na mashirika yanayolenga watu wenye walemavu, tengeneza vifaa kwa taarifa vya umma kuhusu afya ya ujinsia na uzazi na usambaze kwa njia zinazopatikana. | X | X | X |
| Hakikisha kuwa taratibu za idhini huru zinaheshimiwa, ikiwemo wakati watu wenye ulemavu wanaombwa kufanya maamuzi. Taratibu zinapaswa kuzingatia Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu. Wafunze wafanyakazi na watoa huduma jinsi ya kuwasiliana na watu ambao wana ulemavu anuwai.[148] | | X | X |
| Hakikisha vituo vyote vya afya vinafikika kwa urahisi, na kwamba wafanyakazi wa afya ya jinsia na uzazi wanahamasishwa juu ya ujumuishaji wa watu wenye walemavu na wameandaliwa vizuri kutoa taarifa kwa njia anuwai zinazopatikana kwa urahisi. Jumuisha rika balehe la wenye ulemavu. | X | X | X |
| Himiza na hamasisha watu wenye ulemavu na mashirika yao kushawishi juu ya masuala ya haki ya afya ya uzazi, ikiwa ni pamoja na VVU, afya ya uzazi. | X | | X |
| Unda kamati inayoongoza kutetea kupitishwa kwa mtindo wa afya wa jinsia na uzazi ambao hujumuisha watu wenye ulemavu. Wanachama wanapaswa kujumuisha watu wenye ulemavu, wanachama wa mashirika ya watu wenye ulemavu na wawakilishi wa mashirika ya kitaifa, sekta za ulinzi na afya, na mamlaka za kitaifa. | X | | |
| Wasiliana na wanawake, wasichana na vijana wenye ulemavu wakati wa vikao vya habari vya jamii kuhusu afya ya uzazi. | | X | |

[148] Tume ya wakimbizi wanawake, *'Ninaona kuwa inawezekana kujengea uwezo katika ujumuishi wa masuala ya ulemavu katika nyenzo ya wadau wa ukatili wa kijinsia*. Nyenzo namba 9: Mchakato wa ridhaa arifu kwa wahanga wenye ulemavu.





| | Kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **4. Uratibu** | | | |
| Fanya uratibu pamoja na sekta nyingine (kama vile ulinzi, chakula na lishe) katika kuhakikisha mifumo bora ya afya ya uzazi ili kuhakikisha ufanisi katika mifumo ya rufaa. | | X | X |
| Fanya uratibu upande wa afya pamoja na sekta za kulinda, kundi linalofanya kazi kwenye sekta ya afya ya uzazi, maeneo yanayohusiana na unyanyasaji wa kijinsia ili kuhakikiksha kuwa watu wenye ulemavu wanalindwa na wanaweza kupTa vitu vyote vinavyohusiana na kujamiana na afya ya uzazi, taarifa huduma na mahitaji. | | X | |
| Himiza mashirika ya watu wenye ulemavu ya kitaifa na kijamii katika kushiriki kikamilifu katika vikosi kazi vya afya ya uzazi. | X | X | X |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Kusanya na ainisha takwimu kuhusu huduma za afya ya uzazi pamoja na jinsi zinavyotolewa. Nyambulisha taarifa kwa kuzingatia jinsia, umri na ulemavu. | | X | X |
| Fuatilia ufikivu wa huduma za afya ya uzazi. | X | X | X |
| Tumia mchakato wa ufuatiliaji na kutoa taarifa katika kukuza tafakari na uwajibikaji. Pitia kiwango ambacho watu wenye ulemavu wanaweza kuzifikia huduma za afya ya uzazi. | | X | X |

## Rejea


- Kitengo cha afya, benki ya maarifa
- Kikosi kazi cha mashirika mbalimbali katika afya ya uzazi wakati wa majanga. Afya ya uzazi ni kitu muhimu katika huduma za kibinadamu, uk. 1-2
- Kikosi kazi cha mashirika mbalimbali katika afya ya uzazi wakati wa majanga
- Kikosi kazi cha mashirika mbalimbali kuhusu afya ya uzazi wakati wa majanga, mafunzo, jitihada za ushirikiano
- Kikosi kazi cha mashirika mbalimbali kuhusu afya ya uzazi wakati wa majanga, mwongozo kwa mashirika kuhusu afya ya uzazi katika dharura (2018)
- Mradi wa *Sphere*, kitita cha huduma za awali kwa ajili afya ya uzazi (katika kitabu cha Sphere)
- UNFPA, ukimya, uzoefu ambao haujasikika kwa wanawake wenye ulemavu katika afya ya uzazi na ukatili dhidi ya wanawake wa visiwa Kiribati, Solomon na Tonga (2013)
- Tume ya wakimbizi wanawake, taarifa kuhusu ulemavu na afya ya uzazi

## Huduma za majeraha

Watu walio na ulemavu na wasio na ulemavu wako katika hatari ya kupata majeraha na kiwewe wakati wa majanga ya kibinadamu. Taratibu za kawaida zinatekelezwa kutibu kila aina ya jeraha; hata hivyo, ulemavu uliokuwepo hapo awali hauzingatiwi. (Tazama Shirika la Afya Duniani, *Viwango vya chini vya Kiufundi na Mapendekezo ya Utengamao*).

## Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na upangaji** | | | |
| Ainisha vituo vya majeraha na huduma za utengamao na uboreshaji wa mwili katika maeneo yaliyoathirika. Jumuisha vifaa saidizi, bandia na viungo, na huduma za afya ya akili. | X | | |
| Ainisha mashirika ya watu wenye ulemavu katika mahali husika na huduma zingine zinazohusiana na programu katika maeneo yaliyoathiriwa. Tathmini uwepo wake na upatikanaji wake. | X | X | |
| Ainisha wasambazaji wa vifaa saidizi, na upatikanaji wa vitu maalum na vifaa ambavyo watu wenye ulemavu wanahitaji. | X | | |
| Chunguza taarifa zinazopatikana juu ya majeraha mapya na uhitaji hasa wa huduma za afya za muda mrefu. | | X | |
| Elewa mifumo ambayo inawaumiza watu wenye ulemavu, njia yao, majibu na kupona, na upatikanaji wa huduma. | | X | X |
| Tambua vizuizi na hatari wanazokumbana nazo watu wenye ulemavu wanapoenda kupata huduma na mipango inayotoa huduma ya kuponya majeraha. | X | X | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Hamasisha wataalamu wa utengamano na maboresho ya mwili ambao wanaelewa ujumuishaji na wamefundishwa kufanya kazi na watu wenye ulemavu. | | X | |
| Ongeza fedha ili kuboresha huduma za utengamao wa mwili kwa muda mfupi na mrefu. | | X | X |
| Hakikisha kuwa bajeti za programu ya huduma za utengamao na maboresho inajumuisha gharama ya kuondoa vizuizi ambavyo vinazuia ufikivu wa watu wenye ulemavu. | | X | |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Wafunze wataalamu wa ukarabati ambao hufanya kazi katika maeneo yaliyo katika hatari ya majanga. Jumuisha utunzaji mahususi wa majeraha, huduma za afya ya akili na usimamizi wa majanga. | X | | |
| Kuunganisha huduma za utengamao wa viungo katika mipango yote ya majeruhi wa jumla na usimamizi wa majanga, pamoja na itifaki za matibabu na njia ya utunzaji wa majeraha ya kawaida yanayoweza kubalidisha maisha (kupoteza kuona, kusikia au kuongea, majeraha ya uti wa mgongo, na kukatwa viungo). | X | | |
| Kufanya ukaguzi wa upatikanaji wa vituo vya majeraha na huduma za ukarabati viungo. Fikiria upatikanaji wa huduma za kimwili, na upatikanaji wa mawasiliano na taarifa, na huduma. Buni na tekeleza mipango kazi ya utekelezaji kushughulikia vizuizi; Fuatilia. | X | X | |
| Wafunze wafanyakazi wa majeraha na wa utengamao katika kufanya tathmini ya mahitaji. Jumuisha ulinzi mpana wa watu walio na majeraha, na rufaa zao kwenda huduma zingine na sekta (kama makazi, ulinzi na maji na usafi wa mazingira). | | X | |
| Fuatilia mara kwa mara na tathmini mpango kazi ili kuhakikisha kwamba vituo vya majeraha na huduma za utengamao wa viungo zinapatikana kwa urahisi. | | X | |
| Toa vifaa vya bei nafuu, vinavyofaa kutumika kawaida, endelevu au vifaa vya usaidizi wa bure, viungo bandia na mifupa ambayo inazingatia viwango vya kimataifa (kwa mfano, viwango vya viti mwendo vya Shirika la Afya Duniani). | | X | |
| Kutoa matibabu ikiwemo ya upasuaji na utengemao wa viungo, pamoja na huduma za huduma za afya ya kwa watu wanaopata majeraha wakati wa majanga au migogoro. | | X | |
| Hakikisha kwamba watu wenye ulemavu ambao hawajajeruhiwa wanaweza kupata huduma wanazohitaji. Rejesha huduma za kabla ya dharura. | | X | |
| Ili kufikia watu waliojitenga zaidi wenye ulemavu, endeleza huduma za kijamii, na kutoa ufikiwaji na ufuatiliaji. Jumuisha watu wenye ulemavu wanaoishi katika kambi za wakimbizi au za wakimbizi wa ndani, maeneo yaliyo katika uzio na maeneo ya vijijini. | | X | X |
| Anzisha maduka ya kituo kimoja katika kliniki za awali za huduma za afya ili watu wenye ulemavu wasilazimike kwenda sehemu mbalimbali kupata huduma wanazohitaji. | | X | |
| **4. Uratibu** | | | |
| Ratibu sekta zingine kukuza na kutekeleza njia ya rufaa kwa huduma zingine na ulinzi. | | X | X |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Hakikisha vituo vya utengamao na majeraha vinachanganua taarifa kwa kuzingatia jinsia, umri na ulemavu. | X | X | X |

## Rejea


- CBM, Shirika la kimataifa la Handicap, ICRC, WHO, *viwango na mapendekezo ya marekebisho wakati wa dharura* (2016)
- kitengo cha afya, *benki ya maarifa*
- WHO, ISPO, USAID, *mwongozo wa utoaji wa vitimwendo katika muktadha wa rasilimali chache* (2008)
- Shirika la Afya Duniani, *Ushirikiano Katika Teknolojia Saidizi*


## Afya ya akili

Shughuli zinazolinda na kukuza afya ya akili na ustawi wa kisaikolojia zinahitaji kupatikana na kutekelezwa katika sekta zote, ikiwa ni pamoja na sekta ya afya, elimu, ulinzi na lishe.

Katika dharura za kibinadamu, vurugu, hofu na kutokuwa na uhakika kunaweza kusababisha fujo na kumaliza rasilimali za jamii. Kama matokeo, watu hupata athari ambazo zinaweza kudhoofisha utendaji kazi wao wa kila siku na mwingiliano wa kijamii.[149] Katika visa vingi, mienendo hii ni ya muda mfupi au watu wanaweza kuzoea mabadiliko ya ghafla. Kwa msaada mzuri wa kijamii na kihisia, watu wengi watashinda mapito haya magumu. Ili kufanikisha matokeo haya, ni muhimu kutumia na kuimarisha rasilimali katika familia na jamii zinazochochea ustahimilivu na kusaidiana. Katika mizozo ya muda mrefu ya kibinadamu, ukosefu wa tumaini na mfadhaiko ya muda mrefu unaoweza kusababisha sonono ya muda mrefu, kuongezeka kwa hali au ukali wa matatizo ya afya ya akili, pamoja na msongo wa mawazo na kujiua. Watu wengine, haswa watu ambao wameathiriwa sana, au ambao wamewahi kuwa na matatizo ya afya ya akili, au ambao wanakabiliana na ubaguzi na kutengwa, wanaweza kuhitaji msaada wa ziada unaotolewa na wataalamu wa afya ya akili waliofundishwa, au wataalamu wa afya ya akili.

Watu wenye ulemavu wa afya ya akili mara nyingi hukumbana na ubaguzi na kutengwa. Haki zao za kibinadamu zinaweza kukiukwa kwa kutengwa, kufungwa, kuzuiliwa kwa uhuru wao, au vitisho kwa uadilifu wao wa mwili na akili. Hatua za dharura zinapaswa kujumuisha hatua za kurekebisha ukiukwaji wa haki na ukosefu wa usawa ambao ulikuwepo kabla ya majanga, na pia kutoa fursa kwa watu wenye ulemavu wa afya ya akili kufurahia haki zao kikamilifu, pamoja na haki zao za afya pamoja na kuishi kwa heshima.

**Ulemavu wa afya ya akili** katika miongozo hii hutokana na vikwazo vya ushiriki wa kijamii na upatikanaji wa haki zinazohusishwa na afya ya akili au hali ya utambuzi au usumbufu katika tabia ambazo zinaonekana kama hazikubaliki kijamii. Neno kawaida huhifadhiwa kwa watu wenye upungufu zaidi au wa kawaida wa kazi, ambao wanakabiliwa na kutengwa na vikwazo vya kushiriki. Neno mara nyingi hutumiwa kwa wale wenye hali ya afya ya akili ya muda mfupi ambao hupona haraka, wakati mwingine katika kukabiliana na hatua za MHPSS. Wakati wa dharura za kibinadamu, dhiki inayosababisha ulemavu wa kazi mara nyingi ni ya muda mrefu, na ni muhimu si kuweka lebo kama vile hali ya matibabu au ulemavu.

Huduma za afya ya akili hazipaswi kuzingatia tu watu wenye ulemavu wa afya ya kiakili. Inapaswa kuzingatia watu wote katika jamii, pamoja na watu wenye ulemavu ambao hupata viwango tofauti vya dhiki katika mazingira ya huduma za kibinadamu. Walakini, miongozo hii inatambua kuwa watu wenye ulemavu wa afya kiakili wanakabiliwa na aina maalum za ubaguzi wa kimuundo, na wako katika hatari zaidi ya ukiukwaji wa haki za binadamu, na wameonyeshwa wazi katika mikutano ya kufanya maamuzi. Sekta ya ulinzi inapaswa kuangalia kwa karibu vikundi hivi katika idadi ya watu na kuchukua hatua kuhakikisha kuwa wanachama wake wanaweza kushiriki kijamii na katika mambo yote ambayo yanawahusu.

Sekta za afya na ulinzi zinapaswa kufanya kazi kwa karibu ili kulinda, kusaidia na kutunza watu wanaoishi katika magereza, taasisi za ustawi wa jamii na taasisi zingine za makazi, au ambao hawana makazi. Wanapaswa kuchukua hatua kuendeleza na kuimarisha huduma na miundo ya kijamii, ili

Wanapaswa kuchukua hatua kuendeleza na kuimarisha huduma na miundo ya kijamii, ili kuzuia kuwekwa katika makazi maalum na kumaliza matibabu ya kulazimishwa, vurugu, unyanyasaji na ukiukaji mwingine wa haki za binadamu katika maeneo haya. Aina hizi za unyanyasaji zinaathiri watu wenye ulemavu wa afya ya akili na mahitaji yao. Katika kutoa huduma kwa jamii, msaada na mipangilio ya kuishi kwa idadi hii ya watu, sekta ya ulinzi inapaswa pia kukuza ufuatiliaji huru na ufanisi katika taasisi zote, pamoja na magereza, ambayo watu wanazuiliwa, na kupata makazi yanayostahili kwa wale ambao hawana makazi.

Wakati dharura inatokea, afya ya akili na mfumo wa msaada wa huduma ya afya ya akili wa mkoa ulioathiriwa huenda ukapata matatizo. Katika visa vingi, inaweza isiwe na vifaa vya kutoa huduma ya

msingi ya kijamii na inayolenga haki za binadamu na msaada. Mizozo ya kibinadamu ni fursa ya kuwekeza juhudi na rasilimali kujenga mfumo ulio na vifaa kamili katika jamii ambao unaambatana na viwango vya kimataifa vya haki za binadamu.

Mara nyingi ni ngumu wakati wa dharura kufikia mahitaji ya watu wenye ulemavu wa afya ya akili. Hasa katika nchi ambazo hazijaheshimu mkataba wa haki za watu wenye ulemavu. Pale ambapo mifumo ya afya ya akili sio ya kijamii au inayolenga haki za binadamu, mwongozo wa nyongeza unapaswa kutolewa kwa mambo ya msingi ya upatikanaji wa msaada, katika ngazi zote, pamoja na katika jamii na katika familia. Kwa mfano, mipango ya kujenga uwezo inapaswa kuzingatia uanzishaji wa taratibu ambazo zinalinda umuhimu wa utoaji idhini huru (katika matibabu au uchunguzi), iliunga mkono uamuzi na hatua zisizo za kulazimisha.

### Hatua zinazopendekezwa

Mikakati yote inapaswa kuunganishwa na watu wenye ulemavu (pamoja na watu wenye ulemavu wa afya ya akili), familia zao, na mashirika ya watu wenye ulemavu, kwa kushirikiana kwa karibu na wataalam wa MHPSS na watoa huduma katika vikundi vya kiufundi vya MHPSS.

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na upangaji** | | | |
| Kulingana na matokeo ya tathmini, panga majibu ya MHPSS na programu za MHPSS. Hakikisha haya yanashughulikia mahitaji ya watu wenye ulemavu. | X | X | |
| Kuendeleza au kurekebisha sera za kitaifa za afya ya akili, mikakati, mipango na sheria. Hakikisha mfumo wa kitaifa wa MHPSS imejikita katika jamii na unaendana na haki za binadamu. | X | X | X |
| Kwa kutumia mpango wa Shirika la Afya Duniani *kuhusu nyenzo za kupata haki* anzisha maandalizi ya dharura ya taasisi na mipango ya huduma, ikiwa ni pamoja na mipango ya uokoaji. Mipango ya uokoaji inapaswa kulinda viungo vya familia na jamii. | X | X | X |

[149] IFRC, *Mwongozo kwa afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia* (2018).

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Kulingana na yaliyobainika, buni mwitikio na program za MHPSS. Hakikisha masuala haya yanaeleza mahitaji ya watu wenye ulemavu. | X | X | X |
| Unda au boresha sera za taifa kuhusu ulemavu wa akili, mbinu, mipango na sharia. Hakikisha kuwa mfumo wa taifa wa MHPSS upo wa jamii zaidi sambamba na haki za binadamu. | | X | X |
| Unda mpango kuwa tayari na dharura za taasisi lakini pia kuzikabili na mipango ya kuhamisha. Mipango ya kuhamisha inakuwa salama kwa familia na jamii. | X | | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Kuhamasisha bajeti zinazotolewa kwa ajili ya huduma za jamii na MHPSS zinayohusu haki za binadamu na huduma ambazo zinajumuisha watu wenye ulemavu. | | X | X |
| Tenga bajeti na rasilimali ili kupata wasaidizi rika (kujumuisha kutoka mikoa mingine) kusaidia watu wenye ulemavu wa afya ya akili katika maeneo yaliyoathiriwa. | X | X | X |
| Hakikisha kwamba rufaa za kisekta, mapendekezo na maandiko ya awali ya miradi yanajumuisha maoni ya MHPSS. | | X | X |
| Anzisha, wezesha au hamasisha vikundi vya msaada rika, vikundi vya utetezi vinavyoongozwa na watu wenye ulemavu, na msaada wa kijamii. | X | X | X |
| Kusanya rasilimali ili kusaidia shughuli za ufikiwaji kwa watu wenye ulemavu ambao wamewekwa katika taasisi/nyumba, wanaishi kifungoni au wanapokea tiba ya jadi au ya kidini nyumbani. Bajeti hizi zinapaswa kulipia gharama za: huduma muhimu, ufuatiliaji, hatua za kuingilia kati ukiukaji wa haki za binadamu; na ujumuishaji katika jamii. | | X | X |
| Hamasisha wanajamii wenye ushawishi kupinga tamaduni na mitazamo inayoendeleza au kuhalalisha ukiukwaji wa haki za watu wenye ulemavu. | X | X | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Ongeza uelewa katika jamii ya watu wenye ulemavu na haki za watu wenye ulemavu, pamoja na watu wenye ulemavu wa afya ya akili. | X | X | X |
| Jenga uwezo wa wataalam na wasio wataalamu, pamoja na wawakilishi wa mashirika ya watu wenye ulemavu, wanaojitolea na wasaidizi rika. Mafunzo yanapaswa kujumuisha mfumo wa haki za binadamu, mbinu anuwai katika MHPSS, utunzaji wa jamii, kugawana kazi na msaada wa kwanza wa afya ya akili. | X | X | X |





| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Jenga uwezo wa wafanyakazi wa huduma za kibinadamu. Wafundishe jinsi ya kuingiliana katika mazingira ya dharura na watu ambao wana ulemavu wa afya ya akili. | X | X | X |
| Jumuisha huduma za afya ya akili yenye ushahidi katika mfumo wa awali wa huduma ya afya. | X | X | X |
| Toa huduma za MHPSS zilizojikita katika jamii na haki za binadamu ziwepo na zipatikane kwa urahisi kwa watu wenye ulemavu katika ngazi zote za huduma. Tumia mpango kazi shirikishi. | X | X | X |
| Hakikisha huduma za afya ya akili zilizothibitika zipo na zinapatikana kwa watu wenye ulemavu katika ngazi zote za utunzaji.[150] | X | X | X |
| Tekeleza *zana za Haki za Ubora za Shirika la Afya Duniani* kulinda maisha na hadhi ya watu ambao wamewekwa katika taasisi; kuimarisha ufuatiliaji wa haki za binadamu; kuweka katika nafasi mipango ya uokoaji wa taasisi; na kulinda viungo vya familia na jamii wakati wa uokoaji. | X | X | X |
| Endeleza itifaki za kuzuia matibabu ya kulazimishwa, pamoja na kulazimishwa kuwekwa kwenye makazi maalumu, dawa za kulazimishwa, matibabu ya umeme kwa kulazimishwa, na vizuizi vya mwili na kemikali. | X | X | X |
| Chukua hatua kuhakikisha kuwa vituo vya utunzaji vilivyoharibiwa au visivyotumika ambavyo hapo awali watu wenye ulemavu waliwekwa, havifunguliwi. Hamasisha mfumo wa MHPSS na unaohusu haki za binadamu. | | | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Ratibu na vikundi hai vya ufundi vya MHPSS ili kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu wamejumuishwa katika majibu ya MHPSS. | | X | X |
| Kukuza ushirikiano baina ya sekta ili kuhakikisha kuwa mipango ya MHPSS inahusisha (kwa kiwango cha chini) mashirika ya watu wenye ulemavu na watendaji kutoka katika sekta ya afya, ulinzi bobevu wa jamii, ulinzi wa watoto na elimu. | | X | X |
| Anzisha mfumo Madhubuti wa MHPSS katika jamii, unaotegemea njia ya haki za binadamu, inayotoa huduma bora, inayoungwa mkono na mfumo madhubuti na mzuri wa rufaa wa kisekta ambao unajumuisha rasilimali za jamii, waganga wa jadi na vituo vya kidini. | | X | X |
| Pale ambapo watu wenye ulemavu wamewekwa katika taasisi maalumu, tambua wakala atakayechukua jukumu la uondoaji wa taasisi hizo. Tafuta kuhamisha watu kutoka taasisi hadi makazi ya jamii ambayo hutoa msaada unaofaa, wakati unahakikisha utunzwaji wao na ulinzi. | | X | X |

[150] Usimamizi wa matatizo, tiba kwa ajili ya huzuni.

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Anzisha utaratibu wa ufuatiliaji wa programu na huduma za MHPSS, kwa kuzingatia mfumo wa pamoja wa IASC MHPSS wa Usimamizi na Tathmini. | X | X | X |
| Jumuisha watu wenye ulemavu, pamoja na watu wenye ulemavu wa afya ya akili katika kufuatilia mipango na huduma za MHPSS. Shirikisha pia familia zao, watu wa kusaidia na walezi, na mashirika ya watu wenye ulemavu. | X | X | X |
| Kufuatilia kwa utaratibu haki za binadamu za watu wenye ulemavu, kwa kutumia zana za Haki za Ubora za Shirika la Afya Duniani. | X | X | X |
| Kubuni au kuzoea mifumo ya usimamizi wa taarifa na orodha za vituo. Hakikisha kuwa taarifa iliyokusanywa imegawanywa kwa jinsi, umri na ulemavu. | X | | |

## Rejea


- IASC, *mwongozo kwa afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia katika muktadha wa dharura* (2007)
- IASC, *mwongozo wa afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia katika muktadha wa dharura, kitu gani wadau wa masuala ya kibinadamu katika afya wanapaswa kufahamu* (2011)
- IASC, *mwongozo kwa afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia katika muktadha wa dharura: ni kitu gani waratibu wa kambi na viongozi wa kambi wanapaswa kufahamu?* (2014)
- IASC, *mwongozo wa rufaa kwa mashirika mbalimbali katika afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia katika muktadha wa dharura* (2017)
- IASC, *MHPS, mfumo wa kawaida wa ufuatiliaji na tathmini* (2017)
- IASC, *nani yupo wapi, lini, anafanya nini katika masuala ya afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia* (2014, Nyenzo Ya 4W)
- IASC kundi la rejea kuhusu afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia, *afya ya akili na usaidizi wa kisaikilojia katika dharura za kibinadamu, ni vitu gani wasimamizi wa programu wanapaswa kufahamu* (2010)
- Sphere, *kitabu cha Sphere* (2018)
- Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi, *ulinzi wa kijamii na afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia* (2017)
- Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi, *mwongozo wa oparesheni kwa ajili ya afya ya akili na programu ya usaidizi wa kisaikolojia, katika operesheni za wakimbizi* (2013)
- Tume ya Umoja wa Mataifa ya haki za binadamu, *ripoti ya mwakilishi maalum kuhusu haki za kila mmoja kufurahia viwango vya juu vinavyoweza kufikiwa katika afya ya mwili na akili*, A/HRC/35/21, 28 Machi 2017
- Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi, *mwongozo wa oparesheni ya msaada wa kijamii ya afya ya akili na saikolojia katika muktadha huduma za kibinadamu, mafiga matatu katika usaidizi wa watoto na familia* (2018)
- Shirika la afya duniani na shirika la umoja wa mataifa la wakimbizi, *kutathmini afya ya akili na rasilimali* (2012)
- Shirika la afya duniani, *nyenzo ya haki bora* (2012)
- Shirika la afya duniani, *vifaa vya mafunzo kwa haki bora* (2019)






## Magonjwa yasioweza kuambukizwa

Magonjwa yasiyoweza kuambukizwa, au magonjwa sugu, huwa ni ya muda mrefu na hutokana na mchanganyiko wa kigenetikia, kisaikolojia, kimazingira na viashiria tabia. Aina kuu ni magonjwa ya moyo na mishipa (kama vile mshtuko wa moyo na viharusi), saratani, magonjwa sugu ya kupumua (kama ugonjwa wa mapafu na pumu), ugonjwa wa kisukari, na hali ya akili na neva (kama vile shida ya kusahau).[151]
Watu wenye ulemavu wakati mwingine huwa katika hatari kubwa ya kupata magonjwa yasiyo ambukizwa kwa sababu, kwa mfano, wanaweza kuwa wasiotembea sana, wanaishi katika mazingira ya kujilinda kupita kiasi, au wanakula lishe isiyo sawa.
Kulingana na Shirika la afya duniani, suala la kusimamia magonjwa yasiyo ambukizwa wakati wa dharura, ni muhimu:

1. Kutibu magonjwa makali ambayo yanahitaji umakini maalum wakati wa dharura, na kuanzisha mipangilio ya ziada pamoja na utaratibu wa rufaa.
2. Kuendelea na matibabu endelevu (kwa njia ya dawa, teknolojia au vifaa).
3. Kufanya marekebisho ili kukidhi kupungua kwa uwezo wa kukabiliana.
4. Kuratibu utoaji na utunzaji katika anuwai ya watoa huduma na mipangilio.

## Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na upangaji** | | | |
| Jumuisha taarifa zilizogawanywa kwa jinsi, umri na ulemavu katika mchakato wa upimaji wa haraka wa hatari. Weka kumbukumbu ya magonjwa yaliyokuwepo kabla ya majanga. | X | | |
| Fanya kazi na jamii kutambua watu wenye ulemavu ambao wana magonjwa yasiyo ambukizwa na ambao wametengwa kwa sababu ya umbali au unyanyapaa na ubaguzi. | X | X | |
| Shirikisha mashirika ya watu wenye ulemavu katika kutambua vizuizi ambavyo watu wenye ulemavu wanapata wakati wanapopata dawa muhimu wanazohitaji. Tumia maagizo kwa matibabu makali ya hali sugu kupitia "*Interagency Emergency Health Kit*", yaani Vifaa vya Afya vya Dharura kwa Mashirika Mbalimbali. | X | X | |
| Ainisha na pitia itifaki, miongozo na zana za kusimamia magonjwa yasiyoambukizwa na hakikisha wanazingatia na kujumuisha watu wenye ulemavu. | X | X | |
| Ainisha mashirika ya watu wenye ulemavu na watoa huduma zinazohusiana, kwa ajili ya rufaa na msaada. | X | X | |
| Hakikisha kwamba kanuni za huduma zinajumuisha kikamilifu watu wenye ulemavu. Wafunze wafanyakazi wa afya ambao hufanya kazi katika usimamizi jumuishi wa magonjwa yasiyo ambukizwa katika hali za dharura kuelewa na kutekeleza kanuni hizo. | X | X | X |

[151] Kutambua umuhimu wa afya ya akili na usaidizi huduma za kisaikilojia, kipengele maalum kinachoangalia vizuizi kwa watu wenye afya ya akili na wale wanaokabiliana msongo. Angalia afya ya akili na usaidizi wa kisaikolojia.

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **2. Ugemaji wa rasilimali** | | | |
| Saidia maendeleo ya bajeti inayojumuisha magonjwa yasiyo ambukizwa. Hamasisha fedha ili kufidia gharama za kufanya huduma za magonjwa yasiyo ambukizwa katika nyakati za dharura kuwepo na kupatikana kwa watu wenye ulemavu. | X | X | |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Sambaza kwa mapana _vifaa vya afya vya dharura kwa mashirika mbalimbali, kwa ajili ya kutibu magonjwa na hali sugu_. Hakikisha inapatikana kwa watu wenye ulemavu. | X | | |
| Buni na sambaza nyenzo za kukuza afya na elimu ya wagonjwa katika njia nyingi zinazoweza kupatikana kiurahisi (mfano, maneno, machapisho, lugha ya alama, lugha nyepesi, maandishi makubwa, n.k). | X | X | |
| Hakikisha kuwa dawa, itifaki na rufaa kwa ajili ya magonjwa yasiyo ambukizwa huzingatia mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu (kwa mfano, matibabu ya kifafa). | | X | |
| Fanya kazi na mashirika ya watu wenye ulemavu na mashirika yanayolenga walemavu, kuondoa vizuizi vinavyozuia utoaji fanisi na wa haraka wa huduma kwa magonjwa yasiyo ambukizwa kwa watu wenye ulemavu. | X | X | |
| **4. Uratibu** | | | |
| Hakikisha ushiriki fanisi wa watu wenye ulemavu katika mifumo ya uratibu wa magonjwa yasiyo ambukizwa. | X | X | |
| Hakikisha kuwa huduma za afya zinaratibu rufaa baina ya sekta kwa watu wenye ulemavu ambao wana shida zinazohusiana na magonjwa yasiyo ya kuambukizwa. | | X | |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Hakikisha kuwa huduma za afya zinaratibu rufaa baina ya sekta kwa watu wenye ulemavu ambao wana shida zinazohusiana na magonjwa yasiyo ambukizwa. | | X | |
| Kufuatilia ujumuishaji wa watu wenye ulemavu katika upangaji wa mipango ya magonjwa yasiyo ambukizwa na utoaji wa huduma. | X | X | X |
| Jumuisha viashiria mahususi vya magonjwa yasiyoambukizwa katika zana za upimaji wa haraka, pamoja na ule wa awali wa _vitengo tofauti na zana zingine za ufuatiliaji na tathmini_. | X | X | |





## Rejea


- Kitengo cha Afya, _Benki ya Maarifa_
- Kikosi kazi cha mashirika mbalimbali ya Umoja wa Mataifa katika magonjwa yasiyoambukiza, na shirika la afya duniani, _magonjwa yasiyoambukiza katika muktadha wa majanga ya dharura_ (2016)
- Shirika la afya duniani, _mwongozo wa timu za dharura za tiba_
- Shirika la afya duniani, _ukondoishaji wa huduma za magonjwa yasiyoambukiza wakati kujiweka tayari na katika kutoa huduma katika majanga ya dharura)_ (2018)
- Shirika la afya duniani, _kitita cha mambo muhimu katika afua za magonjwa yasiyo ya kuambukiza katika huduma ya afya ya msingi katika muktadha wa maeneo yenye rasilimali chache_ (2010)
- Americares, _magonjwa yasiyo ya kuambukiza katika dharura za kibinadamu_ (2018)

# 16 Ulinzi

Angalia Taarifa na usimamizi wa taarifa, Uratibu na usimizi wa makambi, Elimu, Usalama wa chakula na lishe, Riziki/kazi, Afya, Nyumba na makazi, na Maji na usafi wa mazingira.

## Utangulizi

IASC inaelezea ulinzi 'Kama shughuli zote zinazolenga kuleta heshima kwa ajili ya haki ya mtu kulingana na matakwa ya sheria (kwa mfano, Mkataba wa Haki za Kimataifa za Binadamu, Sheria ya Kimataifa ya Masuala ya Kibinadamu, na Sheria ya Kimataifa ya Wakimbizi)".[152] Ulinzi ni kitovu cha hatua za masuala ya huduma za kibinadamu.[153] Kwa nyongeza mtazamo wa ulinzi unatambua kuwa jamii zilizoathiriwa zina uwezo, haki na zinaweza kudai haki zao, hivyo sio watazamaji au wapokeaji wa misaada pekee.

Kitabu cha Sphere kinatoa kanuni nne za Ulinzi ambazo zinawakilisha mambo muhimu ya ulinzi katika huduma za kibinadamu:[154]

- Kuwezesha usalama, utu na haki za watu na kuzuia kuwaweka katika hatari.
- Kuhakikisha kuwa watu wanapata usaidizi fikivu kulingana na mahitaji yao bila ya ubaguzi.
- Kuwasaidia watu kupona kutoka katika athari za kimazingira au za kisaikolojia zilizobabishwa na vitisho, kuumizwa au kukosewa haki kwa makusudi.
- Wasaidia watu kudai haki zao.

Shughuli za hifadhi zinaweza kuwa:

- Kutoa huduma (kunakolenga kuzuia au kusitisha ukiukwaji wa haki unaoendelea).
- Kurekebisha (kunakolenga kutoa fidia kwa ukiukwaji wa haki uliotokea awali).
- Mazingira (kujenga miundo ya kisheria na ya kitaasisi, kujenga uwezo na uelewa unaohitajika katika kukuza heshima na haki za binadamu).[155]

**Tumia mbinu mtambuka katika hifadhi na hifadhi za kijamii**

Afua za hifadhi ni imara iwapo zitahusisha jamii zilizoathiriwa katika kutoa huduma juu ya hatari wanazokumbana nazo. Hifadhi za kijamii zinalenga katika kuweka jamii zilizoathirika katika mstari wa mbele wa huduma na kuimarisha rasilimali na uwezo. Inafanya kazi na jamii zilizoathiriwa kama washirika kuliko kutegemea kwa wadau wa nje. Mtazamo huu unapaswa kutumiwa na vitengo vya sekta vya ulinzi kwa sababu inawasaidia katika kuainisha hatari za ulinzi na kutengeneza majawabu ambayo yanaweza kutekelezeka kwa mafanikio katika ngazi ya jamii.

[152] IASC, Haki za binadamu na majanga ya asili: Mwongozo wa operesheni na kitabu cha mwongozo kuhusu ulinzi kwa haki za binadamu katika hali za majanga ya asili (2008). Angalia pia sera ya ulinzi ya IASC.

[153] Tamko la IASC, umuhimu wa ulinzi katika masuala ya kibinadamu (2013).

[154] Kitabu cha Sphere (2018).

[155] IASC, haki za binadamu na majanga ya asili: Mwongozo wa operesheni na kitabu cha mwongozo kuhusu ulinzi kwa haki za binadamu katika hali za majanga ya asili (2008).

Shughuli hizi hutekelezwa kupitia hifadhi ya jumla au programu mahsusi za uhifadhi. Katika muktadha wa huduma za kibinadamu, watu wenye ulemavu mara nyingi wanakabiliana na hatari kubwa pamoja na vizuizi vingi katika kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki na kupata huduma za ulinzi. Kwa hiyo ni muhimu kuwaweka katika mstari wa mbele wakati wa kubuni, kutekeleza, na kufuatilia shughuli za ulinzi. Kwa kuongezea, wana familia, walezi na wasaidizi wana jukumu muhimu katika maisha ya watu wengi wenye ulemavu. Ni muhimu kuwazingatia wakati wa kuchambua aina ya ulinzi na hatari zake, kwa sababu wao ni sehemu ya suluhu na wakati mwingine huwa ni wasababishi wa hatari.

*Vitengo vya kimataifa ya ulinzi* vinajumuisha maeneo kadhaa ya majukumu; ulinzi wa watoto; ulinzi dhidi ya ukatili wa kijinsia, makazi na mali, milipuko. Sura hii inaangazia muundo wa Vitengo vya Kimataifa vya Ulinzi.

## Dhana muhimu

**Kukondoisha ulinzi**, wakati mwingine hujulikana kama 'Namna ya kuandaa programu salama,' ni mchakato wa kuingiza kanuni za ulinzi na kukuza ufikivu wenye tija, ushiriki, uwajibikaji, usalama, utu katika misaada ya kibinadamu".[156]

**Kujumuisha ulinzi** inahusisha kuangazia malengo ya ulinzi katika programu mahsusi za kutoa huduma katika sekta mbalimbali (zaidi ya huduma za ulinzi) katika kufikia matokeo ya ulinzi.[157]

**Shughuli mahsusi za ulinzi au shughuli maalum za ulinzi**, wakati mwingine zinaitwa afua zinazojitegemea. Hizi ni shughuli maalum ambazo zinasaidia watu kubaki salama, kujikwamua kutoka katika hatari, na kupata ufikivu wa haki zao.[158] Wadau wa masuala ya kibinadamu walio na utaalamu wa ulinzi hutekeleza shughuli hizi.[159]

'**Kufanya programu bila kuleta madhara**' ni maagizo kwa mashirika ya kibinadamu kufanya utendaji bila kusababisha madhara. Wanapaswa kuzuia kutokea kwa hatari na kupunguza madhara ambayo yanaweza kutokea bila kukusudia kwa sababu ya kazi na usaidizi wao. Wadau wa masuala ya kibinadamu wanahitaji kuwa na uelewa na kuchukua hatua katika kupunguza athari zinazohusiana na uwepo na shughuli zao.[160]

### Miundo ya sheria na miundo mingine[161]


- Mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu
- Mkataba wa haki za watoto
- Mkataba wa katazo la mabomu ya kutegwa na watu
- Mktata wa makombora
- Mkataba wa aina fulani ya silaha, protokali II na V[162]
- Mkataba wa kuondoa aina zote za ukatili dhidi ya wanawake
- Mkataba wa kuondoa aina zote za ubaguzi wa rangi
- Mkataba wa kimataifa wa haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni
- Mkataba wa kimataifa wa haki za kiraia na kisiasa
- Sera ya IASC kuhusu ulinzi katika masuala ya kibinadamu (2016)

[156] *Wadau wa masuala ya kibinadamu walio na utaalamu wa ulinzi hutekeleza shughuli hizi* (2014).
[157] IASC, *sera ya ulinzi katika masuala ya kibinadamu* (2016).
[158] Oxfam na Konga ya ulinzi wa kidunia, *Ulinzi: Hicho ni nini?* (2016).
[159] IASC, *sera ya ulinzi katika masuala ya kibinadamu* (2016).
[160] UNICEF, misingi ya masuala ya kibinadamu (2004). Angalia CDA, *kitabu cha usifanye madhara*.
[161] Angalia pia IASC, *ya IASC kuhusu ulinzi katika masuala ya kibinadamu*, Kiambatishi namba 1: *Normative Framework*.
[162] IASC, *Sera ya IASC kuhusu ulinzi katika masuala ya kibinadamu* (2016).





**Mchoro namba 11 |** Vikwazo katika ufikivu na ujumuishi katika maeneo ya uhifadhi



## Rejea


- *Kitabu cha Sphere* (2018). Angalia Kipengele kuhusu ulinzi
- *Kitengo cha ulinzi wa kidunia*. Angalia nyenzo na miongozo
- Help Age, CBM, Shirika la kimataifa la Handicap, *viwango vya ujumuishi kwa wazee na watu wenye ulemavu* (2018). Angalia kipwngele cha ulinzi
- *Viwango kwa ajili ya ulinzi wa watoto katika masuala ya kibinadamu*
- IASC, *mwongozo wa kukondoisha ukatili wa kijinsia katika afua za masuala ya kibinadamu* (2015)
- IASC, *mchakato wa operesheni wa viwango vya ukatili wa kijinsia* (2008)
- *Mwongozo wa mashirika mbalimbali ya usimamizi wa kesi za ukatili wa kijinsia* (2017)
- IASC na kitengo cha ulinzi wa kidunia, *huduma kwa wahanga wa ukatili wa kingono* (2010)


## Masuala muhimu ya kufanya

Masuala ya muhimu ni lazima yafanyike katika hatua zote za masuala ya huduma za kibinadamu wakati wa kutekeleza programu za ulinzi kwa watu wenye ulemavu.

### Ushiriki

- Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu na mashirika ya watu wenye ulemavu yanashiriki katika kuainisha hatari za ulinzi pamoja na vizuizi katika kufikia ulinzi.
- Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanawakilishwa kikamilifu katika michakato rasmi na isiyo rasmi ya ulinzi ikiwemo michakato ya ulinzi ya kijamii. (Uongozi wa kambi pamoja na makundi ya wanawake na vijana), kwa kuzingatia aina zote za ulemavu pamoja na umri, jinsia na anuwai. Fanya juhudi za makusudi katika kukuza uwakilishi wa makundi yenye uwakilishi mdogo kama vile watu wenye ulemavu wa akili pamoja na ulemavu wa afya ya akili, watu wa asili la eneo hilo, wanawake na wasichana.

### Kushughulikia vikwazo

- Ainisha na fuatilia vizuizi vinavyowazuia watu wenye ulemavu kufikia huduma za ulinzi na pia chukua hatua za kufanya mifumo ya ulinzi na huduma kuwa fikivu kwao. Toa huduma na pia fanya marekebisho stahiki kuwafikia watu wenye ulemavu ambao hawawezi kuondoka nje ya nyumba zao.
- Wasilisha taarifa zote zinazohusiana na uhifadhi kwa kupitia mifumo fikivu, kwa kuzingatia watu wenye uziwi, wenye uoni hafifu, ulemavu wa afya ya akili.
- Pitia sera, miongozo na nyenzo za kisekta kuhakikisha kama zinafuata haki za watu wenye ulemavu na ujumuishi.

### Uwezeshaji na kujengewa uwezo

- Hakikisha kuwa, wakati watu wenye ulemavu wanahitaji kufanya maamuzi binafsi, ikiwemo watu wenye ulemavu wa afya akili, taratibu lazima zifuatwe na wakubali kwa kutoa idhini huru.[163]
- Kupitia mafunzo na kukuza uelewa, wawezeshe wadau wa ulinzi kuwa makini na haki za watu wenye ulemavu na hatari mahsusi za ulinzi wanazozikabiliwa nazo, wawezeshe kupata mitandao ya eneo husika na ya kitaifa ya mashirika ya watu wenye ulemavu, tathmini uwezo wao wa kufanya kazi katika kukondoisha ulinzi na kutoa mafunzo na msaada pindi unapohitajika. Wahusishe katika mifumo ya uratibu wa masuala ya ulinzi.

[163] Angalia ICRC, *viwango vya kitaalamu vya kazi ya ulinzi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na wadau wa haki za binadamu katika migogoro ya kivita na katika hali zingine za vurugu* (2018).





- Kupitia mafunzo na kukuza uelewa, wawezeshe wadau wa ulinzi kuwa makini na haki za watu wenye ulemavu na hatari mahsusi za ulinzi wanazozikabiliwa nazo, wawezeshe kupata mitandao ya eneo husika na ya kitaifa ya mashirika ya watu wenye ulemavu, tathmini uwezo wao wa kufanya kazi katika kukondoisha ulinzi na kutoa mafunzo na msaada pindi unapohitajika. Wahusishe katika mifumo ya uratibu wa masuala ya ulinzi.
- Wahusishe watu wenye ulemavu pamoja na mashirika yanayowawakilisha katika kuhamasisha jamii na shughuli za kufikia watu. Wajengee uwezo katika kuainisha na kutambua watu walio katika hatari ya ukatili au unyanyasaji na chukua hatua stahiki katika kulinda haki zao na kushughulikia ukiukwaji wa haki.[164]

### Kukusanya takwimu na ufuatiliaji

- Kusanya na kisha chambua taarifa za ulinzi kuhusu watu wenye ulemavu. Zichambue kwa jinsia, umri na ulemavu, fanya kwa utaratibu maalum katika programu zote za kibinadamu, katika mifumo yote ya usimamizi wa taarifa za ulinzi, ikiwemo mfumo wa usimamizi wa taarifa za unyanyasaji wa kijinsia, mfumo wa ulinzi wa watoto na kanzidata za kitaifa za kutoa taarifa.
- Kusanya taarifa kuhusu vikwazo katika kudai haki na kuondoshwa kwa vizuizi ambavyo vinazuia kufikia huduma za ulinzi.
- Hakikisha kuwa maadili ya kupata taarifa na kanuni za ulinzi (ikiwemo usiri, kutoa taarifa, idhini huru, ulinzi) yanaheshimiwa wakati taarifa kuhusu watu wenye ulemavu zinapokusanywa na kutumiwa.[165]
- Sambaza taarifa kuhusu mahitaji ya watu wenye ulemavu ya sekta mbalimbali (maji, usafi, afya, elimu) na hakikisha uratibu baina ya sekta.
- Fuatilia ukiukwaji wa haki za watu wenye ulemavu.

## Hifadhi

### Athari za hatari zinazohusiana na hifadhi

- Watu wenye ulemavu wanaweza kukumbana na ukatili na unyanyasaji unaowalenga kwa sababu ya ulemavu wao.[166] Katika tafiti za hivi karibuni kuhusu watu wenye ulemavu katika muktadha wa kibinadamu, asilimia 27 ya walioshiriki katika utafiti walitoa taarifa kuwa wamewahi kupata unyanyasaji wa kimwili na kisaikolojia au aina nyingine za unyanyasaji ikiwemo unyanyasaji wa kijinsia.[167] Ukatili huu unaowalenga watu wenye ulemavu unaweza, kuhusisha kushambuliwa, mauaji,[168] kukataliwa kupewa chakula na dawa, kunyanyaswa, kunyanyaswa kihisia, kupuuzwa kwa hali ya juu, kufungwa minyororo na kifungo. Unyanyasaji wa aina hii mara nyingi hupangwa na watu wanaowafahamu.[169] Ukatili mwingi unaowalenga watu wenye ulemavu hautolewi taarifa au kufuatiliwa, ni programu chache sana hutoa huduma za kufanyia kazi matendo haya.
- Watu wenye ulemavu ambao hawawezi kutoa taarifa kuhusu maisha yao wanaweza kuwa katika hatari kubwa. Tatizo hili hutokea kwa watu wenye ulemavu wa afya ya akili.[170] na watu wanaopata shida ya kuwasiliana. Wakati wa mchakato wa uchunguzi wa kiusalama, kwa mfano watu wenye ulemavu wanaweza kushindwa kujibu maswali yanayohusiana na usalama.[171]

[164] Angalia IASC, *sera ya ulinzi katika masuala ya kibinadamu* (2016), uk. 2.

[165] Angalia ICRC, *viwango vya kitaalamu vya kazi ya ulinzi inayofanywa na wadau wa masuala ya kibinadamu na wadau wa haki za binadamu katika migogoro ya kivita na katika hali zingine za vurugu* (2018), Sura ya 6, Usimamizi wa data na taarifa kuhusu matokeo ya ulinzi uk. 106-108 na CRPD, *Ibara ya 22(2)*.

[166] Angalia shirika la afya duniani, *uwepo na hatari ya ukatili dhidi ya watu wazima wenye ulemavu: mapitio na uchambuzi* (2012) na shirika la afya duniani, *Ripoti ya dunia kuhusu ulemavu* (2011).

[167] Shirika la kimataifa la Handicap, *ulemavu katika muktadha wa kibinadamu-mitazamo kutoka kwa watu walioathirika na mashirika yaliyopo kazini* (2015).

[168] Angalia UNICEF, *ukatili dhidi ya watoto wenye ulemavu: ripoti kwa ufupi* (2005), uk. 6.

[169] *Ibid*.

[170] Shirika la Afya Duniani, *kuhimiza haki na maisha ya kijamii kwa watoto wenye ulemavu wa kisaikolojia* (2015).

[171] Waangalizi wa haki za binadamu, *wanapaswa kuishi hapo mpaka watakapokufa* (2018); Waangalizi wa haki za binadamu, *Kufungwa kama wafungwa* (2015).

- Watu wenye ulemavu kwa sehemu kubwa hukosa nyaraka binafsi (cheti cha kuzaliwa, cheti cha ndoa, hati za kusafiria) kwa sababu nyingi ikiwemo kushindwa kuandikishwa wakati wa kuzaliwa, kunyimwa uwezo wa msaada wa kisheria (kama aina ya unyanyapaa).
- Watu wenye ulemavu ambao hawawezi kutoa taarifa kuhusu maisha yao wanaweza kuwa katika hatari kubwa. Tatizo hili hutokea kwa watu wenye ulemavu wa afya ya akili watu wanaopata shida ya kuwasiliana. Wakati wa mchakato wa uchunguzi wa kiusalama, kwa mfano watu wenye ulemavu wanaweza kushindwa kujibu maswali yanayohusiana na usalama.

**PROGRAMU ZILIZOKONDOISHWA**

Programu za ulinzi zimebuniwa kwa kuzingatia masuala ya jumuishi na kufikika kwa watu wote wakiwemo watu wenye ulemavu, kwa mfano zinahakikisha ufikivu katika programu za ulinzi na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kuhusu masuala ulemavu.

**WALENGWA**

Programu za uhifadhi zinahakikisha kuwa zinazingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa kufanya marekebisho stahiki, kwa mfano kuhakikisha kuwa programu za ugani zinawafikia watu wenye ulemavu waliotengwa au walio mbali na kuwasaidia katika kushiriki katika kufanya maamuzi yanayowakabili.

Mwongozo ufuatao utawasaidia wadau wa uhifadhi katika kuainisha vikwazo vinavyowakabili watu wenye ulemavu pamoja na familia, walezi na wasaidizi wao wakati wanafanya programu za ulinzi katika muktadha wa kibinadamu.

## Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na mipango** | | | |
| Hakikisha kuwa tahmini ya ulinzi inawahusisha watu wenye ulemavu. Wahusishe katika vikundi vya majadiliano na kama watu muhimu katika mahojiano. Tathmini inapaswa kuainisha makundi yaliyo katika hatari ya ukiukwaji wa usalama na unyanyapaa unaohusiana na ulemavu, na watu ambao wanakabiliana na vizuizi katika kufikia huduma za ulinzi. Husisha watu wenye ulemavu waliotengwa au kufungiwa katika nyumba maalumu au jamii. | X | X | X |
| Wakati wa kuweka mipango zingatia hatari ambazo watu wenye ulemavu wanakabiliana nazo, vizuizi ambavyo vinazuia wao kufikia huduma za ulinzi pamoja na hatua mahsusi ambazo zinahitajika katika kuondoa vikwazo. Wezesha watu wenye ulemavu kusaidia katika kupanga vipaumbele vya kisekta vya ulinzi. | X | X | X |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Hakikisha kuwa andiko la mradi linaainisha na kuchambua hatari za ulinzi na uwezo wa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wenye ulemavu. Hakikisha kuwa afua zinahimiza ulinzi na ushiriki wao. | X | X | |
| Andaa michakato ya bajeti jumuishi. Tenga rasilimali katika kuboresha ufikivu na ujumuishi. | | X | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Tengeneza shughuli za ufikiaji, ikiwemo ufikiaji wa kijamii kuwafikia watu ambao wametengwa katika kaya zao au taasisi maalumu. | X | X | X |
| Jumuisha uchunguzi wa kifani na majadiliano kuhusu ulemavu katika mafunzo ya wafanyakazi wa njanja za ulinzi, wafanyakazi na watu wanaoshughulikia masuala ya ufikikaji katika jamii, wawakilishi na kamati ya ulinzi. | X | X | |
| Wasilisha taarifa za ulinzi na kuhusu mifumo ya malalamiko, mrejesho na kutoa maoni katika njia tofauti tofauti na fikivu, chukua hatua katika kuhusisha watu ambao wametengwa katika kaya zao au katika taasisi au wale wanaotengemea msaada wa mawasiliano. | X | X | X |
| Chukua hatua katika kusaidia watu wenye ulemavu katika kupata nyaraka. Tangaza umuhimu wa usajili wa ndoa na kuzaliwa, andaa kituo cha usajili kwa wakimbizi na jamii zilizohamishwa, ikiwemo watu wenye ulemavu, fanya usimamizi wa kisheria wa kesi zilizopo kwa watu wenye ulemavu na ambao wanashindwa kupata nyaraka za kiraia. | X | X | X |
| Hakikisha kuwa huduma za kutafuta za kuunganisha familia zina ainisha na kuheshimu matakwa ya watu wenye ulemavu ambao wametengwa. | | | |
| Husisha wakazi wa taasisi katika shughuli zinazohusiana na ulinzi wana ufikivu wa taarifa zote ambazo zinatolewa kwa watu wengine katika jamii zilizoathirika. | X | X | X |
| Fuatilia na toa taarifa juu ya ukiukwaji wa haki za watu wenye ulemavu, ikiwemo vitendo vya ukatili vinavyowalenga, matibabu ya kulazimishwa, unyanyapaa unaohusiana na ulemavu, na vikwazo katika kufikia huduma za uhifadhi. Fuatilia visa na ondoa vikwazo ambavyo vinawazuia watu wenye ulemavu kufikia huduma za ulinzi pamoja na kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki. | X | X | X |
| Buni na tekeleza afua za ulinzi kwa watu watu wenye ulemavu ambazo tathmini zimebaini kuwa wapo katika hatari. (Tathmini zinatakiwa kuzingatia jinsi na umri). | X | X | X |

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Fanya kazi na mashirika ya watu wenye ulemavu katika kushawishi jamii (viongozi wa kidini na wa kimila, viongozi wa kielimu na vyombo vya habari) kupinga taratibu na tamaduni ambazo zinachochea unyanyapaa kwa watu wenye ulemavu na ukiukwaji wa haki za binadamu. | X | X | X |
| Toa usaidizi wa kitaalamu katika wizara za sheria na wizara zingine katika kuimarisha sera na miundo ya kitaifa. Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu hasa wanawake na watoto, wanalindwa dhidi ya ukatili. | X | X | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Wahusishe watu wenye ulemavu kama ajenda inayojitegemea katika vikao vya uratibu wa uhifadhi. | | X | X |
| Washirikishe watu wenye ulemavu pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu katika vikao vya uratibu wa uhifadhi na kutoa marekebisho stahiki kuwezesha ushiriki wao kikamilifu. | | X | X |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Hifadhi na toa taarifa ya maendeleo ya matokeo ya huduma za ulinzi ambazo zinapunguza hatari kwa watu walioathiriwa.[172] | | X | X |

## Rejea


- Tovuti ya kitengo cha ulinzi wa kidunia
- Viwango vya ujumuishi katika masuala ya kibinadamu kwa watu wazee na watu wenye ulemavu (2018)
- Kamati ya IASC, mwongozo wa operesheni katika ulinzi wa watu walio watika mazingira ya majanga ya asili (2011)
- Kamati ya kimataifa ya msalaba mwekundu, viwango vya kitaalamu vya kazi ya ulinzi (2018)
- OHCHR, kufuatilia mkataba wa haki za watu wenye ulemavu, muongozo wa wasimamizi wa haki za binadamu (2010)
- Oxfam na kitengo cha ulinzi cha kidunia, Ulinzi: Je, ni nini? (2016)
- UNHCR, uelewa kuhusu ulinzi wa kijamii (2013)
- UNHCR, umri, jinsia na sera ya anuai (imepitiwa 2018)


[172] IASC, sera ya ulinzi katika masuala ya kibinadamu (2016).





## Ukatili wa kijinsia

Ukatili wa kijinsia ni kitendo cha hatari ambacho hutendwa tofauti na uhiari wa mtu na katika misingi ya utofauti katika jinsi ya kike na kiume. Hii inahusisha vitendo vya kuumiza mwili, ukatili wa kingono au kiakili au kuteswa kama vile kulazimishwa na vitendo vingine vya kunyima uhuru. Vitendo hivi vinaweza kutokea hadharani au faraghani."[173] Wanawake, wasichana (isojinsi) wanaathirika kwa kiasi kikubwa na ukatili wa kijinsia kutokana na mfumo usiokuwa na usawa kati ya wanaume na wanawake ambao upo katika jamii. Kwa mujibu wa makadirio ya shirika la afya duniani, inakadiriwa kuwa mwanamke mmoja kati ya watatu amekumbana na ukatili wa kijinsia au wa kimwili.[174] Ukatili huwakumba wanawake mara nyingi wakiwa ndani ya mikono ya watu wa karibu. Neno 'Ukatili wa kijinsia' limekuwa likitumiwa zaidi na wadau kuelezea kipimo cha kijinsia katika aina nyingine za ukatili unaotokea kwa wanaume na wavulana, hasa ule ukatili wa kijinsia unaofanywa kwa madhumuni ya kuimarisha taratibu zisizo na usawa kati ya jinsi ya kike na kiume. Mifano ni kama vile ukatili wa kijinsia unaofanywa nyakati za vita unaolenga kumdidimiza mwanamke, kumnyanyua mwanaume au kuhusisha mabaya jinsi ya kike. Ukatili unaofanywa dhidi ya wanaume ni ule unaotokea kutokana mtizamo wa namna wanaume wanavyotakiwa kuwa katika jamii, kuwa wanaume wanatakiwa kutumia nguvu. Inatumiwa na wanaume (mara chache na wanawake) katika kusababisha madhara kwa wanaume wengine.[175] Watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsi moja, na wale wasiojihusisha na mapenzi hukumbana na ukatili wa kijinsia kutokana na dhana inayofikiriwa kuwa ni kukataa "Utaratibu wa kawaida za kijinsia".[176]

Katika dharura yoyote, makundi fulani ya watu katika jamii zilizoathiriwa huwa katika hatari zaidi ya ukatili wa kijinsia. Watu hawa ni wale wenye nguvu ndogo katika jamii, hutegemea wengine katika kuishi na hawaonekani sana katika jamii au kwa maneno mengine wamekandamizwa.

Wakati sababu zingine kama vile umri, ulemavu, mtazamo wa kijinsia, utambulisho wa kijinsia, dini, kabila vinapoungana na unyanyapaa wa kijinsia hatari za ukatili wa kijinsia huweza kuongezeka.[177] Katika muktadha wa kijinsia, wanawake, wanaume, wasichana, na wavulana wenye ulemavu wanakumbana na aina tofauti za unyanyapaa na kukandamizwa, hali inayoongeza hatari za ukatili ikiwemo ukatili wa kijinsia ambao wanakumbana nao. Wanawake na wasichana wenye ulemavu kwa kiwango kikubwa wanakumbana na ukatili wa kijinsia; wao ni wahanga wa unyanyasaji wa majumbani mara mbili ya zaidi ya wanawake wasio na ulemavu. Kutokana na unyanyapaa na ubaguzi unaosababishwa na jinsia na ulemavu, ukatili hutokea kwa namna ya kipekee. Kwa mfano wanawake na wasichana wenye ulemavu wanajikuta katika hali ya kupata matibabu ya kulazimishwa, ikiwemo kulazimishwa kuzaa, na taratibu nyingine za afya ya uzazi kufanywa bila ya ridhaa yao.

Hatari zinazoambatana na ukatili wa kijinsia wakati wa majanga na kuhamishwa

- Wanawake wenye ulemavu hasa wale wanawake na wasichana wenye ulemavu wa afya ya akili na uziwi, wapo katika hatari kubwa ya unyanyasaji wa kingono na aina zingine za ukatili wa kijinsia. kubakwa mara kwa mara na kunakojirudia na wahalifu mbalimbali ni ukatili wa kijinsia unaofanywa mara kwa mara na kutolewa taarifa.
- Wanawake wenye ulemavu ambao wamekuwa katika mahusiano ya kinyonyaji au ambao wamekuwa wakijihusisha na ngono ya kibiashara wamekuwa wakikumbana na unyonyaji wa kijinsia mara kwa mara. Hatari zinazoambatana zinahusisha umaskini wa hali ya juu na kutofikiwa kwa mahitaji ya usaidizi.[178]
- Ukatili wa kijinsia kwa wanaume na wavulana wenye ulemavu wa akili umekuwa ukitolewa taarifa katika muktadha wa aina mbalimbali. Hatari zinazoambatana na hili ni pamoja na rangi, ukabila na jinsia, ukizingatia na hali ya ulemavu pamoja na wigo mpana wa utambulisho wa mtu.[179]
- Wasichana wenye ulemavu wapo katika hatari kubwa ya ndoa za utotoni, hasa katika muktadha wa kuwa wakimbizi

[173] Waangalizi wa haki za binadamu, kufungwa kama wafungwa (2015).
[174] IASC, mwongozo wa kukondoisha afua za ukatili wa kijinsia katika masuala a kibinadamu: kupunguza hatari, kuhimiza uthabiti na kusaidia urejesho (2015).
[175] Ibid, uk. 5.
[176] Ibid.
[177] Ibid.
[178] Imeripotiwa in Burundi na Ethiopia.
[179] Imeripotiwa in Burundi, Jordan na Lebanon.

kwa muda mrefu. Hatari zinazojitokeza kutokana na muingiliano wa sababu mbalimbali kama vile msongo wa mawazo wa kijamii na kiuchumi, kukosa usawa wa kijinsia, umri na ulemavu.[180]

Walezi wa kike wanaweza kukutana na unyanyasaji wakati wanapojaribu kufikia huduma au usaidizi kwa ajili ya waume zao, au kwa ajili ya familia inayoongozwa na mwanaume mwenye ulemavu. Mabinti walio katika umri wa ujana wanaweza wakaondolewa shuleni ili kusaidia shughuli za ulezi katika kaya.[181] Wajumbe katika familia pamoja na mamlaka au wadau wa masuala ya huduma za kibinadamu wanaweza wasisikilize au kutowaamini wanawake na wasichana wenye ulemavu wanaotoa taarifa kuhusu ukatili au wakati wanapozungumzia kuhusu ngono salama na mahusiano. Aina hizi za unyanyasaji au unyanyapaa zinapunguza ufikivu wa huduma na hivyo kuchochea ubaguzi, unyanyapaa na mitazamo mibaya ya kitamaduni; mara kwa mara, zinazidisha kutokukamatwa kwa wahalifu.

Mwongozo ufuatao utawasaidia wadau wa masuala ya kibinadamu ambao wanafanya kazi katika masuala ya ukatili wa kijinsia kuainisha na kushughulikia vikwazo vinavyowakabili watu wenye ulemavu pamoja na familia, wasaidizi na walezi wao, wakati wanapo jaribu kufikia mifumo ya kuzuia ukatili wa kijinsia na kupata huduma za masuala ya ukatili wa kijinsia katika muktadha wa huduma za kibinadamu.

## Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiandaa | Kutoa huduma | Kurejesha a jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini uchambuzi na mipango** | | | |
| Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanahusishwa katika mashauriano ya kijamii kuhusu ukatili wa kijinsia. Mashauriano hayo yanapaswa kuzingatia umri na jinsia.[182] | X | X | |
| Tathmini mitazamo na dhana kuhusu ujumuishi wa masuala ya ulemavu katika ukatili wa kijinsia kwa wafanyakazi na watoa huduma.[183] | X | X | |
| Ainisha mashirika ya watu wenye ulemavu yaliyopo katika eneo husika. Tambua wanawakilisha akina nani na kiwango ambacho wana uwezo wa kufanya kazi ya utambuzi salama na rufaa za wahanga wa ukatili wa kijinsia kwa huduma stahiki.[184] Chukua hatua kuziba mapengo katika uwezo wao. | X | X | |

[180] Tume ya wakimbizi wanawake na UNICEF, *ujumuishwaji wa masuala ya ulemavu katika ulinzi wa mtoto na program za ukatili wa kijinsia Lebanon* (2018).

[181] Imeripotiwa in Jordan.

[182] Tume ya Wakimbizi Wanawake na kamati ya kimataifa ya uokozi, *kujenga uwezo kwa watu wenye ulemavu katika programu za ukatili wa kijinsia katika muktadha wa kibinadamu. Nyenzo ya masuala ya ukatili wa kijinsia kwa wadau* (2005) Notisi ya muongozo inasema ya kwamba wadau wa masuala ya kibinadamu na wadau wengine ambao wanafanya kazi katika masuala ya ukatili wa kijnsia wanapaswa kufanya mashauriano ya kijamii kuhusu hatari za ukatili wa kijinsia. Asilimia 10-15 ya wajumbe wa jamii wanaohusika katika kubuni, kusimamia na kutathmini ukatili wa kijinsia wanapaswa kuwa ni watu wenye ulemavu sambamba na viwango vya kimataifa kuhusu ukusanyaji salama wa taarifa kuhusu ukatili wa kingono katika muktadha wa kibinadamu. Hii inamaanisha kuwa mtu mmoja au wawili wenye ulemavu kutoka katika kila umri na kundi rika maalum la kijinsia, na kwa nyongeza watu wenye aina mbalimbali za ulemavu, wanapaswa kushiriki. Sambamba na hilo ni vema kuwahoji baadhi ya watu. mahojiano yanaweza kufanywa katika eneo la anae hojiwa hatua zinapaswa kuchukuliwa katika kuainisha na kuondoa hatari.

[183] *Ibid.* Notisi ya 2 ya mwongozo inasema kuwa wadau wa masuala ya kibinadamu pamoja na wadau wengine ambao wanafanya kazi katika masuala ya ukatili wa kijinsia wanaamini kuwa kuzuia ukatili wa kijinsia na huduma za mwitikio sio za muhimu au sahihi kwa watu wenye ulemavu, au kuhofia kufanya uharibifu' kama wanahusishwa katika shughuli. Wafanyakazi wa masuala ya ukatili wa kijinsia wanaweza kukosea iwapo watadhani wahanga wa ukatili wenye ulemavu wa akili, hawana uwezo wa kufanya maamuzi yao wenyewe, wanaweza kulipeleka kwa wahudumu kuhusu aina gani ya msaada au rufaa unaostahili au wanaweza kutumia mtazamo unaowalenga wahanga. Wafanyakazi wote wa masuala ya ukatili wa kijinsia wanapaswa kupewa mafunzo kuzingatia tabia na mitazamo yao juu ya ulemavu na kufanya mahojiano kwa uwazi kuhusu kufanya kazi na watu wenye ulemavu. Angalia nyenzo na rasilimali.

[184] *Ibid.* Notisi namba 3 ya muongozo kuhusu mashirika ya watu wenye ulemavu wana ufahamu kuhusu watoa huduma rafiki kwa watu wenye ulemavu. Kama watu wa kwanza kwa wahanga wenye ulemavu, mashirika ya watu wenye ulemavu wanahitaji mafunzo juu ya misingi ya utambuzi salama na rufaa. Angalia mashirika ya watu wenye ulemavu ambayo yana ukaribu na makundi ya watu wenye ulemavu yaliyokandamizwa, ikiwemo watu wenye ulemavu wa akili na wasichana wenye ulemavu ambao wapo katika hatari kubwa ya ukatili wa kijinsia.





| | Kujiandaa | Kutoa huduma | Kurejesh a jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Waalike watu wenye ulemavu ili kusaidia katika kupanga vipaumbele vya masuala ya ukatili wa kijinsia wakati mipango ya mahitaji mahsusi ya kijinsia na ya ulemavu kwa watu wenye ulemavu inashughulikiwa, pamoja na hatari na ukiukwaji wa haki za binadamu ambazo wanakabiliana nazo. | X | X | X |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Andaa andiko la kushughulikia hatari za ukatili wa kijinsia kwa wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wenye ulemavu. | X | X | X |
| Tafuta fedha na andaa bajeti jumuishi ambayo itatenga rasilimali za kuboresha ufikivu na ujumuishi. | | X | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Ajiri watu wenye ulemavu kama wafanyakazi, watu wanaojitolea na wadau wa kuhamasisha jamii. Chukua hatua katika kufikia usawa wa kijinsia katika shughuli za kukomesha ukatili wa kijinsia.[185] | X | X | X |
| Jumuisha na rasimisha masuala kuhusu watu wenye ulemavu katika mafunzo ya ukatili ya kijinsia. Weka mafunzo ya kifani na majadiliano kuhusu watu wenye ulemavu katika kutoa mafunzo na nyenzo za kukuza uelewa katika jamii.[186] | X | X | |
| Toa mafunzo kwa mashirika ya watu wenye ulemavu hasa yale yanayoongozwa na watu wenye ulemavu kuhusu kuainisha kwa usalama wahanga wa ukatili wa kijinsia. | X | X | X |
| Imarisha sera na itifaki za kitaifa, ikiwemo taratibu, mifumo ya usimamizi wa kesi na mifumo ya rufaa. Hakikisha inatumia mfumo wa kumuweka mhanga kama kipaumbele na kuwajibika, kuhurumia na kujali kwa wahanga wa ukatili wenye ulemavu. | X | X | X |
| Wezesha mifumo salama na inayofikika ya kutolea malalamiko kwa kufuata viwango vya uhifadhi kutoka katika nyenzo kutatua changamoto za unyonyaji wa kijinsia na unyanyasaji (PSEA).[187] | X | X | X |

[185] *Ibid.* Mwongozo namba 4 unatambua kuwa tafiti zinaonesha kuwa wanawake wenye ulemavu katika muktadha wa masuala ya kibinadamu, mara kwa mara wana uwakilishi mdogo katika mfumo wa uongozi katika jamii. Kuwatumia wanawake wenye ulemavu kama wahamasishaji katika jamii pamoja na maafisa wa ustawi wa jamii inaongeza umakini katika hili kundi na pia kukuza heshima katika ujuzi na uwezo wa watu wenye ulemavu baina ya wafanyakazi wa masuala ya kibinadamu na katika jamii (WRC/IRC 2015).

[186] Tume ya Wakimbizi Wanawake na kamati ya kimataifa ya uokozi, *kujenga uwezo kwa ajili ya kujumuisha ulemavu katika programu za ukatili wa kijinsia katika muktadha wa masuala ya kibinadamu. Nyenzo ya watendakazi katika masuala ya ukatili wa kijinsia* (2005) Muongozo namba 5 unasema ya kuwa watu wenye ulemavu pamoja na walezi wao wanapaswa kujumuishwa katika mafunzo kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia, ambapo inapaswa kuhusisha masomo na mifano inayowalenga wanawake, watoto na vijana wenye ulemavu katika sehemu ya kazi na kupata ujuzi wa kufanya kazi (angalia kipengele cha nyenzo na rasilimali).

[187] *Ibid.* Mwongozo namba 8 unasema mashirika yasiyo ya kiserikali, mashirika ya kimataifa na mifumo ya umoja wa mataifa wanao wajibu wa kutokomeza unyonyonyaji wa kijinsia na kunyanyaswa na wafanyakazi wao. Wadau wote wanaofanya kazi katika mwitikio wa masuala ya kibinadamu ikiwemo wale wanaofanya katika eneo la ukatili wa kijinsia, wanapaswa kuhakikisha kuwa jamii zilizoathiriwa zinatoa ripoti juu ya ukiukwaji unafanywa na wafanyakazi katika namna salama, inayofikika na yenye usiri. Angalia UN Doc. 3ST/SGB/2003/13, 9 Oct 2003; kwa taarifa zaidi. angalia *tovuti ya PSEA*.

| | Kujiandaa | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Hakikisha kuwa wahandisi na wasanifu majengo wanatumia misingi ya usanifishaji kwa ajili ya watu wote wakati vituo vya wanawake, vituo vya afya, nyumba salama na mifumo ya usafirishaji inapojengwa.[188] | X | X | X |
| Wezesha ushiriki wa wanawake na wasichana wenye ulemavu katika mazungumzo ya amani na kujenga amani, inayoendana sambamba na maazimio ya kimataifa.[189] | | | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Husisha watu wenye ulemavu kama ajenda inayojitegemea katika vikao vya uratibu wa masuala ya ukatili ya kijinsia. | X | X | |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Fuatilia ni watu wangapi wenye ulemavu (ukichambua kwa umri na jinsia) wanahudhuria shughuli za ukatili wa jinsia.[190] | | X | |
| Mifumo ya usimamizi wa taarifa kama vile mfumo wa usimamizi wa taarifa za ukatili wa kijinsia unapaswa kuchambuliwa kwa jinsia, umri na ulemavu sambamba na utendaji salama na wenye maadili katika ukusanyaji na usambazaji wa data za ukatili ya kijinsia. Hii itawezesha kutambua iwapo jinsia fulani au kundi rika fulani la watu wenye ulemavu limeondolewa. | X | X | |

## Rejea


- Kikosi kazi kuhusu eneo la utendaji kazi kwa masuala ya ukatili wa kijinsia, *kitabu cha kuratibu afua za ukatili wa kijinsia katika muktadha wa kibinadamu* (2010)
- Eneo la uwajibikaji katika ukatili wa kijinsia, *kitabu cha kuratibu masuala ya ukatili wa kijinsia katika dharura* (2019)
- Eneo la uwajibikaji katika ukatili wa kijinsia, viwango vya kuzuia na kutoa huduma kuhusu ukatili wa kijinsia wakati wa dharura (2019, kipo katika hatua za kuchapishwa)
- IASC, *kitabu cha jinsia kwa ajili ya masuala ya kibinadamu* (2018)
- IASC, *mwongozo wa kukondoisha afua za ukatili wa kijinsia katika masuala ya kibinadamu* (2015)
- *Mwongozo wa mashirika mbalimbali katika usimamizi wa matukio wa ukatili wa kijinsia* (2017)


[188] *Ibid.* Mwongozo namba 6 'Usanifishaji kwa wote' unamaanisha kuwa usanifishaji wa bidhaa, mazingira, programu na huduma zinazo tumika kwa watu wote, kwa kiasi kikubwa, bila ya kuhitaji marekebisho, kuhakikisha kuwa majengo na miondombinu mingine zinafikika hutumia kwa makadirio asilimia 1 ya gharama za ujenzi. Ni nafuu zaidi kuliko kuja kutengeneza wakati jengo limeshakamilika.

[189] Hii inaendana na azimio namba 1325 la baraza la usalama la umoja wa mataifa kuhusu wanawake, amani na usalama, hutambua athari za vita na migogoro kwa wanawake na wasichana na linatambua jukumu muhimu ambalo wanawake wanafanya katika kuzuia migogoro, usuluhishi wa migogoro, kutengeneza na kujenga amani. Azimio hilo linanasa wadau wote kuongeza ushiriki wa wanawake na kuweka masuala ya jinsia katika juhudi zote na amani na usalama za umoja wa mataifa. Angalia Taasisi ya amani ya Marekani, '*UNSCR 1325 ni nini?*'

[190] Tume ya Wakimbizi Wanawake na kamati ya kimataifa ya uokozi, *kujenga uwezo kwa ajili ya kujumuisha ulemavu katika programu za ukatili wa kijinsia katika muktadha wa masuala ya kibinadamu. Nyenzo ya watendakazi katika masuala ya ukatili wa kijinsia* (2005). Muongozo namba 7 unasema kuwa ni muhimu kufuatilia idadi ya watu wenye ulemavu wanaotumia huduma na programu za ukatili wa kijinsia ili kuelewa iwapo kama programu zinawafikia wale wenye uhitaji zaidi. Angalau asilimia 15 ya washiriki wa shughuli za ukatili wa kijinsia inapaswa kuwa ni watu wenye ulemavu, uwiano huu haufikiwi. (WRC/IRC 2015).






- UNFPA, *viwango vya kuzuia na kutoa huduma kuhusu ukatili wa kijinsia katika dharura* (2015)
- Shirika la Afya Duniani, Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi duniani na UNFPA, *usimamizi wa kitabibu kwa wahanga waliobakwa* (2004)
- Shirika la Afya Duniani, Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi duniani. Na UNFPA, *usimamizi wa kitabibu kwa watoto na vijana wa rika waliobakwa* (2016)
- WRC na IRC, *kujengea uwezo ujumuishi wa masuala ya ulemavu katika programu za ukatili wa kijinsia katika muktadha wa masuala ya kibinadamu* (2015)
- WRC ukatili wa kijinsia Lebanon: *usimamizi wa matukio kwa wahanga na wanawake walio katika hatari, watoto na vijana wenye ulemavu* (2018)


## Ulinzi wa mtoto

Wakati wa majanga ya kibinadamu, watoto wanawekwa katika hatari za ukatili, unyanyasaji, kupuuzwa na unyonyaji. Ulinzi wao unaweza kuwa dhaifu kwa kuwa familia zao huwekwa katika shida ya ziada na mitandao ya usaidizi katika jamii huharibika[191]. Madhara ya watoto wenye ulemavu yanaweza kuonekana dhahiri kwa sababu wanakabiliwa na ubaguzi na unyanyapaa na wanaweza kuwa na njia chache za kukabiliana na majanga hayo. Matokeo yake ni kuwa wanakuwa katika hatari kubwa ya haki zao kukiukwa. Kwa mujibu wa kikosi kazi cha Ulinzi wa Mtoto wa Awali, kimsingi, 'kutengwa' huathiri maendeleo ya mtoto kufikia uwezo na talanta zake. Watoto waliotengwa wanakuwa katika mazingira ya ukatili, kunyanyaswa, unyonyaji na kupuuzwa. Majanga ya kibinadamu na huduma zake yanaweza kufanya kutengwa kuwa kubaya zaidi au kutoa fursa ya mabadiliko."[192]

Tafiti zinaonesha kuwa watoto wenye ulemavu wanaweza kuwa wahanga wa ukatili mara tatu au mara nne zaidi ya watoto wasio na ulemavu.[193] Zaidi kuna aina fulani za ukatili ambazo ni mahsusi kwa watoto wenye ulemavu. Mifano inahusisha ukatili unaotokea chini ya kivuli cha kurekebisha tabia, kulazimishwa kupata watoto kwa wasichana wenye ulemavu au kulazimishwa kutoa mimba.[194]

Sambamba na tafsiri ya ibara ya kwanza ya Mkataba wa Haki ya Mtoto, mtoto anaelezewa kama ni mtu aliye chini ya umri wa miaka 18.

Mkataba wa Haki ya Mtoto unaweka kanuni nne juu ya haki za mtoto ambazo zinatumiwa katika masuala ya kibinadamu:

- **Kuishi na kuendelea.** Wafanyakazi katika masuala ya huduma za kibinadamu wanatakiwa kuzingatia namna ambavyo dharura na huduma zinaweza kuathiri maendeleo ya mtoto.
- **Kutokuwa na ubaguzi.** Wafanyakazi katika masuala ya huduma za kibinadamu wanapaswa kushughulikia aina za ubaguzi na nguvu katika kutoa huduma.
- **Ushiriki wa mtoto.** Wafanyakazi katika masuala ya huduma za kibinadamu wanapaswa kuwawezesha watoto kushiriki kikamilifu katika hatua zote za kujiandaa na katika kutoa huduma katika masuala ya kibinadamu.
- **Maslahi bora ya mtoto.** Maslahi bora ya mtoto yanatakiwa kuwa ndio msingi wa kuzingatia katika hatua zote zinazochukuliwa kuhusu mtoto.[195]

### Hatari na athari zinazohusiana na ulinzi wa mtoto

- Katika nchi nyingi, watoto wenye ulemavu mara kwa mara huwekwa katika taasisi au vituo maalum,[196] wakati wanapokuwa katika hatari za unyanyasaji, unyonyaji na kupuuzwa. Vituo hivyo huwa katika viwango vya chini na kukosa ufuatiliaji. Wahalifu wa ukatili na unyonyaji kwa nadra sana huwajibishwa.[197]
- Kuwaweka watu katika makazi maalum kunaongeza hatari za biashara ya watoto wenye ulemavu. Tafiti zinaonesha kuwa wasichana

[191] Kikosi kazi cha ulinzi kwa watoto, *viwango vya ulinzi wa watoto katika muktadha wa kibinadamu* (2019).

[192] *Ibid.*

[193] Hughes K. et al., *uwepo na hatari za ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu: mapitio na uchambuzi* katika Lancet, 2012, doi: 10.1016/S0410-6736(11)61851-5.

[194] UNICEF, *hali ya watoto duniani: watoto wenye ulemavu* (2013).

[195] Kikosi kazi cha ulinzi kwa watoto, *viwango vya ulinzi kwa watoto katika muktadha wa kibinadamu* (2019).

[196] Angalia Lumos, *watoto katika taasisi: picha ya kidunia* (2017).

[197] Jukwaa la sera ya mtoto ya Afrika, *Ripoti ya Afrika kuhusu ukatili dhidi ya watoto* (2014).

wenye ulemavu wapo katika hatari ya kutekwa kwa sababu ya ulemavu wao kutokana na dhana kuwa hawataweza kutoroka.[198]

- Katika jamii za kusini mwa nchi za Sahara, dhana kuwa viungo vya watu wenye ualbino vina nguvu za kimiujiza zimepelekea vitendo vya kutekwa na kukatwa viungo zaidi kwa watoto wenye ualbino.[199]
- Watoto wenye ulemavu wana uwezekano mkubwa wa kutosajiliwa wakati wa kuzaliwa. Jambo hili linaongeza watoto kuwa katika hatari, ikiwemo ndoa za utotoni na kukosa utaifa, pamoja na kuharibu ufikiaji wao wa elimu, huduma za afya na huduma zingine za msingi.[200]
- Watoto wenye ulemavu waliotengwa kutoka kwa walezi wao huwa katika hatari kubwa. Wanafamilia wanaweza kuwa ndio watu pekee ambao wanajua namna ya kuwajali watoto wenye mahitaji mahsusi au namna ya kuwasiliana na watoto.[201] Watoto wenye ulemavu wanaweza kushindwa kuwasilisha taarifa muhimu kwa ajili ya ufuatiliaji wa familia na kuungana. Watoto wenye ulemavu wasioambatana na familia zao wanaweza kuondolewa katika mifumo ya malezi iwapo familia zao zitawakataa.
- Wasichana wenye ulemavu wapo katika hatari kubwa ya ukatili wa kijinsia,[202] ikiwemo kubakwa, unyonyaji wa kingono na unyanyasaji.[203] Jambo hili linaweza kuwaweka katika kupata ukimwi na kupuuzwa.[204] Ingawa tafiti katika suala hili ni chache, wasichana wenye ulemavu wapo katika hatari kubwa ya ndoa za kulazimishwa za utotoni.
- Watoto wenye ulemavu wapo katika hatari ya kufanyishwa kazi hatari kama vile umalaya na kuwa ombaomba.
- Watoto wenye ulemavu hasa wale wenye ulemavu wa akili, wapo katika hatari ya kuchuliwa kufanya kazi katika vikundi vya kijeshi.

Mwongozo ufuatao unaweza kuwasidia wadau wa masuala ya kibinadamu wanaofanya kazi za ulinzi wa mtoto katika kuainisha na kuondoa vizuizi ambavyo watu wenye ulemavu, pamoja na familia zao, wasaidizi na walezi wao wanakabiliana nazo pale wanapojaribu kuzifikia huduma za ulinzi wa mtoto katika muktadha wa huduma za kibinadamu.

## Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na mipango** | | | |
| Husisha wasichana na wavulana wenye ulemavu katika tathmini stahiki za kiumri pamoja na mashauriano ikiwemo tathmini ya haraka ya ulinzi wa mtoto. | X | X | |
| Hakikisha kuwa watoto wenye ulemavu wanashiriki katika maamuzi ya ulinzi wa mtoto katika masuala yanayowahusu, hakikisha kuwa taratibu zinafanyika kwa usiri. | X | X | |

[198] Leonard Cheshire Disability, *Ulemavu bado umeachwa nyuma: Njia za elimu jumuishi kwa wasichana wenye ulemavu* (2017).

[199] *Ripoti ya mtaalamu humu juu ya kufurahia haki za binadamu kwa watu wenye ualbino*, A/HRC/34/59, 10 Januari 2017, aya ya 29.

[200] Shirika la Umoja wa Mataifa la Wakimbizi, *Unahitaji kufahamu: muongozo wa kufana kazi na watu wenye ulemavu katika mazingira ya uhamisho* (2019). Angalia pia kikosi kazi ukatili dhidi ya wanawake wenye ulemavu: *Muhtasari wa asili yake, upeo wake, visababishi na matokeo yake* (2012).

[201] UNICEF, *hali wa watoto ulimwenguni, watoto wenye ulemavu* (2013).

[202] *Ibid*.

[203] Tume ya wanawake wakimbizi, *ukatili wa kijinsia miongoni mwa wanawake na wasichana wenye ulemavu waliohamishwa* (2012).

[204] UNICEF, *ukatili dhidi ya watoto: Muhtasari wa ripoti* (2005).





| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Husisha watoto wenye ulemavu pamoja na familia zao katika kuainisha vikwazo ambavyo vinawazuia kufikia afua za ulinzi wa mtoto na maeneo rafiki kwa mtoto. Waalike katika kutoa maoni ya namna ya kuondoa vizuizi na kufanya maboresho. | X | X | X |
| Hakikisha kuwa timu zilizo teuliwa kufanya tathmini za ulinzi wa mtoto pamoja na mpango wa programu zina usawa wa kijinsia; hakikisha kuwa uwakilishi wa watu wenye ulemavu katika timu hizo zina usawa wa kijinsia. | X | X | |
| Hakikisha kuwa mipango inashughulikia mahitaji mahsusi na hatari kwa watu wenye ulemavu. Husisha watu wenye ulemavu katika muktadha wa vipaumbele vya ulinzi wa mtoto. | X | X | X |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Hakikisha kuwa maandiko yote na mapendekezo ya miradi yanazingatia na kuchambua hatari za ulinzi wa mtoto na uwezo wa wasichana na wavulana wenye ulemavu. Hakikisha kuwa afua zinashughulikia ulinzi na kuhimiza ushiriki wa wasichana na wavulana wenye ulemavu. | X | X | |
| Tafuta fedha na andaa mfumo wa bajeti jumuishi ambao utatenga rasilimali kwa ajili ya kuhamasisha ufikivu na ujumuishi. | | X | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Fanya uchambuzi wa taarifa za ulemavu katika mfumo wa usimamizi wa taarifa za ulinzi wa mtoto na nyenzo zote za kukusanya data (*tumia moduli ya Kundi la Washington Group Kuhusu Ufanyakazi wa Mtoto iliyoandaliwa na UNICEF*). | X | X | |
| Ongeza uwezo wa wafanyakazi na watu wanaojitolea kuhusu uelewa kwa kutumia mtazamo wa haki katika masuala ya ulemavu. | X | X | |
| Toa mafunzo na msaada katika kutoa malezi na kwa wanaotoa malezi kuhusu mahitaji ya watoto wenye ulemavu. | X | X | X |
| Toa mafunzo kwa wafanyakazi wa ulinzi wa watoto juu ya ulemavu, jumuisha mafunzo ya kifani na majadiliano juu ya ukatili, unyonyaji na unyanyasaji wa watoto wenye ulemavu katika mafunzo ya msingi. Jumuisha maafisa ustawi wa jamii, wafanyakazi wa kufikia jamii ya mbali na wafanyakazi wa kutoa elimu, wahudumu wa afya, wawakilishi wa ulinzi na kamati husika. | X | X | |
| Chagua maeneo ya shughuli za ulinzi wa mtoto ambayo yanafikika, pale ambapo haiwezekani, fanya marekebisho na toa marekebisho | X | X | X |
| Kuza uelewa wa haki za watoto wenye ulemavu, jadili haki za watoto (walio na wasio na ulemavu) pamoja na familia zao, pamoja na viongozi wa kijamii, viongozi wa dini, viongozi wa kimila, wafanyakazi wa sekta ya afya na wa elimu na jamii kwa ujumla. | X | X | X |

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Ainisha masuala ya kiusalama ya watoto wenye ulemavu kama vile kuonewa, hatari ya kuumia, na unyanyasaji wa kimwili na wa kingono. Chukua hatua za kuondoa na kukomesha hatari hizo. | | X | X |
| Jumuisha vijana wenye ulemavu katika shughuli ambazo zitawasaidia kujenga uthabiti wao. Weka uongozi na imarisha mitandao yao. Zingatia shughuli za burudani, michezo na za kitamaduni, elimu na stadi za maisha.[205] | X | X | X |
| Ainisha washauri wenye ulemavu, himiza washauri kuonesha uongozi wao, stadi na uwezo wao kukabiliana na mitazamo hasi juu ya ulemavu. Zingatia kuanzisha mfumo wa marafiki kwa vijana wenye | X | X | |
| Himiza ufikivu wa usajili wa vizazi kwa watoto, wakiwemo watoto wenye ulemavu. | | X | X |
| Ainisha watoto wanaoishi katika makazi maalumu ikiwemo watoto ambao wametengwa na kuachwa wakati jamii zinapohama. Pale ambapo ni kwa maslahi bora ya mtoto, wajumuishe katika taratibu za kufuatilia na kuziunganisha familia. | | X | X |
| Zingatia matakwa ya watoto wasioambatana na familia zao pamoja na watoto wenye ulemavu waliotengwa ambao wanahitaji uangalizi mbadala. | | X | |
| Hakikisha kuwa jitihada za kuzuia au kutoa huduma kupinga aina mbaya za ajira kwa watoto zinahusisha watoto wenye ulemavu. | | X | X |
| Hakikisha mfumo wa usimamizi wa kesi ni jumuishi. Ainisha ufikivu wake. Toa mafunzo kwa wafanyakazi juu ya namna ya kufanya kazi na watoto wenye uleamavu. Kwa mfano wape stadi za uendeshaji katika mfumo wa mawasiliano fikivu na kuwafanya waelewe juu ya haki za watoto wenye ulemavu na hatari wanazokabiliana nazo. | | X | X |
| Tumia timu za ufikiaji katika kuwafikia watoto wenye ulemavu ambao hawawezi kusafiri katika maeneo ya usajili au maeneo rafiki kwa watoto. Hakikisha kuwa wanatembelewa katika maeneo ya makazi ikiwemo katika vituo walivyowekwa kizuizini. | | X | X |
| Fanya kazi na jamii katika kujumuisha watoto wenye ulemavu pamoja na wazazi wao katika mifumo ya kijamii ya ulinzi wa mtoto. | X | X | X |
| Toa msaada katika kuwezesha familia na walezi wa watoto wenye ulemavu kufikia usaidizi. | X | X | X |
| Hakikisha kuwa ufuatiliaji na mifumo ya kutoa taarifa ikiwemo Mfumo wa Ufuatiliaji na Utoaji Taarifa za Uchimbuaji wa Makaburi, taarifa za ukiukwaji wa haki za binadamu kwa watoto wenye ulemavu ipo. | | X | X |

[205] Kikosi kazi cha ulinzi kwa mtoto, viwango vya ulinzi kwa mtoto katika muktadha wa masuala ya kibinadamu (2019).





| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **4. Uratibu** | | | |
| Jumuisha watoto wenye ulemavu kama ajenda ya uratibu wa ulinzi wa kundi la watoto. | | X | X |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Fanya tathmini ya takwimu za ulinzi wa mtoto katika ngazi ya majumbani kwa kutumia nyenzo za ufuatilizji; nyambulisha takwimu kwa jinsia, umri na ulemavu. Himiza timu za ufuatiliaji kutumia njia za ukusanyaji wa taarifa ambazo zimeshajaribiwa katika muktadha wa msaada wa kibinadamu, kama moduli ya Kundi la Washington Group Kuhusu Ufanyakazi wa Mtoto iliyoandaliwa na UNICEF. | | X | |

## Rejea


- Muungano wa ulinzi kwa mtoto katika masuala ya kibinadamu, *kitabu cha watoto waliotengwa na kuachwa* (2017)
- *Mtandao wa huduma bora*
- *Ulinzi kwa mtoto katika mtandao wa mafunzo ya majanga*
- Kikosi kazi cha ulinzi kwa watoto, *viwango vya ulinzi kwa watoto katika masuala ya kibinadamu* (2019)
- Kikosi kazi cha ulinzi kwa watoto, *mwongozo wa mashirika mbalimbali katika usimamizi wa matukio na ulinzi wa mtoto* (2014)
- Mtandao wa wadau wa masuala ya ukatili wa kijinsia, *huduma kwa watoto ambao ni wahanga*
- Kitengo cha ulinzi wa kidunia, *kikosi kazi cha ulinzi kwa watoto*
- Kamati ya kimataifa ya msalaba mwekundu, *kanuni za mwongozo za mashirika mbalimbali kwa watoto walioachwa na kutengwa* (2004)
- UNICEF, *Kuwahusisha watoto wenye ulemavu katika masuala ya kibinadamu*
- UNICEF, *Watoto wenye ulemavu katika hali za migogoro ya vita* (2018)
- Tume ya wakimbizi wanawake na mfuko wa watoto, *ukatili wa kijinsia kwa watoto na vijana wenye ulemavu, nyenzo kwa wadau wa ulinzi wa watoto* (2016)

## Nyumba, ardhi na mali

Watu walioathiriwa na dharura za kibinadamu wanaongezeka kuishi katika maeneo ya mjini, makazi yasiyo rasmi na vituo vya pamoja kuliko katika makambi au makazi yaliyopangwa. Wadau wa masuala ya kibinadamu wanahitaji kuzingatia changamoto na fursa ambazo zinaibuka kwa watu wenye ulemavu waliohamishwa.[206]

Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu la mwaka 1948 linatambua kuwa makazi ya kutosha ni sehemu ya haki kuwa na maisha bora. Kifungu cha 25 kinasema kuwa 'kila mtu ana haki ya maisha ya kiwango bora kwa ajili ya afya na ustawi wake binafsi na familia yake, ikiwemo chakula, mavazi, huduma za matibabu na huduma za kimsingi za kijamii. Mkataba wa Kimataifa wa Uchumi, Jamii na Haki za Kitamaduni wa mwaka 1966, pia unatambua haki ya makazi bora unaotambulika kujumuisha usalama wa kisheria wa umiliki, upatikanaji wa huduma, vifaa na miundombinu, unafuu, makazi, ufikivu, eneo, na utoshelevu wa kitamaduni.[207]

Haki ya kumiliki mali inafahamika kama haki ya kufurahia kuwa na nyumba, na umiliki wa mali zingine bila ya bugudha au ubaguzi. Katika muktadha wa masuala ya kibinadamu, kutambua haki hii kunaweza kujumuisha ulinzi wa mali na umiliki ambao umeachwa nyuma na watu waliokimbia ghasia au majanga ya asili au kutoka katika uporaji, uharibifu au uholela au kuchukua mali kwa njia haramu, kazi au matumizi.[208]

Migogoro inayotokana na makazi, ardhi na mali ni ya kawaida katika muktadha wa kibinadamu kutokana na kazi za ziada, kupotea kwa nyaraka za umiliki, mauzo ya lazima na kinyume cha sheria, ukosefu wa usalama wa umiliki, usawa hafifu wa mgawanyo wa ardhi, migogoro inayoendelea juu ya ardhi na mali.[209]

### Hatari zinazoambatana na nyumba, makazi na mali

- Baadhi ya watu wenye ulemavu wanakabiliana na aina mbalimbali za unyanyapaa katika masuala ya makazi. Watu wenye ulemavu waliohamishwa wanaweza kukumbana na unyanyapaa kutokana na ulemavu wao pamoja na ubaguzi wa rangi na ubaguzi kwa misingi ya utaifa, na wanaweza kupoteza mifumo ya kukabiliana na mifumo ya usaidizi wakati wa dharura. Wengine wanashindwa kudai haki za kumiliki makazi kwa kuwa wamepoteza nyaraka muhimu[210] au hawawezi kuhoji vitendo vya kibaguzi kwa sababu ya kukosa hadhi ya kisheria.[211] Matokeo ni kwamba watu wenye ulemavu waliohamishwa wanakosa makazi na wanashindwa kukodi makazi bora, wanaweza kulazimishwa kuishi katika maeneo yasiyo salama na wanaweza kuwa katika hatari ya kufukuzwa.[212]
- Unyanyapaa wa aina mbalimbali wa ubaguzi unawakumba wanawake wenye ulemavu ambao wanakabiliana na vikwazo vingine vya kijinsia ambavyo vinawazuia katika kupata haki ya nyumba, ardhi na mali. Wajane, waliotelekezwa au kupewa talaka wanaweza kumiliki mali au kupata mali kupitia ndugu wa mwanaume.[213]Wanawake wenye ulemavu hulazimishwa kuishi katika makazi yasiyo salama pia wapo katika hatari kubwa ya ukatili ikiwemo ukatili wa kijinsia.[214]
- Watu wenye ulemavu mara nyingi hukosa haki ya kuchagua wapi pa kuishi na waishi na nani, kwa sababu za moja kwa moja za ulemavu au kwa sababu za kunyimwa fursa za kufanya uchaguzi. Wanawake wanakosa haki ya kuchagua, kwa mfano iwapo wanakosa ufikivu wa usafiri na huduma zingine, kukosa taarifa au umaskini uliopindikia.[215]
- Baadhi ya watu wenye ulemavu wanawekwa katika taasisi bila ridhaa yao na wanashindwa kuondoka katika taasisi hizo. Hali hizo zote huwafanya kukosa haki ya kuchagua kwa uhuru maeneo ya kuishi. Hii ni hatari hasa kwa watu wenye ulemavu wa akili.[216]
- Kulazimishwa kuwekwa katika taasisi hutokea kama matokeo yasiyo ya moja kwa moja ya kutoheshimu haki ya makazi bora. Katika baadhi ya taasisi kwa mfano mataifa hayatoi usaidizi kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha wao kuishi katika jamii pamoja na wengine; Kwa wengine, hawawezi kumudu gharama za makazi.[217]
- Gharama za makazi zinaweza kuwaathiri kwa kiasi kikubwa watu wenye ulemavu kwa sababu wanakabiliana na gharama za ziada (mfano, kwa ajili ya matibabu) pamoja na vikwazo ambavyo vinawazuia katika kupata ajira.[218]
- Viwango vikubwa vya umaskini na unyanyapaa vinaweza kulazimisha watu wenye ulemavu kukaa katika makazi duni na makazi yasiyo rasmi.[219]
- Kukosa makazi kunaweza kuwaathiri kwa kiasi kikubwa watu wenye ulemavu. Katika hali zingine hii hutokea wakati watu wenye ulemavu wanatolewa katika taasisi bila ya kusaidiwa vya kutosha ili kuishi katika jamii. Umaskini na unyanyapaa ni moja ya visababishi.[220]
- Uwezo wa kisheria unaposhindwa kutambuliwa, watu wenye ulemavu wanaweza wakashindwa kuruhusiwa kuingia katika makubaliano ya kukodisha au kumiliki mali. Kwa kuongezea, wanaweza kupata ubaguzi wakati wa kurithi mali.

Mwongozo ufuatao utaweza kuwasaidia wadau wa masuala ya kibinadamu wanaofanya kazi katika masuala ya makazi, ardhi na mali kuainisha na kuondoa vikwazo vinavyowakabili watu wenye ulemavu pamoja, familia zao pamoja na walezi wao wakati wanapojaribu kufikia programu za nyumba, ardhi na makazi katika muktadha wa huduma za kibinadamu.

## Hatua zinazopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesh a jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na mipango** | | | |
| Kupitia uchambuzi shirikishi, ainisha vikwazo ambavyo vinawazuia watu wenye ulemavu katika kutambua haki yao ya nyumba, ardhi na makazi. Fanya uchambuzi wa taarifa kwa jinsia, umri, husisha watu wanaoishi katika taasisi. | | X | X |
| Fanya kazi na mashirika ya watu wenye ulemavu pamoja na wataalamu wa masharika ya watu wenye ulemavu katika kufafanua aina za ubaguzi ambao unawakumba watu wenye ulemavu. Ainisha njia za kisheria za kukumbuka. | X | X | X |

[206] Angalia mfano, tume ya wakimbizi ya Norway, *notisi ya muongozo kuhusu masuala ya HLP katika makazi yasiyo rasmi na vituo vya pamoja kusini mwa SYRIA* (2017). NRC inatambua kuwa kuna muongozo mdogo unapatikana kuhusu makazi, ardhi na mali katika makazi yasiyo rasmi na vituo vya pamoja, ambavyo ni kawaida nchini Syria.

[207] *Kamati ya Umoja wa Mataifa ya haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni ya umoja wa mataifa, mapendekezo namba 4:* haki ya kupata nyumba bora (Kifungu cha. 11(1) sheria), 13 Disemba 1991.

[208] *IASC, Ulinzi katika majanga ya asili*.

[209] Tume ya wakimbizi Norway na IFRC, *umuhimu wa kuelezea masuala ya nyumba, ardhi na mali (HLP) changamito katika mwitikio wa masuala ya kibinadamu* (2016).

[210] *Ibid*.

[211] Shirika la makazi duniani na OHCHR, *Haki za makazi bora, ukweli kuhusu haki za binadanmu na. 21 (chapisho. 1)* (2009).

[212] Tume ya wakimbizi Norway na IFRC, *umuhimu wa kuelezea masuala ya nyumba, ardhi na mali (HLF) changamoto katika mwitikio wa kibinadamu* (2016).

[213] Angalia mfano, tume ya wakimbizi ya Norway, *haki za wanawake waliohamishwa katika makazi, ardhi na mali* (2018).

[214] Angalia, tume ya wakimbizi Norway na IFRC, *Umuhimu wa kuelezea masuala ya nyumba, ardhi na mali (HLF) changamoto katika mwitikio wa kibinadamu* (2016).

[215] Shirika la Makazi Duniani, *haki ya makazi bora kwa watu wenye ulemavu wanaoishi mijini: kuelekea katika miji jumuishi* (2015).

[216] *Ibid*.

[217] Mjumbe maalum wa umoja wa mataifa katika nyumba bora kama jambo mojawapo la haki katika viwango bora vya maisha, *makazi bora kama jambo mojawapo katika haki na viwango vya kuishi na haki kakika kutobaguliwa katika muktadha huo*, A/72/251 72b, 12 Julai 2017.

[218] Shirika la Makazi Duniani, *hasi za makazi bora kwa watu wenye ulemavu wanaoishi mijini: kuelekea katika miji jumuishi* (2015).

[219] Shirika la Makazi Duniani na OHCHR, *haki za makazi bora, ukweli kuhusu haki za binadanmu na. 21 (chapisho 1)* (2009).

[220] Shirika la Makazi Duniani, *hasi za makazi bora kwa watu wenye ulemavu wanaoishi mijini: kuelekea katika miji jumuishi* (2015).

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Kwa kushirikiana na mashirika ya watu wenye ulemavu, ainisha huduma (kama vile huduma za nyumbani na za jamii) ambazo zitawezesha na kuwasaidia watu wenye ulemavu kuishi kwa uhuru. | X | X | X |
| Hakikisha kuwa mipango inahusisha mahitaji ya watu wenye ulemavu, pamoja na hatari wanazokabiliana nazo. Husisha watu wenye ulemavu katika kuweka vipaumbele vya makazi, ardhi na mali. | X | X | X |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Hakikisha kuwa maandiko ya miradi yanachunguza uwezo wa kisheria na uwezo wa kusoma na kuandika kuhusisha watu wenye ulemavu. | X | X | |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Saidia mitandao ambayo inatetea watu wenye ulemavu kuwa na fursa sawa za kupata haki ya nyumba, ardhi na makazi katika hali za kibinadamu. Himiza kampeni ambazo zinahamasisha haki ya nyumba, ardhi na makazi pamoja na kampeni ambazo zinahamasisha misingi ya kanuni ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu Wenye Ulemavu. | | X | X |
| Jumuisha mifano mizuri na majadiliano kuhusu ulemavu katika kutoa mafunzo kwa wafanyakazi kwenye programu za nyumba, ardhi na makazi. Jumuisha wafanyakazi, wawakilishi wa ulinzi pamoja na kamati mbalimbali. | X | X | X |
| Wakati wa kutenga makazi ya dharura, zingatia kutoa kipaumbele kwa makundi ambayo yapo katika hatari ikiwemo watu wenye ulemavu. | | X | |
| Boresha ufikivu wa makazi, huduma za makazi na miundombinu ikiwemo usafiri. (Angalia kipengele cha nyumba na makazi kwa msaada zaidi). | | X | X |
| Fanya kazi na mashirika ya watu wenye ulemavu katika kutetea ukombozi wa mali bila ya ubaguzi. Haki ya watu wenye ulemavu katika kumiliki mali inapaswa kutambuliwa; pia wanapaswa kufurahia ufikivu wa taarifa na msaada wa kisheria. | | X | X |
| Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanaweza kudai ukombozi wa mali, na pia taratibu za kukomboa mali zinafikika. Toa taarifa na mafunzo katika kuboresha elimu ya sheria; saidia watu wenye ulemavu ambao wanahitaji msaada katika kukamilisha taratibu za madai.[221] | | X | X |

[221] Kanuni za Pinheiro zilizoundwa kama viwango vya kimataifa vya ukombozi wa makazi, ardhi na mali, kwa wakimbizi na watu waliohamisha. Angalia kituo cha haki za makazi, kanuni za Pinheiro.



| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Wajumuishe watu wenye ulemavu katika michakato ambayo itawasaidia wakimbizi na watu waliohamishwa katika kupata nyaraka za nyumba, ardhi na makazi. | | X | X |
| Unganisha watu waliohamishwa, mashirika ya watu wenye ulemavu na mashirika ya kijamii ikiwemo jumuiya za wapangaji katika kutetea haki ya nyumba, ardhi na makazi. | | X | X |
| Hakikisha kuwa mifumo ya ufuatiliaji na utoaji wa taarifa, inatoa taarifa kuhusu ukiukwaji wa haki za nyumba, ardhi na makazi kwa watu wenye ulemavu. | X | X | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Husisha watu wenye ulemavu kama ajenda unaojitegemea katika vikao ya uratibu wa masuala ya nyumba, ardhi na makazi. | | X | X |
| Wahusishe watu wenye ulemavu na mashirika ya watu wenye ulemavu katika vikao vya uratibu wa masuala ya nyumba, ardhi na makazi. Fanya marekebisho stahiki kuwezesha ushiriki wenye tija. | | X | X |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Jumuisha taarifa za watu wenye ulemavu katika nyezo za ufuatiliaji ngazi ya kaya. | | X | |

## Rejea


- Shirika la chakula duniani na mengineyo, ukombozi wa makazi na mali kwa wakimbizi na waliohamishwa katika kanuni za Pinheiro (2007)
- IASC, mfumo wa kutoa masuluhisho ya kudumu kwa watu waliohamishwa (2010)
- Tume ya wakimbizi Norway na IFRC, umuhimu wa kuelezea masuala ya makazi, ardhi na mali, changamoto katika kutoa huduma za kibinadamu (2016)
- Tume ya wakimbizi Norway Mwongozo wa kitaalamu katika kuelezea masuala ya Nyumba, Ardhi na Mali Katika Makazi yasiyo Rasmi au Makambi na Vituo vya Pamoja Syria Kaskazini (2017)

## Kutegua mabomu ya kutegwa ardhini

Shughuli za uteguaji wa mabomu ya ardhini zinalenga kupunguza hatari na uharibifu kwa raia na wafanyakazi katika huduma za kibinadamu wanaoshughulikia hatari za milipuko.[222]

Nguzo tano za uteguaji wa mabomu ardhini ni:

- **Kuondoa milipuko yote na mabaki ya milipuko ya kivita**. Huu ni mchakato wa kutumia utafiti wa kitaalamu na usio wa kitaalamu katika kukusanya taarifa za hatari za milipuko na silaha, na kuziondoa. Lengo ni kuondoa athari zinazoambatana na milipuko na mabaki ya milipuko ya kivita, ili raia waweze kurejea makwao na kuendelea na shughuli zao kwa usalama.

- **Elimu ya kutambua hatari** inahusisha shughuli (kama vile taarifa, kampeni, mafunzo na mashauriano na jamii) ambayo yataweza kupunguza hatari ya kuumia kutokana na milipuko kwa kukuza uelewa na kuhimiza kubadili tabia.

- **Usaidizi kwa wahanga** una lengo la kuhakikisha kuwa watu wenye ulemavu, ikiwemo wahanga wa milipuko wanashiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika jamii kwa hali ya usawa. Hii inahusisha kuchukua hatua katika kufikia viwango vya juu vya afya, marekebisho stahiki, msaada wa kisaikolojia, elimu jumuishi, na hifadhi ya jamii, kazi na ajira, pamoja na ushiriki na ujumuishi katika jamii na maisha bora. Inahusisha shughuli za kufikia mahitaji ya majeruhi, wahanga, watu wengine wenye ulemavu, familia za majeruhi na waliouawa, na jamii zilizoathirika. Shughuli za wazi zinahusisha huduma za matibabu, marekebisho, msaada wa kisaikolojia, ujumuishi katika jamii, elimu jumuishi na ujumuishi wa kiuchumi, ikiwemo hifadhi ya jamii. Ukusanyaji wa taarifa kuhusu mahitaji ya wahanga pia unahitajika. Sheria na sera za kulinda na kuhimiza haki za wahanga zinahitaji kufanyiwa tathmini na kutumiwa.

  Kutokubaguliwa, kutambua haki za binadamu, kutambua wajibu wa kijinsia, na kutambua muktadha wa maendeleo ni kanuni muhimu. Kifungu namba 5 (2a) cha "*Convention on Cluster Munitions*" kinasema kuwa programu za usaidizi kwa wahanga zinapaswa kutobagua wahanga katika vitengo, watu wenye ulemavu pamoja na watu ambao ni majeruhi au wamepata ulemavu kutokana na sababu zingine.[223]

- **Uteketezaji wa hazina** inahusisha wigo mpana wa shughuli za kuteketeza hazina za milipuko na silaha nyingine.

- **Utetezi unahusisha** shughuli za kuhamasisha msaada kwa ajili ya uteguaji wa milipuko na kushawishi nchi wanachama katika kuruhusu, kusaini na kutekeleza "*Anti-Personnel Mine Ban Conven- tion, Convention on Cluster Munitions, Convention on Certain Conventional Weap-ons*" pamoja na mikataba mingine kama vile mkataba ya haki za watu wenye ulemavu.

Hatari na athari zinazoambatana na uteguaji wa mabomu ardhini

- Watu wenye ulemavu wanaweza kukosa ufikivu wa programu za elimu ya kutambua hatari. Na matokeo yake yanaweza kufanya wasiwe na habari juu ya hatari ambazo milipuko inaweza kusababisha au tabia za usalama ambazo zitaweza kukomesha hatari hizo.

- Watu wenye ulemavu wanaweza kulazimiswa kutumia tabia zisizo salama. Kwa mfano iwapo vyoo havifikiki, inaweza kuwalazimu kutumia maeneo ya vichaka pembezoni mwa makazi ambapo milipuko inaweza kupatikana.

- Watu wenye ulemavu wanaweza kuwa na ushawishi mdogo kuliko wengine juu ya kufanya maamuzi ya kuachilia ardhi au kuruhusu kusafishwa. Wanaweza kutoshirikishwa katika michakato au maamuzi ya kuhamia ni ardhi ipi imekatazwa kusafishwa, ambayo imepigwa marufuku kutumiwa na pia ambayo haina hati ya ardhi. Kwa sababu hizi pamoja na nyingine, watu wenye ulemavu wanaweza kutengwa kutoka katika fursa na maendeleo na ustawi wao unaohusiana na shudhuli za kutegua milipuko ardhini.

[222] Konga ya ulinzi wa kidunia, uteguaji wa mabomu (2018).

[223] *Mkataba wa makombora* (2008), angalia tume ya haki za binadamu ya umoja wa mataifa, *somo la dhima kuhusu haki za watu wenye ulemavu chini ya kifungu namba 11 ya mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu katika hali za hatari na dharura za kibinadamu*, A/HRC/31/30, 30 Novemba 2015, aya ya 19.





Mwongozo ufuatao utawasidia wadau wa masuaala ya kibinadamu wanaofanya kazi katika masuala ya milipuko ya ardhini katika kuainisha na kuondoa vikwazo vinavyowakabili watu wenye ulemavu pamoja na familia zao, wasaidizi na walezi wakati wanapojaribu kufikia programu za kutegua milipuko katika muktadha wa huduma za kibinadamu.

## Hatua zinazaopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na mipango** | | | |
| Waalike watu wenye ulemavu pamoja na mashirika ambayo yanawakilisha watu wenye ulemavu kushiriki katika juhudi za kutambua namna milipuko inaweza kuathiri jamii zilizoathirika. Wahusishe katika kuweka vipaumbele vya maeneo ya kusafisha na kuweka alama. | | X | X |
| Hakikisha kuwa mipango inashughulikia mahitaji mahsusi ya watu wenye ulemavu pamoja na hatari wanazokabiliana nazo, jumuisha watu wenye ulemavu katika kuweka vipaumbele katika sekta ya uteguaji wa milipuko. | X | X | X |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Hakikisha kuwa maandiko ya miradi kuhusu uteguaji wa milipuko yanazingatia watu wenye ulemavu bila ya kujali visababishi vya ulemavu wao. | | X | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Chukua hatua katika kuhakikisha kuwa shughuli za mashauriano katika jamii zinazingatia na kuhusisha watu wenye ulemavu, mashirika ya watu wenye ulemavu pamoja na mashirika ya wahanga. Zingatia kuwajengea uwezo katika ngazi ya jamii ili kuwezesha watu wenye ulemavu pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu kutathmini hatari, kusimamia taarifa, kukuza mipango ya kupunguza hatari na kutetea afua za kutegua milipuko na aina zingine za usaidizi.[224] | | X | X |
| Jumuisha mifano halisi kutoka maeneo mengine na majadiliano kuhusu ulemavu katika kujumuisha ulemavu katika kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wanaohusika na uteguaji wa mabomu, jumuisha jamii, wafanyakazi na wawakilishi wa ulinzi pamoja na jamii. | X | X | |
| Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanajumuishwa katika kufanya maamuzi na makabidhiano ya ardhi iliyosafishwa kwa jamii pamoja na maamuzi juu ya namna ya kutumia maeneo yaliyosafishwa. | | | X |

[224] UNICEF na CICHD, *viwango vya kimataifa vya uteguaji wa mabomu (IMAS) Mifano bora ya elimu ya kupunguza hatari ya mabomu ya kutegwa kitabu cha mwongozo* 1 (2008) na IMAS 04.10, toleo la pili, 1 Januari 2003 (kama kilivyorekebishwa tarehe 1 Disemba 2004) 3.157.

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Hakikisha kuwa fidia isiwe mbadala wa huduma za hifadhi ya jamii.[225] | | | X |
| Wahusishe watu wenye ulemavu pamoja na mashirika yanayowawakilisha katika kubuni, kutekeleza na kutathmini hatari, shughuli za kielimu, ikiwemo kupitia elimu ya makundi rika. | | X | |
| Hakikisha kuwa elimu ya kutambua hatari na taarifa inatolewa katika mifumo fikivu: badilisha vifaa vya elimu ili viendane na mahitaji ya ulemavu husika. | | X | |
| Shauriana na watu wenye ulemavu na mashirika ya watu wenye ulemavu katika kuanisha mifumo ya mawasiliano. | X | X | |
| Wahusishe watu wenye ulemavu na mashirika yao katika kubuni na kutoa elimu katika makundi rika. | | X | |
| **4. Uratibu** | | | |
| Kwa utaratibu maalum, husisha watu wenye ulemavu katika majukwaa ya uratibu wa shughuli za uteguaji wa mabomu ardhini. | | X | |
| Fanya uratibu pamoja na sekta husika katika kuhakikisha kuwa rufaa za watu wenye ulemavu zinatekelezwa bila ya kujali visababishi vya ulemavu wao. | | X | X |
| Wajumuishe watu wenye ulemavu na mashirika yao katika vikao vya uratibu wa kutegua milipuko na kutoa marekebisho stahiki katika kuwezesha ushiriki wenye tija. | | X | X |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Fuatilia na toa taarifa kuhusu vipimo ambavyo vitachukuliwa katika kuboresha ufikivu katika elimu ya kutambua hatari na uchambuzi wa aina mbalimbali za athari za milipuko na mabaki ya milipuko baada ya vita katika misha ya watu wenye ulemavu. | | X | X |

## Rejea


- Kituo cha kimataifa cha masuala ya kibinadamu kuondoa mabomu cha geneva (GICHD), *mwongozo wa mabomu ya kutegwa na mabaki ya milipuko wakati wa vita* (2007)
- Orodha ya taarifa zenye uhalisia ya shirika la kimataifa la Handicap, *namna ya kutekeleza mahitaji ya usaidizi kwa wahanga?*
- IMAS, *viwango vya kimataifa vya uteguzi wa mabomu ya ardhini*
- *Tovuti ya maeneo ya uwajibikaji katika uteguaji wa mabomu*
- UNICEF na GICHO, IMAS, *elimu ya hatari za mabomu muongozo wa mifano bora 1: utangulizi kuhusu elimu ya hatari za mabomu ya kutegwa ardhini* (2005)
- UNICEF, *Usaidizi kwa wahanga wa mabomu ya kutegwa ardhini na mabaki ya milipuko ya vita: Mwongozo unaolenga usaidizi wa wahanga walio watoto* (2014)
- Umoja wa Mataifa, *Sera ya Umoja wa Mataifa katika usaidizi wa wahanga wa mabomu ya kutengwa ardhini* (2016)
- Umoja wa Mataifa, *mwongozo wa masuala ya jinsia katika programu za mabomu ya kutegwa ardhini* (2010)
- Umoja wa Mataifa, *mkakati wa Umoja wa Mataifa kuhusu mabomu ya kutegwa ardhini (2019-2023)* (2018)
- *Kituo cha rasilimali za kusaidia wahanga wa mabomu ya kutegwa ardhini pamoja na ufuatiliaji wa makombora*


[225] Ofisi ya kamishina mkuu wa haki za binadamu ya umoja wa mataifa, *somo mahsusi kuhusu haki za watu wenye uleamvu chini ya ibara 11 ya mkataba wa kimataifa wa haki za watu wenye ulemavu katika hali za hatari na dharura za kibinadamu*, A/HRC/31/30, 30 Novemba 2015, aya ya 12.

# 17 Malazi na Makazi

## Utangulizi

Katika hatua za mwanzoni za dharura, makazi ni kiini muhimu cha kuishi, pamoja na usambazaji wa maji, usafi wa mazingira, chakula na huduma ya afya. Makazi yana jukumu muhimu katika kupunguza mazingira magumu na kujenga ustahimilivu katika jamii.[226]

Sekta ya malazi na makazi inakusudia kuhakikisha utu, faragha na usalama wa watu walioathirika huku ikiwapatia kinga dhidi ya hali ya hewa.

Wakati wa shughuli za kibinadamu, sekta ya malazi na makazi pia inachukua jukumu muhimu katika kujumuisha watu wenye ulemavu, kwa sababu ya athari zake kwa mazingira yaliyojengwa na vizuizi vya mazingira na majukumu yake muhimu katika ulinzi wa kibinafsi na maisha.

Gharama ya kuwekeza katika makazi yasiyokuwa na vikwazo ambayo yanaheshimu kanuni za usanifishaji kwa ajili ya wote wakati vifaa vya makazi vinatayarishwa ni ya chini sana kuliko gharama ya kurekebisha makazi baada ya ujenzi. Faida za makao yasiyo na vikwazo hunufaisha watu wenye ulemavu lakini pia watoto, wazee na watu ambao ni wagonjwa au wamejeruhiwa.

Makazi yanapaswa kukidhi mahitaji ya watu wenye kila aina ya ulemavu. Kwa kuongezea, wanapaswa kuruhusu nafasi ya kutosha kwa watunzaji, wafanyakazi wa msaada na wanafamilia.

Tazama sehemu Ulinzi, hususani katika masuala ya ukatili wa kijinsia wa kingono na nyumba, ardhi na makazi.
Hakikisha uratibu wa maji na usafi wa mazingira.

### Sheria na miundo mingine

- Mkataba wa haki za watu wenye ulemavu (ibara ya 9 na 19)
- Maendeleo endelevu Lengo namba 11
- 
- Makazi III: Ajenda mpya ya makazi ya mijini
- Ofisi ya Kamishna Mkuu Wa haki za binadamu Wa Umoja Wa Mataifa, na Shirika la Umoja wa Mataifa la makazi, haki ya makazi bora (orodha ya kweli namba 21 toleo la 1)

## Dhana muhimu

**Makazi** hutambuliwa kama "Nafasi inayofunikwa inayoweza kutoa mazingira salama na yenye afya na faragha na hadhi kwa wale wanaoishi ndani yake". Baada ya muda, nafasi hii inayoweza kukaa inaweza kubadilika kutoka hali ya dharura mpaka kuwa makao ya kudumu.[227] Usaidizi wa makazi ni pamoja na (mara nyingi hujumuisha njia na suluhisho za aina mbalimbali: vifaa vya makazi na mahema na usambazaji wao; msaada wa pesa taslimu; msaada wa kukodisha; utoaji wa vifaa vya ujenzi; kazi; matengenezo; mafunzo na msaada wa kiufundi; ujenzi wa nyumba, n.k.

[226] IFRC, *Nyumba na makazi*.

[227] Kwa ajili ya Umoja wa Mataifa, DFID na kituo cha kumbukumbu za nyumba, angalia *nyumba, makazi na urejesho*-(muongozo wa masuala ya ukatili wa kijinsia).

Msaada wa makazi unajumuisha hatua tatu: dharura, kurejesha katika hali ya kawaida na suluhu za kudumu. Kawaida awamu hizi huingiliana, na huduma za makazi zinapaswa kutekelezwa kwa namna endelevu na, isiyoingiliwa. Katika muktadha wa migogoro, awamu hazitabiriki kwa uwazi, kwa sababu watu wanaweza kuhamishwa mara nyingi au kwa muda mrefu.

**Makazi** hupangwa kijamii, kiuchumi, kijiografia na mara nyingi kwa kuzingatia masuala ya kisiasa na kiutawala. Ni mahali ambapo wanadamu wanaishi na kufanya kazi. Katika muktadha wa kibinadamu, makazi yanaweza kugawanywa kulingana na ukubwa, muda (hali ya kawaida), hali, na uhalali.[228]

**Makazi ya mapito** ni pamoja na makazi ya haraka yanayowekwa baada majanga, yaliyotengenezwa kutoka kwa vifaa ambavyo vinaweza kuboreshwa au kutumiwa tena katika miundo ya kudumu zaidi au kuhamishwa kutoka kuwa ya muda hadi kuwa maeneo ya kudumu. Yanalenga kuwezesha mabadiliko ya idadi ya watu walioathirika kwenda kwenye makazi ya kudumu zaidi.[229]

**Makazi ya dharura** inahusu utoaji wa msaada wa msingi na wa haraka wa makazi ambayo ni muhimu kuhakikisha kuishi walioathiriwa na majanga wanaishi. Inajumuisha suluhu za majibu ya haraka kama vile utengano wa vitu vya makazi (maturubai, kamba, vifaa, mahema, vifaa vya joto), ujenzi wa makao ya muda, na usambazaji wa vitu vya nyumbani.

**Familia karibishi** zinaweza kuwa marafiki au familia, au familia za wenyeji, ambao hutoa makao ya muda katika nyumba zao kwa watu waliohamishwa na majanga ya asili au mzozo. Kwa kawaida, huu ni mpangilio wa muda mfupi lakini unaweza kuendelea ikiwa uhamishaji utachukua muda mrefu.[230]

**Vitu ambavyo si chakula** ni vitu vingine isipokuwa chakula kinachotumiwa katika muktadha wa huduma za kibinadamu wakati wa kutoa msaada kwa wale walioathiriwa na hatari ya asili au shida. Zinaweza kujumuisha magodoro, blanketi, karatasi za plastiki, vifaa vya usafi, feni au hita, n.k.[231]

(Tazama pia ufafanuzi wa usanifishaji kwa ajili ya wote na ufikiaji katika sehemu ya dhana muhimu).

## Vikwazo/Vizuizi

Makazi yana jukumu muhimu katika kusaidia ujumuishaji na ushiriki. Dharura za kibinadamu mara nyingi huathiri mazingira yaliyojengwa na kuweka vizuizi vipya ambavyo usanifu na ujenzi wa makazi na makao zinaweza kusaidia kuondoa. Programu ya makazi na ujumuishaji inawawezesha watu wenye ulemavu kuchangia zaidi kwenye jamii zao, kushiriki zaidi katika mashauriano na kufanya maamuzi, na kuwezesha ulinzi wao wenyewe.

## Rejea


- *Kitabu cha Sphere* (2018)
- Help Age, CBM, shirika la kimataifa la Handicap, *viwango vya ujumuishi wa masuala ya kibinadamu kwa wazee na watu wenye ulemavu* (2018)
- IFRC, *chini ya dali moja, nyumba na makazi jumuishi katika dharura* (2015)
- AusAid, *mwongozo wa usanifishaji wa ufikivu, kanuni za usanifishaji kwa wote kwa programu za msaada za Australia* (2009)
- Shirika la kimataifa la Handicap Nepal, *mwongozo wa kutengeneza nyumba za dharura zisizo na vikwazo* (2009)


[228] *Kitini cha USAID/DFDA mawasilisho ya nyumba na makazi katika chuo kikuu cha Harvard*, 19 Aprili 2018.
[229] IFRC, *nyumba za muda  ubunifu namba 8* (2011).
[230] IOM, Tume ya wakimbizi Norway, UNHCR, *Nyenzo ya usimamizi wa makambi* (2015), uk. 18.
[231] Imechukuliwa kutoka shirika la Umoja wa Mataifa la wakimmbizi Syria, *bidhaa zisizo za chakula*.





**Mchoro namba 12 |** Vizuizi vya ufikiaji na ujumuishaji katika makazi

### JINSI MADHARA YA MAJANGA YANAVYOZIDI KWA WATU WENYE ULEMAVU NDANI YA MAKAZI

**ATHARI ZA MAJANGA**

Kutokuwepo kwa usalama, kuvunjika kwa mitandao ya kijamii, uharibifu wa miundombinu, kuhamishwa, kufungwa kwa huduma.

**VIZUIZI VINAVYOJITOKEZA**

**Vikwazo vya kimazingira:**
- Maskani na maliwato yasiyofikika
- Taarifa isiyofikika kuhusu makazi
- Ukosefu wa vitu vya nyumbani vinavyokidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu
- Eneo lisilotosha la makazi yanayopatikana

**Vikwazo vya kimtazamo:**
- Mitazamo hasi na unyanyapaa dhidi ya watu wenye ulemavu
- Ukosefu wa maarifa na ufahamu ndani ya watendaji wa kibinadamu na mashirika kuhusu jinsi ya kukidhi upatikanaji na mahitaji mengine ya watu wenye ulemavu

**Vikwazo vya kitaasisi:**
- Ukosefu wa uwezo wa kiufundi wa kukuza ujumuishwaji wa watu wenye ulemavu katika makazi
- Viwango vya sekta, miongozo na sera hazizingatii mahitaji ya watu wenye ulemavu
- Ukosefu wa bajeti kuhakikisha maskani na makazi yanayofikika
- Ujenzi usiozingatia misingi ya usanifishaji kwa ajili ya watu wote
- Taratibu na sera za kitaasisi zinabagua watu wenye ulemavu
- Ukosefu wa takwimu sahihi kuhusu watu wenye ulemavu

**Hatari zinazowakabili watu wenye ulemavu**

Vurugu, umaskini, hatari za mazingira, kuzorota kwa afya, kukataliwa, kutengwa

## Masuala muhimu ambayo ni lazima yafanyike

Masuala muhimu ni lazima yafanyike katika hatua zote za huduma za kibinadamu wakati wa kutekeleza programu za makazi kwa watu wenye ulemavu.

### Ushiriki

- Hakikisha kwamba watu wenye ulemavu, familia zao, na mashirika ya watu wenye ulemavu wanashiriki katika kutambua vizuizi vinavyozuia ufikiaji wa watu wenye ulemavu, na katika kupanga, kubuni, kutekeleza, kutazama na kutathmini makazi.
- Hakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanawakilishwa sawa, kwa kuzingatia aina tofauti za ulemavu na vilevile umri, jinsia na utofauti. Fanya juhudi za pamoja za kukuza vikundi ambavyo havina uwakilishi, ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu ya akili, watu wa kiasili wa eneo hilo, wanawake na wasichana katika shughuli rasmi na zisizo rasmi, kufanya maamuzi na utawala.
- Shirikisha watu wenye ulemavu katika ukuzaji wa mifumo ya ushiriki wa jamii, na maoni na njia za malalamiko, ili kuhakikisha ufikiaji mzuri na bila malipo.

### Kushughulikia vikwazo

- Tambua na fuatilia vizuizi vinavyozuia watu wenye ulemavu kupata misaada ya dharura, na hatua zinazoboresha ufikiaji. Toa makazi mazuri na fikivu ili kuwezesha ujumuishaji kamili wa watu wenye ulemavu.
- Tumia kanuni za usanifishaji kwa wote katika kubuni makazi na kupanga makazi. Jenga maeneo ya jamii yenye kivuli au mahali pazuri ambapo panafaa kwa mazingira ya hali ya hewa.
- Toa zana zote za kufanyia tathmini na utoaji taarifa, na habari zote na mawasiliano kuhusu makazi kwa njia fikivu, kwa kuzingatia watu wenye ulemavu wa kusikia, kuona, afya ya akili na kijami.
- Tekeleza mikakati ya kupunguza unyanyapaa unaosababishwa na ulemavu. Chukua hatua za kuifanya jamii ifahamu zaidi haki za watu wenye ulemavu. Anzisha vikundi rika ambavyo vinajumuisha watetezi wa binafsi wenye ulemavu wa afya ya akili.
- Pitia sera, miongozo na zana za kisekta kuhakikisha zinaongelea kwa uwazi haki ya watu wenye ulemavu na ujumuishwaji.

### Uwezeshaji na kukuza uwezo

- Jenga uwezo wa makazi na wafanyakazi wa sekta ya makazi. Toa mafunzo juu ya haki za watu wenye ulemavu na mwingiliano kati ya ulemavu na jinsia, umri, hali ya uhamiaji, dini na ujinsia.
- Kujenga uwezo wa mashirika ya watu wenye ulemavu wa kushirikiana na mashirika yanayojishughulisha na makazi, kutambua zana na rasilimali, bainisha changamoto za ramani, uwezo na vipaumbele, kujenga ujuzi wa misaada ya kibinadamu na kuimarisha uratibu.
- Kushirikiana na mashirika ya watu wenye ulemavu na watu wenye ulemavu katika kukuza na kutoa mafunzo.

### Ukusanyaji wa taarifa na ufuatiliaji

- Kukusanya na kuchambua taarifa ya makazi kuhusu watu wenye ulemavu; tofautisha taarifa kwa jinsia, umri na ulemavu. Fanya hivi kwa utaratibu maalum katika mzunguko wa programu za huduma za kibinadamu. Ambapo taarifa za kuaminika hazipatikani au haziwezi kukusanywa, tumia makadirio ya asilimia 15 ya kuenea kwa ulemavu ulimwenguni.[232]
- Hakikisha kuwa watu wenye ulemavu na mashirika ya watu wenye ulemavu wamejumuishwa kama watoa taarifa mahususi kuhusu vizuizi na viwezeshi. Watoa taarifa wanapaswa pia kuzingatia masuala mapana, kama vile umri na jinsia.





Vitendo vinavyopendekezwa hapa chini vinafuata njia pacha. Vinahakikisha kuwa watu wenye ulemavu wana haki sawa na fursa za makazi na wanaweza kuchangia katika juhudi za kuwaondoa wazuiaji na kukuza ujumuishaji kamili na ushiriki mzuri na wenye tija.

**PROGRAMU ILIYOKONDOSHWA**

Mipango ya makazi na hatua zimeundwa ili kuhakikisha kuwa zinajumuisha na kupatikana kwa watu wote, ikiwa ni pamoja na watu wenye ulemavu.

**WALENGWA**

Usambazaji makazi na programu za makazi hutambua mahitaji binafsi ya watu wenye ulemavu, ikiwa ni pamoja na huduma za dharura na urejeshaji hali.

## Mikakati inayopendekezwa

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesh a jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi na mipango** | | | |
| Wadau wa masuala ya ramani. Jumuisha mashirika ya kitaifa na mashirika ya serikali yenye vitengo vinavyoshughulikia ulemavu na makazi (huduma za kijamii, nyumba, kazi za umma, n.k). | X | | |
| Changanua mapungufu katika utaalamu wa kiufundi kuhusu misingi ya usanifishaji kwa wote na ufikikaji. Ajiri wadau ambao wanaweza kujaza mapengo haya. Panua ajira ili kujumuisha watu wenye ulemavu na mashirika ambayo yanawakilisha watu wenye ulemavu. | X | X | |
| Tathmini huduma za makazi ya hivi karibuni na ubuni huduma ambazo zinakidhi mahitaji ya watu walio na aina tofauti za ulemavu. Jenga maktaba ya mifano bora, pamoja na nyaraka za kiufundi na zana, ili kukuza maarifa na ujifunzaji katika tasnia hii. | X | | |
| Shirikisha mashirika ya watu wenye ulemavu katika tathmini ya athari na uwezo na fanya ziara za pamoja katika makazi ya dharura. | X | | |

[232] Shirika la Afya Duniani na Benki ya Dunia, Ripoti ya dunia kuhusu ulemavu (2011).

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu, fanya ukaguzi wa ufikivu wa malazi ya dharura na upange marekebisho ya muundo unaoweza kupatikana ili kuondoa vizuizi. | X | X | |
| Fikiria mahitaji ya watu wenye ulemavu tangu mwanzo na kondoisha ujumuishaji wa jumla katika nyanja zote za huduma ya makazi. | X | X | X |
| Pitia zana za tathmini za makazi na malazi na badilisha maswali ili yawe jumuishi kwa watu wenye ulemavu na onesha mtazamo wa jinsia na umri. (Tazama mada ya kutambua vizuizi). | X | | |
| Fanya kazi na kamati za utayarishaji wa ndani (mahali zilipo), ili kuleta pamoja uzoefu wa ulemavu na utaalamu wa kiufundi. | X | | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Tambua washiriki wa timu yako, au ajiri wafanyikazi, ambao wana ujuzi na uzoefu wa ujumuishaji wa masuala ya ulemavu. | X | X | X |
| Anzisha bajeti shirikishi ambayo inatenga rasilimali kukuza ufikiaji na ujumuishaji na kulipia gharama za kurekebisha makazi na vifaa vya makazi kukidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu. | X | X | |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Shirikisha mashirika ya watu wenye ulemavu na watu wenye ulemavu katika kushauriana juu ya suluhu zinazofaa kuhusu makazi ya dharura kwa watu walio na aina tofauti za ulemavu. | X | X | |
| Tambua na uweke nafasi salama za makazi ili kupunguza hatari za ulinzi ambazo watu wenye ulemavu wanakabiliwa nazo. Toa vipaumbele kwa wanawake, vijana na wale walio na ulemavu wa afya ya akili. | | X | X |
| Pamoja na mashirika ya watu wenye ulemavu, tambua njia bora za usambazaji wa vifaa vya makazi. Chaguzi ni pamoja na vituo vya usambazaji vinavyopatikana, utoaji wa huduma mlango kwa mlango, mfumo wa marafiki pamoja na walengwa wengine, usafiri uliofadhiliwa, mistari ya kipaumbele, n.k. | X | X | X |
| Tumia ngazi mtelezo za muda mfupi ili kuongeza ufikikaji. Zingatia majengo ya umma na vituo vya huduma, pamoja na maeneo ya usambazaji. | | X | X |
| Tafuta kaya ambazo zinajumuisha watu wenye ulemavu kwenye viwanja ambavyo vipo karibu na mitandao ya msaada, vituo vya maji, vifaa vya usafi, | | X | |
| Wasiliana na watu wenye ulemavu ili kuelewa mahitaji yao ya katika kufikia mahema. | | X | |



| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Wakati wa kutafuta suluhu za makazi ya kudumu, toa kipaumbele kwa kaya ambazo zinajumuisha watu wenye ulemavu; ruka hatua ya mpito. | | X | |
| Wasiliana na watu wenye ulemavu ili kutathmini upatikanaji wa malazi. Fanya uchambuzi kuhusu mahitaji ya watu wenye ulemavu ambao wanaishi ndani yao. Badilisha malazi ya muda kadri ya inavyotakiwa. | X | X | |
| Wasiliana na watu wenye ulemavu ili kutathmini upatikanaji wa malazi. Fanya uchambuzi kuhusu mahitaji ya watu wenye ulemavu ambao wanaishi ndani yao. Badilisha malazi ya muda kadri ya inavyotakiwa. | | | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Ikiwezekana, ratibu usambazaji wa pamoja na sekta zingine ili kupunguza mzigo kwa watu wenye ulemavu na mitandao yao ya msaada. (Kwa mfano, pendelea kugawanya kidogo kidogo). | | X | X |
| Pamoja na sekta nyingine, tambua maeneo bora kwa kaya zilizo na watu wenye ulemavu; au kuleta huduma muhimu (maji, usafi wa mazingira, chakula) karibu nao. | | X | |
| Tumia njia za uratibu kutambua familia zinazoweza kukaribisha watu wenye ulemavu. | | X | |
| Ukiwa na mashirika ya watu wenye ulemavu, tengeneza na ujenge makazi ya mpito ukitumia kanuni za muundo wa ulimwengu. | | X | X |
| Tafuta makazi ya mpito kwa watu wenye ulemavu karibu na vifaa vya usafi vinavyopatikana, vituo vya maji na huduma; hii huwafanya wawajibike kwa njia nyingine. | | | X |
| Wakati ukarabati na urekebishaji unahitajika, fanya ukaguzi wa ufikivu pamoja na tathmini ya uharibifu. | | | X |
| Tambua majengo yanavyofaa kukodisha, ambayo yanafikika na yanahitaji marekebisho madogo au yasiyohitaji marekebisho kabisa. | | | X |
| Ajiri watu wenye ulemavu watakaofanya kazi katika ujenzi. (Tazama mada kuhusu afua za fedha taslimu). | | X | X |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Shirikisha watu wenye ulemavu na mashirika ya watu wenye ulemavu katika michakato ya ufuatiliaji. Toa kipaumbele kwa watu wenye ulemavu ambao wanaishi katika makazi maalum. | | X | X |
| Fanya njia za malalamiko, mrejesho na maoni kuwa fikivu kwa watu wenye ulemavu. | X | X | |

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Fuatilia upatikanaji wa malazi na makazi (kwa ukaguzi, au kwa kushauriana na mashirika ya watu wenye ulemavu au watu wenye | | X | |
| Wateue wanawake, wanaume, wasichana na wavulana wenye ulemavu katika timu za ufuatiliaji. Hakikisha timu hizo zinawakilisha anuwai za ulemavu. | | X | |
| Fuatilia kwa karibu hatari za kinga ambazo watu wenye ulemavu wanapata katika maeneo na aina tofauti za makazi. Fuatilia mara kwa mara. | | X | |

## Rejea


- CBM, *njia zenye tija katika kujenga usimamizi wa miradi jumuishi, ubunifu na upangaji wa miradi*
- GPDD, *nyenzo ya ujenzi jumuishi Haiti* (2010)
- Shirika la kimataifa la Handicap, *Haïti: Abri transition- nel* (2011)
- Shirika la kimataifa la Handicap, *ulemavu na walengwa walioathirika* (2014)
- Shirika la kimataifa la HelpAge na Handicap, *utafiti kuhusu utoaji wa fedha wa masuala ya kibinadamu kwa wazee na watu wenye ulemavu* (2012)
- Shirika la kimataifa la HelpAge na IFRC, *mwongozo wa ujumuishi kwa wazee katika programu ya nyumba za dharura* (2012)
- IFRC, *nyumba za mpito, ubunifu namba 8* (2011)
- IFRC, *kitabu cha usalama wa nyumba: Taarifa muhimu kuhusu ujenzi salama* (2011)
- IFRC, *makazi baada ya majanga, ubunifu namba 10* (2013)
- IFRC, CBM, shirika la kimataifa la Handicap, *Wote Chini ya dali moja : Nyumba na makazi ambayo ni jumuishi wakati wa dharura* (2015)
- Shirika la kimataifa la HelpAge, *kuhakikisha ujumuishi wa wazee katika tathmini ya awali ya mahitaji wakati wa dharura* (2012)
- IFRC, *mwongozo wa thathmini katika dharura* (2008)
- UNHCR na shirika la kimataifa la Handicap, *mwongozo namba 1 wa mambo ya kufahamu: Kufanya kazi wa watu wenye ulemavu katika maeneo ya kuhamishwa* (2011)
- Shirika la kimataifa la Handicap Nepal, *mwongozo wa kutengeneza makazi ya dharura yasiyokuwa na vikwazo* (2009)
- IASC makazi ya dharura, *kuchagua NFI kwa ajili ya nyumba* (2008)
- ICRC na IFRC, *katalogi ya vitu wakati wa dharura* (2009 toleo la tatu)
- IFRC, *kitini cha nyumba cha IFRC* (2009)
- IFRC, *kitabu cha nyumba salama, taarifa muhimu kuhusu ujenzi salama* (2011)
- IFRC na shirika la kimataifa la Oxfam, *mwongozo katika vipimo vya utumiaji wa mabati ya plastiki katika masuala ya kibinadamu* (2007)
- Shirka la kimaifa la Handicap, *tathmini ya ufikivu ya kambi ya wakimbizi ya Zaatari* (2012)
- IOM na UNHCR, *kituo cha pamoja cha miongozo* (2010)
- Jones, H. na Wilbur, J., *mkusanyiko wa teknolojia fikivu za maji na usafi wa mazingira* (2014)
- IOM, Tume ya Wakimbizi Norway, shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi, *nyenzo za kutawala kambi* (2015)
- Shirika la Umoja wa Mataifa la wakimbizi, *kitabu kuhusu dharura* (2007, toleo la tatu). Angalia sura ya 13, bidhaa na usambazaji
- IFRC, *tathmini ya athari na uwezo*
- Idara ya haki ya Marekani, *orodha ya makazi ya dharura* (2007)
- AusAid, *mwongozo wa ubunifu wa ufikivu, misingi ya usanifishaji kwa wote kwa programu za misaada za Australia* (2009)
- IDDC, *kujenga maendeleo jumuishi, ukondoishaji wa masuala ya ulemavu katika uratibu* (2008)
- Kitengo cha dunia kuhusu nyumba, *kikosi kazi cha ujumuishi wa watu wenye ulemavu katika programu ya nyumba na makazi*
- Kitengo cha dunia kuhusu nyumba, *usambazaji wa vifaa vya nyumba, na mwongozo wa fedha katika kupunguza hatari za ukatili wa kijinsia*
- *Kiongozi cha maeneo ya kupigia kura cha sheria ya watu wenye ulemavu Marekani*

# 18 Maji na Usafi wa mazingira

## Utangulizi

Haki ya maji na usafi wa mazingira ni moja kati ya haki za binadamu. Maji ya kunywa ya kutosha, usafi wa mazingira na usafi vyote huchangia kwenye afya njema. Sekta ya maji safi na usafi wa mazingira (WASH) inahakikisha kuwa haki hii inapatikana kwa wote, hata katika nyakati za majanga. WASH ni zaidi ya masuala ya maji pekee, inashughulikia usafi wa mazingira, usambazaji wa maji, usafi (usimamizi wa kinyesi na usimamizi wa taka ngumu) na udhibiti wa visambaza magonjwa. Pia inategemea maarifa kutoka katika nyanja tofauti, pamoja na uhandisi, afya ya umma, mawasiliano na mabadiliko ya tabia. Katika sehemu hii, udhibiti wa visambaza magonjwa hautozungumziwa kwa sababu kuna taarifa chache kuhusu umuhimu wa sekta hii kwa watu wenye ulemavu.

Mahitaji ya maji yanatofautiana kulingana na mazingira ya kuishi. Kwa kuzingatia watu wenye ulemavu, sekta hii lazima izingatie mambo anuwai, mfano kama muktadha ni mjini au kijijini, janga ni kwa sababu ya ugomvi au majanga asilia, na kama mazoea ya kijamii na kidini yanaathiri matumizi ya maji.

Kwa kuongezea, matumizi ya maji yanaathiri ulinzi. Ugomvi wa silaha na kukosa usawa kunaathiri ulinzi wa maji kwa mtu mmoja mmoja ama kundi. Ushindani katika mahitaji ya maji, kwa ajili ya matumizi na madhumuni ya nyumbani na maisha, kunaweza kusababisha wasiwasi juu ya suala la ulinzi. Ulinzi binafsi na usalama ni muhimu katika sekta ya WASH, ili kutambua hatari ambayo inaambatana na ukusanyaji wa maji, uchafuzi wa maji, kinyesi, na usimamizi wa usafi wa hedhi.[233]

Tazama mada ya Ulinzi. Sekta za Afya na Elimu elimu zinatakiwa zihakikishe kwamba wadau wa WASH wanatumia sehemu hii wanaposhughulikia shida za WASH katika mashule na vituo vya afya.

WASH ina nafasi muhimu katika kuhakikisha ustawi wa watu, kujumuisha watu wenye ulemavu na familia zao ambao wanaweza kuhitaji kupata kiasi cha ziada cha maji, sawa na vifaa vya ziada au vya muhimu kwa ajili ya usafi, na kuwa na upatikanaji wa uhakika wa miundombinu ya maji na usafi wa mazingira. Watu wenye ulemavu wanaoishi katika kutengwa au taasisi maalum, au ambao hawajajumuishwa kwenye huduma iliyokondoishwa, mfano elimu, wanaweza kuondolewa kwenye taarifa zinazohusiana na WASH hivyo kuwa katika hatari kubwa zinazohusiana na afya na maji, ambazo zinaweza kuhatarisha maisha yao au familia zao.

### Sheria na mifumo mingine

- Haki ya maji imetafsiriwa kama haki ya kila mmoja, kwa ajili ya utoshelevu, usalama, unaokubalika na unaofikika na wa gharama nafuu ya maji kwa ajili ya matumizi binafsi na ya nyumbani".[234]
- Mkataba wa haki za watu wenye ulemavu
- Lengo namba 6 la Malengo ya Maendeleo Endelevu

[233] Kitabu cha Sphere (2018). Angalia sura kuhusu maji na usafi wa mazingira.

[234] Kamati ya Umoja wa Mataifa kuhusu haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni, mapendekezo ya jumla namba 15 kuhusu haki za maji (ibara namba 11 na 12 katika mkataba) E/C.12/2002/11, 20 Januari 2003.

## Dhana muhimu

**Usafi** ni mazoea ya kutunza watu na vituo vya umma na mazingira yao safi kuzuia magonjwa au kusambaa kwa magonjwa.

**Kuhamasisha usafi** kunaunga mkono tabia na ushiriki wa jamii na hatua za kupunguza hatari ya magonjwa. Jitihada iliyokondoishwa ya kukuza usafi, iliyobadilishwa ili kukidhi utamaduni wa eneo na mahitaji ya muktadha, ni muhimu katika mafanikio ya huduma ya WASH.

**Usambazaji wa maji** ni utoaji wa maji kwa mahitaji binafsi au matumizi ya nyumbani. Ni lazima itofautishwe na umwagiliaji na maji kwa ajili ya matumizi ya viwanda. Katika hali fulani maalum na katika kipindi kifupi, inaweza jumuisha maji kwa ajili ya mifugo. Kiwango cha chini cha maji salama yanayotolewa katika hali ya dharura inatofautiana kulingana na muktadha. Ni kati ya lita 5 mpaka 50 (au zaidi) kwa mtu kwa siku. Maji yanaweza kusambazwa na huduma za umma, mashirika rasmi au yasiyo rasmi ya kibiashara, mashirika ya kijamii au watu binafsi. Mipango ya usimamizi pia hutofautiana sana kulingana na muktadha.

**Usafi wa mazingira** ufafanuzi wake unaweza kutofautiana. Ufafanuzi mwembamba unahusu utoaji wa vifaa na huduma za utupaji salama wa kinyesi cha binadamu na mkojo na usindikaji wake. Ufafanuzi mpana unahusu pia utunzaji wa hali ya usafi, kupitia huduma kama vile ukusanyaji wa taka, utupaji na mifereji ya maji taka.

**Udhibiti wa kinyesi** inahusu utupaji salama wa kinyesi, katika hali ambayo haitochafua mazingira, maji, chakula au mikono. Utupaji salama wa kinyesi cha binadamu ni mojawapo ya njia kuu za kuvunja mzunguko wa maambukizi ya magonjwa ya kinyesi-kinywa (*feacal oral deseases*). Mazoea ya kujisaidia haja kubwa hutegemeana sana na utamaduni.

**Usimamizi wa taka ngumu** unahusu mchakato wa kukusanya na kutibu taka ngumu. Mara nyingi husimamiwa na mamlaka ya umma, ukusanyaji wa taka ngumu na mfumo wa utupaji taka unaweza kuvurugika kwa dharura, kupelekea kuingilia kati kwa watendaji wa huduma za kibinadamu.

**Udhibiti wa visambaza magonjwa** inahusu vitendo vyote vinavyoweza zuia au kuondoa wanyama na wadudu (kiujumla vikiitwa visambaza magonjwa) ambavyo husambaza vimelea vya magonjwa. Ambapo hakuna tiba ya magonjwa iliyopatikana (virusi vya Zika, virusi vya West nile na homa ya Dengu), udhibiti wa visambaza magonjwa ni njia pekee ya kulinda kundi la wanadamu. Itafanikiwa kwa kupitia hatua mbalimbali. Udhibiti wa mazingira huondoa au hupunguza nafasi ambapo vijidudu visambazavyo magonjwa huzaliana (mfano maji yaliyosimama, taka ngumu, taka za chakula na kifusi) au kupunguza mawasiliano na vijidudu vinavyosababisha magonjwa (mfano, kwa kusambaza vyandarua). Udhibiti wa kemikali hutawanya mawakala wa kemikali (kwa kunyunyizia au kufukiza) ambao huua, huzuia au kuvuruga mzunguko wa uzalishaji wa vijidudu vinavyosambaza magonjwa. Katika matendo ya kibinadamu, udhibiti wa mazingira ni juhudi za pamoja za WASH na sekta za makazi, wakati udhibiti wa kemikali (na mara chache ugawaji wa vyandarua) mara nyingi huratibiwa na sekta ya afya.

**Hali ya kutoshikilia mkojo au kinyesi** inatokea pale mtu anaposhindwa kudhibiti mtiririko wa mkojo au kinyesi. Ni hali tata ya kiafya na kijamii ambao unaweza kusababisha unyanyapaa, kutengwa kwa jamii, msongo wa mawazo, na kutoweza kupata huduma, elimu na nafasi za kazi. Mara nyingi hali hii haijatolewa taarifa lakini watu anuwai wanaishi na kiwango cha kutoweza kushikilia kinyesi au mkojo.

WASH inahusiana na sekta nyingi za kibinadamu, shughuli zake zinaweza kuendeleza ulinzi na afya ya watu wenye ulemavu pamoja na kundi la watu lililoathiriwa. Kutokuwa na hali ya usafi na usafi wa mazingira unaolegalega, unaoleta hatari kubwa katika ulinzi na afya.

## Rejea


- *Kitabu cha Sphere* (2018)
- Shirika la kimataifa la Handicap CMB, HelpAge, *viwango vya ujumuishi wa wazee na watu wenye ulemavu* (2018). Angalia kipengele kuhusu maji na usafi wa mazingira
- *Ufikivu kwa wote katika Muktadha wa Dharura: muongozo wa kuhakikisha ufikivu katika miongombinu ya muda mfupi, vifaa vya maji na usafi wa mazingira, usambazaji na shughuli za mawasiliano kwa watu wenye ulemavu pamoja na watu wengine walioathirika* (2009)






**Mchoro namba 13 |** Vizuizi vya upatikanaji na ujumuisho katika maji na usimamizi wa mazingira

### JINSI ATHARI ZA MIGOGORO ZINAVYOZIDI KWA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA MASUALA YA MAJI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

**MATOKEO YA MIGOGORO**

Kukosekana kwa usalama, kuvunjika kwa mitandao ya kijamii, uharibifu wa miundombinu, uhamishwaji, kufungwa kwa huduma

**VIZUIZI VINAVYOONGEZEKA**

**Vikwazo vya kimazingira:**

- Vifaa vya WASH visivyoweza kufikika kiurahisi au vifaa kama maliwato, vyanzo vya maji, vifaa vya usafi, vyombo vya maji, n.k.
- Taarifa zisizopatikana kiurahisi na ishara kuhusu huduma za WASH, vifaa na programu
- Maeneo machache ya upatikanaji huduma

**Vikwazo vya kimtazamo:**

- Mitazamo hasi na ubaguzi wa watu wenye ulemavu
- Kukosa ufahamu na maarifa kwa watendaji wa sekta WASH na mashirika katika kuwasiliana na watu wenye ulemavu na kuhakikisha ujumuishaji wao katika programu za WASH

**Vikwazo vya kitaasisi:**

- Ukosefu wa uwezo wa kiufundi wa kukuza ujumuishaji wa watu wenye ulemavu katika WASH
- Viwango vya sekta, miongozo, na sera hazizingatii mahitaji ya watu wenye ulemavu
- Kukosekana kwa bajeti ya kuhakikisha upatikanaji wa maliwato na vifaa na mahitaji mengine ya WASH
- Aina za ujenzi na minyororo ya usambazaji haizingatii ufikikaji na kanuni ya usanifishaji kwa ajili ya watu wote
- Ukosefu wa taarifa kamili kuhusu watu wenye ulemavu

**Hatari wanazokumbana nazo watu wenye ulemavu**

Ukatili, umaskini, majanga ya mazingira, kuzorota kwa afya, kunyanyapaliwa kwa sababu ya ukosefu wa huduma za WASH, kutengwa, kuachwa

## Masuala muhimu na ya lazima kufanya

Masuala ya 'Lazima kufanya' lazima yafanyike katika hatua zote wakati programu ya WASH inapotekelezwa kwa ajili ya watu wenye ulemavu.

### Ushiriki

- Hakikisha kwamba watu wenye ulemavu, familia zao na mashirika ya watu wenye ulemavu, wanahusishwa kikamilifu katika kutambua vikwazo, na katika kupanga, kubuni, kutekeleza na kutathmini WASH na sera zinazohusiana na programu. Wahusishe katika kufanya maamuzi.
- Hakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanawakilishwa kwa usawa kwa kuzingatia utofauti wa ulemavu, pamoja na jinsia, umri na utofauti. Fanya jitihada za lazima kukuza uhusishwaji wa makundi yasiyowakilishwa itoshavyo, kujumuisha watu wenye ulemavu wa afya ya akili, watu asilia ya mahali hapo, wanawake na wasichana katika miundo rasmi na isiyo rasmi.
- Tengeneza ushirika na mashirika ya watu wenye ulemavu na mashirika mengine yanayofanya kazi katika sekta ya WASH. Wahusishe katika kusaidia watu wenye ulemavu na kuwakilisha kwa ajili na kuhamasisha ujumuishi katika ya huduma za WASH.

### Kushughulikia vizuizi

- Tambua na fuatilia vizuizi vinavyozuia upatikanaji wa vifaa vya WASH, pamoja na viwezesho vitakavyofanya vipatikane kiurahisi. Kwa kiwango cha chini hakikisha kwamba asilimia 15 ya vifaa vinapatikana kiurahisi. Jumlisha vyanzo vya maji, maliwato na sehemu za usambazaji. Fanya marekebisho stahiki, kwa mfano utoaji wa vifaa saidizi na andaa huduma za kuwafikia watu ili kuongeza ujumuishaji wa watu wenye ulemavu katika huduma zote na vifaa vya WASH.
- Himiza au dai watoa huduma wote wa WASH kutekeleza kanuni za usanifishaji kwa ajili ya wote wanapopanga au kujenga miundombinu ya WASH.
- Toa nyenzo zote za tathmini na taarifa zote na mawasiliano juu ya programu ya WASH na kufuatilia (kukuza usafi, sehemu na muda wa usambazaji, usimamizi wa vyanzo vya maji) kwa aina mbalimbali zinazopatikana kiurahisi, kwa kuzingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu wa kusikia, kuona na afya ya akili.[235]
- Tekeleza mikakati ya kupunguza unyanyapaa unaohusiana na ulemavu, chukua hatua kufanya jamii ifahamu haki za watu wenye ulemavu. Anzisha vikundi vya usaidizi rika ambavyo vinajumuisha utetezi binafsi kwa watu wenye ulemavu wa afya ya akili.
- Hakiki sera za kisekta, miongozo na zana ili kuhakikisha kwamba zinaongelea wazi haki za watu wenye ulemavu katika ujumuishi na ufikikaji.

### Kuwezesha na kukuza/kuendeleza uwezo

- Kondoisha ulinzi wa kawaida na hatua za kulinda hatua zote za WASH. Wajulishe watu wenye ulemavu kuhusu hatua hizi na jinsi ya kuzipata. Tambua masuala ya kijinsia na baadhi ya hatari za ulinzi na uhifadhi.
- Jenga uwezo wa wafanyakazi wa WASH. Toa mafunzo ya ufahamu juu ya haki za watu wenye ulemavu, pamoja na uhusiano wake na masuala ya umri, jinsia, hali ya uhamiaji, dini na hali ya kingono.
- Fanya watendaji wa WASH wawe na ufahamu zaidi juu ya hatari na vikwazo ambavyo watu wenye ulemavu wanakumbana navyo na kuviondoa kwa kufuata kanuni za kibinadamu.

[235] Shirika la kimataifa la HelpAge, *viwango vya ujumuishi katika masuala ya kibinadamu kwa wazee na watu wenye ulemavu*. Angalia kipengele cha maji na usafi wa mazingira.





- Jenga uwezo wa mashirika ya watu wenye ulemavu kufanya kazi katika programu ya WASH na wezesha ushiriki wao wa maana katika kubuni, kutekeleza na kufuatilia huduma za WASH.
- Husisha watu wenye ulemavu na mashirika ya watu wenye ulemavu katika kuhamasisha jamii na shughuli za kuwafikia watu.

### Ukusanyaji wa taarifa na ufuatiliaji

- Pitia viwango na zana za WASH kuhakikisha kuwa zinaruhusu ukusanyaji wa taarifa juu ya watu wenye ulemavu, zikijumuisha taarifa za ubora na habari juu ya vizuizi na viwezeshaji.

Masuala yanayopendekezwa hutumia njia pacha. Yanahakikisha watu wenye ulemavu wana haki sawa na nafasi sawa katika upatikanaji wa programu na huduma za WASH, kuondoa vikwazo na kukuza ujumuishaji kamili na ushiriki mzuri.

**PROGRAMU ILIYOKONDOISHWA**

Programu za WASH na hatua nyingine zimeundwa na kubadilishwa kuhakikisha kwamba zinajumuisha na zinapatikana kwa kila mmoja, pamoja na watu wenye ulemavu.

**WALENGWA**

Programu za WASH kutosheleza mahitaji binafsi ya watu wenye ulemavu, kwa kuongeza maji, vifaa vya kusaidia tatizo la kutoweza kushikilia kinyesi au mkojo, viti vya maliwato, mafuta ya utunzaji wa ngozi nakadhalika.

## Hatua zinazopendekezwa

### Maji na usafi wa mazingira kwa ujumla na usambazaji wa maji

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi, na kupanga** | | | |
| Tambua mashirika ya watu wenye ulemavu na watoa huduma; kusanya taarifa zinazohusiana na WASH kwa watu wenye ulemavu. | X | | |
| Tambua na changanua hatari na vikwazo ambavyo watu wenye ulemavu wanakumbana navyo wanapohitaji kupata huduma za WASH, vifaa na taarifa. Panga hatua za kupunguza na kuviondoa. | X | | |
| Kusanya na hakikisha kufikiwa kwa viwango vya kitaifa na kimataifa katika upatikanaji wa huduma za WASH. | X | | |
| Buni au badilisha miundombinu ya WASH kwa kulingana na kanuni ya usanifisha kwa ajili ya watu wote ili kuhakikisha kwamba inapatikana. | X | | X |

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Hakiki zana za tathmini ya haraka za *WASH,* hakikisha inajumuisha maswali na viashiria kuhusu hali ya ulemavu. | X | | |
| Hakikisha kwamba vifaa vya elimu (mfano, kuhusu ukuzaji wa usafi) zinasambazwa katika njia mbalimbali zinazopatikana kiurahisi kwa watu wenye ulemavu. | X | | |
| Fundisha wafanyakazi wa WASH kuhusu ujumuishi wa watu wenye ulemavu. Zingatia mazoea, viwango, zana, na muundo wa programu. | X | | |
| Tambua maeneo ya watu wenye ulemavu kabla majengo ama vifaa vya WASH havijajengwa, hasa kama baadhi ya maeneo hayafikiki kiurahisi. | X | X | X |
| Hakikisha kwamba tathmini za kisekta zinazingatia taarifa za WASH zikitenganishwa kwa jinsia, umri na ulemavu. | | X | |
| Hakikisha kwamba tathmini za kiufundi zinatathmini uwepo wa miundombinu inayofikika. | | X | |
| Washirikishe watu wenye ulemavu kabla ya kutenga miundombinu ya maji, ukizingatia mahitaji yao maalumu. Fanya hivyo sambamba na tafiti za kaya. | X | X | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Jumuisha watu wenye ulemavu wakati wa kuandaa na kupanga bajeti ya mipango ya kutoa huduma za WASH au miradi ya rufaa ya kuonekana. | | X | |
| Weka bajeti ya gharama ili kufanya huduma na miradi ipatikane kiurahisi. | | X | |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Wakati wa kuweka viwango vya usafi na vifaa vya utu, fikiria mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu. | X | | |
| Sambaza miongozo na zana za WASH. Kama ni lazima, panga mafunzo maalumu kwa ajili ya wafanyakazi watekelezaji. | X | X | |
| Endeleza vitengo na mashirika ya WASH katika kushauriana na watu wenye ulemavu. | | X | |





| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Kufanya kazi na serikali za mitaa na mashirika ya watu wenye ulemavu katika kuendeleza viwango vya WASH katika mashule, mahospitali na majengo ya umma. Katika kubuni haya, zingatia mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu. | | | X |
| Jenga miundombinu ya WASH ambayo inapatikana kiurahisi kwa watu wenye ulemavu ukizingatia mahitaji yao maalumu. | | X | X |
| Shauriana na husisha watu wenye ulemavu kuhusu kuamua maeneo maji na miundonmbinu ya usafi itakapokaa, kubuniwa, kujengwa na kutunzwa. Unapokuza usafi wa mazingira shauriana nao vilevile. | X | X | X |
| Badilisha maumbo na uzito wa vibeba maji kuwa katika uwezo wa watu wenye ulemavu, na vifaa hivyo kuwa vinapatikana. | X | X | |
| **4. Uratibu** | | | |
| Alika mashirika ya watu wenye ulemavu kushiriki katika uratibu wa WASH na vikundi vya kufanya kazi za kiufundi. | X | X | X |
| Andaa miundombinu ya WASH inayofikika katika kushauriana na taasisi husika na vitengo vya makazi. Fuata hatua zile zile katika kuweka familia ambazo zina mahitaji fulani yanayohitaji kuwa karibu na miundobinu ya jamii. | | X | |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Hakikisha kwamba zana za ufuatiliaji za kawaida zinazokuzwa na sekta zina upatikanaji wa miundombinu ya WASH. | | X | |
| Jumlisha viashiria vya ulemavu katika ufuatiliaji wa kawaida na ule wa kukusanya taarifa za ubora; zibuniwe kuruhusu utengano kwa ulemavu. | | X | |
| Alika watu wenye ulemavu kushiriki katika ukaguzi wa 'mafunzo', juhudi za kutambua mifano na utendaji mzuri, na ukubaliwaji wa mapendekezo kwa programu za WASH. | | | X |
| Jumuisha watu wenye ulemavu katika kamati, kuwahimiza katika kuyatambua na kuyaonesha mahitaji yao. Kuhakikisha wanakuwa na fursa ya kupata maji ya kutosha na vituo vya maji. | | X | |

## Usafi

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi, na kupanga** | | | |
| Wakati wa kutengeneza vifaa vya mawasiliano, weka pia mipango ya kupunguza unyanyapaa. Chukua hatua kuondoa vizuizi vya kijamii, kimwili na kimawasiliano ambazo zinawazuia watu wenye ulemavu kupata huduma na vifaa vya WASH. | X | X | |
| Jumbe zinapaswa kuwa zinafikika, zikijumuisha vidokezo vya jinsi ya kudumisha usafi binafsi. | X | X | |
| Ongeza vifaa ambavyo watu wenye ulemavu wanahitaji katika vifaa vyao vya usafi. Jumuisha vifaa kwa ajili ya tatizo la kutoshikilia haja (nepi za watu wazima, pamba za kunyonya haja, taulo za kike zinazoweza kutupwa ama zinazoweza kutumika tena, godoro linaloweza kufulika na lisilovuja, ndoo ya pili na sabuni ya nyongeza). | X | X | X |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Jumuisha katika bajeti gharama ya kuchapisha na kusambaza jumbe za WASH katika njia mbali mbali zinazoweza kupatikana kiurahisi. | X | X | X |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Kuanzisha jumbe za kuendeleza usafi kwa njia mbalimbali zinazoweza kupatikana kiurahisi (kwa mdomo, vipeperushi, lugha ya ishara, lugha rahisi kusoma/iliyo wazi, n.k). | X | X | |
| Kuagiza wafanyakazi wa kutangaza usafi kutoa taarifa za WASH katika ngazi ya kaya. Hakikisha wanafamilia wote wana fursa ya kupata habari zinazosambazwa. | | X | |
| Kukuza uelewa wa wafanyakazi kuhusu matumizi ya vifaa vya ziada vya usafi na utupaji wake. | X | X | |
| Wanawake wenye ulemavu wanaweza kuhitaji fursa ya upatikanaji wa vifaa rahisi na tofauti vya usimamizi wa usafi wa hedhi. Rekebisha vifaa vya usafi wa hedhi ili kukidhi mahitaji yao. Fikiria kusambaza pamba ya kunyonya haja/damu, taulo za zinazoweza kutupwa ama zinazoweka kutumika tena, nguo za ndani, sabuni, kifaa maalumu cha kuhifadhia chenye mfuniko na kamba na vibanio vya kuanikia. | X | X | |
| Hakikisha kwamba watu wenye shida ya kutembea wanapata fursa ya kupata vifaa na miundombinu ya usafi, mfano sabuni, maji na mabomba. | | X | |





| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Hakikisha kwamba vifaa vya usafi vinagawanywa na vinapatikana kwa urahisi na watu wenye ulemavu. Chagua sehemu ya kugawanyia ambayo sio mbali sana na kundi la watu lililoathiriwa. Hakikisha huduma hizi zinapatikana kwa watu wasio na ulemavu na watu wenye ulemavu. (Kwa mfano, kuweka matuta, reli, na kamba za kuongozea katika vituo vya maji). Kutoa vifaa kwa watu wenye ulemavu ambao hawana uwezo wa kusafiri mpaka vituo vya ugawaji. | | X | |
| Kila inapowezekana, watangulize watu wenye umri mkubwa na wale wenye ulemavu katika foleni ya ugawaji bidhaa. Andaa mistari maalumu au muda maalumu wa kuwagawia kama watapenda. | | X | X |
| Weka sehemu ya kukaa, chakula na maji ya kunywa salama katika maeneo ya kugawia. Gawa vifaa katika hali ya kuzingatia jinsia na katika hali inayojali utu wa watu. | | X | X |
| **4. Uratibu** | | | |
| Sambaza jumbe zihusuzo usafi katika njia mbalimbali zinazoweza kupatikana kiurahisi. | X | X | |
| Hakikisha kwamba jumbe za usafi zinazingatia mahitaji maalumu ya watu wenye ulemavu. | X | X | |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Hakikisha kwamba taratibu za ufuatiliaji na tathmini zinahusisha watu wenye ulemavu na kuzingatia maoni yao. | | X | X |

## Usafi wa mazingira (Uthibiti wa kinyesi na usimamizi wa taka ngumu)

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| **1. Tathmini, uchambuzi, na kupanga** | | | |
| Tambua na changanua hatari na vikwazo ambavyo watu wenye ulemavu wanakumbana navyo wanapohitaji kupata vifaa vya WASH. Panga hatua za kupunguza na kuziondoa. | X | | |
| Weka vifaa vya WASH katika umbali unaofaa kutoka kwa kila kimoja na kutoka katika nyumba za watu. Weka sehemu za kunawia karibu na maliwato, weka maeneo ya umma ya kutupa taka mbali kidogo na makazi ya watu. | X | X | |

| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Buni njia zisizo na vikwazo za ufikiwaji wa vifaa vya usafi wa mazingira. | X | | |
| Chukua hatua kufanya miundombinu ya jamii (masoko, vituo vya afya, mashule) vifikike kwa urahisi. Fanya makazi binafsi yafikike kiurahisi pia. Katika maliwato ya umma, weka vifaa maalumu kwa ajili ya watu wenye ulemavu. | X | X | X |
| Kukikosekana kwa tathmini ya kina, fikiria kwamba asilimia 15 ya vifaa vipya na vilivyokarabatiwa lazima viwe fikivu kwa kila mtu pamoja na watu wenye ulemavu. | X | | |
| Hakikisha kwamba watu wenye ulemavu na familia zao wanahusishwa kabla ya utupaji wa taka. Fikiria kinyesi na vifaa vya usafi vya hedhi na vifaa vya kuzuia hali ya kutoshikilia haja. Hakikisha kwamba mipango ya utupaji taka ni salama, inaheshimu utu na kuondoa unyanyapaa. | X | X | |
| **2. Ugemaji rasilimali** | | | |
| Husisha watu wenye ulemavu kwenye kuandaa bajeti ya mipango ya huduma za WASH au miradi ya rufaa ya kuonekana. | | X | |
| Hakikisha kwamba mapendekezo na bajeti zinajumuisha gharama za kufanya vifaa na huduma zipatikane kwa urahisi. | | X | |
| **3. Utekelezaji** | | | |
| Andaa semina za kuongeza uelewa kwa familia juu ya umuhimu wa upatikanaji wa maliwato kwa ajili ya uhuru na utu wa watu wenye ulemavu. | | X | |
| Fanya vizuizi vya choo kupatikana kiurahisi kwa kuweka matuta na vishikizo vya mikono. Tengeneza milango mipana kutosha kuruhusu kiti mwendo. | | X | X |
| Hakikisha vizuizi ni vikubwa na vya kutosha kwa kiti mwendo pale mlango ukifungwa. | | X | X |
| Weka bomba ambazo ni rahisi kutumia kwa ajili ya kunawa mikono. | | X | X |
| Weka mifumo ya mifereji ya maji ili kuzuia kutokuwa na utelezi wa sakafu. | | X | X |






| | Kujiandaa na kujiweka tayari | Kutoa huduma | Kurejesha jamii katika hali ya kawaida |
|---|---|---|---|
| Kila wakati shauriana na jamii juu ya mipangilio ya utupaji wa taka salama na mazoea ya usafi. Shirikisha jamii kuhusu eneo, muundo na usahihi wa vifaa vya usafi wa mazingira. Fikiria upatikanaji wa mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu: wanahitaji kusafiri kufika maliwatoni, kufikia maliwato na kuwa na uwezo wa kuchuchumaa au kukaa katika maliwato. | X | X | X |
| Shauri na saidia watoa msaada na saidia watu juu ya mbinu za kuthibiti kinyesi majumbani. Wataarifu jinsi ya kutupa kinyesi kwa usalama na usafi. | | X | |
| Weka vyombo vya kuhifadhi taka vilivobadilishwa sawasawa na mahitaji tofautitofauti ya watu wenye ulemavu. Hakikisha kwamba vinawekwa sehemu ambapo wenye ulemavu wanaweza kuvifikia. | | X | X |
| Fundisha wafanyakazi wa huduma za kibinadamu na programu kuhusu mahitaji ya WASH ya watu wenye ulemavu. Hakikisha kwamba vifaa vimetengenezwa kwa kuzingatia ufikikaji. Huduma zinatakiwa zizingatie utu wa watu, kuwa sahihi na rahisi kutunza. | X | | |
| Tengeneza maagizo na alama katika aina mbalimbali zitakazopatikana kiurahisi ambazo zinaeleza jinsi ya kutupa taka kwa usalama na usafi. | X | | |
| **4. Uratibu** | | | |
| Hakikisha majengo ya umma (mfano shule, hospitali) yana maliwato ya kutosha na yanayofikika. | X | X | |
| Shirikisha watu wenye ulemavu kutoa maoni kuhusu mahali ambapo vituo vya taka ngumu za jamii zimewekwa ama kuandaliwa. | X | | |
| **5. Ufuatiliaji na tathmini** | | | |
| Fuatilia jinsi watu wenye ulemavu wanavyotumia maliwato. Nakili asilimia za wanaosema kwamba maliwato yanakidhi mahitaji yao na asilimia ya wasioridhika. Tumia taarifa hii kuendeleza usafi na ubora wa vifaa na huduma. | | X | X |

# 19 Viambatanisho

## Kiambatanisho namba 1 | Kufanya marekebisho stahiki

Hatua mbili zinazohitajika ili kufanya marekebisho stahiki.

1. Ainisha vitu ambavyo watu wenye ulemavu wanahitaji kushiriki (majadiliano shirikishi)




2. E lezea katazo la marekebisho stahiki (bila ubaguzi).

Zingatia kila rasilimali uliyonayo. Zingatia manunuzi elekezi kutoka kwa watoa huduma wa nje angalia kama suluhu ililotolewa haiwezi kukidhi mahitaji ya watu wanaolengwa.

Kama hamna chaguo lililopatikana kukidhi mahitaji ya mtu, kushindwa kukidhi hitaji lake sio ubaguzi.

| ULIZA | Kweli | Si kweli |
|---|---|---|
| Je, ni vigumu kufanya haya marekebisho kwa sababu hayapatikani? | | |
| Je, ni vigumu kufanya au kupata marekebisho haya kwa wakati katika kukidhi malengo? | | |
| Je, si halali kutoa hitaji hilo? | | |

## Maswali elekezi katika kuhalalisha katazo la kutofanyika kwa marekebisho stahiki

Kila sababu za kukataa marekebisho stahiki ni lazima ijikite katika vigezo vinavyoeleweka na kuwasilishwa kwa wakati kwa mtu anayehusika.[236]

Maswali yafuatayo yakupe mwongozo wakati wa kutathimini ombi la marekebisho stahiki au kulikataa katazo bila ubaguzi wa ulemavu. Tafadhali zingatia kuwa tathimini inaishia katika jibu hasi katika swali la kwanza, kama jibu ni chanya, endelea na swali linalofuata.

1. **Je, ni halali kufanya marekebisho yanayohitajika?**

(Kwa muktadha huu, sheria imaanishe kuwa hakuna katazo la kisheria linalozuia marekebisho stahiki. Kutokuwepo kwa kanuni zinatoa jukumu la kufanya marekebisho stahiki, hakumaanishi marekebisho hayo yasifanyike. Kutokuwajibika kunaweza kutafsiriwa kama kitendo cha unyanyapaa kwa kigezo cha ulemavu. 'Kinyume cha sheria' maana yake ni sheria au kanuni ambayo inakataza marekebisho stahiki yanayopendekezwa, hata kama hili ni kweli, wadau wanapaswa kupata ruhusa kama inavyostahili au kuwezekana).

- **Kama marekebisho si halali, kutofanya marekebisho stahiki sio ubaguzi**. (*"Marekebisho haya hayawezi kutolewa kwa sababu yamezuiwa kisheria"*).
- **Kama katazo ni halali, nenda swali linalofuata.**

2. **Je, inawezekana kufanya marekebisho? (Je, hitaji linapatikana?). Je, kinachohitajika kinapatikana?**

(Hili swali linataka kuelezea kama hitaji linatekelezeka mahali popote na wakati wote linapohitajika. halitathmini kama ni la muhimu, au linafaa kukidhi malengo yake, au ikiwa rasilimali zinazopatikana, ikijumuisha rasilimali za nje ambazo zinaweza kupatikana kirahisi, zinapatika kulipia gharama zilizopo).

- **Kama haiwezekani kufanya marekebisho, katazo la marekebisho stahiki sio ubaguzi.** *("Hili ombi la marekebisho haliwezekani kumalizika/kufikia mwisho kwa sababu sio rahisi kupata bidhaa ama huduma inayohitajika katika soko la ndani au soko linalopatikana")*.
- **Kama ombi la kufanya marekebisho stahiki linaweza kumalizika, nenda swali linalofuata.**

3. **Marekebisho yanahitajika ni muhimu na linafaa? (Je, kinachohitajika kurekebishwa ni muhimu na kinafaa?) Je, linaweza kuondoa vikwazo husika na kuhakikisha linatambua kupatikana kwa haki kwa hali ya usawa na wengine?**

(Hili swali linaangalia kama marekebisho yanayohitajika yanakidhi lengo. Je, linachangia katika kuondoa vikwazo na hivyo kuwezesha watu wenye ulemavu kuweza kufanyia kazi haki zao kwa hali ya usawa na watu wengine?)

- **Kama marekebisho hayawezi kukidhi lengo au halitaweza kutenda haki, kukataliwa kwake sio ubaguzi.** *("Rekebisho hili haliwezi kufanyika kwa sababu halikidhi lengo linalokusudiwa na halitachangia katika kuondoa vikwazo")*.
- **Kama katazo linakidhi lengo, nenda swali linalofuata.**

4. **Je, marekebisho yanayohitajika yataleta madhara kwa watu wengine kulinganisha na wengine?**

(Swali hili linatathimini kama ni mzigo au kama madhara yatatokea katika mchakato wa kutoa marekebisho yanayohitajika. Kujibu swali hili kunahitaji uamuzi wa uwiano/usawa. Je ni sahihi kutumia rasilimali zinazohitajika kufanya marekebisho (kwa muda, gharama, matokeo, n.k) ili kupata lengo linalohitajika, nini ni starehe ya haki husika?).

- **Kama marekebisho yanayohitajika yameamuliwa kuwa ni mzigo na yataleta madhara makubwa kuyakataa sio ubaguzi.**

Yanaweza kuwa mzigo usiofaa au kuleta madhara, kwa mfano:

- Marekebisho ni gharama, na hakuna njia nyingine ya kupata kinachohitajika.
- Marekebisho ni gharama kubwa kiasi kwamba yanaweza kuhatarisha lengo la programu.
- Kufanya marekebisho kunaweza kudhoofisha kazi za msingi za programu.
- Kuzingatia mengine yanayoendana katika malengo ya mahitaji yangeweza kudhoofisha kazi za msingi katika programu.

- **Kama marekebisho yanalohitajika hayajatolewa maamuzi kama suala litakaloleta uzito au madhara, uamuzi wa kukataa marekebisho stahiki unaweza kubagua kwa sababu ya ulemavu.**

---

[236] Kamati ya CRPD, Mapendekezo ya jumla namba 6 kuhusu usawa na kutobaguliwa, CRPD/C/GC/6, aya ya 27.

## Kiambatanisho namba 2 | Zana za kutenganisha taarifa

| Zana | Matumizi | Jinsi inavyotumika katika mpango wa huduma za kibinadamu |
|---|---|---|
| Maswali kuhusu ulemavu ya kundi la Washington.[237] | Zana hii ina maswali sita ambayo yanaweza kuwekwa katika sensa na tafiti. Maswali yanawezesha kupatikana kwa taarifa za kuweza kufahamu mlinganisho wa hali za ulemavu ulimwenguni. | Matumizi ya zana hii kwa mashirika ya kibinadamu yanaongezeka na hivi sasa inajaribiwa katika maeneo mengi ya muktadha wa huduma za kibinadamu.[238]<br><br>Zingatia: Maswali ya kundi la Washington hayaelezei wazi matatizo ya kiafya au kutambua vikwazo vya watu wenye ulemavu. |
| Maswali kuhusu ulemavu yaliyoboresha na kundi la Washington | Zana hii inajumuisha maswali yaliyoongezwa ili kupata taarifa ya hali ya ufanyaji kazi wa sehemu ya juu ya mwili, hasira na msongo wa mawazo. | |
| Maswali yaliyokuzwa ya kundi la Washington. | Hii zana ina maswali ya nyongeza (jumla 37) ambayo yamejikita katika kupata hali ya hasira na msongo wa mawazo, maumivu, uchovu, matumizi ya vifaa saidizi, miaka ya kuishi na ulemavu na sababu za kimazingira. | Baadhi ya huduma za kibinadamu zimeongeza maswali katika vipengele vya hasira, na msongo wa mawazo katika dodoso la kundi la Washington. |
| Maswali ya kundi la Washington katika ufanyaji kazi wa mtoto la UNICEF. | Zana hii ni ndefu kuliko maswali ya kundi la Washington. Zana hii inakusanya taarifa kwa watoto na vijana wa miaka 2 hadi 17; mtu anayehojiwa anatakiwa kuwa ni mlezi mkuu. | Dodoso hili limekuwa likitumika katika *mipangilio* isiyo na rasilimali (kwa mfano, imewekwa katika tafiti za MICS 6 ambayo inashughulikia hatari nyingi katika huduma za kibinadamu). |
| Dodoso la Shirika la afya duniani kuhusu ulemavu. | Hili ni dodoso kwa ajili ya watu wote kwa ujumla na limesaidia katika kugundua vikwazo vya kimazingira ambavyo vinazuia ushiriki kamilifu wa watu wenye ulemavu. Toleo fupi lina maswali 40: Toleo refu lina maswali mengi/zaidi. | Mpaka sasa zana hii bado haijajaribiwa na watu wanaofanya kazi katika huduma za kibinadamu. |
| Kitini cha Shirikila la Afya Duniani Kuhusu Kupima Ulemavu, toleo la 2.0. | Zana hii inatoa muhtasari imara wa utendaji katika maeneo sita ya kwenye mzunguko wa maisha. Kama vile utambuzi, ujongezi/kutembea, kujitunza, kuelewana, shughuli za kimaisha na ushiriki. Matoleo tofauti ya zana yamekuwa yakitolewa ili kukidhi mahitaji ya makundi tofauti. Zana hii ina vitu kuanzia 12-36 na kila kimoja kina | Zana hili imeshajaribiwa na watu wanaofanya kazi katika huduma za kibinadamu na katika maeneo mengine zaidi ya 100. |

[237] Matoleo mengine ya kundi la maswali la Washington kuhusu ulemavu zimetengenezwa. Leonard Cheshire and Humanity & Inclusion wametengeneza moja inayoitwa kundi la maswali la Washington kuhusu ulemavu lililoboreshwa, lina maswali 12 na maswali 6 yamewekwa katika seti fupi. Pamoja na maswali ya nyongeza yanayohusu wasiwasi, huzuni na mjongeo wa mwili.

[238] Leonard Cheshire and Humanity & Inclusion, *ubinadamu na ujumuishwaji, ukusanyaji wa data kuhusu ulemavu: muhtasari wa matumizi ya kundi la maswali la Washington kwa ajili ya wadau wa maendeleo na masuala ya kibinadamu* (2018).





## Kiambatanisho namba 3 | Vyanzo sahihi vya taarifa rejea

| Taarifa inayohitajika | Vyanzo vya takwimu | Masuala ya kuzingatia |
|---|---|---|
| **Je, kuna watu wangapi wenye ulemavu?** | Idara za takwimu serikali, Kwa mfano:<br>• Elimu.<br>• Afya.<br>• Taarifa za uandikishaji shule. | Takwimu za tarifa za ulemavu zinatakiwa zichukuliwe kwa uangalifu kwa sababu zinatofautiana sana na zinatumia njia nyingi na mbalimbali za upatikanaji wake.<br><br>Zingatia kuwa mifumo mingi ya taarifa za utawala haziwaweki watu wenye ulemavu kwa sababu wanakosa ufukivu/kuzifikia. Taarifa za kutengwa zina nguvu (watoto walioko nje ya mfumo rasmi wa shule) lakini ni vigumu kuzipata kutoka katika kanzidata.<br><br>Mara nyingi taarifa za kiafya hujikita kidogo katika mapungufu ya ulemavu lakini zinaweza zikaruhusu baadhi ya dhana kupatikana au kutumika (kwa mfano katika utendaji kazi). |
| | Usajili wa wakimbizi, wakimbizi wa ndani na wahamiaji. | Taarifa za usajili zinaweza kutowajumuisha watu wenye ulemavu kutokana na njia zinazotumika (kwa mfano vidokezo vya kuona au taarifa za kiafya). |
| | Kitengo cha Umoja wa Mataifa cha takwimu.[239] | Takwimu kuhusu ulemavu katika ngazi ya kitaifa. |
| | "Humanitarian Data Exchange" (HDX). | HDX ni jukwaa ambalo linawezesha mashirika kuweka taarifa zao zipatikane kwa watumiaji wengine. Mpaka mwezi Novemba mwaka 2018, chini ya asilimia moja ya taarifa za HDX zilihusu ulemavu, lakini tafiti kubwa zinaweza kutumia ulemavu kama kiashiria. |

[239] Mbali na kutumia sensa na makadirio ya tafiti za kitaifa za uwepo wa ulemavu katika nchi nyingi, kitengo cha umoja wa mataifa cha kanzidata ya takwimu kinahusisha idara kuhusu aina za ulemavu uliohusishwa katika tafiti za kitaifa na katika kesi nyingi kama mifano ya nyenzo zake.

## Kiambatanisho namba 3 *(inaendelea...)*

| Taarifa inayohitajika | Vyanzo vya takwimu | Masuala ya kuzingatia |
|---|---|---|
| Vikwazo vipi vinazuia upatikanaji wa usaidizi? | Utafiti na tathimini, kama vile:<br>• Utafiti wa kaya (mfano MICS na DHS) iliyofanywa na watendaji wa masuala ya kibinadamu.<br>• Tathimini kuhusu eneo iliyofanywa na watendaji wa masuala ya kibinadamu.<br>• Taarifa zilizotunzwa na mashirika ya watu ulemavu, au mashirika mengine yenye utaalamu. | Hivi karibuni MICS awamu ya 6 (tangu 2017)[240] na DHS (tangu 2016) wametumia maswali ya kundi la Washington kupanga maswali mafupi[241] kwa watu wazima. MICS ametumia Maswali ya Kundi la Washington kupitia UNICEF kuhusu ufanyaji kazi wa mtoto kuweza kutathmini hali ya ulemavu.<br>Zingatia Sampuli na njia unayotumia kukusanya taarifa, ushauri, na malengo yao. Hii hushawishi aina ya taarifa zinazowekwa kwenye taarifa maalum. |
| | Taarifa za kutegua mabomu ya ardhini. | Hii taarifa imetengenezwa maalum kufuatilia matukio yanayoendana na mabomu ya ardhini na mabaki ya mabomu. |
| | Ukaguzi wa ufikikaji. | Hii hufuata mbinu ya orodha ya maswali[242] kutathimini kiwango cha upatikanaji na usalama wa vifaa, majengo na utoaji wa huduma. Inawezekana hufanywa na mashirika ya watu wenye ulemavu na asasi za kiraia. |
| | Mifumo ya ufuatiliaji baada ya usambazaji. | Kama zinachanganuliwa kwa hali ya ulemavu inawezekana kujua vikwazo ambayo watu wenye ulemavu wanakumbana navyo pamoja na matukio ya unyonyaji na hatari zingine za ulinzi. |

240 Katika mbinu zake, data za MICS zinapaswa kutafsiriwa kwa umakini ili kupata uwepo wa ulemavu. Miongoni mwa watu wazima, ni wale tu wenye umri wa kati ya miaka 15 mpaka 49 ndio waliofanyiwa utafiti, hii inaondoa wazee ambao ndio wana uwezekano mkubwa wa kuwa na ulemavu. Kwa watu wazima, MICS inawalenga watu ambao wanaweza kutoshiriki kwa kuwa hawana uwezo, hii inaweza kutafsiriwa na watakwimu kama kuhusisha watu wengi wenye ulemavu. Tafiti za DHS zimeweza kukabiliana na hivi vizuizi kwa kiwango fulani kwa njia ya kufanya usaili katika ngazi ya kaya, ambapo viongozi wa kaya wanaweza kutoa majibu kwa niaba ya hao wenye ulemvu. DHS pia inahusisha uwanda mpana wa umri na kwa hivyo kupata kundi la wazee wenye ulemavu kwa ukamilifu Zaidi.

241 *Kundi la maswali la Washington*, liliundwa kwa kutumia sensa na tafiti. maswali haya yanaakisi fikra kuhusu ulemavu kwa kutumia viwango vya shirika la afya katika kutambua ulemavu. (ICF) kama moduli ya dhana. Maswali hayo yanauliza kama watu wanapata ugumuwa kufanya kazi zao kama vile (kutembea, kuona, kusikia, kutambua, kujihudumia na kuwasiliana) na yaliyotengeneza kwa ajili ya jamii yote kwa ujumla. Hata hivyo, lengo lilikuwa katika kazi na uwezo wa nyenzo kutumika kwa haraka na kirahisi katika namna mbalimbali ikiwemo tathimini ya mahitaji ya kibinadamu.

242 Mwongozo kuhusu ukaguzi wa ufikivu, angalia handicap international, *kufanya ukaguzi wa ufikivu katika nchi za vipato vya kati* (2014).





## Kiambatanisho namba 3 *(inaendelea...)*

| Taarifa inayohitajika | Vyanzo vya takwimu | Masuala ya kuzingatia |
|---|---|---|
| | Mrejesho au utaratibu wa malalamiko. | Hii inaweza ikakupa mtazamo juu ya vikwazo vya watu wenye ulemavu na jinsi anavyotosheka/wanavyokumbana na huduma ya usaidizi. Lakini mifumo ya mrejesho mara nyingi haipatikani kwa watu wenye ulemavu. Hii ni hali halisi hasa kama ni suala nyeti; mara nyingi mifumo ya mrejesho huwa haijulikani au hufanywa siri. Hivyo wahusika wanaweza wasichambue taarifa kwa kuzingatia suala la ulemavu. |
| | Kubadilishana taarifa. | Kwa kuongezea taarifa kuhusu idadi ya watu wenye ulemavu, HDX inajumuisha taarifa juu ya vikwazo na viwezeshaji. |
| | Utaratibu maalum wa tume ya haki za binadamu na mapitio ya pamoja katika vipindi mbalimbali. | Utaratibu wa kitaifa na kimataifa wa haki za binadamu unaweza kutoa taarifa juu ya vikwazo na majanga, ukiukwaji wa kisheria na mahitaji ya mtu mwenye ulemavu. Mifumo hii ni pamoja na mashirika ya haki za binadamu, kamati ya watu wenye ulemavu pamoja na muwakilishi maalumu wa haki za watu wenye ulemavu. |
| Je, ni mahitaji gani na majanga/hatari zipi zinawakabili watu wenye ulemavu? | Mifumo ya usimamizi wa habari, kama vile:<br>• Mfumo wa taarifa za ukatili wa kijinsia<br>• Mfumo wa taarifa za ulinzi wa watoto<br>• Mifumo ya usimamizi wa kesi za ulinzi/kiusalama. | Ufuatiliaji wa matukio unaweza kupendekeza mapungufu ya jinsi ambavyo taarifa imetolewa, kwa mfano watu wenye ulemavu mara zote hawawakilishwi/huwakilishwa chini ya kiwango. Changamoto za maumbile, taasisi, na vizuizi vya kimawasiliano, na mtazamo wa kijamii, na unyanyapaa, unaweza kuzuia watu wenye ulemavu kutumia huduma za ufuatiliaji wa kesi. |
| | Tathimini kama vile:<br>• Tathimini za mahitaji.<br>• Tathmini shirikishi. | Watu wenye ulemavu wanaweza kuwa hawajajumuishwa katika mfumo, ambapo huweza kufanya taarifa kuwa chache au zisizoaminika. Kwa mfano watu wenye ulemavu wanaweza kuwa wamefichwa, au hawawezi kupitia mchakato, au tathimini hazikufikiria kutafuta taarifa kuhusu sababu za athari/majanga (mfano; vikwazo katika kupata msaada). |

## **Kiambatanisho namba 4 |** Mambo ya kuzingatia wakati wa kutathmini taarifa za rejea

| | |
|---|---|
| **Je, dhana ya ulemavu inaelewekaje?** | Utafiti na kanzidata hufafanua ulemavu kwa njia anuwai. Wengine huzingatia udhaifu, wakati wengine wanavutiwa na masuala ya ushiriki, ufikikaji na mahitaji ya msaada.<br><br>Masafa ya vikoa vya walemavu ambavyo zana ya ukusanyaji wa taarifa zinazingatia (kuweza kutoka sehemu moja mpaka nyingine, kuona, kusikia akili, n.k) vitashawishi ni nani taarifa zake zimewekwa kwenye kumbukumbu.<br><br>Katika mazingira tofauti ya kitamaduni, dhana ya ulemavu hutofautiana. Hii inashawishi ni nani anayetambuliwa, na anayejitambulisha mwenyewe kama mtu mwenye ulemavu. Kwa mfano, kasoro zinazohusiana na uzee au uharibifu uliopatikana wakati wa mizozo/ugomvi sio kila mahali hutambuliwa kama ulemavu. |
| **Je, unyanyapaa/unyanyasaji ni sababu?** | Mara nyingi, ulemavu hufichwa au haueleweki kwa sababu ulemavu unanyanyapaliwa. Hii inaweza kuathiri ubora wa ukusanyaji wa taarifa, kwa sababu watu wenye ulemavu wanaweza kusita kujitambulisha, wanaweza kufichwa au kutokubaliwa na familia zao. Na kwa sababu wanaofanya utafiti, na wafanyakazi wa huduma za kibinadamu pia wanaweza kuwa na upendeleo.<br><br>Maswali ya moja kwa moja kama vile ("Je, una ulemavu?") ambayo yanahitaji majibu ya aina mbili (ndiyo au hapana) mara nyingi husababisha kupatikana kwa taarifa chache kuhusu ulemavu, kwa sababu ya kunyanyapaa au wahojiwa wanatofautiana katika uelewa wao kuhusu ulemavu. Pia taarifa kuhusu ulemavu zinaweza kuwa nyeti kwa sababu za kisiasa. |
| **Ni nini kinachohesabiwa kama ulemavu?** | Ulemavu upo kwenye wigo; mtu ana kiwango kidogo au kikubwa cha ulemavu. Mkusanyiko wa taarifa unaweza kuweka vizingiti tofauti kuhusu nani hafikiriwi kuwa na ulemavu. |
| **Kwa kusudi gani taarifa zilikusanywa?** | Kusudi la kukusanya taarifa huathiri ni nani anatambuliwa kuwa na ulemavu. Kwa mfano, utafiti wa kiafya, sensa ya jumla ya watu na utafiti wa hali ya kaya unaweza kuchukua vigezo tofauti kutambua watu wenye ulemavu. |
| **Je, sampuli ina ufikiaji mdogo?** | Watu wengine wenye ulemavu, haswa wale ambao wametengwa nyumbani au wanaishi katika taasisi maalum, hawawezi kujumuishwa katika michakato ya ukusanyaji wa taarifa. Suala hili linaathiri haswa watoto wenye ulemavu. |
| **Je, taarifa zimesanifishwa?** | Takwimu zilizokusanywa kabla ya majanga inawezekana zisiweze kuonyesha idadi ya watu katika eneo hilo la baada ya majanga. Idadi kubwa ya watu wanaofurika hubadilisha idadi ya watu katika eneo husika. Kipindi cha mizozo na majanga huongeza idadi na uwiano wa watu wenye ulemavu. |





## **Kiambatanisho namba 5 |** Mifano ya viashiria

Angalia pia: Viashiria vya Haki za Binadamu katika Mkataba wa Haki za Watu Wenye Ulemavu katika kuunga mkono Ajenda ya 2030 inayojumuisha Ajenda ya Maendeleo Endelevu

| Eneo la mada | Mfano wa shughuli/kiashiria cha kiwango cha juu |
|---|---|
| **Afya** | Idadi ya nyenzo na huduma za afya zilizojengwa kwa kuzingatia kanuni ya usanifishaji kwa wote. |
| **Afya** | Idadi ya watu wenye ulemavu ambao wanapata huduma za mazoezi, pamoja na visaidizi vya teknolojia saidizi. |
| **Elimu** | Idadi ya madarasa yaliyojengwa/yaliyokarabatiwa kwa kuzingatia kanuni ya usafinishaji kwa ajili ya wote. |
| **Maji na usafi wa mazingira** | Idadi ya maliwato zilizojengwa kulingana na kanuni ya usafinishaji wa ajili ya wote. |
| **Maji na usafi wa mazingira** | Idadi ya jumbe kuhusu usafi zikitolewa kwa kiwango cha chini cha aina mbili (zilizoandikwa na za mdomo). |
| **Usalama wa chakula na lishe** | Idadi ya vituo vya usambazaji au masoko yaliyoundwa upya au kujengwa kwa mujibu wa kanuni ya usafinishaji wa ajili ya wote. |
| **Ulinzi** | Idadi ya wafanyakazi, washirika na jamii zilizofundishwa kufanya kazi pamoja na watu wenye ulemavu. |
| **Ulinzi** | Malalamiko yanayodai unyanyasaji dhidi ya watu wenye ulemavu, ubaguzi kwa misingi ya ulemavu, na ukiukaji mwingine wa haki. |
| **Kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa** | Asilimia au idadi ya wafanyakazi wa ukatili wa jinsia waliofundishwa kuhusu ujumuishaji wa watu wenye ulemavu. |
| **Kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji wa** | Idadi ya wanawake wenye ulemavu wanaoshiriki katika mifumo ya kijamii ya kuzuia na kukabiliana na unyanyasaji na ukatili wa kijinsia. |
| **Ulinzi wa mtoto** | Idadi ya watoto na vijana wenye ulemavu wanaoshiriki katika kamati za haki za watoto na miundo mingine ya kijamii kwa ajili ulinzi wa watoto. |
| **Ulinzi wa mtoto** | Idadi ya wafanyakazi wa ulinzi wa watoto waliofundishwa kutoa msaada kwa watu wenye ulemavu wa afya ya akili na shughuli za burudani kwa watoto, pamoja na watoto wenye ulemavu. |
| **Nyumba, ardhi na mali** | Idadi ya mashirika ya watu wenye ulemavu waliofundishwa kushiriki katika masuala ya makazi, ardhi na mali. |
| **Kutegua mabomu** | Idadi ya mashirika ya watu wenye ulemavu na watu wenye ulemavu waliofundishwa kushiriki katika kupunguza hatari na shughuli za elimu. |
| **Kutegua mabomu** | Idadi ya watu wenye ulemavu ambao wanashiriki kwenye shughuli za kijamii katika kutambua na kutathmini janga/athari. |
| **Malazi** | Idadi ya makazi na malazi yaliyoboreshwa kuimarisha upatikanaji wake. |
| **Uratibu wa kambi na usimamizi** | Idadi ya watu wenye ulemavu wanaowakilisha jamii katika mfumo wa uongozi. |
| **Uratibu wa kambi na usimamizi** | Idadi ya tathmini shirikishi iliyofanyika ambayo inahusisha watu wenye ulemavu. |

## Kiambatanisho namba 6 | Vigezo vya tathmini kupitia lenzi inayojumuisha ulemavu

| Vigezo vya tathmini[243] | Ufafanuzi | Mfano wa mambo yanayohusiana na ulemavu |
|---|---|---|
| Kuwa sawa, muhimu | Kiwango ambacho shughuli za binadamu zinazingatia mahitaji, na hivyo kuongeza umiliki, uwajibikaji na uhalali wa gharama. | Marekebisho yaliyojengwa katika kuboresha ufikivu; watu wenye ulemavu wanashiriki katika ngazi ya kubuni na utekelezaii. |
| Ufanisi, kwenda na wakati | Kiwango ambacho shughuli hufikia kusudi lake; na kama inafanya hivyo kwa muda unaofaa. | Watu wenye ulemavu wanaweza kufikia; na wanaona faida nzuri. |
| Ufanisi/unafuu wa gharama | Matokeo yanayotarajiwa, yale ya ubora na idadi hupatikana kutoka kwa shughuli zinazofanyika; matokeo mbadala hayafikii matokeo sawa kwa gharama ya chini. | Hali ya ufikiaji unashughulikiwa tangu mwanzo, kuboresha ufanisi na unafuu wa gharama. |
| Matokeo/athari | Hupima athari pana za kijamii, kiuchumi, kiufundi na kimazingira za programu. Inajumuisha matokeo ambayo yamekusudiwa, yasiyotarajiwa, mazuri, hasi, jumla (sekta) na ndogo (kaya). | Kama watu wenye ulemavu wanafaidika sawa; kama watu wenye ulemavu wamepata athari zisizotarajiwa. |
| Muunganiko | Kiwango ambacho shughuli za hali ya dharura ya muda mfupi huzingatia muktadha wa eneo na wasiwasi za muda mrefu. | Athari kwa ujumuishaji wa huduma za kitaifa/za mitaa. Kama mifumo ya ndani/kitaifa inayotoa teknolojia ya kusaidia, elimu-jumuishi, n.k, imeimarishwa; kama mashirika ya watu wenye ulemavu yameongezewa uwezo. |
| Eneo lililofikiwa | Kiwango ambacho vikundi vikubwa vya idadi ya watu wanaokabiliwa na majanga ya kutishia maisha vilifikiwa. | Kiwango cha ufikiaji wa watu wenye ulemavu. |
| Mfanano wa sera na vitendo | Kiwango ambacho sera ziko sawa na huzingatia haki za kibinadamu na haki za huduma za kibinadamu. | Kiwango ambacho hatua za huduma za kibinadamu zinatii Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu. |
| Uratibu | Kiwango ambacho majukumu ya wadau tofauti yameratibiwa ili kukuza ufanyaji kazi wa pamoja na kuepusha mapungufu, kurudia jitihada na kusababisha migogoro ya rasilimali. | Kiwango cha ushiriki wa mashirika ya watu wenye ulemavu na wahusika wengine wenye walemavu katika huduma za kibinadamu; ubora wa uratibu. |
| Ulinzi | Kiwango ambacho watu walioathirika wanalindwa dhidi ya vurugu, unyanyasaji, unyonyaji na madhara mengine, kwa kuzingatia haki na uwezo wao. | Kiwango ambacho hatari zinazowakabili watu wenye ulemavu zinatambuliwa, kuondolewa au kupunguzwa. |

[243] OECD-DAC, *Mwongozo wa kutathmini usaidizi wa masuala ya kibinadamu katika hali za dharura* (1998).





## Kiambatanisho namba 7 | Uwajibikaji kwa watu walioathirika na ulinzi dhidi ya unyonyaji wa kingono na unyanyasaji

Jedwali lifuatalo linaonyesha jinsi watendaji wa huduma za kibinadamu, pamoja na vikundi, wanaweza kufikia ahadi na vigezo vya ubora wa Viwango vya Kibinadamu vya Msingi kwa kujumuisha watu wenye ulemavu.

| Ahadi za viwango vya kibinadamu vya Msingi na vigezo vya ubora: | Je, wahusika wa huduma za kibinadamu wanawezaje kuunga mkono hii? |
|---|---|
| 1. Jamii na watu walioathiriwa na majanga wanapokea msaada unaofaa kwa mahitaji yao.<br>**Vigezo vya ubora:**<br>• Huduma za kibinadamu zinafaa na zinatakiwa. | • Angalia njia ya kawaida ya kutathmini mahitaji. Wasiliana na ushirikishe watu wenye ulemavu wakati wa kutengeneza na kuweka vipaumbele vya huduma za kibinadamu.<br>• Wasiliana mara kwa mara na watu wenye ulemavu, kama wanachama wa jamii zilizoathiriwa, ili kuhakikisha ikiwa/kama mipango na shughuli za huduma za kibinadamu zinafaa na zinahusiana. |
| 2. Jamii na watu walioathiriwa na majanga misaada ya kibinadamu wanayohitaji kwa wakati unaofaa.<br>**Vigezo vya ubora:**<br>• Huduma za kibinadamu ni nzuri na zinakuja kwa wakati unaofaa. | • Fafanua vigezo na malengo ya utoaji wa msaada kwa wakati, kulingana na vipaumbele vya watu walioathirika. Watu wenye ulemavu ni kundi muhimu ambalo linapaswa kupata kila aina ya taarifa iliyosambazwa kuhusu usaidizi.<br>• Mara kwa mara wasiliana na watu wenye ulemavu ili kufuatilia jinsi wanavyoridhika na ubora, muda na ufanisi wa ubora. |
| 3. Jamii na watu walioathiriwa na majanga hawaathiriwi vibaya na wamejiandaa zaidi, wanastahimili na hawako hatarini kutokana na hatua za huduma za kibinadamu/misaada ya kibinadamu.<br>**Vigezo vya ubora:**<br>• Huduma za kibinadamu zinaimarisha uwezo wa wenyeji na zinaepuka athari mbaya. | • Fafanua mikakati ya kawaida ya kuimarisha uwezo wa wenyeji. Chukua hatua za kuwashirikisha watendaji wa mitaa na jamii katika kusimamia huduma za kibinadamu. Kuza uwezo wa watu wenye ulemavu kuwa hodari, kuweza kupata taarifa wanayohitaji, na kujua ni lini na vipi wanaweza kupata huduma.<br>• Wasiliana mara kwa mara na watu wenye ulemavu wakati unafuatilia athari mbaya ambazo huduma za kibinadamu zinaweza kuwa nazo kwa jamii zilizoathiriwa au hatari ambazo zinaweza kusababisha. |
| 4. Jamii na watu walioathiriwa na shida/janga wanajua haki zao na wanapata habari na kushiriki katika maamuzi yanayowaathiri.<br>**Vigezo vya ubora:**<br>• Huduma za kibinadamu zinategemea mawasiliano, ushiriki na maoni. | • Andaa mkakati wa mawasiliano kwa watu wenye ulemavu. Weka njia mbili za mawasiliano kulingana na mahitaji na upendeleo wao wa kupata taarifa. Fanya mkakati huo kuwa sehemu muhimu ya juhudi pana za kushiriki na kuwasiliana na jamii zilizoathiriwa.<br>• Andaa mkakati wa ushiriki na ushiriki wa jamii katika usimamizi na michakato ya kufanya uamuzi. Hakikisha inaelezea jinsi watu wenye ulemavu watakavyoshiriki. Fanya ushiriki wao na ujumuishwaji kuwa sehemu ya msingi ya mkakati wa ushiriki wa jamii. |

## Kiambatanisho namba 7 *(inaendelea...)*

| Ahadi za Viwango vya Kibinadamu vya Msingi na vigezo vya ubora: | Je, wahusika wa kibinadamu wanawezaje kusaidia hii? |
|---|---|
| | • Mara kwa mara wasiliana na watu walioathiriwa kupata maoni juu ya ubora wa huduma na uhusiano wao na watoa misaada. Watu wenye ulemavu wanapaswa kutoa maoni juu ya miundo ya miradi kila wakati.<br>• Toa taarifa juu ya hali ya watu wenye ulemavu (vikwazo, hatari, uwezo…) katika mikutano ya washirika na vitengo, katika mifumo ya uratibu kati ya mashirika na sekta mtambuka. Tumia taarifa hizo kuboresha miradi.<br>• Jumuisha mashirika ya watu wenye ulemavu katika miradi, muundo wa maoni na njia za malalamiko na mrejesho na wakati wa kuainisha mifumo iliyopo na mpya.<br>• Kusambaza taarifa na kuongeza uelewa juu ya Mkataba wa Haki za Watu wenye Ulemavu (CRPD) na vyombo vingine vya ulinzi wa kisheria. |
| 5. Jamii na watu walioathiriwa na shida/janga wanafikia njia salama na zinazofaa kushughulikia malalamiko.<br><br>**Vigezo vya ubora:**<br><br>• Malalamiko yanakaribishwa na kushughulikiwa. | • Tambua njia zinazofaa zaidi kwa ajili ya kupata maoni, mrejesho na malalamiko. Fikiria kutumia majukwaa ya kawaida.<br>• Weka itifaki wazi na majukumu ya washirika wote katika huduma za kibinadamu na wadau wakati wa kushughulikia malalamiko juu ya masuala nyeti kama vile kinga dhidi ya unyonyaji wa kingono na unyanyasaji, unyanyasaji wa kijinsia, ubaguzi kwa misingi ya ulemavu, au kinga nyingine hatari.<br>• Mara kwa mara wasiliana na watu walioathiriwa kupata maoni juu ya upatikanaji na usahihi wa mifumo ya malalamiko.<br>• Tumia njia mbalimbali za mawasiliano zinazoweza kufikiwa na watu wote wenye ulemavu (pamoja na lugha ya alama, maandishi ya nukta nundu, taarifa zinazoweza kupatikana kwa kupitia teknolojia ya mawasiliano, vifaa vinavyosomeka kwa lugha rahisi, n.k).<br>• Hakikisha njia za maoni na malalamiko zinalinganishwa na muktadha na mahitaji ya mawasiliano ya wote.<br>• Hakikisha kuwa njia za maoni ambazo zinatoa taarifa juu ya ubora wa msaada na ulinzi zinapatikana kwa wote na ni za siri. |





## Kiambatanisho namba 7 *(inaendelea...)*

| Ahadi za Viwango vya Kibinadamu vya Msingi na vigezo vya ubora: | Je, wahusika wa kibinadamu wanawezaje kusaidia hii? |
|---|---|
| 6. Jamii na watu walioathiriwa na majanga wanapokea misaada iliyoratibiwa na ya ziada.<br><br>**Vigezo vya ubora:**<br><br>• Huduma za kibinadamu zimeratibiwa na ni nyongeza. | • Hakikisha kuwa uratibu wa huduma za kibinadamu (pamoja na vitengo) unapatikana na unajumuisha watendaji wa ndani. Hakikisha inazingatia mahitaji ya jamii kwa jumla, na haswa juu ya mahitaji ya watu wanaofanya kazi na kwa watu wenye ulemavu.<br>• Toa taarifa mara kwa mara kwa washirika na vitengo, na katika ngazi ya kikundi, ili kutambua kwa pamoja na kutekeleza hatua zinazoshughulikia mapungufu yaliyopo.<br>• Wasiliana mara kwa mara na watu wenye ulemavu, na vikundi vingine vya watu walioathirika, wa umri tofauti na jinsia, ili kubaini ikiwa usaidizi umeratibiwa. |
| 7. Jamii na watu walioathiriwa na majanga wanaweza kutarajia utoaji wa misaada iliyoboreshwa wakati mashirika yanajifunza kutokana na uzoefu na tafakari.<br><br>**Vigezo vya ubora:**<br><br>• Wahusika wa kibinadamu wanaendelea kujifunza na kuboresha. | • Tambua mapungufu yoyote katika uwezo wa wahusika wa kibinadamu na uunde mkakati wa pamoja wa kujenga uwezo ikiwa inahitajika.<br>• Hamasisha msaada wa kutosha, rasilimali watu na ufadhili kusaidia uwezo wa washirika wa ndani kutoa msaada bora.<br>• Mara kwa mara wasiliana na watu wenye ulemavu na vikundi vingine katika idadi ya watu walioathirika, wa umri tofauti na jinsia, kupata maoni juu ya uhusiano kati ya watoa misaada na watu wenye ulemavu. |
| 8. Jamii na watu walioathiriwa na shida wanapokea msaada wanaohitaji kutoka kwa wafanyakazi wenye uwezo na wenye kusimamiwa vizuri na wanaojitolea.<br><br>**Vigezo vya ubora:**<br><br>• Wafanyakazi wanaungwa mkono kufanya kazi zao kwa ufanisi na watendewa haki na kupewa usawa. | • Tambua mapungufu yoyote katika uwezo wa wahusika wa kibinadamu na uunde mkakati wa pamoja wa kujenga uwezo ikiwa inahitajika.<br>• Hamasisha msaada wa kutosha, rasilimali watu na ufadhili kusaidia uwezo wa washirika wa ndani kutoa msaada bora.<br>• Mara kwa mara wasiliana na watu wenye ulemavu na vikundi vingine katika idadi ya watu walioathirika, wa umri tofauti na jinsia, kupata maoni juu ya uhusiano kati ya watoa misaada na watu wenye ulemavu. |

## Kiambatanisho namba 7 *(inaendelea...)*

| Ahadi za Viwango vya Kibinadamu vya Msingi na vigezo vya ubora: | Je, wahusika wa kibinadamu wanawezaje kusaidia hii? |
|---|---|
| 9. Jamii na watu walioathiriwa na majanga wanaweza kutarajia mashirika yanayowasaidia kusimamia rasilimali kwa ufanisi na kwa maadili.<br><br>**<u>Vigezo vya ubora:</u>**<br><br>• Rasilimali zinasimamiwa na kutumika kwa uwajibikaji na kwa kusudi lililokusudiwa. Fafanua vigezo vya kawaida vya kiufundi na ubora kwa miradi na mgao wa fedha, pamoja na vigezo vya ushiriki wa jamii na ushiriki. | • Weka vigezo vya kawaida vya kiufundi na ubora kwa ajili ya miradi na mgao wa fedha, pamoja na vigezo vya ushiriki wa jamii na ushiriki kwa ujumla.<br>• Kuweka wazi utaratibu wa ufuatiliaji na utoaji wa taarifa za matumizi ya rasilimali, pamoja na masuala ya ufisadi au upendeleo.<br><br>• Wasiliana mara kwa mara na watu wenye ulemavu, kama kikundi kidogo cha watu walioathirika, kupata taarifa juu ya jinsi rasilimali za misaada zinavyotumika.<br><br>• Wafundishe wafanyakazi kuhusu ujumuishaji wa ulemavu na walio katika sekta ya ulemavu kabla ya kuondoka.<br><br>• Taja waziwazi hali ya ulemavu, jinsia na mzunguko wa maisha katika maelezo ya kazi, tathmini, hadidu za rejea na mifumo ya ufuatiliaji.<br><br>• Kuza ushirikiano na mashirika ya watu wenye ulemavu. Wape fedha na uwape msaada. Hakikisha kwamba makubaliano yote ya ushirikiano yanalingana na Mkataba wa Watu wenye Ulemavu, na unahakikisha kuwa watu wenye ulemavu watafurahia ulinzi na ufikiaji wa msaada na wanastahili kushiriki kikamilifu katika maamuzi na shughuli ambazo zinawahusu. |

**Jedwali lifuatalo linaeleza jinsi ya kuhakikisha kujumuishwa kwa watu wenye ulemavu katika ahadi nne za watendaji wa huduma za kibinadamu.**

| Ahadi za IASC Kuhusu Uwajibikaji kwa Walioathirika na Ulinzi Dhidi na Unyonyaji wa Kingono | |
|---|---|
| **Kanuni za IASC zinathibitisha kwamba watendaji wa kibinadamu watafanya:** | **Hii inamaanisha nini?** |
| 1. **Uongozi**<br><br>Onyesha kuheshimu uwajibikaji kwa watu walioathirika na ulinzi dhidi ya unyanyasaji wa kingono kwa kutekeleza, kuweka masuala ya uwajibikaji katika taasisi na katika programu za kibinadamu na katika michakato ya mipango mikakati katika ngazi ya nchi, pamoja na kuanzisha mifumo sahihi ya usimamizi katika kusikiliza na kutendea kazi vipaumbele ya watu walioathirika katika mantiki ya uratibu, ikiwemo unyonyaji wa kingono, unyanyasaji, kabla, wakati na baada ya dharura. | Wadau wa masuala ya kibinadamu wanawajibika na jamii zilizoathirika wanapaswa kuangalia ujumuishi wa ulemavu katika kila hatua za programu za masuala ya kibinadamu. Wanapaswa kujumuisha sauti za watu wenye ulemavu katika michakato ya kufanya maamuzi. Hii inahitaji uongozi na msaada wa waratibu katika taasisi za kibinadamu ikiwemo viongozi wa vitengo na viongozi wa taasisi. |
| 2. **Ushiriki**<br><br>Kupitisha utaratibu wa shirika ambao unawapa kipaumbele na kuwawezesha wanawake, wanaume, wasichana na wavulana, pamoja na watu waliotengwa na walio katika hatari zaidi kati ya jamii zilizoathiriwa, kushiriki na kuchukua jukumu kubwa katika maamuzi ambayo yataathiri maisha, ustawi, utu na ulinzi wao. Pitisha na dumisha ushirikiano sawa na watendaji wa ndani ili kujenga uhusiano wao wa muda mrefu na uaminifu ndani ya jamii. | Wahusika wa kibinadamu watafafanua, kutekeleza na kuratibu hatua zinazofaa zaidi na zinazofaa ili kuwezesha watu wenye ulemavu, na vikundi vingine vya watu walioathiriwa, wa umri tofauti na jinsia, kushiriki katika michakato ya kufanya maamuzi ya mradi, pamoja na kazi za vitengo.<br><br>Watahimiza na kusaidia washirika kutekeleza njia zinazowapa kipaumbele watu na kushiriki katika kazi zao.<br><br>Wataimarisha na kutanguliza uwezo wa wenyeji na kukuza usawa, uhusiano wa heshima na watendaji wa ndani, kulingana na Viwango vya Kibinadamu vya Msingi na Kanuni za Ushirikiano. |
| 3. **Taarifa, maoni na hatua**<br><br>Pitisha utaratibu wa shirika ambazo zinatoa kipaumbele na kusikiliza jamii, kushughulikia maoni na kuchukua hatua za marekebisha. Anzisha na unga mkono utekelezaji wa njia zinazofaa za kutaarifu na kushughulikia malalamiko yanayohusiana na SEA. Panga, sanifu na simamia programu za ulinzi na usaidizi ambazo zinahusika na utofauti na maoni yaliyotolewa ya jamii zilizoathirika. | Wahusika wa kibinadamu watafafanua na kutumia njia sahihi zaidi na zinazofaa za kusambaza habari kwa watu wenye ulemavu na vikundi vingine vya rika na jinsia tofauti kwa watu walioathirika. Watakusanya na kuchambua maoni na watatumia maoni hayo katika michakato ya kufanya maamuzi. Watatoa taarifa kwa watu walioathiriwa kama hatua za kurekebisha zimechukuliwa.<br><br>Wahusika wa kibinadamu na waratibu wa vitengo, kwa msaada kutoka kwa Wakala na Kiongozi wa Kitengo, watahakikisha kuwa washirika wanaelewa na wanasaidiwa kutekeleza majukumu yao ya PSEA. Wataweka itifaki za wazi jinsi watakavyoshughulika na kutoa taarifa juu ya maoni nyeti na malalamiko. |
| 4. **Matokeo**<br><br>Pima matokeo yanayohusiana na AAP- na PSEA katika kiwango cha wakala na jamii, pamoja na viwango kama vile Kiwango cha Kibinadamu cha Msingi na Viwango vya chini vya Uendeshaji kwenye PSEA; Mwongozo Bora wa Mazoezi wa Kuanzisha Njia za Malalamiko Zinazotegemea Jamii-Wakala na Taratibu zake za Uendeshaji wake. | Wahusika wa kibinadamu watafafanua viashiria vya kupima matokeo kwa watu wenye ulemavu na vikundi vingine vilivyoathiriwa, pamoja na hatua za kuridhika na matokeo.<br><br>Watahakikisha kuwa washirika wana uwezo, na wanasaidiwa, kutumia na kupima ujuzi, ubora, ulinzi na viwango vya uwajibikaji. |